# Shahidi Kwa Ajili Ya Ubinadamu

# Shahidi Kwa Ajili Ya Ubinadamu



Sayyid Ali Naqi Naqvi

Kimetafsiriwa na
Mganga B. Mnuve

Al-Islam.org

**Author(s):**

Sayyid Ali Naqi Naqvi [1]

**Publisher(s):**

Al Itrah Foundation [2]

Kitabu kilichoko mikononi mwako ni tarjumi ya kitabu cha Kiingereza kwa jina la: The Martyr For Mankind. Sisi tumekiita: Shahidi Kwa Ajili Ya Ubinadamu. Kitabu hiki kinazungumzia masaibu yaliyotukia Karbala.

Get PDF [3] Get EPUB [4] Get MOBI [5]

**Translator(s):**

Mganga B. Mnuve [6]

**Topic Tags:**

Karbala [7]
History [8]
Muharram [9]

**Person Tags:**

Imam Husayn [10]

# Neno La Mchapishaji

Kitabu kilichoko mikononi mwako ni tarjumi ya kitabu cha Kiingereza kwa jina la: *The Martyr For Mankind.* Sisi tumekiita: *Shahidi Kwa Ajili Ya Ubinadamu.* Kitabu hiki kinazungumzia masaibu yaliyotukia Karbala.

Masaibu ya Karbala ni maarufu sana. Kila mwaka unapofika mwezi wa Muharram, Waislamu duniani kote hufanya majlisi (mikusanyiko) kwa ajili ya kuomboleza masaibu yaliyompata Imam Husain (as) – mtoto wa Imam Ali (as) na Fatima (as) ambaye ni mjukuu halisi wa Mtukufu Mtume (saww).

Kwa hakika masaibu haya yanazidi kuwa maarufu kadiri miaka inavyozidi kwenda. Waislamu wanazidi

kuathiriwa mno na masaibu haya, na kuwa na hamu ya kutaka kujua zaidi masaibu haya yaliyompata mjukuu huyu wa Mtukufu Mtume (saww) yametokana na nini na yamesababishwa na nini hasa.

Kama ilivyo vitabu vyingi vinavyohusu masuala ya dini vimeandikwa kwa lugha za kigeni, vivyo hivyo maelezo ya masaibu haya mengi yamo kwenye lugha za kigeni, na hivyo Waislamu wengi wazungumzaji wa Kiswahili wamekuwa hawazipati habari hizi moja kwa moja kupitia kwenye vitabu, ila kwa kuhudhuria majlisi.

Tumekiona kitabu hiki ni chenye manufaa sana, hususan wakati huu wa maendeleo makubwa ya elimu katika nyanja zote. Kutokana na ukweli huu, Taasisi yetu ya Al-Itrah Foundation imeamua kukichapisha kitabu hiki kwa lugha ya Kiswahili, kwa madhumuni yake yaleyale ya kuwahudumia Waislamu, hususan wazungumzaji wa Kiswahili.

Tunamshukuru ndugu yetu, Mganga B. Mnuve kwa kukubali jukumu hili la kukitarjumi kitabu hiki. Vilevile tunawashukuru wale wote walioshiriki kwa njia moja au nyingine hadi kufanikisha kuchapishwa kwake.

**Mchapishaji:**
**Al-Itrah Foundation**
**S. L. P. 19701**
**Dar-es-Salaam. Tanzania**

# Shahidi Wa Mwanandamu No 1

# Dibaji

Kwa jina la Allah, Mwingi wa Rehema Mwingi wa Ukarimu.

"Sifa zote njema zinamstahiki Allah Mola wa ulimwengu na rehema na baraka zimshukie mbora wa Wajumbe wake na juu ya kizazi chake kitoharifu."

Nchini Saudi Arabia, sana sana sehemu kubwa ya nchi ni jangwa, Muhammad Bin Abdallah, akijitangaza kuwa ni Mtume karne sita baada ya Kristo alifundisha na kuhubiri dini kubwa ya kuleta mapinduzi ya Uislamu ambayo bila ya kubadili msimamo ilithibitisha umoja kamili wa Allah na ilikana ibada za masanamu, kiumbe binafsi na nguvu. Mafundisho haya yalitishia nguvu na uwezo kwa wale waliokuwa katika madaraka huko Arabuni wakati huo, na kwa mujibu huo wakawa maadui wa Mtume wa kuuana hasa.

Bani Umayyah waliuongoza upinzani dhidi ya Uislam ambao ulifanya ubora na ukamilifu katika utendaji kazi wa mtu, kama mwanaadamu kuwa kigezo cha sifa na heshima. Bani Umayyah hawakuweza kulingana na viwango hivi na Abu Sufyan bin Harb bin Umayyah kwa uchungu sana aliupinga Uislam. Baada ya kupatwa na shida nyingi kwa miaka mingi akiwa katika mji wake wa Makka Mtume alihamia Madina kuokoa maisha yake. Tukio hili lilikuwa ndiyo mwanzo wa zama za ***"HIJRA."***

Maadui wa Mtume mara kwa mara walijaribu kubomoa athari za Muhammad mjini Madina. Mashambulio yao yalipelekea kufika katika kupiganwa vita vingi, ambavyo katika hivyo vilivyokuwa vikubwa sana vilikuwa vile vya Badr, Uhud na vita vya Mtaro (Khandaq). Ushindi wa Uislam uliuvunjavunja kabisa uwezo na nguvu za Bani Umayyahh ambao waliukubali Uislamu ili kuokoa nafsi zao na wakati huohuo kutumia mitego ya imani mpya kuuharibu kutokea ndani yake.

Hawakuwa na muda mrefu wa kungojea, kwani kifo cha Mtume kiliyatupa mambo ya Waislam katika vurugu na wale ambao walibahatika kupata kuchaguliwa au kuteuliwa kama warithi wake waliona inafaa kukubaliana katika uimarishaji wa mamlaka ya Bani Umayyah nchini Syria ambao juu ya huo wakawa watawala. Waliukandamiza usawa wa Kiislam, wakazipinga amri za Qur'ani na kwa kiasi kikubwa wakayapotosha mafundisho ya Mtume.

Watetezi wa Uislamu hawakuweza kuvumilia mateso ya Bani Umayyah. Wakati Ali, binamu na mkwe wake Mtume, na uungwaji mkono wake usioshindika, alipotawalishwa kama Khalifa, aliingia kwenye vita vya kumwaga damu vya Siffin dhidi ya Muawiya, mtawala wa Syria (Sham) kitukuu cha Umayyah. Kazi ya Ali ilikuwa bado kabisa kukamilishwa wakati alipopigwa dharuba mbaya sana ya upanga wakati wa swala yake ya asubuhi.

Mwanawe mkubwa, Hasan, alimrithi na alilazimishwa kwa kubanwa kufanya mkataba wa amani na Mu'awiyah. Huyu Mu'awiyah alivunja ahadi zote ambazo aliyafanya na akafanya Hasan kutiliwa sumu kwa siri (na mkewe) katika chakula. Hasan (alipokufa) alirithiwa na mdogo wake Husein.

Miaka kadhaa baadaye Mu'awiyah alifariki dunia (mwaka 60 A.H.) na mtoto wake mpotovu, Yazid, akawa mtawala wa Syria. Urithi wake uliandaliwa na baba yake lakini alikuwa anatambua changamoto dhidi ya utawala wake kutoka kwa Husein. Kwa hiyo, aliamuru al-Walid bin Utba bin Abi Sufyan, gavana wa Madina, kuchukua kiapo cha utii cha Husein kwake yeye (Yazid). Hili lilikuwa ombi lisilowezekana (kukubaliwa) na Husein akatoka Medina kwenda Makkah pamoja na wategemezi wake wote kwa ajili ya kutafuta usalama (wa maisha yao). Makkah ni mahali patakatifu pa Mwenyezi Mungu na kwa hiyo pakawa ni lazima pawe ni mahali penye usalama. Hapa napo pia aligundua mipango inayotayarishwa ya kumuua. Katika siku ambazo Waislam kutoka ulmwenguni kote walikuwa wanajiandaa kwenda Makka kwa ajili ya utekelezaji wa ibada za Hijja, Husein aliondoka kwenda Kufa ambako alikuwa ameitwa alikuwa tayari alikwishampeleka binamu yake aitwaye Muslim bin Aqil kuona na kukadiria hali halisi ilivyokuwa kule.

Pamoja na kuwepo mambo machache tofauti, watu wa Kufa walishindwa kuziheshimu ahadi za msaada zilizopelekwa kwa Husein baada ya Ubaydullah bin Ziyad kuchukua ugavana. Muslim alisalitiwa na

akauawa kikatili sana. Husein hakuweza kurudi Makkah, wala kusonga mbele kwenda Kufa kutoka mahali ambapo jeshi lenye silaha lilisonga mbele ili kumkamata na kumfanya mateka. Alilazimishwa kusimama Karbala.

Hapo majeshi makubwa yalikusanyika na kuungana ili kumshurtisha Husein ale kiapo cha utii kwa Yazid au akabiliane na maangamizi na kifo.

Kutoka mwezi saba ya Muharram, Husein na masahaba zake, pamoja na watoto wadogo walizuiwa kupata maji. Husein alijadiliana kuhusu amani na kamanda (mkuu) wa majeshi ya Yazid, Umar bin Sa'd, ambaye alishaw– ishika kutokana na dhamira zake za kuheshimika kwamba aandike kwa gavana wa Kufa, akipendekeza suluhisho la amani kuhusu mzozo huu. Ubaydullah, hata hivyo, aliuchukulia msimamo wa kibusara wa Husein kama ni dalili ya udhaifu, na akasisitiza tu juu ya kiapo kisichostahili kwa ajili ya Yazid. Hili likakataliwa.

Vikosi vingi vya Ubaydullah vilianzisha mashambulizi juu ya Husein katika usiku wa mwezi tisa Muharram. Kwa shingo upande kabisa walimpa mjukuu wa Mtume mapumziko ya usiku tu ili utumike katika swala. Labda Husein naye pia alikuwa anataka kutoa fursa nyingine kwa rafiki na adui pia ili kufikiria upya suala lote zima na kutenda alivyoona ndiyo bora mno. Aliwaacha huru masahaba zake pia kwenye kiapo cha utii kwake, na akawashauri wachukue nafasi hiyo ya ufuniko (ulinzi) wa usiku ili kwenda popote pale walipotaka. Masahaba zake waaminifu na watiifu, kwa sauti moja walikataa kumtelekeza (kumwacha peke yake).

Asubuhi iliyofuatia vita hivi vya kifisadi na kiukatili visiyo na ulingano wa majeshi vilipiganwa mpaka karibu na nusu ya mchana wa tarehe kumi Muharram, marafiki wa Husein na wafuasi wake walijitoa mhanga kwa ajili ya utukufu wa haki na uadilifu na kwa ajili ya Allah. Kisha jamaa zake wakawasili katika uwanja wa vita. Miongoni mwao mtoto wake mkubwa Ali Akbar alikuwa wa kwanza kuyaonja mauti. Shujaa wa mwisho kuuweka chini uhai wake alikuwa Abbas bin Ali, ndugu shujaa wa Husein.

Kifo chake kilivunja kabisa ile nguvu ambayo alibakiwa nayo Husein ambaye kishapo alimchukua mtoto wake mchanga, Abdallah, aliyekuwa na umri wa takriban miezi sita, na akamyanyua katika mikono yake akimuombea maji. Hata hivyo, kutoka kule kwenye kundi la askari wengi wa Yazid, jawabu lilikuwa ni mshale tu ambao uliichana shingo ya mtoto mchanga huyo asiye na hatia.

Sasa ikabakia kwa Husein kutoa huo mhanga mkuwa. Ingekuwa ni rahisi zaidi kwake kufanya hivyo kwanza kabisa kabla ya kuachana na wafuasi waaminifu, marafiki wa tangu zamani, wapwa, watoto na kaka zake. Lakini aliahirisha kujitoa kwake mhanga mpaka mwisho ili kwamba mtihani wake uweze kuwa mrefu mno kuliko yote, wenye tofauti kubwa sana na wenye maumivu makali sana kuliko yote. Akiwa peke yake na aliyevunjika moyo, huku amezunguukwa pande zote na maadui wasio idadi, Husein aliuawa baada ya ushujaa mkubwa mbele ya maadui zake duni na waoga. Kichwa chake kisha kikanyanyuliwa juu juu kwenye ncha ya mkuki, na mwili wake na ile ya masahaba zake ikakanyagwa kanyagwa na farasi.

Kambi yake ilichomwa moto na vitu vyao kuporwa na wanawake wa nyumba takatifu kabisa ya Bara Arabu waliachwa bila hifadhi ya kufunika vichwa vyao na wakatembezwa kutoka mji mpaka mwingine kama wafungwa.

Mwanamume pekee aliyebaki wa familia ya Husein, ambaye ni mwanae aliyekuwa mgonjwa, Ali, alifungwa minyororo na, pamoja na ndugu zake wanawake, wakatembezwa kwa miguu kutoka Karbala mpaka Kufa na hadi Damascus (Syria).

Haya ni maelezo kwa muhtasari tu yaliyo ya wazi kabisa kuhusu msiba wa Karbala. Ulitokea nchini Iraq miongoni mwa Waislam. Umuhimu wa ujumbe wa Karbala umevuka mipaka finyu ya eneo la tukio na mpangilio wa jamii yote kwa sababu ya uhusiano wake wenye athari nyingi na kubwa kwa wanadamu wote.
Mvuto huu wenye kuenea pote wa matukio ya Karbala hautokani tu na tabia ya kibinadamu ya kuwaonea huruma wenye kuonewana Husein alipatwa na misukosuko ya kunyang'anywa, kufiwa, kufanyiwa ukatili na ufidhuli kwa namna ambayo hakuna yeyote aliyewahi kupatwa nayo – bali pia kwa vile alipatwa na ukatili wote huu katika kutetea njia ya sawa, uhuru wa dhamira, haki na uadilifu na kuufichua upotofu na udhalimu wa watesaji wake.

Kwa kutoa mihanga kama hiyo isiyokadirika na kulinganishika kwa njia ya utulivu, azma, subira na kwa rikodi isiyo na doa ya matendo matukufu, Husein alitumikia lengo linalochangiwa kwa kufanana katika dini zote, la uendelezaji wa tabia ya mwanadamu kufikia ubora wa kimaadili.

Ni ubinadamu kushikilia furaha na kukwepa huzuni. Kwa hivyo kila mahali matukio ya furaha yanasherehekewa. Ni kifo cha kishahidi tu cha Husein ambacho ndicho kinakumbukwa kwa maombelezo katika nchi za mbali. Kwa vile picha hii bainifu sana imeadhimisha maombolezo ya msiba wa Karbala kwa zaidi ya miaka 1300, inawezekana kuwa kwamba kutoka kwenye huzuni na machozi hutiririka faida kwa waombolezaji.

Hakuna tukio katika historia limekusanyia lenyewe rundo kubwa la maaandishi kama la msiba wa Karbala, lakini hakuna hata kitabu kimoja pekee ambacho mtu anaweza kwa urahisi kurejea ili kuyafahamu matukio ya msiba huu katika mtazamo wao wa kihistoria, matokeo yake na maelezo muhimu kwa kinaganaga. Inatumainiwa kwamba kitabu hiki cha sasa kitasaidia kukidhi haja hii.

**S.A.N.N.**

# Sura Ya 1: Mababu (Wahenga)Watukufu Wa

# Husein

Ibrahim anachukua nafasi ya pande zote, akiwa anatukuzwa na Mayahudi, Wakristo na Waislam sawasawa. Qur'ani inaonyesha kabisa kwamba Mtume wa Uislamu alidai kuifuata dini (imani) ya Ibrahim ambaye aliwaita wafuasi wake Waislam[1]. Ahadith nyingi zenye kuhusu maisha yake ni sehemu ya urithi wa Kiislam na kwa kiwango kikubwa sana zimeathiri mwendo wa Kiislam na maadili.

Ibrahim alikuwa na watoto wawili wa kiume, Is'haak na Isma'il ambao walikuwa kimpangilio ni mababu wa Waisrael na wa Mtume wa Uislamu.

Ibrahim na Isma'il waliinua Ka'aba iliyoko Makka ambayo dini iliifanya mahali pa kukutania watu wote wa ulimwengu mzima. Na miaka ilivyokuwa inapita hii iliota nafasi ya maana sana kwa kizazi cha Ibrahim.

Uislamu unatilia umuhimu mkubwa maelezo ya kimungu yasemayo kwamba Ibrahim alikuwa ameamriwa na Mungu kumtoa kafara mwanawe Isma'il, na akawa tayari kwa kutekeleza mtihani huo mkubwa kwa utulivu mkubwa. Isma'il, pia aliridhia utekelezwaji wa maatakwa ya ki-Mungu, lakini kitendo hasa cha kuchinja kiligeuzwa katika wakati wa mwisho kabisa, uingiliaji kati wa mbinguni ukambadilisha Isma'il kwa mnyama ambaye alitolewa karara badala yake. Hata hivyo ilitangazwa kwamba kafara hilo ambalo limeakhirishwa lingekuwa lije kufanywa kwa chinjo kubwa katika njia ya Mwenyezi Mungu.[2] Uislamu unaadhimisha tukio hili kila mwaka kama Idd al-Adh'ha au Id al-Qurbani, sherehe ya kuchinja (kutoa kafara).

Vizazi vya watoto wawili wa Ismail, Nabit na Qaydhan vilifanya makazi katika Hijaz na vikazaana na kuongezeka kwa idadi kubwa sana. Mmoja wa watoto wa mwanzoni wa Nabit, aliyeitwa Adnaan alikua na kupata umaarufu mkubwa. Vizazi ishirini na moja na karibuni miaka 600 inasimama kati yake na Mtume wa Uislamu ambaye nasaba yake kwa Adnaan haipingiki, na imetolewa katika kiambatisho "A". Hata hivyo, bado kuna wasiwasi kwamba ni yupi katika watangulizi wake alijipatia jina la Quraish. Wakati mmojawapo wa mababu (wahenga) wa Mtume, Qussay, vizazi vitano tu vilipita kutoka yeye, alipopanda madarakani, akaunganisha wato- to wa Nadhr na wakaling'oa kabila la Khuzaa likiwa ndiyo walezi wa Ka'aba, wakaichukua Makka mikononi mwao, wakajenga makazi hapo, wakajenga ukumbi wa halmashauri, wakapanga kanuni za sheria za mwenendo wa kijamii na wakaandaa utaratibu wa kuwapatia chakula na maji mahujaji waendao Hijja[3]

Abd Manaf, mwana wa Qusay, alijipatia jina (umaarufu) mwenyewe katika wakati wa uhai wa baba yake.[4] Mwanae Amri, aliyefahamika zaidi kama Hashim aliwazidi ndugu zake na akapendelewa peke yake kupanga mpango wa kuwapatia maji na chakula mahujaji waendao Hijja.

Alianzisha safari (misafara) za kibiashara kwenda Sham (Syria) na Yemen, na katika wakati wa uhaba aliwahudumia watu wa Makka kwa kuwapatia vipande vya mikate iliyokatwakatwa na kuchovya kwenye supu, akajipatia jina la Hashim, *'Hashm'* likiwa na maana ya "kuvunja vunja', meng'enya n.k. kwa lugha

ya kiarabu.[5]

Hashim alirithiwa na ndugu yake aliyeitwa Muttalib ambaye alifuatwa na mtoto wa Hashim, Shayba, ajulikanaye kama Abd al-Muttalib, ambaye aliwapita kwa utukufu na madaraka wale wote waliomtangulia kabla yake[6] na akapewa cheo cha ***Sayyidul-Batha'*** (kiongozi wa Makka)[7]. Wawili kati ya watoto wake wa kiume walikuwa Abdallah na Abu Talib.

Abdul-Muttalib alikuwa ameapa kumtoa mhanga mwanawe Abdallah, lakini aliweza kuepuka kufanya hivyo kwa kutoa mhanga mbadala wa ngamia mia moja.[8]

Abdallah alimtangulia baba yake kufa, na Abu Talib akarithi shughuli na utukufu wote wa baba yake. Jukumu lake kubwa kabisa, hata hivyo, lilikuwa la uangalizi wa malezi ya mtoto yatima wa Abdullah, Muhammad.

Mapema katika maisha yake mtume huyu wa baadaye alijipatia jina la *Amin* (mwaminifu) kutokana na uaminifu wake na kutegemewa kwake. Waarabu walikabidhi vitu vyao vya thamani kwake kwa ajili ya hifadhi salama na walikuwa wakikubali maamuzi yake katika masuala muhimu.

Uvunjikaji wa sheria wa jumla na uonevu ulifuatia kifo cha Abdal-Muttalib na dhuluma dhidi ya wanyonge na wageni walikaa bila ya kuadhibiwa. Wakati Muhammad bin Abdullah alikuwa amekaribia miaka ishirini aliungana na ndugu zake na baadhi ya makabila mengine ya Ki-Quraishi kuanzisha mapatano (mkataba) muhimu sana (*hilf-alfudul*), ambao kwawo wale wote waliohusika walikula kiapo ambacho kiliwalazimisha kuunga mkono njia ya wenye kuonewa, kupata haki za waliodhulumiwa waliotenzwa nguvu na hasara zao kufidiwa.

Kiapo hiki kilikwenda kinyume na msimamo wa desturi wa Ki-Arabu ambao ulihusisha kutetea fungamano (muungano) la kikabila tu, ambalo wakati mwingine lilikuza migogoro midogo midogo na kufikia kuwepo visasi vya kurithi vya kikabila. Kizazi cha Hashim kiliongoza katika kujaribu kuondosha hali hii ya mwenendo wa kitaifa na kuifanya haki, uadilifu na mwenendo mwema viheshimike mahali pote.

Ali alizaliwa na Abu Talib ndani ya Ka'aba mjini Makka, upendeleo ambao hakuupewa mtu mwingine yeyote yule. Muhammad wakati huo alikuwa na umri wa takriban miaka 30 (thelathini). Wakati Ali alipokuwa bado ni mchanga, njaa iliipiga Makka, na ikamwacha Abu Talib katika mazingira magumu sana, hivyo Muhammad alimchukua Ali kwenda kuishi pamoja naye ili kumwondolea ami yake sehemu ya mzigo wake.

Karne ya saba ya zama za Ukristo ilikuwa kipindi kisichokuwa na ufumo cha ujahilia wakati Uislamu ulipotokea huko Uarabuni. Kwa miaka kadhaa ujumbe wa dini (imani) mpya ulihubiriwa kwa siri sana. Kisha Mtume akaamriwa na Mungu aufikishe kwa ndugu zake wa karibu.[9]

Mtume kwa hiyo aliwaita watoto wote wa kizazi cha Abdul Muttalib, na akijitangaza mwenyewe kama

Mtume wa Mwenyezi Mungu, alilingania upweke wa Mungu (*Tawhid*), na akawauliza wageni waliokusanyika hapo kama ni nani miongoni mwao angemuunga mkono katika kueneza ujumbe wa Uislamu kwa kuelewa wazi kwamba huyo angekuwa ni ndugu, wasii na mrithi wa Mtume. Suala hili aliliuliza kwa kulirudia rudia, lakini kila wakati alikuwa ni Ali tu, ingawa alikuwa bado ni mdogo sana, ndiye aliyejibu, akimuahidi usaidizi kamili. Mtume alimtangaza Ali kama ni ndugu, wasii na mrithi wake.

Kwa ueneaji wa Uislamu, uabudu masanamu ulifikia kukataliwa waziwazi, na kwa sababu hiyo Maquraishi wakawa maadui wa Mtume wasio na huruma na wakaazimia kumdhuru. Madhali Abu Talib alikuwa hai haiba yake yenye nguvu ilimzuia Mtume wa Uislamu kupatwa na huzuni.

Baada ya vifo vya Abu Talib na mke wa Mtume, Khadija, mateso ambayo alikuwa akabiliana nayo yaliongezeka ukali na marudio ya mara kwa mara, na Mtume akaamua kuondoka kwenda Madina. Walipozipata habari hizi, maquraishi waliizunguka nyumba yake usiku mmoja ili wamuue, lakini Mtume aliwatoka akimwacha Ali amelala katika kitanda chake.[10]

Kutoka kwa Mtume kwenda Madina, kuitwako *Hijra*, hakukuzuia uchokozi dhidi ya Waislam, na vita kama vile vya Badr, Uhud na Khandaq (mtaro) ilibidi vipiganwe, na ulikuwa wakati wote ni upanga wa Ali ndio ulileta ushindi wa kung'ara kwa Uislamu.

Mtume alimwozesha binti yake Fatima kwa Ali kwa mujibu wa amri ya ki-Mungu, na aliyakataa maombi ya wengine wengi kwa ajili ya posa ya kipande hiki cha nyama na damu yake mwenyewe,[11] kiongozi wa wanawake wa peponi, ambaye kwamba Mtume alitumia kusimama wakati wowote Fatima alipokuwa akimtembelea. Kutokana na wazazi wa heshima kama hao, Ali na Fatima, walizaliwa watoto wawili wa kiume, Hasan na Husein.

Vipi Husein angeweza kusahau desturi za hali ya juu na sifa zisizo na kifani ambazo familia yake walikuwanazo siku zote tangu zama za kale? Aliwakilisha kawaida ambayo ilikuwa na rekodi isiyovunjika ya utoaji mhanga. Ni lazima awe amesikia jinsi gani babu yake mkubwa (mhenga) Ibrahim alivyoandaa kumtoa kafara mwanawe kwa kutii amri ya mbinguni, jinsi gani babu yake Abdul-Muttalib, alivyomtoa kafara mwanawe Abdullah, jinsi gani mhenga wake Hashim alivyoitumia mali kwa ajili ya kutoa huduma kwa wanadamu, na jinsi gani familia yake ilivyochukua wajibu mkubwa katika kuifanya *hilf al-fudul* kuwasaidia waliokuwa wanateswa na kusimamia haki kwa ajili ya wanaokandamizwa. Kwa hakika Husein alishikilia kwamba kiapo hicho kiliendelea kuwa halali kutumika.

Husein alijua kwamba babu yake mzaa mama yake, Mtume Muhammad (s.a.w.w.), alipatwa na taabu nyingi na mateso yasio na mwisho katika kuu- tangaza na kuueneza Uislamu, kwamba babu yake mzaa baba yake, Abu Talib, alimlinda Mtume na Uislamu kwa nguvu zake zote na uwezo wa haiba yake, kwamba wakati wowote hatari ilipotishia Uislamu, wa kwan- za kukabiliana nayo na kuipiga vita hiyo, bila ya kujali matokeo yote yatakayomtokea, alikuwa ni baba yake, Ali bin Abi Talib.

Ni kawaida tu kwamba simulizi za matendo haya bora na mwenendo wa wahenga wake ni lazima viwe vimewasha moto wa fikira na mawazo ya kijana Husein na kuzaa ndani mwake tamaa ya kutenda

matendo makubwa kama hayo ya ucha-Mungu, ya utii kwa utashi wa Mungu, kutumikia haki na kuiletea heshima familia yake tukufu.

1. Qur'an 2:128
2. Qur'an; 37:107
3. Ibn Is'haaq, al-Sira, uk. 52-56
4. Ibn Is'haaq, uk. 55
5. Ibn Is'haaq, uk. 58
6. Ibn Is'haaq, uk. 61
7. Ibn Is'haaq, uk. 25
8. Ibn Is'haaq, uk. 66 - 68
9. Qur'ani; 26:214
10. Ibn Is'haaq, uk. 223
11. Sahih Bukhari, Juz. 2, uk. 74, 185, 189 na Sahih Muslim, Juz. 2, uk. 290

# Sura Ya 2: Bani Hashim Na Bani Umayyah

Habari zinaeleza kwamba wakati Hashim na Abd Shams, baba wa Umayyah walipozaliwa kama mapacha, kidole cha mmoja wao kilikutwa kimenasa kwenye paji la uso la mwingine. Kilikatwa ili kuwatenganisha vichanga hao, na damu ambayo ilitiririka kutoka kwenye jeraha ilichukuliwa kuonyesha ishara ya ndege mbaya ya kumwaga damu kati ya vizazi vyao.[1]

Umayyah alianza kusababisha nia mbaya kati yake na ami yake, Hashim. Kichocheo kikubwa cha wivu wake kilipatikana katika kipindi cha njaa ambayo iliipiga Makka, Hashim alipata kukubalika sana kwa umma kwa kule kuwagawia wakazi wa mji chakula kingi ambacho kilikuwa katika namna ya vipande vya mikate iliyovunjwa vunjwa na kuchovyekwa katika supu.

Umayyah akatafuta kwenda sambamba na ukarimu huu kwa kujitia kufanya vitendo vya ukarimu ambao hauna maana na mara baada ya muda mfupi wa kutosha uligunduliwa nia yake isiyo nzuri. Katika hali ya mfadhaiko, Ummayah alileta changamoto kwa Hashim la kushindania madai yake ya ubora mbele ya msuluhishi huru anayekubalika. Moja ya masharti lilikuwa kwamba upande utakaoshindwa utahamishwa kutoka Makka kwa kipindi cha miaka 10. Msuluhishi huyo aliamua dhidi ya Umayyah ambaye alihamia Sham (Syria) kwa miaka 10. Hivyo ukatokea uadui kati ya Bani Hashim na Bani Ummayah na uliendelea kuwepo kati yao kwa vizazi vingi.[2]

Kuzaliwa kwa Mtume miongoni mwa Bani Hashim lilikuwa pigo lililovunjavunja heshima ya Bani Umayyah. Kwa hiyo, wao waliutazama utume wa Muhammed kama ushindi wa Bani Hashim na walimfanyia upinzani mkali mno.

1. Tabari, Kitabu al-Ta'rikh, Juz.1 uk. 1089
2. Tabari, Kitabu al-Ta'rikh, Juz. 1 uk. 1090

# Sura Ya 3: Uislamu Na Ujumbe Wake

Kipindi cha kabla ya Uislamu cha historia ya Uarabuni kinaitwa “kipindi cha zama za ujahilia” au “zama za giza”. Isije ikamaanisha kwamba Waarabu walikuwa hawazitambui sanaa na njia za maisha ya kijamii. Karne nyingi kabla ya kudhihiri Uislamu, Arabuni ya Kusini iliendeleza ustaarabu uliostawi na ilijishughulisha na biashara zenye kustawi.

Tungo zao za kishairi zikiwa na baadhi ya vielelezo bora kabisa vya fasihi ya Kiarabu, zinaonyesha kwamba Waarabu walikuwa wana viwango vya hali ya juu kabisa vya ujasiri, ukarimu, ukaribishaji, uaminifu, upendo wa kindugu na upendo wa ndoa. Wakati ambapo walikuwa wanashughulika zaidi na ibada ya sanamu, hawakuwa kwamba hawatambui kabisa kuwepo kwa Mungu Mmoja.

Walikusanyika kila mwaka mjini Makka kwa ajili ya kutekeleza Hijja, lakini walikuwa hawajui kabisa umuhimu halisi wa mikusanyiko hii. Dini nyingine zilizofuatwa katika nchi hiyo zilikuwa Uyahudi wa kuabudu moto na Ukristo. Waarabu walifanya misafara ya biashara kwenda Hijaz, Iraq na Syria. Hata hivyo hali ya jumla ya matatizo na ufukara ndani ya jangwa iliwafanya wawe mabahili, na wakajiingiza katika vita vya kulipiza kisasi, mara nyingi vikienea na kuendelea kwa miaka mingi. Dhana zilizoeleweka vibaya (visivyo) za kujistahi mara nyingi ziliwasababishia kuwauwa watoto wa kike walio wachanga.

Wazo la usawa wa binaadamu lilipuuzwa kabisa katika jamii ambamo ndani yake mlikuwa na ushindani binafsi, wivu wa kivikundi na chuki ya kikabila.

Ilikuwa ni katika mazingira haya kwamba Muhammad bin Abdallah aliyechaguliwa na Mwenyezi Mungu alitokea kueneza ujumbe wa Uislamu. Alikabiliana na kazi ya sulubu. Ingekuwa ni rahisi zaidi kwake kuwarudisha washenzi, watu wasiostaarabika, wanaoishi katika hali ya asili kuliko kuirudisha tena kwenye mwenendo mzuri ule utaratibu wa jamii wenye maradhi.

Ilibidi afundishe uvumilivu, unyenyekevu na msamaha kwa wale ambao kwao sifa hizi zilionekana kuwa dalili za unyonge. Ilibidi afundishe usawa wa binadamu na udugu kwa wale ambao walijivunia nasaba zao. Uislamu pia, umeharamisha matumizi ya pombe (ulevi) matendo ya uchezaji kamari na michezo ya bahati nasibu na kutoa au kupokea riba – yote haya yakiwa maarufu sana miongoni mwa waarabu. Pia ulichukia sana matendo mengine yote maovu.

Uislamu ulileta ujumbe wa uhuru kwa kila mtu kutoka kwenye pingu za ukasisi, kutoka kwenye udhalimu wa wenye ukwasi (utajiri) ambao waliyatumia vibaya matunda yaliyotokana na kazi ngumu za wengine, na kutokana na ukatili wa mabwana kwa wafungwa wao. Pia Uislamu ulitoa faraja kwa wanawake ambao walikuwa wamenyimwa hata zile haki za kibinadamu za kimsingi. Uislamu ulifundisha uhuru, undugu na usawa na kwa mara ya kwanza katika historia ya mwanadamu ulitoa kwa watu wote haki kamili za kiraia na kibinaadamu, ukiamsha matumaini mapya katika nyoyo za waliodhulumiwa na mafukara.

Uislamu ulibashiri kutokuwezekana kupata usawa wa nje wakati watu wakiwa wamejigawa katika makabila mbalimbali na mataifa.

Lengo la Uislamu, kwa hiyo, lingeweza kupatikana kwa mapinduzi ya kisomi, na ulijaribu kuvuta uzingativu wa watu kwenye mamlaka mamoja pekee, kuutengeneza mwishilizio wake bila ya kuingiliwa na vitu vya kimaada.

Njia pekee ya kupata kukubalika kwa jumla kwa ajili ya usawa wa watu wote na undugu ni kuanzisha uhusiano wa moja kwa moja kati ya wingi wa vikundi na umoja mkuu. Kwani ina maana kwamba sehemu za huo wingi zingekuwa baadae zinalingana.

Lakini umoja mkuu ambao wanaadamu wote lazima wauelekee inabidi kwa lazima uwe si wa kimaada kwani vile vyote ambavyo ni vya kimaada vitakuwa ni vyenye kutegemea mipaka mbalimbali kama ile ya umbali, nafasi na idadi. Kwa hiyo, ilikuwa jambo lenye umuhimu sana kwamba mawazo ya mwanadamu yangelenga kwenye ule uwezo usiokuwa wa kimaada, uliozidi ule wa mwanadamu, ambao, kwa kutofungwa na ile mipaka ya nafasi, vipimo na viwango, ungebeba uhusiano kwa kila mtu, na ambao kila mtu alihusika nao. Uwezo huu ni yule Mungu mmoja aliyedhihirishwa na Uislamu kwa kufanyiwa ibada na watu wote, Muumba wa vitu vyote.

Kutambua kwamba wanadamu wote ni viumbe vya Mwenyezi Mungu kumefanya ujenzi wa hali ya usawa na undugu miongoni mwa watu kuwa mwepesi vya kutosha. Baadhi ya dini zimemfanya Mungu kuwa ni wao pekee, na wafuasi wao wanadai kuwa ni watoto Wake. Uislamu umekanusha madai kama haya na kuwafundisha Waislamu kutamka kwamba: “Yeye (Allah) ni mlinzi wetu na mlinzi wenu.” Wakati uki- wafanya wanadamu wote kuwa ni sawa, ulifanya uwezo na ubora kuwa ni sifa ambazo zinaamriwa pekee na tabia za mtu mwenyewe.

Utekelezaji tu wa wajibu wa mtu kama mwanadamu ndio ulivutia ubora wa hali ya juu kabisa. Hivyo tabia za asili zilikataliwa katika kuyachukua mamlaka kwa nguvu za idadi ya watu uongozi na mambo mengine kama hayo. Ubora wa tabia na usafi wa maadili vilisisitizwa sana. Mtume aliutangaza ujumbe wake kwenye kuwaendeleza wanaadamu na ukamilifu wa tabia njema.

Mwislam ameelezewa kuwa ni yule mtu ambaye amejisalimisha kabisa kwa Mwenyezi Mungu. Usawa kwa wote, kimaumbile na kiasili ulitangazwa katika Aya ya Qur’ani, “**Amekuumbeni kutokana na nafsi moja.**”1 Waarabu waliambiwa kwamba nafasi ya kipaumbele haitokani na utaifa; Mquraishi kwa asili hakuwa mbora juu ya asiyekuwa Mquraishi. Matendo yalifuata maagizo mwongozo na maadili ya Mtume. Alimteua Bilal, mtumwa wa Kihabeshi, kuwa mwadhini wake, na wakati mtu mmoja alipolizungumzia jambo hili kwa dharau, Aya ya Qur’ani iliteremshwa ikisema, “**Enyi watu kwa hakika sisi tumekuumbeni (nyote) kutokana na mwanamume na mwanamke,**”2 hivyo kwamba wanadamu wote ni sawa.

Uislamu kwa kweli kabisa unataka kusimamisha serikali ya Mungu. Serikali ya Mungu inasimama moja kwa moja katika uadilifu na usawa. Qur’ani inawaelekeza Waislam, “...**Na mnapohukumu baina ya**

**watu, hukumuni kwa uadilifu,"**[3] na tena inasema **"Wala kuchukiana na watu kusikufanyeni kutotenda uadilifu. Fanyeni uadilifu. Hivyo ndio kuwa karibu mno na uchamungu. Na mcheni Mwenyezi Mungu."**[4]. Kwa sababu hiyo Mtume alitangaza, "Hakuna mtu aliye mbora juu ya mwingine isipokuwa tu kwa sababu ya imani yake na ucha–Mungu." Hata hivyo ingawa alikuwa hodari kuendesha mamlaka yasiyofungwa juu ya wafuasi wake, Mtume kamwe hakujiita yeye mwenye, au kufikiria kwamba yeye alikuwa mfalme.

1. Qur'an; 4:1
2. Qur'an; 49:13
3. Qur'an; 4:58
4. Qur'an; 5:9

# Sura Ya 4 : Uislamu Na Majeshi Ya Kuzuia Mapambano

Sheria, matendo na desturi za Uislamu, kwa ufupi, mfumo wake wa kijamii, ulianzisha wakati wa uhai wa Mtume. Kwa kusababisha mabadiliko haya makubwa, ilimbidi avumilie machungu mazito sana mateso na matatizo makubwa kwake yeye mwenyewe na akakabiliana na upinzani mkali kabisa kutoka kwa wale ambao nafasi yao ya utawala ilitishiwa na Uislamu.

Miongoni mwa mambo mengine, kwa mfano, ulipiga marufuku utozaji na ulipaji wa riba, ukaondoa chanzo chenye manufaa cha mapato kwa wale ambao waliutumia mpango huu. Uislamu pia ulifundisha kwamba utukufu miongoni mwa watu, sana ulitegemea juu ya ubora wa tabia (mwenendo) wa utekelezaji kamilifu kabisa wa wajibu wake mtu.

Hili lilikuwa tishio la hatari sana kwa wale ambao hadhi zao katika jamii zilitegemea kabisa juu ya mali, utajiri na rasilimali za kimaada zilizo sawa na hizo. Kinyume cha hayo, Uislamu uliendeleza kuwepo matumaini kwa mtu masikini sana kupata heshima na utukufu kama atakuwa ametimiza yale yaliyotakiwa kwake katika utekelezaji wa wajibu wake na uchamungu.

Bani Umayyah chini ya uongozi wa Abu Sufyan, wakichochewa na wingi wa uadui na wivu wa zamani na wa karibuni, waliuongoza upinzani kwa Mtume. Alirushiwa mawe. Malundo ya uchafu yalitupwa juu yake na usumbufu mwingi usio na mwisho, mateso na udhalilishaji vilitumiwa dhidi yake. Maisha yake yalitishwa na ami yake, Abu Talib, alimwondoa na kumpeleka kwenye sehemu ya usalama ya ngome yake ya mlimani ambako huko waliipitisha (walikaa) miaka mitatu kwa kujitenga kabisa. Maquraishi walikataa kabisa maingiliano (ushirikiano) ya kijamii na Bani Hashim.

Ndani ya mwaka mmoja wa ufungaji wa sura hii ya msuso wa kijamii, ami yake Mtume, Abu Talib, na

mkewe kipenzi, khadija, walifariki dunia na upinzani kwa Mtume ulibuni njama ya kumuua (Mtume). Alitorokea Madina, akimwacha Ali, binamu yake, akiwa amelala fofofo kitandani mwake.

Hata huko Madina Mtume na wafuasi wake hawakupata nafuu yoyote ile kutokana na vitendo vibaya visivyo vya huruma vya maadui zake ambao waliishambulia Madina zaidi ya mara moja, hata kumlazimisha Mtume kupingana nao.

Vita vya kwanza vya Uislamu, vilipiganwa Badr ambamo Waislam 314 tu,[1] waliokuwa na farasi watatu tu,[2] kwa mafanikio makubwa waliyashinda majeshi yaliyokuwa bora na imara ya Bani Ummayah. Hamza bin Abdul Muttalib, Ubaydah bin Harith na Ali bin Abi Talib walikuwa miongoni mwa mashujaa maarufu wa Bani Hashim.

Ali alifanya mambo makubwa ya ajabu ya ushujaa kiasi kwamba maadui walivunjika moyo. Hasara ya kuhuzunisha kwa Bani Hashim ilikuwa kwamba Ubayda aliuawa. Upande wa Bani Umayyah ulipata hasara nyingi: mtoto wa Abu Sufyan, Hanzal, aliuawa na Ali, ambaye alimchukua mateka mwingine katika watoto wake, (aliyeitwa) Amr. [3]
Hind, mke wa Abu Sufyan aliomboleza vifo vya baba yake, Utba; ami yake, Shayba; na nduguye, al-Walid [4]. Misiba hii ilimzidi nguvu Abu Sufyan kiasi kwamba aliweka nadhiri ya kutokuoga mpaka awe ameon- goza mashambulizi dhidi ya Mtume.

Vita nyingine muhimu kati ya Mtume na makafiri vilipiganwa katika mwaka wa 3 A.H. kule Uhud.[5] Abu Sufyan alikuwa amekusanya jeshi la askari 3,000 wakati Mtume alikuwa na wanajeshi wapatao 700 tu,[6] na farasi wawili. Idadi kubwa ya wanawake ilifuatana na Abu Sufyan kulitia ari na moyo jeshi lake kwa muziki wao wa kijeshi na nyimbo. Hapa pia, Waislam walishinda kupitia ushika upanga mahiri na bora wa Ali bin Abi Talib.

Hamza, ami yake Mtume aliuawa katika vita hivi, na Hind mke wa Abu Sufyan katika kudharau mwenendo wote mwema wa kibinadamu alilichomoa ini lake na akajaribu kulila. [7] Alijipamba kwa kuvaa masikio na viungo vingine vya miili ya wale waliouawa katika vita. Matendo hayo ya kinyama huonyesha kusisitiza kuwepo kwa chuki ya muda mrefu ambayo Bani Umayyah walikuwa nayo dhidi ya Hashim kwa ujumla na hususan kwa Mtume mwenyewe.

Maquraishi walifanya jaribio la mwisho katika mwaka wa 5 A.H. kuupiga Uislamu na kuumaliza. Walifanikiwa kuwapata Mayahudi kwenye kusudio lao na wakaibuka na jeshi lenye askari 10,000 kwa ajili ya “vita ya Makundi” dhidi ya waislam ambao idadi yao ilikuwa ya watu 3,000.

Maadui hawa wa Uislamu kwa mara nyingine tena walishindwa na shujaa wao Amr bin Abd-Wudd alianguka chini kwa upanga wa Ali (aliuawa).

Na hapo Abu Sufyan aliondoka kwenda Makka akiwa amevunjika moyo na tamaa ya kupigana tena na Mtume ikawa imevunjwa kabisa moyoni (mwake).

Alipoona kwamba Maquraishi hawakudhihirisha ishara za uvamizi kwa kipindi kirefu kidogo, Mtume aliongoza baadhi ya Waislam kwenda Makka kufanya Umra au Hijja ndogo, pamoja na ngamia wa kuchinja kuwatoa kafara. Alipogundua kwamba Khalid bin al–Walid alikuwa anajiandaa kumzuia, Mtume aliiacha njia aliyokuwa anaifuata.

Tendo hili la Mtume la kipatanishi lilipelekea kutiwa sahihi kwa mkataba wa amani kati yake na Maquraishi. Mkataba huo ulipiga marufuku vita kati ya makundi hayo kwa kipindi cha miaka kumi, na ukaacha wazi kwa wengine kujiunga na upande wowote waupendao. Iliamuliwa kwamba Waislam wangerudi bila ya kutekeleza ibada hiyo ya Hijja na warudi tena Makka katika mwaka ufuatao na kuikamilisha hija hiyo ndogo ya Umra ndani ya muda wa siku tatu tu na kisha wautoke mji.

Pia (mkataba) huo uliandaa kwamba mtu yeyote yule atakayetorokea kwenye kundi la Muhammad bila ya ruhusa ya mlezi wake lazima arudishwe kwa mlezi wake, lakini kama Quraishi akitoka kwenye ufuasi wa Muhammad huyo asirudishwe. Baadhi ya masharti haya yalikuwa kwa wazi kabisa yasiyo na manufaa kwa Waislamu na baadhi yao walifikiria kuwa ni dalili ya unyonge kutia saini mkataba kama huo. Kwa kweli misingi ya imani ya baadhi ya Waislam ilitingishwa na mkataba wa Hudaibiyyah, kama unavyoitwa.

Mtume aliyakubali masharti yasiyolingana ya mkataba huu ili kukwepa kushutumiwa kwa uchokozi. Aliyachunga masharti ya mkataba kwa maandishi na mazingatio. Mtume alirudi Makka mwaka uliofuata na akatekeleza hijja ndogo ya Umra kama ilivyoelezwa katika mkataba.

Makabila ya Khuzaa na Bakr yalikuwa na hisia za uadui yenyewe kwa yenyewe zilizojengeka kwa muda mrefu, kabila la Khuzaa lilikuwa lenyewe limejishirikisha kwa Mtume, na kabila la Bakr lilijiunga na makafiri.

Mkataba wa amani, kama tulivyokwishaona ulitoa haki ya kukomesha uhasama kati ya makundi haya kwa kipindi ya miaka kumi, na kwa maana hii, hili pia lilitumika kwa makundi yaliyoungana na watiaji sahihi wakuu wa mikataba huo. Kwa hiyo watu wa kabila la Khuzaa waliweka chini silaha zao na wakashtukizwa kwa ghafla na kabila la Bakr ambao kwa siri wakisaidiwa na Maquraishi, waliwaua watu wengi wao wakati wakiwa katika sala zao.

Maelezo ya mauaji haya makubwa yalisimuliwa kwa huzuni kubwa kwa Mtume na msaada wake ulitafutwa kwa kusihiwa sana kiasi kwamba mara moja alikwenda Makka kuwasaidia watu wa kabila la Khuzaa, akiwa amekasirishwa sana na uvunjwaji wa masharti ya mkataba na kwa tabia ya kikatili na ya kufehedhesha ya Maquraishi.

Makafiri walikuwa katika mtawanyiko kabisa na alipogundua hakuna njia nyingine zozote zile za kusalimisha maisha yake, Abu Sufyan aliingia katika Uislam.[8] Mtume wa Uislamu alitoa msamaha siyo kwake tu (Abu Sufyan) bali aliufikisha kwa wale ambao walipata hifadhi ndani ya nyumba yake.

Kisha akawaacha huru watu wote wa Makka. Baada ya haya, hata Hind mke wa Abu Sufyan aliukubali

na kuingia katika Uislam kama kwa hakika walivyofanya watu wote maarufu wa kabila la Maquraishi.

Kukubali Uislamu kwa Bani Umayyah na wapinzani wengine wa Uislamu hakukulazimu kuleta badiliko katika hisia zao halisi kuhusu Mtume.

1. Ibn Ish'haq, uk 336
2. Ibn Ish'haq, 741/Ibn Hisham: Sirat, Juz. 1.uk. 407
3. Ibn Ish'haq, uk. 313
4. Ibn Ish'haq, uk. 358
5. Ibn Ish'haq, uk. 370 – 391
6. Ibn Ish'haq, uk. 373
7. Ibn Ish'haq, uk. 385
8. Ibn Ish'haq, uk. 546

# Sura Ya 5: Kuzaliwa Kwa Husein Na Maisha Yake Ya Utotoni

Mtoto wa pili wa Ali bin Talib na Fatima, binti ya Mtume alizaliwa mwezi wa 5 Shabaan mwaka wa 3 A.H., na aliitwa kwa jina la Husein na Mtume.

Baba yake alijibainisha mwenyewe kama askari asiyeshindika wa Kiislam, aliyekuwa tayari kuzichukua zile kazi zenye hatari sana katika kuulinda Uislamu. Mama yake alionyesha mfano wa tabia mzuri sana kwa wanawake na akaongezea nguvu mafundisho ya baba yake kwao kwa kuwapa maonyesho ya vitendo.

Husein na kaka yake mkubwa walikabidhiwa wote kwenye malezi ya mapenzi na upendo mkubwa wa mwalimu mtukufu kama huyu mjumbe mkuu wa Mwenyezi Mungu, ambaye lengo lake pekee lilikuwa ni kuzitakasa roho.[1] Watoto waliokuzwa katika hali na mazingira ya kimungu mara walipata ubora wa kupigiwa mfano wa tabia na ukamilifu wa maadili.

Tabia nzuri za wajukuu wake ziliwafanya kuwa vipenzi wakuzidi mno kwa Mtume. Aliwataka watu wengine kushiriki katika upendo wake huu na akatangaza, akasema: "Mtu yeyote yule awapendaye hawa, huyo amenipenda mimi na yeyote ambaye atawafanyia uadui huyo ni adui yangu.[2]

Alimwomba Mwenyezi Mungu kuwa shahidi kwamba yeye aliwapenda sana sana wote wawili.[3] Husein alijua, hata hivyo, kwamba Mtume alijizatiti na kujitoa kwa ajili ya mafanikio na utukufu wa Uislamu, na kwamba asingesita kumtoa mhanga kwa ajili ya hilo, kama uhifadhi wa Uislamu ungetaka hivyo.

Mtume alitoa changamoto kwa Wakristo wa Najran nchini Yemen kwa ajili ya shindano la kiroho

(*mubahila*) ambalo ndani yake washindani walikuwa waombe laana ya Mwenyezi Mungu ianguke juu ya kundi amba- lo madai yao yalikuwa ya uwongo. Mtume aliwataka waje na watoto wao, wanawake wao na nafsi zao wenyewe. Yeye (mtume) alimchukua pamoja naye Hasan, Husein, Fatima na Ali. Wakristo walifadhaishwa sana kwa kutokea kwa kundi la Mtume kiasi kwamba walikataa kushindana na wakalipa jizya (kodi) kwake.4

Tukio hili limepata kutajwa katika Qur'ani,5 na miongoni mwa malengo lililoyatumikia ilikuwa kuwafunza watu wa Nyumba ya Mtume kubeba majukumu mazito, na kuwaonyesha watu kwamba ni wao tu pekee wangeweza kutegemewa katika kuulinda Uislamu, na kwamba Uislamu ulimtegemea kila mtu – mwanamume, mwanamke na mtoto – kutoa mchango wake kwa ajili ya usalama wake (Uislamu).

Mtume alieleza wafuasi wake mara nyingi sana kuwafuata Ahlul Bayt wake. Wakati fulani aliwaambia (watu) kwamba anaacha nyuma yake (anawaachia) vitu viwili vizito mno: Kitabu cha Mungu (Qur'ani) na watu wa nyumbani kwake na kivifuata viwili hivyo kungewazuia watu kupotea. Alisisitiza kwamba Hasan na Husein walikuwa ndio viongozi wa vijana wa peponi.

Alibainisha umuhimu wa maana sana wa Husein wakati aliposema "Kama vile maisha ya Husein yanavyotokana na mimi ndivyo uhai wangu unavyotokana na Husein,"6 akiwa na maana yake kwamba ujumbe wake ungehuishwa na Hussein.

Husein alikuwa hajafikia umri wa miaka 7 wakati Mtume alipofariki dunia katika mwezi wa Rabiul-Awwal, mwaka wa 11 A.H.

1. Qur'an; 2; 129 na 151
2. Ibn Maja, Sunan, Juz. 1 uk. 33
3. Sahih Muslim, Juz. 2 uk. 282
4. Irshad, Kur. 116-119
5. Qur'an; 3:131
6. Ibn Maja, Sunan, Juz. 1 uk. 33

# Sura Ya 6: Awamu Ya Pili Ya Maisha Ya Husein

## Tangu Kifo Cha Mtume Mpaka Kuuawa Kwa Ali. ( 11 A.H. Mpaka 40 A.H.)

Kifo cha Mtume kiliwaingiza watu wa familia yake kwenye maombolezo makubwa. Miongoni mwa wale ambao walihuzunika sana hasa walikuwa ni binti yake Fatima na wajukuu zake, Hasan na Husein. Huzuni ya Fatima ilikuwa hailiwaziki kabisa kiasi kwamba alilia kilio cha kumwombeleza baba yake mchana na usiku bila kupumzika kiasi kwamba watu waliona haiwezikani kula chakula chao au kuweza

kupumzika katika mji wa Madina.

Baada ya malalamiko mengi ya kukaririwa yaliyofanywa kwake kuhusu namna gani maombolezo yake yalivyovuruga maisha ya kawaida mjini Madina, alikubali kwenda kwenye uwanja wa makaburi ya Al-Baqi ili aweze hapo kujishughulisha na uombolezaji wake bila kuzuiliwa juu ya pengo lake lisilozibika.

Ama kuhusu wajukuu zake, Hasan na Husein kifo cha Mtume kilileta mateso yasiyoelezeka. Alitoa upendo mwingi sana juu yao na akawalea kwa uangalifu mkubwa na mapenzi katika njia za Uislamu.

Alichukua hatua za kuwaonyesha wafuasi wake kulikuwa na umuhimu kiasi gani kwao katika kuwapenda wajuu zake, na kuwa kuzembea kidogo kabisa katika jambo hili kulimuudhi sana Mtume kutokana na kuwa katika kitovu cha mambo ya Uislamu. (Vijana waliona kwamba watu wa nyumba ya Mtume, ahlul bayt wake walikuwa wamenyimwa madaraka yote, na kwa nje walikuwa wakionekena hawana mamlaka).

Husein lazima atakuwa ameona kwamba baba yake Ali bin Abi Talib alikuwa amejitoa kutoka mambo ya kidunia ili kujizamisha zaidi tu katika kuikusanya Qur'ani katika utaratibu wa uteremsho (wahyi) wake. Somo la kwamba hata katika hali na mazingira yaliyokuwa magumu kiasi gani watu wa nyumba ya Mtume hawakuweza kuacha kuutumikia Uislam, na kwamba kama Qur'ani ilivyokuwa iwe pamoja nao wakati wote, ni lazima wai- hifadhi na kuilinda, lisingeweza kumpotea Husein.

Katika saa hii ya mtihani, Husein aliona kwamba baadhi ya marafiki kama vile ami yake Mtume, Abbas bin Abdul-Mutallib na washirika wasio waaminifu kama Abu Sufyan bin Harb, mkuu (chifu) wa ukoo wa Bani Umayyah, walimshauri Ali kujaribu kuchukua udhibiti wa dola ya Kiislamu yeye mwenyewe.

Abu Sufyan alimchochea Ali, akisema kwamba ilikuwa siyo sawa kwamba moja ya familia zilizo za chini mno ichukue udhibiti juu yake, na kwamba angempatia askari wa farasi kumsaidia. Ali alimpa jibu la mkato akimwambia, "Naapa kwa jina la Mwenyezi Mungu, wewe bado ni adui wa Uislamu."[1]

Hii ilidhihirisha jinsi Ali alivyokuwa imara katika kuyaweka maslahi ya jumla ya jamii mbele zaidi kuliko maslahi yake mwenyewe, na pia kutokuaminika kwa uingiaji wa Abu Sufyan katika Uislamu, na ikawa kama onyo dhidi ya unafiki ambao kwa sura ya marafiki wa uwongo na maadui wenye kudhuru, ni wenye kuleta madhara makubwa zaidi kuliko wawezavyo kufanya maadui wenye kujitangaza kwa dhahiri.

Miezi michache baada ya kifo cha Mtume, Husein alimpoteza mama yake pia. Kutoka kwenye umri mdogo wa miaka saba mpaka kufikia umri wa ujanadume wa miaka thelathini na nane, Husein aliishi chini ya uongozi wa baba yake aliyejaaliwa kipaji, mwenye elimu, mwenye busara na mwadilifu, na lazima atakuwa amepata picha ya ushirikiano huu mpaka mwisho wa siku zake.

Lazima atakuwa amefahamu kwamba, wakati alipohitajika, baba yake bila ya kinyongo aliyatatua matatizo yaliyowakabili Waislamu, na alitoa ushauri wake kuhusu mipango muhimu na safari zenye nia

maalum bila kusita, na ingawaje alisikitishwa sana na uzimwaji wa madai yake juu ya ukhalifa.

Fursa ilijitokeza yenyewe kwa Ali kupata kusimikwa kuwa khalifa wakati wajumbe wote wa baraza la ushauri walioteuliwa na Umar wakati wa kifo chake kuchagua mrithi wake walipokubali kumteua Ali kwa nafasi hiyo iwapo kwa nyongeza ya kufuata sheria za Qur'ani, hadithi na mwendo (sunna) wa Mtume, atakubali pia kufuata hadithi na mienendo ya watawala wawili waliomtangulia yeye. Ali alikataa kukubaliana na ahadi hizi mbili za mwisho na akatupilia mbali ahadi hiyo ya ukhalifa.

Kutokana na mwenendo wa baba yake, Husein alijifunza utumiaji wa kivitendo wa somo muhimu ambalo juu ya hilo, hapo baadaye tabia na mwenendo wake mwenyewe ulitegemea. Aliona kwamba mfumo wa sheria za Kiislam na matendo ya watawala wa Kiislam kwa dhahiri kabisa yalikuwa mambo mawili tofauti na kwamba njia za watawala hazikuweza kutafsiriwa kuwa, au kulinganishwa na mwenendo chini ya mfumo wa sheria ya Uislamu.

Kwa kweli ulikuwa mfumo huu ambao ulikuwa uwafunge watawala wa Kiislam kwa daraja lile lile la ulazimishaji kama ulivyowafunga Waislam wote kwa ujumla. Na wakati mtawala yeyote anapofuata njia zilizo tofauti na kanuni za Uislamu, ilikuwa ni jukumu la Waislam kuilinda dini (imani) na kutoona muhanga wowote kwa ajili ya lengo hilo kuwa na thamani sana.

Katika mwaka wa 31A.H. mabinti wa Yazdigard Mfalme wa Uajemi (Iran), walileta Madina kama wafungwa baada ya kuuawa kwake. Ali na Husein waliwaokoa kutokana na makundi ya wadhalilishaji, na Husein akamuoa mmoja wao, aliyeitwa Shahrbanawayh.

Katika kukaribia mwisho wa miaka ya utawala wa Uthman, khalifa wa tatu, watu walianza kujihisi kutoridhika kabisa na utawala wake, na hata wakaishia kwenye kufanya matendo ya vurugu. Ali aliingilia kati mara nyingi sana ili kuleta amani na akafanya baadhi ya malalamiko kuweza kurekebishwa. Aliwashauri wafanyaghasia kutawanyika na warudi walikotoka.[2] Lakini Marwan, mkwe na katibu wa khalifa alionyesha ukatili sana kiasi kwamba jitihada za Ali katika kuleta amani zilishindwa, na waasi wakayazingira makazi ya khalifa ambaye maombi yake ya mdomo ya kupatiwa maji yalisikiwa na Ali.

Ali aliwaagiza wanawe, Hasan na Husein, kupeleka maji kwa Uthman katika hali ya hatari kubwa sana kwa maisha yao binafsi. Khalifa huyo hata hivyo, aliuawa na kundi lililokuwa na vurugu nyingi.

Inastaajabisha kwamba ingawaje khalifa alibakia kushambuliwa hapo Madina kwa siku 49,[3] hakuna hata mkazi mmoja wa mji huo alijitokeza kuja kumwokoa, na kwamba alibakia bila kuzikwa kwa muda wa siku tatu na kwamba hatimaye mabaki ya mwili wake hayakupata nafasi katika eneo la makaburi ya Waislam.[4]

Baada ya ghasia kutulia Waislam waliamua kumweka Ali kama khalifa wao. Katika matukio yote ya nyuma ya uchaguzi wa khalifa, Ali alikuwa amehoji kwa nguvu sana kuhusu ubora wa madai yake juu kazi hiyo, lakini sasa hakuwa tayari kabisa kuukubali (ukhalifa), kwani aliona kwamba katika miaka iliyoingilia kati, serikali ya Kiislam ilichukua sura na ari ya falme za kikoo, ambayo ilikuwa na urahisi usio

rasmi usiyopatana na moyo wa kupenda usawa wa Uislamu.

Ali asingeweza kuvumilia uozo uliokuwepo katika utawala uendelee, na alijua kwamba katika kujaribu kuusimamisha angezusha wimbi la upinzani usiodhibitika ambao ungechukua muda mrefu kuudhibiti, na kwamba kwa wakati huohuo angejiweka kwenye hali ya kuitwa mtawala asiyefaa. Hata hivyo Waislamu walisisitiza kwamba aukubali tu ukhalifa, na Ali kwa shingo upande sana alikubali kufanya hivyo. Katika mwezi wa Dhil-Hijja mwaka wa 35 A.H. Waislam walitoa kiapo cha utii kwa Ali kama khalifa wao.

Baada ya Ali kuchukua madaraka, wasiwasi wake uligeuka kuwa kweli. Watu hawakuwa na mwelekeo wa kutekeleza maelekezo (maagizo) yake. Baadhi ya Waislam mashuhuri kama vile Usamah bin Zayd, Hasan bin Thabit, Abdallah bin Umar na Sa'd bin Abi Waqqas walijizuia kutoka kiapo cha utii kwake. Ali, hata hivyo hakuchukua hatua yoyote dhidi yao kwa vile katika Uislamu "hakuna kulazimishana katika dini."

Kushikilia Syria kwa Mu'awiyah kulitiwa nguvu na kile kipindi kirefu cha ugavana wake wa nchi hiyo, na Ali alishauriwa ambakishe yeye pamoja na maofisa wote walioteuliwa na Uthman katika nafasi zao za kazi, kama hatua ya uangalifu mpaka watakapokuwa wamejinyenyekesha wenyewe kwenye udhibiti wake.

Ali alikataa kukikubali kipande hiki cha ushauri ambacho kingekuwa na maana ya kuunga mkono udhalimu na uharibifu wa watendaji hawa, na kwa kweli ni kama kushiriki kwenye maovu haya. Ali alimwandikia Mu'awiyah barua akimwambia alivyoikubali kwa shingo upande kazi ya ukhalifa na akamtaka apate viapo vya utii kutoka kwa watu wa nchi yake kwa ajili ya khalifa mpya.

Pia alimtaka Mu'awiyah aje yeye mwenyewe pamoja na ujumbe wa watu wa Syria.[5] Mu'awiyah hakutekeleza lolote katika maelekezo haya, na uadui wa toka zamani ulimshawishi kuzua shitaka la uwongo la mauaji ya Uthman dhidi ya Ali dhidi ya yule ambaye hata yeye pia alimwasi. Mwanazuoni mkubwa wa Kisunni, Ibn Hajr amemnukuu Marwan bin al-Hakam akiwa amekiri kwamba hakuna aliyekuwa na msaada mkubwa zaidi kwa Uthman kuliko Ali, na kama alivyokuwa amesema kwamba matumizi ya lugha chafu dhidi ya Ali yalifanywa kwa sababu, kwani bila kufanya hivyo Bani Umayyah wasingeweza kusimamisha mamlaka yao.[6]

Mu'awiyah alichukua hatua za aina mbalimbali kuwachochea watu wa Syria dhidi ya Ali. Mikutano iliyohudhuriwa na watu wengi ilifanyiwa mara kwa mara katika msikiti wa swala za jamaa wa Damascus kuomboleza mauaji ya Uthman ambamo shati lake lililolowa damu na vidole vilivyokatwa vya mke wa khalifa (Uthman) vilionyeshwa kwa makundi makubwa ya watu ambao walipandisha sauti za maombolezo, na katika mfadhaiko huu wa huzuni walishawishiwa kulipizia kisasi mauaji yake.[7]

Wakati maendeleo haya kiuchochezi yalipokuwa yanafanyika nchini Syria, Talha na al-Zubeir waliweka upinzani mkubwa kwa Ali, wakiungwa mkono na Aisha, mjane wa Mtume na binti ya Abu Bakr, khalifa wa kwanza.

Ali alikwishakuwa mtu mzima na kwa kipindi kirefu aliishi maisha ya faragha. Hata hivyo, alijiandaa kwenda vitani na kupigana dhidi ya Aisha kuzilinda sheria na kanuni za Uislamu na za haki kwa nguvu zake za kawaida kwani jukumu la ulinzi wao ulikuwa hasa juu yake yeye. Kampeni hii ilikomea katika kutokea vita ya Ngamia, kwani Aisha aliliongoza jeshi lake kutoka kwenye kiti chake juu ya ngamia, na kushindwa kwake kabisa mnamo mwezi 10 Rabiul Thaaniya mwaka wa 36 A.H.

Katika wakati wa ushindi wake Ali alimtendea Aisha kwa uungwana na ukarimu usio na kifani na alimpeleka Madina kwa heshima kubwa akisindikizwa na askari ambao wote walikuwa wanawake waliojifanya kama wanaume.

Huko Syria vurugu na uchochezi wa ghasia viliendelea bila kupungua nguvu. Maombolezo kwa ajili ya Uthman yaliendelea kufanywa kwa mwaka mzima kamili na watu wengi wa Syria walichukua nadhiri ya kujiepusha na raha za kidunia mpaka wawe wamewaua wale wote ambao walimuua Uthman, hivyo Mu'awiyah akafanikiwa kuiamsha nchi yake dhidi ya Ali mpaka mwishowe vita vya Siffin vilikuja kupiganwa kati yake na Ali.

Ni lazima itajwe kwamba mpaka wakati wa mwisho kabisa kabla ya kuanza kwa vita Ali alijitahidi kwa kusisitiza kuwashauri wapinzani wake kutenda kwa busara na uadilifui na kutafuta kuungana na wanaodhaniwa kuwa ni maadui zao. Hata hivyo ushauri wake wa usuluhishi ulikataliwa na damu ya Waislam ikamwagika kwa wingi sana.

Kama kawaida, Ali aliliagiza jeshi lake lisianze mashambulizi, wakiliachia jeshi la maadui kuanza vita. Pia alikataza ufukuziaji wa adui aliyeshindwa, kumuua adui aliyejeruhiwa, kuukatakata mwili wa mtu aliyekwishakufa, alikataza kulazimisha kuingia katika hema bila ya kuruhusiwa, kupora mali ya adui na kusababisha madhara kwa wanawake hata katika hali ya kuchokozwa.

Wakati wa vita, majeshi ya Mu'awiyah yalitwaa udhibiti wa mto Furati (*Euphrates*) na yakasimamisha hudumu ya ugavi maji kwa jeshi la Ali ambalo liligeukia katika kutumia nguvu na hatimaye wakapata tena udhibiti juu ya mto huo. Ali alikataa kulipiza kisasi kwa kusimamisha huduma za kulipatia maji jeshi la Mu'awiyah, na akajishusha mwenyewe kufikia kiwango cha maadui zake.

Ali alipata uchungu sana kuona damu nyingi ya waislamu inamwagika katika vita vya Siffin, na akamwambia Mu'awiyah kwamba kwa vile vita halisi ilikuwa kati yao wawili, ingekuwa ni unyofu juu yao (Ali na Mu'awiyah) kuliamulia jambo hili kwa kukutana wao wawili katika pambano la watu wawili tu. Mu'awiyah hakutoa jibu, akiogopa kwamba asingeweza kunusurika katika pambano kama hilo. Kwa hiyo, yeye alishikilia tu kuwatoa muhanga wengine kwa malengo yake binafsi.

Mu'awiyah, alitembelea uwanja wa vita kwa nadra, wakati Ali alikuwa akionekana kila mahali ndani yake akiliongoza jeshi lake, wakati mwingine akilielekeza na zaidi sana yeye mwenyewe akiwa katikati ya vita vyenyewe. Alitamani kupata shahada na akaapa kwamba mapigo elfu moja ya upanga kwenye kichwa cha mtu yalikuwa yanastahimilika zaidi kuliko kifo cha kuteseka muda mrefu kitandani mwake mtu.[8]

Mwenendo wake sasa ulifuata mkondo uleule wa kutokusita kujihatarishia kifo kwa ajili ya Uislamu kama ulivyofuatilia hapo mapema katika maisha yake wakati alipolala katika kitanda cha Mtume usiku, Mtume alipotorokea Madina.

Husein na ndugu zake walihusika kikamilifu katika vita hivyo na wakamtumikia baba yao kwa uimara mkubwa katika nyakati za hatari kubwa kabisa.

Wasingeweza kutenda kinyume kabisa kwani walikuwa watoto wa Ali ambaye alikuwa amemwambia Husein wakati wa vita hivi kwamba ilikukwa haina tofauti muhimu kama ni kifo kimwangukie au ni yeye akiangukie kifo.[9]

Siku moja wakati vita ambapo vilipokuwa vimepamba moto, Ali alionekana akiliangalia jua ili kuhakikisha kama wakati wa swala ya mchana umekwishaingia. Alipoulizwa kama huo ulikuwa ni wakati wa kuswali katikati kabisa ya vita, Ali alijibu, “Ni kitu gani tunachokipigania basi?” Alifundisha kwamba swala ni lazima zisimamishwe katika wakati wake makhsusi iwe inamiminika mishale au moto.

Ili kuifupisha vita, siku moja Ali alifanya shambulio kubwa kabisa juu ya maadui, akiendeleza mashambulizi hadi usiku mzima uliofuatia. Wakati kulipopambazuka, watu wa Syria walikuwa wameshindwa vibaya sana na idadi yao kubwa walikuwa wameuawa na wengine kujeruhiwa.

Ilionekana kwamba wasingeweza kukwepa kushindwa kwa muda mrefu. Amr bin Aas, mshauri wa Mu’awiyah, alikimbilia kwenye hila ya kunyanyua nakala za Qur’ani Tukufu juu zikiwa zimechomekwa kwenye ncha za mikuki na kupandisha sauti zao juu wakidai kwamba tofauti kati ya pande husika zirejeshwe kwenye Kitabu cha Mwenyezi Mungu (Qur’ani) kwa ajili ya uamuzi.

Ali alikwisha ng’amua mtego wa hila hii na akawashauri wafuasi wake dhidi ya kuangukia katika mtego huu uliowekwa na watu wale ambao kamwe hawakuamini Uislamu wala hawakuwa na heshima yoyote juu ya Qur’ani. Aliwakumbusha pia kwamba ombi kama hilo alilokuwa amelitoa yeye kabla ya kuanza kwa vita lilikuwa limekataliwa.

Lakini watu wengi wa jeshi la Ali walikuwa wamepotoka katika kukataa maagizo yake na wakageuka dhidi yake, na hata kumtishia maisha yake. Wakati utovu wa nidhamu kamili ulipozidi ndani ya jeshi lake, Ali alisitisha mapigano. Masuala kati ya pande mbili hizi zenye kushindana yalipelekwa kwa wasuluhishi wawili, Amr bin al-Aas na Abu Musa al-Ash’ari.

Amr bin al-Aas alimwakilisha Mu’awiyah na watu wa Syria na Abu Musa al-Ash’ari alilazimishwa juu ya Ali kuwa kama mwakilishi wake, kinyume kabisa na alivyotaka mwenyewe, na akawa kama mwakilishi wa wakazi wa Kufa. Tabia ya Abu Musa huko nyuma ilikuwa imeonyesha mwelekeo wake usiopendeza kumhusu Ali ambaye alikubali kuchaguliwa kwake kwa ajili tu ya kukwepesha umwagaji wa damu ndani ya kundi lake.

Makundi hayo mawili yalikubaliana kutii uamuzi wa Mwenyezi Mungu na Kitabu Chake na sio kitu

kingine kile. Wasuluhishi walikuwa chini ya masharti ya kuiweka Qur'ani wakati wote katika mazingatio na kuifanyia kazi, na kama hawakupata mwongozo kutoka humo, ilikuwa watende kwa mujibu wa matendo na kanuni za Mtume zisizotiliwa shaka. Ali alichukua tahadhari kuwasisitizia kwamba hawakupewa mamlaka yoyote yale ya kuamua kwa kulingana na fikra zao binafsi. Mkataba huu ulifanyika mwezi 13 Safar, 37 A.H.

Makubaliano haya yalikuwa hata bado hayajaanza kutekelezwa wakati fitna mpya ilipoinua kichwa chake kibaya katika sura ya makhariji ambao walinyanyua ndani ya jeshi la Ali ule wito wa makelele kwamba hakuna hukumu isipokuwa ya Mwenyezi Mungu. Kwa hiyo, wao waliuchukulia ule uteuzi wa hivi karibuni wa wasuluhishi kuwa ni wenye makosa na wakamshinikiza Ali kupigana na Mu'awiyah na wakaahidi kumsaidia. Ali alikataa kuwakubalia akisema kwamba Qur'ani inaagiza kwamba neno lililowekewa ahadi lazima liheshimiwe. Ma-Khariji wakageuka kuwa wasaliti kutoka kwenye Uislamu na wakaunda kundi lao tofauti.

Wasuluhishi wakapuuza kabisa masharti yote ya chombo cha usuhulishi na wakadharau sheria za Qur'ani. Amr bin al-Aas alikuwa bingwa mkubwa katika hila na akamfanya Abu Musa al-Ash'ar kuwa mjinga kabisa. Alimmvutia Abu Musa al-Ash'ari kwa tabia yake ya kiheshima kwamba kwa kweli yeye alimheshimu sana Abu Musa kuwa ni mkubwa na mbora kwake, na kwa hiari kabisa akamkubalia kutangulia.
Kati yao wenyewe, walitokea kuamua kuwatangaza wote wawili Mu'awiyah na Ali kuwa hawafia kushika wadhifa wa ukhalifa na (wakaamua) kuwapa Waislam haki ya kuchagua khalifa mwingine.

Wakati muda ulioteuliwa wa kutoa tangazo la uamuzi wa wasuluhishi ulipofika, Abu Musa al al-Ash'ari aliombwa na Amr bin al-Aas kutangaza uamuzi huo, ambao akautangaza kama walivyokubaliana kati yake na Amr bin al-Aas.

Kisha Amr bin al- Aas alisimama kusema kwamba kwa vile Abu Musa anamwakilisha Ali, alikubaliana na uamuzi wake wa kumuuzulu Ali kutoka kwenye ukhalifa. Akaongoza kwamba akiwa kama mwakilishi wa Mu'awiyah, yeye anausimika ukhalifa juu yake.

Uamuzi huu usio wa udanganyifu ulisababisha vurugu na miongoni mwa wale waliokuwepo, na wasuluhishi wakafanyiwa fujo. Uamuzi ukakataliwa na pande zote. Ushindani kati ya pande zote ukabakia bila kufumbuliwa. Tukio hili liliimarisha ile rabsha ya mgawanyiko katika safu za kundi la Ali na liliwapa Makhariji muda wa kujiweka sawa ili kuweza kumpinga Ali kwa upinzani mkali katika vita vya Nahrawan ambayo vilifuata.

Hata baada ya vita vya Nahrawan ambamo Makhawarij walipata kipigo na kushindwa kabisa, bado utovu wa nidhamu, vurugu na uchochezi wa maasi ulikuwa bado haujang'olewa kabisa ndani ya jeshi la Ali. Alikuwa kwa kweli katika masaibu yasiyopendeka. Alikuwa na mzigo wa wafuasi wasio waaminifu waliogawanywa na kutoelewana na mfarakano. Makhawarij ambao walikuwa hawakupigana au walitoroka kule Nahrawan walichochea hisia za kufanya uasi dhidi yake miongoni kwa watu. Mu'awiyah

aliitumia nafasi hiyo ya kukosekana umoja uliokuwepo Kufa.

Aliyatumia majeshi yake kuchochea ghasia katika nchi za Kiislam na alikimbilia matendo kama hayo kama ya kuwaondolea wapinzani, kama vile Malik al- Ashtar,[10] kwa kuwafanya watiliwe sumu au kwa njia nyingine za kudanganyifu, kama katika suala la Muhammad bin Abu Bakr, ambaye alikuwa amelelewa na Ali na alikuwa mmoja wa wafuasi wake watiifu mno.

Alipelekwa na Ali kuwa gavana wa Misri na kwa ombi la Mu'awiyah, Amr bin al-Aas aliongoza jeshi dhidi yake kwa ushirikiano kabambe na kikosi cha wahaini wa Kimisri[11]. Hili liliishia katika kushindwa kwa Muhammad bin Abu Bakr na kuuawa kwake. Mabaki ya mwili wake kisha yalichomwa moto.[12]

Alipoona kwamba ilikuwa vigumu kumshinda Ali katika vita vya viwanja vya wazi, Mu'awiyah alitumia mbinu vita vya msituni kama njia ifaayo ya kuiweka dola ya Kiislam katika hali ya hofu, fujo na ghasia wakati wote.

Idadi ya mashambulizi kama hayo ya ghafla na kukimbia yalifanywa na wafuasi wa Mu'awiyah, na baadhi walizuiliwa kwa nguvu na kurudishwa nyuma. Shambulizi la kikatili sana la namna hiyo liliongozwa na Busr bin Abi Artat dhidi ya Hijaz, tukio ambamo alilazimisha viapo vyao vya utii kwa Mu'awiyah kutoka kwa wakazi wa Makkah na Madina, na akawachinja watoto wawili wa kiume wa Ubaydullah bin Abbas nchini Yemen.

Ali alikuwa anajishughulisha katika kujiandaa kupambana na tishio hili, lakini katika wakati ule ule Ibn Muljam al-Muradi alimpiga dhoruba kichwani kwa upanga uliotiwa sumu wakati akiwa yuko katika kusujudu mbele ya Mwenyezi Mungu ndani ya msikiti wakati wa swala ya asubuhi (alfajiri) ya siku ya mwezi 19 Ramadhani mwaka wa 40 A.H. Siku tatu baadaye, Ali akawa hayupo tena katika ulimwengu huu (akafariki dunia).

1. Irshad, uk. 136, Tabari, Juz.1, uk. 1827-8
2. Tabari, Juz. 1 uk. 2969 na 2971
3. Tabari, Juz.1 uk. 3009
4. Tabari, Juz.1 uk. 3008
5. Nahjul-Balaghah, Juz. 2, uk. 140
6. Ibn Hajr, al-Sawaaiq, uk. 33
7. Tabari, Juz. 1, uk. 3091
8. Irshad, uk. 177
9. Tabari, Juz. 1, uk. 3294
10. Tabari, Juz. 1, uk. 3401
11. Tabari, Juz. 1, uk. 3404
12. Tabari, Juz. 1, uk.3406

# Sura Ya 7: Uwezo Wa Bani Umayyah Na Namna Zake Za Utaratibu Wa Kisiasa

Bani Umayyah walilazimika kuukubali Uislamu ili kuyaokoa maisha yao, na siyo kwa imani yoyote ile kuhusu ubora wa ujumbe wake. Matokeo yake waliendelea kuendekeza, katika nyoyo zao hisia za chuki na uadui juu ya dini (imani) yao mpya waliyoipata, na walisubiri kwa shauku kubwa kuipata fursa ya kuuangamiza mwenendo wake, kwani waliona kwamba ilikuwa nje ya uwezo wao kufanya jaribio la wazi la maangamizi yake ya mara moja.

Walifikiria mpango unaofaa sana wa kiutendaji kuziharibu na kuzichafua tabia na sifa pambanuzi za Uislamu ambazo zilivunjilia mbali uwezo wao. Ilikuwa ni kutumia kivuli cha Uislamu wenyewe kuidhuru imani yake, na kuufagilia njia ufufuaji upya wa maadili na fursa zilizokuwepo kabla ya kudhihiri Uislamu.

Kwa ufupi, walikuwa wanafiki. Madhara kidogo sana yaliyopatikana au kutegemewa kuwapata Waislam yalileta furaha ya kiuovu iliyofichika kwa Bani Umayyah.

Hivyo katika vita vya Uhud, pale watu wote walipokimbia isipokuwa Waislamu wachache waaminifu, Abu Sufyan alionyesha furaha yake kwa lile alilolifikiria kuwa ni ushindi wa sanamu la kipagani liitwalo al–Uzza.[1]

Hadithi kuhusu namna gani Ali alivyozuia jaribio la kwanza la Abu Sufyan la kutaka kuvuruga Uislamu kwa kukataa kuukubali msaada wa kijeshi alioupewa na yeye Abu Sufyan wakati Abu Bakr alipowekwa kuwa Khalifa kuliko madai yake Ali ambayo yamekwishasimuliwa.

Ali mara moja alikwishauona mchezo huu wa Abu Sufyan na akamwambia kwamba yeye (Abu Sufyan) alikuwa ni adui wa Uislamu na Waislamu.

Abu Sufyan bila kusita alibadilika, na kwa mafanikio makubwa akajadiliana masharti ya ushirikiano na wapinzani wa Ali. Khalifa wa kwanza alipeleka jeshi kubwa kuivamia nchi ya Syria katika mwaka wa 13 A.H., na miongoni mwa wale ambao waliongoza jesi hili walikuwamo watoto wawili wa Abu Sufyan, Yazid (bin Abu Sufyan) na Mu'awiyah.

Abu Sufyan mwenyewe alishughulika kama msimuliaji wa hekaya kwa ajili ya burudani ya viongozi wa vita,[2] na binti yake na mkwewe pia walishiriki katika vita hii. Baada ya ushindi wa Syria, Yazid bin Abu Sufyan aliteuliwa kuwa gavana wa nchi hiyo. Alipokufa alirithiwa na ndugu, yake, Mu'awiyah.[3]

Wakati wa kipindi cha ugavana wa watoto wao, Abu Sufyan na Hind, ambaye alikuwa ameachika, walipata manufaa mengi za kiuchumi. Hind alitanguliziwa fedha kiasi cha dirham 4,000 kutoka kwenye Hazina ya taifa ambazo aliziwekeza katika biashara yenye faida kubwa sana.

Abu Sufyan alilipwa dinari mia moja kama gharama za kujikimu wakati alipotembelea Damascus,[4] ingawaje bado alikuwa na nia mbaya dhidi ya Uislamu kwani yeye hakuweza kuzishinda hisia za huruma alizozichukua kwa ajili ya wa-Byzantine, waliokuwa kwa wakati huo wakipigana huko Yarmuk dhidi ya Waislamu.

Uthman alikuwa Khalifa mnamo mwaka wa 23 A.H. na Abu Sufyan akamshauri kuimarisha mamlaka yake kwa msaada wa ndugu zake, Bani Umayyah. Aliongeza kwamba ni mamlaka ya kidunia tu ndiyo yenye maana, kwani hakuweza kuelewa imma pepo au jahannam.

Abu Sufyan na watu wa familia yake waliugeuza ukhalifa wa Uthman kwa manufaa kamilifu kabisa. Sehemu za Hims, Qinnasrin na Palestina ziliongezewa kwenye milki ya Mu'awiyah na akawa mtawala wa Syria yote.[5]

Inaelekea kwamba ushauri wa Abu Sufyan ulipelekea kwenye uharibifu wa Uthman na hatimaye kuuawa kwake. Katika mahojiano yake ya kwanza na Uthman kuhusu marekebisho ya kufanywa katika utawala, Ali alimwonya akisema, "Unatoa tahafifu zisizo za kawaida na upendeleo kwa ndugu zako, unapuuzia makosa yao, hata Mu'awiyah humwonyi wakati anapofanya mambo bila ya idhini yako, na humshutumu wakati anapotangaza kwa uwongo kwamba matendo yake yana kibali chako."

Madaraka makubwa kama hayo yalikuja kutumiwa na Mu'awiyah kiasi kwamba ikaanza kusemwa waziwazi kwamba angekuja kumrithi Uthman kwenye Ukhalifa. Akihisi mustakabali wake kuwa salama kabisa, Mu'awiyah alipuuzia kwenda Madina kumsaidia Uthman dhidi ya waasi ingawa alikuwa amefika karibu na mji ule. Alipendelea kuwa mtazamaji tu katika masaibu ya Khalifa huyo mzee kutoka kwenye umbali ulio salama. Mshauri wake mkuu na muungaji mkono, Amr bin al-Aas kwa wazi kabisa alichochea vurugu na uasi dhidi ya Uthman na akarudi Palestina kungojea kusikia matokeo ya jitihada zake.

Bani Umayyah walitwaa njia zote za wafalme baada ya kujiimarisha wenyewe katika madaraka. Katika utukufu na fahari iliyoingizwa katika maisha kwenye makasiri yao, ule utulivu, usawa na undugu wa Uislamu ulikuwa hauna nafasi yoyote ile, ukiwa mahali pao pamechukuliwa kabisa na ustaarabu wa kidunia.

Pombe ilianza kutumika kwa uhuru kabisa hususan na watu matajiri, na pale mmoja wa masahaba wa Mtume alipofungua mifuko iliyojazwa na vileo, Mu'awiyah aliudhika sana na akifikiria kwamba yuko kwenye umri wa kupungukiwa na akili. Kuvuka mipaka dhidi ya sheria na kanuni za Qur'ani na hadithi na mwenendo wa Mtume uliongezeka sana na Masahaba wazee wa Mtume walizidi kutengewa na Mu'awiyah.

Inaelekea kwamba kikubwa zaidi kilikuwa ni mamlaka ya Mu'awiyah, kilichokuwa chini zaidi ni makubaliano yake na kanuni na sheria za Uislamu na utamaduni wake halisi. Matokeo yake, vigezo vya tabia na sifa pambanuzi za desturi zilizoagizwa na Uislamu kwa ajili ya maisha ya jamii ya kawaida zilikuwa zimepuuzwa kabisa, kama mfano ulionyeshwa wa kuhamishwa kwa Abu Dharr kulikoamriwa na

Uthman kwa kuombwa na Mu'awiyah.

Abu Dharr alikuwa sahaba wa Mtume aliyeheshimiwa sana, lakini alizungumza wazi wazi ilipokuja nafasi ya kusema kweli. Alishutumu kwa ujasiri mkubwa kuhusu kuhodhi mali na isitumiwe kuwasaidia wenye njaa na dhiki. Alikuwa akizunguuka kwenye mitaa mjini Damascus akikariri Aya ya Qur'ani, yenye maana, "**Wale ambao wanakusanya fedha na dhahabu katika masanduku ya hazina zao na hawautumii utajiri katika njia Mwenyezi Mungu, basi wangojee wakati utakapofika vipaji vya nyuso zao vitakapobabuliwa kwa moto wa Jahannam**."[6]

Abu Dharr alifukuziwa sehemu yenye kuhuzunisha wasiokaa watu na ali- poshindwa kuvumilia taabu za maisha hapo, akafariki dunia katika mwaka wa 33 A.H. Mke wake na binti yake walikuwa pamoja naye, na kwa matataizo makubwa waliweza kuuosha mwili wake na kuuvisha sanda. Kwa tukio la bahati ya pekee, Abdallah bin Mas'ud, sahaba wa Mtume alifika hapo na akaomboleza kifo na misiba ya Abu Dharr, na akauzika mwili wake.

1. Tabari, Juz. 1, uk. 1418
2. Tabari, Juz. 1, uk. 2095
3. Tabari, Juz. 1, uk. 2860
4. Tabari, Juz. 1, uk. 2766 na 2767
5. Tabari, Juz. 1, ukarasa 2866
6. Tabari, Juz. 1, uk. 2859

# Sura Ya 8: Mgogoro Kati Ya Watetezi Halisi Wa Uislamu Na Wahusika Wakuu Wa Syria Baada Ya Mtume

Baada ya kifo cha Mtume, walikuwa ni *Ahlul al-Bayt* wake ambao ndiyo walidumisha uhai wa kanuni kuu za Uislamu na kuyahifadhi yale maadili aliyokuwa akitafuta kuyasimamisha.
Katika makao ya serikali za Waislam, hali za maisha zilishindana kwa ubora na fahari kwa kutumia pesa zilizopatikana kutokana na utekaji nyara au, kutozwa kama ushuru kwenye nchi zilizowekwa chini ya utii. Dhuria ya Mtume, hata hivyo, iliendelea kuishi maisha ya kawaida, ya kutojishaufu, na kupitia matumizi yao binafsi, wakitumia kila walichokiweza kuwasaidia mayatima wajane na masikini kwa ujumla.

Tofauti kali ambazo zilitenganisha mtindo wao wa maisha kutokana na ule wa maisha ya hali ya juu wa wale ambao lengo lao lilikuwa kutwaa mamlaka na starehe zake nyingi kwa kawaida ziliishia katika migogoro. Vita kati ya Mu'awiyah na Ali havikuwezekana kuzuilika.

Dhuria ya Mtume, kama wafuasi halisi wa Uislamu, walisimama kwa ajili ya kuziondoa tofauti zote miongoni mwa Waislam, na kusimamisha usawa na undugu, kuhifadhi utoaji wa stahili kwa ubora wa tabia na ukamilifu katika utekelezaji wa wajibu wake mtu kama mwanadamu.

Ulimbikizaji wa mali (utajiri) katika hazina ya serikali kwa ugawaji wa baadaye kama msaada maalum au hiba binafsi ziliashiria dalili ya upendeleo na ulielekea kutia nguvu ushindani miongoni mwa wapokeaji wake, Ali aliisimamisha desturi hii. Alitumia ugawaji wa kila siku, kwa mazingatio makali ya uadil– ifu kila kitu kilichokuwa kimeingizwa katika hazina.

Watu ambao walifaidika na vitendo hivi vya upendeleo kabla ya Ali kuwekwa kama Khalifa lazima watakuwa wameathiriwa vibaya sana na mpango wa Ali wa ugawaji wa fedha ya serikali miongoni mwa Waislam.

Bani Umayyah walikuwa hawana wasiwasi katika kutumia fedha ya umma kama ilivyofaa kwenye lengo lao la kupata uungwaji mkono na watu, na walifanikiwa katika hilo, wakabakisha idadi ndogo tu ya watu kumfuata Ali. Matokeo haya haya ya ifuatia kutokana na mazingira magumu ambamo kwa ujumla Ali aliendesha maisha yake.

Watu kwa kawaida huwafuata watu ambao kiuchumi hawajambo na ambao wanaweza kuwasaidia wakati wa haja. Kwa hiyo, wale ambao walikuwa macho yao wameyakazia katika bahati hiyo kubwa, walipendelea kwenda kwa Mu'awiyah zaidi kuliko kumfuata Ali. Bani Umayyah pia walipendelea madai ya waarabu kama taifa, kuwa bora zaidi kuliko wasiokuwa Waarabu. Hili lilikuwa likipingana moja kwa moja na mafundisho ya Uislamu, na Hadith na Sunnah (mwenendo) wa Mtume wake.

Ubaguzi wa Bani Umayyah ulisababisha mlipuko wa tatizo la Waarabu dhidi ya wasiokuwa Waarabu. Kama watetezi halisi wa kanuni na misingi ya Uislamu na utekelezaji wake, Bani Hashim hawakuweza kuyakubali madai ya Waarabu kuwa wao wawe bora zaidi kuliko wasiokuwa Waarabu. Fikra hii inapata kuungwa mkono kutokana na ukweli kwamba Bani Abbas ambao walikuwa wanatokana na Bani Hashim, katika chagamoto yao kwa utawala wa Bani Umayyah waliwapata waungaji mkono wengi kutokana na watu wasiokuwa Waarabu wa Iran.

Kutokana na sababu zilizotajwa katika ibara zilizotangulia na kwa sababu ya uadui ambao Bani Umayyah na makabila mengine walikuwa nao juu yao, dhuria ya Mtume kwa kawaida walipata uungwaji mkono mdogo zaidi wa watu wa nchi yao kuliko walivyoungwa mkono Bani Umayyah.

# Sura Ya 9: Mkataba Wa Hasan Na Mu'awiyah Na

# Matokeo Yake Yasiopendeza.

Kabla ya kuutoka ulimwengu, Ali alifanya wasia akiwaagiza watoto wake, Hasan na Husein, hasa kuhusu wajibu wao kwa Mwenyezi Mungu, Kitabu Chake, kwa masikini na wanyonge, na mambo mengine kama hayo.[1] Aliwaelekeza kuhakikisha kwamba ni muuaji wake tu ndio auawe kulipiza kuuawa kwake.[2]

Baada ya kifo cha Ali, Hasan alikubaliwa kwa pamoja na Waislam kama khalifa wao kama ilivyopendekezwa na Abdullah bin Abbas, wakati watu wote ambao walikusanyika kwa ajili ya maziko hayo walipojiunga na Hasan katika kuomboleza juu ya kifo cha baba yake mashuhuri huyu. Kisha Waislam kwa hiari yao walitoa kiapo cha utii kwa Hasan kama ilivyopendekezwa na Ibn Abbas.

Katika wakati huu muhimu, Hasan aliwataka watu kukubali kumfuata yeye aidha akiwa amechagua kwenda vitani au kuishi katika amani. Hii ilikuwa mwezi 21 Ramadhan, 40 A.H.[3]

Wakati ambapo nchi bado iko katika maombolezo na Hasan alikuwa hajap– ata muda wa kutosha kukamilisha mipango yake kwa ajili ya utawala unaofaa kwa nchi za Kiislam, Mu'awiyah alianza tena mchezo wake aupendao sana wa kuamsha hisia za kutoridhika miongoni mwa wakazi wa nchi za Waislamu. Aliwaweka wapelelezi na mawakala wachochezi wa ghasia katika sehemu ambazo zina maovu mengi na fitna kama vile miji ya Kufa na Basra kuchochea vurugu na utovu wa nidhamu.

Hasan alikerwa sana na udukizi huu wa Mu'awiyah katika maeneo yaliyo chini ya utawala wake na akamwandikia kwa kulenga kuvuta mazingatio yake kuhusu kuingilia huku kusiko na sababu.

Alilalamika pia kwa Mu'awiyah kwamba yeye Mu'awiyah amewahi kuripotiwa kuwa amemtukana Ali mwenye kuheshika ambaye wakati huo alikuwa amekwishakufa, na akamwambia kwamba hilo lilikuwa tendo lisilofaa kabisa. Aliongeza kusema kwamba kama Mu'awiyah alitaka vita, basi anaweza kujiandaa nayo. Mabadilishano zaidi ya mawasiliano na Mu'awiyah yalisaidia tu kuweka wazi kwamba alikuwa na hisia za uadui usiozimika dhidi ya Ali ambao hata kifo chake Ali pia hakikusaidia hata kidogo kupunguza uadui huo.

Kwa kupita muda, shughuli za kutotulia za wapelelezi na watoa habari wa Mu'awiyah zilianza kupata nguvu zaidi na ukamilifu. Hata hivyo, Hasan alikuwa amejiandaa zaidi kupigana vita na Mu'awiyah kuliko kuhatarisha misingi ya haki na uadilifu.

Hata hivyo, hali ya mambo haikuonekana kuwa ya uhakika moja kwa moja, kwani mbali na njama mbaya za kiovu za Mu'awiyah, watu walikuwa wameanikwa kwenye vishawishi vya kichochezi vya mabaki ya kikundi cha Khawariji ambacho kilikuwa kimeshindwa vita lakini kilikuwa hakikuangamizwa kabisa na kutoweka katika jamii kiasi cha kukosa wapenzi wa kukionea huruma kikundi chao kilichoshindwa.

Ali mwenyewe alionyesha kukirihika na kuudhika kwa kukosekana umoja na kuwepo utovu wa nidhamu ambao sasa ulipenya na kuingia katika jeshi lake na katika wakati fulani aliendа hata kufikia hatua ya kupenda Mu'awiyah angekubali kubadilisha mfuasi wake mmoja kwa watu wawili wa Ali kama kubadilisha dhahabu kwa fedha.

Hao ndio aina ya watu ambao Hasan alikuwa afanye nao kazi. Aliwajua fika kama Mu'awiyah alivyojua kwa kupitia majasusi na watoa habari wake. Akitiwa moyo kwa hali ya mambo iliyokuwepo wakati huo, Mu'awiyah bila kutegemewa aliishambulia Iraki. Hujr bin Adi alizunguka huku na huko kuandikisha askari wa kumsaidia Hasan, lakini alikutana na majibu yasiyoridhisha. Miongoni mwa wale ambao walijitokeza kuja kusaidia walikuwa watu duni waliokuwa wanataka tu kupora, baadhi yao ambao walikuwa wameshinikizwa kufanya hivyo na watemi wao wa kikabila, Khawariji ambao kwa hali yoyote walitaka kupigana na Mu'awiyah, na watu mmoja mmoja walio watiifu wa madhehebu ya shia.[4]

Hasan alimpeleka Qays bin Sa'd bin Ubada al-Ansar akiliongoza jeshi la watu 20,000 na yeye mwenyewe akabakia huko Sabat. Alipoushuhudia uadui wa kisaliti wa wafuasi wake alisimama kuwapa nasaha za ubora wa kutenda mambo kwa makubaliano na umoja. Alikuwa hata bado hajamaliza hotuba yake wakati Khawariji walipoleta fujo, wakisema, “Ametoka kwenye Uislam na kuwa mwasi”[5]. Hasan alifanyiwa shambulizi la ghafla, lakini makabila tiifu (kwa Hassan) ya Rabi'a na Hamadan yalimwokoa, na kuwatawanya washambuliaji wake.

Hasan aliondoka kwenda Mada'in ambako huko Khawarij mmoja alimjeruhi kwa sime. Jeraha hilo lilichukua muda mrefu sana kupona. Kisha Hasan alianza tena maandalizi ya kupigana na Mu'awiyah, ambaye hata hivyo, kwa upande mmoja alitoa pendekezo la amani kwa masharti yoyote yale ambayo Hasan angeyaona yanakubalika. Mu'awiyah pia alimpelekea Hasan barua za wale viongozi wa jeshi la Hassan ambao walimkaribisha kuishambulia nchi yao na hata pia kumwahidi kumtoa Hasan kama mateka wake, au kumuua.[6]

Katika mazingira haya, ilikuwa haifai kurefusha hali ya vita na kwa mujibu wa yale ambayo Mtume na Ali wameyafanya katika matukio yafananayo na hili, Hasan alikubali kufanya mkataba wa amani na Mu'awiyah. Masharti ya mkataba ambayo yalianza kutumika katika mwezi Rabiul Awwal au Jamadil Awwal, mwaka wa 41 A.H.[7] yalikuwa:

(1) Mu'awiyah angetawala nchi za Kiislamu kwa mujibu wa Kitabu cha Mwenyezi Mungu, Sunna za Mtume na Makhalifa wake waadilifu;

(2) Mu'awiyah atakuwa hana haki ya kuteua mrithi wake kwenye nafasi ya Ukhalifa;

(3) Wakazi wa nchi zote za Kiislam kama vile Syria, Iraki, Hijaz na Yemen watalindwa;

(4) Maisha, mali na heshima za mashia wote wa Ali, popote pale watakapokuwa wanaishi lazima walindwe kwa usalama;

(5) Mu'awiyah asingefanya jaribio lolote lile, la wazi au la siri, juu ya maisha ya Hasan na Husein au ya yeyote yule mwingine ahusikanaye na familia ya Mtume, wala vinginevyo, kumfanyia ukatili, kumtisha au kumdhuru yeyote yule katika wao.

Ugomvi wa Hasan na Mu'awiyah uliibuka hasa kutokana na matakwa ya Hasan kutaka kuilinda misingi na kanuni za sharia na za imani. Sharti la kwanza la mkataba liliufanya kuwa wajibu kwa Mu'awiyah kutenda kwa mujibu wa sheria za Qur'ani na Sunna za Mtume na makhalifa wake waadilifu.

Halikuthibitisha tu bali lilimtaka Mu'awiyah akubali kwamba kabla ya kutiwa sahihi kwa mkataba huo utawala wa Syria ulikwishakosea dhidi ya sheria za Qur'ani na sunna za Mtume na makhalifa wake waadilifu. Lilithibitisha pia kwamba misingi na kanuni za sheria na imani ziko mbali kabisa na zile sheria za serikali za kidunia na matendo ya watawala wa kidunia.

Kifungu cha pili cha mkataba huu kilimzuia Mu'awiyah kuteua mrithi wake ili kudhibiti ile hali ya kufuata njia za wafalme ambao waliwataja warithi wao bila ya kuzingatia sifa na pia kumvua madaraka ya kumteua kama mrithi wake yule ambaye mwenendo wake usingepatana na amri za sheria za Qur'ani, na sunna za Mtume na za Makhalifa wake waadilifu.

Hitimisho la mkataba lilileta ufidhuli usiostahili kabisa juu ya Hasan kutoka kwa wafuasi wake wadanganyifu na wasaliti na ongezeko kubwa la nchi zake kuwa chini ya utawala wa Mu'awiyah. Muda mfupi tu baaada ya amani kurudishwa, Mu'awiyah aliuambia mkusanyiko wa Waislam karibu ya mji wa Kufa kwamba lengo na kusudio lake pekee la kwenda kupigana vita lilikuwa ni ili yeye akubalike kama mtawala mkuu wa Iraki na nchi nyingine za Waislamu, na kwamba utimilizwaji wa masharti ya mkataba na Hasan yalitegemea juu yake yeye tu.[8]

Kuteka madaraka kulikofanywa na Mu'awiyah kulimpa hamasa ya kumtukana Ali mbele ya watoto wake, Hasan na Husein. Hasan alitoa majibu mafupi lakini yenye kueleweka vizuri sana.
Husein aliuchunguza mwelekeo wa malengo ya serikali ya wakati huo kwa ukaribu zaidi, na akatambua kwamba mtihani wa mwisho ulikuwa ungojewe katika hali ya ukimya.

Hasan aliitoka mji wa Kufa na kwenda Madina ambako Husein pia aliungana naye. Ili kuleta mgawanyiko kati ya ndugu wawili hawa Bani Umayyah walieneza uvumi wa uwongo kwamba Hasan na Husein walikuwa na maoni tofauti kuhusu mkataba wa amani na Mu'awiyah. Uvumi huo ulipotea kwa haraka sana, kwani ndugu hawa wawili walikuwa pamoja kabisa.

Husein alijua kwamba Hasan aliamua kuyaacha madaraka ya kidunia ili tu kuondoa uwezekano wa vita ingawa alikuwa hajaamua kabisa kuikimbilia silaha kama hatua ya mwisho kumaliza mzozo huu. Ukiashiria kwa uwazi kabisa utendaji wa kina wa akili yake, ulikuwa ni ule ukweli kwamba Hasan alikuwa akisikika mara kwa mara akiyakariri mashairi yenye maana ya kwamba: "Yeyote yule aufanyaye upanga kuwa kinga yake huzawadiwa kwa amani ya pekee na uhuru kutokana na matatizo: imma kuutoka ulimwengu huu upesi sana, au kubakia ndani yake katika kufurahia faraja adilifu".

“Kamwe usitafute urahisi, ni tabia isiyofaa kabisa. Huwezi kuipata heshi- ma ila kwa kupitia kupata taabu na matatizo”[9]

Kwa kuhitimishwa mkataba huo, Bani Umayyah walijiona wenyewe kuwa huru kutenda lolote walilolitaka, na walipuuza kuyaheshimu masharti ya mkataba.

Kama Mu’awiyah angetimiza sharti la kwanza la mkataba kutenda kwa mujibu wa amri za kisheria za Qur’ani na sunna za Mtume na makhalifa waongofu, angekuwa amehesabiwa kuwa mmoja kati yao. Lakini hata Waislam wa madhehebu ya Sunni hawatoi madai yoyote kama hayo kwake. Wanashikilia kwamba ukhalifa wa haki ulidumu kwa miaka thelathini tu baada ya kifo cha Mtume, na kipindi hiki kilimalizika wakati wa hitimisho la mkataba kati ya Hasan na Mu’awiyah.

Kulikuwepo na mifano mingi ambayo ndani yake mahitaji ya umuhimu wa sharti la kwanza la mkataba yamevunjwa. Inaonyesha kwamba manufaa ya kisiasa yalimshawishi Mu’awiyah kumtangaza Ziyad, mwana wa Sumayyah, kuwa ni ndugu yake. Hekeya hii si ya bure tu bila maslahi na ingefaa kuelezewa hapa kwa ufupi.

Mama yake Ziyad, aitwaye Sumayyah, alikuwa kijakazi aliyeachwa huru. Aliolewa na Ubayd ambaye alikuwa mtumwa wa mtu mmoja wa ukoo wa Bani Thaqif na akamzaa Ziyad ambaye alilelewa na kukuzwa na al-Mughira bin Shu’ba, na alikua na akawa kijana mwenye akili na aliyesoma sana. Umar alimfanya kuwa gavana wa Basra, na baadaye Ali alimteua kuwa gavana wa Fars (Uajemi).

Baada ya kuuawa Ali, Ziyad mwanzoni alikasirika vibaya sana kutokana na vitisho vya Mu’awiyah, lakini katika mwaka wa 44 A.H., Mu’awiyah alimtangaza kuwa ndugu yake,[10] kwa vile Abu Sufyan alifahamika kuupi- tisha usiku katika urafiki haramu na Sumayyah. Kuanzishwa kwa uhusiano huu wa undugu kati ya Ziyad na Mu’awiyah kulileta mtikisiko miongoni mwa Waislam kwa ujumla na hususan miongoni mwa masahaba wa Mtume, kwa sababu ilikuwa kinyume na hadithi ya Mtume aliyokuwa akiitamka mara kwa mara kwamba mtoto atahusishwa na wazazi walio wanandoa, ila mawe ndio majaaliwa ya mtu mzimifu.

Mu’awiyah hakujali hasira za watu kwa ujumla kwa sababu kulikuwa na manufaa kwake kule kuununua utiifu wa Ziyad na dhuria wake kwa ajili ya malengo yake.

Mu’awiyah alianzisha na kuingiza matendo mengi yaliyopingana na sheria na kanuni za Kiislam. Hivyo alipunguza kiwango cha zaka kitolewacho kwenye sikukuu ya Id-el-Fitr kutoka kiwango cha pishi moja hadi kufikia vibaba viwili tu kwa kila mtu. Alivaa mapambo ya dhahabu, nguo zili- zotengenezwa kwa ngozi za wanyama wenye kula nyama wawindaji, ingawa alikuwa anatambua sana kwamba matendo hayo yalikatazwa au kuharamishwa na Mtume.
Katika siku ya Arafa wakati wa ibada za Hija utaratibu wa “talbiya” umaanishao “Ee Allah, mimi niko hapa nikiitekeleza ibada Yako. Wewe huna mshirika”, iliyokuwa ikitamkwa kwa kukaririwa kama sehemu ya matendo muhimu. Mu’awiyah alilikataza tendo hili. Abdallah bin Abbas, mtu aliye na elimu sana, alikanusha ukatazaji huu wa talbiya katika nyakati nyingi.

Mu'awiyah alikuwa akitumia kumimina fadhila zake kwa waimbaji ingawaje Uislamu unachukia muziki. Sa'id Khathir, mtu aliyejishughulisha sana katika kufuatilia mambo maovu aliimba na kujipatia mafanikio makubwa katika baraza la Mu'awiyah. Ibn al-Faqih, mwanachuo maarufu, ameandika kwamba Mu'awiyah alikuwa mtu wa kwanza kuweka vituo vya ulinzi vya polisi, kuwahanithisha (kuwahasi) wanaume kuwafanya matowashi na kuhifadhi fedha katika hazina za taifa. Mu'awiyah aliazisha utaratibu wa kupokea, kama wafalme, zawadi katika nyakati za sherehe za Waajemi za Nauruz (mwaka mpya) na *Mihrajan* ambazo katika miaka fulani fulani zilimpatia dirham milioni kumi.

Kaida za Kiislamu ziliangukia katika kupuzwa kabisa. Bukhari anaandika kwamba wakati fulani Abu Darda, sahaba wa Mtume alionekana kuwa katika hali ya kukasirika sana kwa vile hakuona katika watu dalili yoyote ile ya kumfuata kwao Mtume, isipokuwa tu kwamba walitekeleza swala za jamaa. Malik amesimulia kwamba isipokuwa kwa wito wa kwenda kusimamisha sala (*adhana*) hakuna hata moja kati ya matendo ya Kiislam ya miaka ya nyuma lililoweza kuonekana.

Mu'awiyah hakulitaja hata jina la Mtume kwa heshima inayostahili, na mtu mmoja mzee ambaye Mu'awiyah alimhoji alimnyanyua kwa nguvu wakati mzee huyo alipomwuliza Mu'awiyah kuhusu Mtume, akimtaja kirahisi tu kama "Muhammad." Mzee huyo alimuuliza Mu'awiyah kwa nini yeye hakulitaja jina hilo kwa heshima inalolistahili na kumwita Mtume wa Mungu Muhammad tu, basi!

Wakati fulani, ili kuzuia werevu muovu wa Amr bin Aas wa kumdhalilisha yeye mbele ya macho ya watu wa Misri, aliwafanya watu wa ujumbe wao wawe na nidhamu ya kuogopa kiasi kwamba wote walimwita Mu'awiyah kama Mtume wa Mungu. Mu'awiyah hakujali kuaadhibu, au hata pia kuwaonya tu dhidi ya kufuru hii.

Watu wanawafuata watawala wao katika dini kama vile wanavyowafuata katika kila kitu kingine. Wakati mtendaji mwenye mamlaka makuu alipokuwa hajali sana katika utekelezaji wa kanuni na matendo ya Uislamu, watu (wengi) lazima watakuwa bado wana mwelekeo mdogo wa kuzifuata. Kwa kweli, dini ilikuja kuwa kitu cha kuuzwa kwa mnada.

Wakati fulani Hatat bin Yazid na watu wengine watatu walikwenda kum- wona Mu'awiyah ambaye alimpa Hatat dirham elfu sabini (70,000) wakati wale wengine watatu walipata kila mmoja dirham laki moja. Hatat alilalamika dhidi ya utendewaji huu wa kibaguzi na Mu'awiyah akamwambia kwamba kile kiwango kikubwa zaidi kiliwakilisha bei ya imani ya wenye kupokea. Hatat mara moja alijitoa kuiuza imani yake kwa kiwango hicho.[11]

Waislam wachache wacha-Mungu, ambao walikuwa bado wangali hai walichoshwa na maisha. Al-Hakam bin Amr akiongoza kampeni kwa upande wa Mashariki alikataa kukubaliana na amri ya Mu'awiyah ya kupeleka kwenye hazina ya serikali ngawira za vita katika mwaka wa 50 A.H. badala ya kuzigawa ngawira hizo miongoni mwa askari kwa mujibu wa desturi ya zamani.

Hata hivyo, alishikwa kwa vitisho vikubwa mno kiasi kwamba alikiombea kifo chake na alifariki muda mfupi tu baadaye.[12]

Ili kufuta kumbukumbu za Bani Hashim, Mu'awiyah alijaribu kuiondoa mimbari ya Mtume kwa nia ya kuisafirisha kwenda Syria. Hata hivyo, aliacha kutekeleza mpango wake huo na alipatwa na ugonjwa wa kupooza uso katika mwaka huo huo.[13]

Tukiacha ukiukwaji wa sharti la pili la mkataba kwa ajili ya kuja kuelezea baadaye, tungeweza kushughulika na uvunjwaji wa sharti la tatu ambalo lilieleza kwamba nchini Syria, Iraki, Hijaz na Yemen ulinzi ungetolewa kwa watu bila ya kuangalia sehemu za nchi walizotokana nazo.

Chakusikitisha hasa ni ule ukiukwaji wa sharti hili. Ziyad bin Sumayyah alifungulia ulafi wa umwagaji damu ambao shabaha yake kuu ilikuwa ni wakazi wa Iraki. Adhabu zilikuwa zikitolewa bila makosa ya aina yoyote ile kutendeka, watu walikuwa wanafungwa jela bila kufanywa uchunguzi na kutia watu vilema na kuua kwa kutumia visingizio vidogo sana ikawa ni kawaida ya kila siku.

Wakati Samura bin Jundab alipochukua nafasi ya Ziyad huko Basra alitokea kuwa dhalimu aliyekuwa na kiu ya kumwaga damu zaidi kuliko hata mtangulizi wake na alifanya watu wasiopungua elfu nane (8,000) kuuliwa kwa upanga ndani ya miezi sita tu.

Aliwaua watu 47 ambao waliihifadhi Qur'ani kwa moyo. Samura aliwaamuru watu wasijizoeshe kutembea tembea kwenye mitaa ya jamaa baada ya usiku wa manane. Mtu mmoja aliwasili hapo kutoka sehemu za shamba na alitiwa mbaroni kwenye mtaa wa jamaa wakati wa masaa yaliyopigwa marufuku kutembea. Samura alikubali kwamba mtu huyo alikuwa hatambui kuhusu amri zake hizo lakini hata hivyo alimuua kwa "manufaa ya Umma". Mtu mwingine alilipa zaka kwa Samura na alikuwa akiswali msikitini wakati mtu mwingine alifika hapo na kumuua. Mifano mingi ya ukatili wa namna hiyo iliweza kuzidishwa sana.

Sharti la nne la mkataba kwamba maisha, mali na heshima za wafuasi (Shi'a) wa Ali lazima zilindwe kutokana na madhara lilikiukwa kwa ufisadi kabisa. Taabu iliyokuwa ndogo sana ambayo shi'a wa mjini Kufa na Basra waliipata ilikuwa kwamba walilazimishwa kuziacha nyumba zao ili kuwapa nafasi wafuasi wa Mu'awiyah na (wao) walipelekwa Qinsrin, sehemu isiyokaliwa na watu nchini Syria, kwenda kuishi huko katika kambi ya kijeshi.

Hujr bin Adi na masahaba zake waliitwa kwenda Syria na waliuawa ingawa walitamka wazi kwamba walikuwa ni Waislam, na kwamba wal- ishikilia neno lao hilo la ahadi na hawakuwa waasi. Kosa lao tu na ambalo halikuweza kusameheka kabisa lilikuwa ni kule kukataa kwao kumtukana Ali.

Sayfi bin Faysal al-Shaybani, mmoja wa watu maarufu sana miongoni mwa marafiki wa Hujr alipigwa bila huruma wakati alipomwambia Ziyad kwamba alimchukulia Ali kwa heshima kubwa kabisa. Mateso yaliendelezwa na kisha Sayfi aliulizwa tena kuhusu alivyojihisi kumhusu Ali.

Sayfi alirudisha jibu kama lile lile la mwanzo tena kwa nguvu ya nyongeza na hoja. Alikuwa miongoni mwa watu kumi na mbili pamoja na Hujr bin Adi ambao walipelekwa Syria. Wengine wawili waliungana nao baadaye. Katika watu hawa kumi na nne, saba waliachiwa huru kwa mapendekezo yaliyofanywa

kwa ajili yao, watu sita waliuawa kwa upanga, na mmoja aliyeitwa Abd al-Rahman bin Hassan al-Anaz alichaguliwa kwa ajili ya adhabu ya mfano, akiwa mfuasi mtiifu zaidi kwenye njia ya Shi'a. Ziyad alimzika mtu huyu akiwa angali hai.[14]

Hujr bin Adi alikuwa miongoni mwa watu wale ambao waliuawa. Alikuwa ni mtu aliyetukuzwa sana katika ulimwengu wote wa Kiislam. Mauaji yake yaliombolezwa kwa kina sana na Waislam wote, Shi'a wa mjini Kufa wakichukulia kuwa ni msiba mkubwa mno.

Wakati Aisha, mjane wa Mtume, aliposikia kwamba Ziyad ameandaa taarifa dhidi ya Hujr, yeye alimpelekea ujumbe kupitia kwa Abd al-Rahman bin Harith bin Hisham kumwogopa Mwenyezi Mungu. Mjumbe alikuwa amechelewa sana kumfikia Ziyad na Hujr alikuwa amekwisha uawa. Wakati Aisha aliposikia mwisho wa kuhuzunisha wa Hujr, alizungumzia kwamba kama Mu'awiyah asingejua kwamba wakazi wa Makka walikuwa wameachwa na dalili yoyote ile ya ujasiri, asingekuwa na ujasiri wa kumwita Hujr na masahaba wake wakiwa wamefungwa minyororo kwenda Syria na kumuua. Aliongeza kusema kwamba mtoto wa mwanamke ambaye alikula ini la Hamza alijua kwamba ujanadume ulikoma kuwepo.

Alithibitisha kwamba kwa elimu yao na mafanikio yao watu hawa wangefaa kuonekana kama kichwa na akili ya Uarabuni.

Wakati Mu'awiyah alipokuja Madina na akamtembelea Aisha, anaonekana alimshambulia vikali kuhusu kifo cha Hujr kiasi kwamba Mu'awiyah aliu- funga mjadala akisema, "Tuache mimi na Hujr peke yetu. Suala hili litachambuliwa mbele ya Mwenyezi Mungu."

Wakati Abdallah bin Umar mtoto wa Khalifa wa pili aliposikia kuuawa kwa Hujr katika sehemu ya sokoni alisimama na akaomboleza kwa kun- yanyua sauti kubwa.

Rabi bin Ziyad al-Harith gavana wa Khurasan, alipatwa huzuni sana kwa kuuawa kwa Hujr na utepetevu wa jumla wa Waislam kiasi kwamba anyanyua mikono yake juu mbinguni kuomba, akiwaomba Waislam ambao walikuwa wamejikusanya pamoja kwa ajili ya swala ya Ijumaa waitike kwa kusema "Amin." Aliomba, (akisema), "Ee Mwenyezi Mungu! Kama kuna lolote lile zuri kwa (mja wako) Rabi'i, (basi) muondolee uhai." Dua yake ilikubaliwa, na baada ya kuutoka msikiti, hakuwa amekwenda mbali sana wakati alipoanguka na akafariki.

Inaonyesha kwamba Mu'awiyah mwenyewe baadaye alitambua kwamba Hujr bin Adi aliuawa kwa makosa. Alisikika akijisemea kichini chini, "Ee, Hujr itanibidi nije kukutana na siku ndefu kwa mauaji yako," wakati alipoona mwisho wake unakaribia haraka.

Amr bin al-Hamiq al-Khuzai alikuwa anaheshimiwa sana kama Mtume alivyopeleka salaam zake kwake. Yeye pia aliuawa kwa maelekezo yaliyotolewa na Mu'awiyah.

Matukio haya yaliwahuzunisha vikubwa Shi'a wa Ali. Aliposikia kwamba malalamiko mengi yamepelekwa kwa Husein dhidi ya kuuawa kwa Hujr, na Husein mwenyewe alikuwa amehuzunishwa

sana na tukio hili na akihofia kwamba Husein angesimama kufanya uasi dhidi yake, Mu'awiyah alimwandikia barua iliyojaa vitisho.

Husein alimpelekea jibu, na akiuweka kando unyamavu wake wa kawaida, alisimulia, moja baada ya lingine, matukio yote ambayo ndani yake masharti ya mkataba na Hasan yalikuwa yamekiukwa, na akatoa maelezo ya kumbukumbu yenye kugusa kuhusu kifo cha Hujr, na akamwambia kwamba hakuna kilichosababisha huzuni kubwa zaidi kuliko ukhalifa na utawala wake.

Sharti la tano la mkataba lilimwajibisha Mu'awiyah asifanye jaribio la wazi au la siri, kuleta madhara kwa Hasan na Husein au yeyote yule mwingine ahusikaye na familia ya Mtume, Sharti hili lilikiukwa vibaya sana, ingawa pia dhuria wa Mtume wenyewe walijitoa kabisa kwenye shughuli za nchi.

Hasan alitendewa utovu wa heshima mbaya wa kificho na maafisa wa serikali. Hata wakati mwingine pia walitumia lugha chafu dhidi yake, nia ikiwa ni kuwachockoza na kuwatumbukiza Bani Hashim kwenye matendo ya vurugu, ili kwamba Mu'awiyah aweze kupata kisingizio cha kumwaga damu yao, lakini uvumilivu mkubwa wa Hasan ukalizuia tukio la ghafla kama hilo kufanyika.

Bani Umayyah kisha wakageukia kwenye hatua za siri ili kulipata lengo lao, na walitumia hongo na sumu katika kumwondoa duniani Hasan. Mu'awiyah alimkodi Ju'da, mke wa Hasan, kwa malipo ya dirham mia moja elfu na kumwaahidi baadaye kuolewa na mwanawe, Yazid.

Hasan alikufa, kwa kutiliwa sumu na Ju'da (mkewe), mnamo mwezi 28 Safar, mwaka wa 50 A.H. Alikuwa ametoa ombi la kuzikwa kando ya kaburi la Mtume, lakini akitarajia kutokea matatizo, aliamuru kwamba kama maziko yake karibu na kaburi la Mtume yatapingwa basi azikwe karibu na kaburi la nyanya (bibi) yake mzaa baba, Fatima, binti Asad katika eneo la makaburi ya al-Baqi.

Husein aliuchukua mwili wa ndugu yake kuelekea kwenye kaburi la Mtume, lakini alizuiwa kumzika hapo na Bani Umayyah ambao walion- gozwa na Marwan. Husein alikasirishwa sana na uingiliwaji kati huu, lakini kwa kustahi matakwa ya Hasan (ndugu yake) alimzika katika eneo la al- Baqi[15].
Kifo cha Hasan kilikuwa ni msiba mkubwa kwa watu wa Bani Hashim ambao waliendelea kumwombelezea kwa kipindi cha mwezi mzima. Husein aliendelea kufuata njia ya amani kama vile (alivyofanya) ndugu yake.

Wakati Shi'a wa Irak walipomtaka akubali viapo vyao vya utii kwake, Husein aliwaambia kwamba isingekuwa sawa kuukana mkataba uliofanywa na Hasan kwani wao walifungwa na mkataba huo. Alipendekeza kwamba suala lote zima lingeangaliwa upya baada ya kufa Mu'awiyah.

1. Abu al-Faraj al-Isfahani, Kitabu. Maqatil, uk. 38-40
2. Kitabu: Maqatil, uk. 36
3. Kitabu: Irshad, uk. 280 - 281
4. Kitabu: Irshad, uk. 282
5. Kitabu: Irshad, uk. 283
6. Kitabu: Irshad, uk. 28

7. Kitabu: Sawa'iq, uku. 81
8. Kitabu: Irshad, uk. 286
9. Kitabu: Kitab al-Baladan, uk. 53 cha Bin al-Faqih al-Hamadan
10. Kitabu: Tabari, uk. 69-70
11. Kitabu: Tabari, Juz. 2, uk. 96 - 97
12. Kitabu: Tabari, Juz. 2, uk. 110-110
13. Kitabu: Tabari, Juz. 2, uk. 92
14. Kitabu: Tabari, Juz. 2, uk. 142
15. Kitabu: Irshad, uk. 287 - 288

# Sura Ya 10: Kuteuliwa Kwa Yazid Kama Mrithi Wa Mu'awiyah

Mu'awiyah aliutumia uhai wake mrefu katika kufurahia madaraka na mali (utajiri). Kwa muda mrefu alikuwa ameilea tamaa ya kuacha baada ya kufa kwake, mamlaka yake na madaraka yake kwa mwanawe Yazid.

Vitu viwili vilimzuia Mu'awiyah kutoa athari ya kivitendo ya tamaa yake hiyo; (kwanza) mkataba na Hasan ambao ulimnyima haki ya kumteua mrithi wake na (pili) tabia mbaya isiyofaa ya mwanawe, Yazid. Mu'awiyah alikuwa katika namna ya kupendeza sana, amekiuka vipengele vingine vya mkataba, na kuvunjiwa kwa sharti la kukataza uteuzi wa mrithi wake hakukumletea tatizo lolote lile.

Kipingamizi kilichokuwa kizito hasa hasa kwa kulifikia lengo lake kilikuwa katika kutambua kwake kwamba pendekezo la kumteua Yazid kama mrithi wake katika nafasi ya ukhalifa lisingevutia uungwaji mkono mdogo tu bali pia kutapingwa kwa nguvu zote na watu waliokuwa na umuhimu na kuchukiwa na watu kwa ujumla.

Hata hivyo, (Mu'awiyah) alijitahidi kuwaondoa wale watu, kwa kiasi ilivyowezekana, ambao wangekuwa washindani hatari wa Yazid juu ya Ukhalifa. Hivyo aliafanya Abd al-Rahman bin Khalid atiliwe sumu (afe) na akamteua yule muuaji kuwa mkusanyaji wa kodi ya zaka wa sehemu ya Hims.[1]

Al-Mughira bin Shu'ba alikuwa haendani vyema na Mu'awiyah wakati akifanya kazi kama gavana wa mji wa Kufa. Ili ajipendekeze kwa Yazid alitoa dokezo kwa Yazid afanye atangazwe kama mrithi kwenye kiti cha Ukhalifa.

Mu'awiyah ambaye alikuwa kamwe hajawahi kuchukua matu- maini yoyote ya kupata pendekezo la namna hiyo kutoka kwa mtu yeyote yule mwenye akili, mara moja alimwita al-Mughira kuongea naye juu ya pendekezo lake hili. Al-Mughira alimhakikishia kufuzu kwa mpango huu huko Kufa na akasema kwamba, pamoja na Ziyad kama gavana, Basra nayo pia lazima watayapokea kwa kuyapendelea

matakwa hayo ya Mu’awiyah.

Aliporudi Kufa, Mughira aliwaita watu mashuhuri wafahamikao kwa kuyaunga mkono kwao mafunzo ya Bani Umayyah na akawasihi wangojee ujumbe wa Mu’awiyah na wamsisitizie juu yake yeye kuhusu uteuzi wa Yazid kama mrithi wake. Jibu kwa ombi lake lilikuwa la kukatisha tamaa na al-Mughira alitumia fedha kiasi cha dirham elfu thelathini kupata kwa pamoja ujumbe unaokubalika ambao mwanawe Musa aliuongoza kwenda kwa Mu’awiyah, ambaye alikuwa mjanja sana wa kutoweza kudanganywa na mwonekano wa mambo. Baada ya kutoa uhakikisho wa kawaida kwa wajumbe, Mu’awiyah alimuuliza Musa kwa faragha kwamba ni kiasi gani baba yake alichokuwa amelipa kwa kununua imani zao. “Dirham elfu thelathini,” lilikuwa ndiyo jibu.

Kisha Mu’awiyah alimwita Ziyad ambaye alimtangaza kwa kosa kuwa ni ndugu yake kama hatua ya kupatia manufaa ya kisiasa, na akamfahamisha lengo lake hili. Ziyad alikuwa na mashaka makubwa sana kuhusu uhalali wa uteuzi wa mwasherati mwenye shari kama Yazid kwa ajili ya ukhalifa katika kumrithi Mu’awiyah, na akamtaka ushauri Ubayd bin Ka’b al- Numayri ambaye alishauri kwamba Yazid aambiwe arekebishe mwenendo wake kama anapenda kushinda juu ya maoni ya watu kuunga mkono uteuzi wake.

Ziyad alitoa jibu fupi kwa Mu’awiyah akisema kwamba haraka isiyo na mpango itakuwa na madhara kwenye mafanikio ya lengo lao.[2]

Al-Mughira alifariki dunia mwaka wa 49 A.H. au mwaka mmoja baadaye akiwa na umri wa miaka sabini.[3] Ziyad alimrithi kama gavana wa Kufa. Aliwahi kufanywa kuwa gavana wa Basra, Khurasan na Sijistan katika mwaka wa 45 A.H. na Mu’awiyah ambaye baadaye aliongezea Bahrain na Oman kwenye mamlaka yake. Katika Ramadhani ya mwaka wa 53 A.H.

Ziyad pia alifariki dunia, na akitambua kwamba waunga mkono waliobaki pia nao wangekufa hivi karibuni, Mu’awiyah alitangaza urithi wa Yazid kwenye kiti cha Ukhalifa na watawaliwa walilazimishwa kukubaliana na mpango huo...........

Ingeweza kuonekana kwamba al-Mughira alikwisha uandaa uwanja vizuri sana kwa kupata mwitikio wa uhakika kwenye uteuzi wa Yazid kama mrithi wa Mu’awiyah, kwani waunga mkono maarufu wa Bani Umayyah wa Kufa walikwishapatikana, kukubaliana na matakwa ya Khalifa. Ziyad alimfuatia al-Mughira katika ugavana wa Kufa, na wakati akiwa Basra hakushindwa kuendeleza mafanikio ya mpango wa Mu’awiyah ingawa kwa tahadhari kubwa na shauku isiyozuilika.

Hata hivyo, huko Kufa, wote kwa pamoja, Ziyad na mwanawe Ubayd Allah waliwatia watu hofu kubwa kiasi kwamba hakuna hata mtu mmoja aliyethubutu kuzipinga amri zao. Kwa upande wa Syria, ilikuwa ndio ngome kuu ya Bani Umayyah na kama ilivyokwishaelezewa, Abd al-Rahman bin Khalid bin al-Walid, mshindani aliyefaa kwa kiti cha Ukhalifa, alikwishaondolewa kwenye njia ya Yazid.

Sa’id, mwana wa Khalifa aliyeuawa, Uthman, alilalamika dhidi ya uteuzi wa Yazid kwa urithi huo, akidai

yeye mwenyewe alikuwa uzao bora, na kumkumbusha Mu'awiyah kwamba mengi ya madaraka yake zaidi yamepatikana kutoka kwa Uthman.

Madai haya yalikubalika, lakini Mu'awiyah alidai kuwa alikuwa ameulipa ukarimu wa Uthman kwake yeye kwa msaada alioutoa kwa Khalifa aliyekufa kwa kulipiza kisasi juu ya wauaji wake na kudai gharama ya fidia ya damu yake. Aliongeza kwamba kama nyumba yake ingekuwa imejaa watu kama Sa'id, wao wote kwa pamoja wasingelingana na Yazid.

Kisha Mu'awiyah alimwandikia Marwan gavana wa Madina, atoe kiapo cha utii kwa Yazid ambaye amemteua kama mrithi wake, na pia apate viapo kama hivyo kutoka kwa watu wa Madina. Hili lilimuudhi na kumkasirisha sana Marwan ambaye alimwona Mu'awiyah huko Damascus na akapinga kwa nguvu sana dhidi ya utenzi wa Yazid kwenye nafasi ya Ukhalifa kama kumpendelea kijana asiye na uzoefu na ujuzi wowote juu ya watu wanaoweza kupatikana wenye uzoefu unaofahamika wa kiutawala. Mu'awiyah alimtuliza kwa kusema kwamba yeye amefanywa kuwa mrithi wa Yazid.

Abd al-Rahman bin Abi Bakr alikuwa amechukizwa sana na uteuzi huu, akieleza kwamba Abu Bakr alikuwa hakuacha wosia wa upendeleo wa kurithi mwanawe, na kwamba Mu'awiyah amefuata njia na taratibu za Makaizar na wafalme wa kidunia. Maoni haya yaliungwa mkono na Imam Husein, Abdallah bin Zubeir, Abdallah bin Umar, Abdallah bin Abbas na Aisha, mjane wa Mtume.

Mu'awiyah lazima atakuwa amejua, kwa wasiswasi wake mkubwa sana, kwamba wapinzani wote hawa juu ya uteuzi wa Yazid kama mrithi wa baba yake katika nafasi hiyo walikuwa na nafasi zenye umuhimu mkubwa katika ulimwengu wa Kiislam.

Inaweza kukumbukwa pia kwamba wale wote ambao, miongoni mwa madhehebu mbalimbali za Kiislamu, waliokuwa wakionekana kana kwamba wameirithi dhamana halisi katika mambo yenye kuhusiana na Waislam, waliungana katika kutokukubaliana kwao juu ya uchaguzi wa Yazid kurithi kama Khalifa wa Uislamu.

Baadhi yao hawa walishikilia msimamo wao na walifanya ujasiri mkubwa kabisa katika matokeo ya baadaye yaliyokuwa mabaya mno, wakati wengine walikubali kulazimishwa kuuacha msimamo wao.

Mu'awiyah alijaribu kuwanyamazisha kwa njia ya vitisho au kuwapata kwa kuwapa mafungu makubwa makubwa ya fedha.

Katika kuitembelea kwake Madina aliongea kwa njia ya dharau sana na Imam Husein, akimwita (Imam) mwanakondoo wa kafara ambaye damu kwa hakika kabisa itakuja kumwagwa tu. Alipokutana na Abdallah bin Zubeir, ambaye alimfananisha na pomboo, alisema kwamba mkia wake ungekamatwa na kunyongwa nyongwa. Alimshutumu Abd al-Rahman bin Abi Bakr kwa kuwa katika hatua ya utu uzima ya uzulufu dhaifu (kipindi cha upungufu wa akili kutokana na uzee). Abdallah bin Umar hakuwa na hali bora zaidi.[4]

Wakati vitisho vilipothibitika kuwa havisaidii kitu, Mu’awiyyah alitoa vivutio vya mali ili kufanikisha lengo lake. Alipelekea pesa kiasi cha dirham elfu kumi kwa Abd al-Rahman bin Abi Bakr ambaye alikataa kubadilisha imani yake kwa manufaa ya kidunia. Majibu ya Abdallah bin Umar yalikuwa hayo hayo kwa zawadi sawa na hiyo. Imam Husein pia alikataa kupokea zawadi na fungu kubwa la fedha alilopelekewa na Mu’awiyah.

Aisha alichukua nafasi ya mbele katika kuupinga uteuzi wa Yazid kwenye nafasi ya Ukhalifa.
Jalal al-Din al-Suyuti anasimulia kwamba siku moja, akimwona Mu’awiyah akichukua kiapo cha uti kwa Yazid huko Madina, Aisha aliita kwa sauti kubwa akisema, “Nyamazeni! Mnafanya nini? Je, kuna Khalifa yeyote yule wa nyuma aliyepata kiapo cha utii kwa ajili ya mtoto wake?” Papo hapo Mu’awiyah alizifunga shughuli hizo.

Al-Hasan al-Basri anasema: “Mu’awiyah alifanya mambo manne, kila moja lilitosha kwa kuangamia kwake: Aliuchukua Ukhalifa kwa kusaidiwa na wapumbavu wasiojua kitu bila kushauriana na umma wote, ingawaje hata Masahaba wa Mtume walikuwa wanapatikana. Alimteua mtoto wake ambaye alikuwa mlevi na alibakia saa zote akiwa amelewa kuwa mrithi wake, alivaa dhahabu na hariri, na alichezea chombo cha muziki aina ya gitaa.

Tatu, alimtangaza Ziyad kuwa mtoto wa Abu Sufyan dhidi ya hadithi ya Mtume ambayo ilimpa mtoto nasaba au ukoo kutokana na wanandoa (mume na mke) na aliitenga adhabu ya kupigwa mawe mpaka kufa kwa mzinifu. Ya nne, alimuua Hujr na masahaba zake.[5]

Mu’awiyah alijua kwamba mtu wa kwanza aliye na umuhimu miongoni mwa kundi la watu wakubwa na mashuhuri wanaopinga uteuzi wa Yazid alikuwa Husein na hakupoteza muda katika kumwambia wakati wa ziyara yake mjini Madina kwamba yote ameyapata katika mpango wake isipokuwa watu watano wa kabila la Quraish wakiongozwa na yeye (Husein). Husein alishangaa, na alimuliza Mu’awiyah kama kweli alifikiria watu hawa walikuwa wakiongozwa na yeye.

Vile Mu’awiyah alivyoyarudia madai yake, Husein alipendekeza kwamba awaite hawa, wanaofikiriwa kuwa wafuasi wake, na awatake kuapa kiapo cha utii kwa mtoto wake. Kama wangefanya hivyo, Mu’awiyah hakuhitajia kuhofia hatari yoyote ile kutoka kwa Husein peke yake.
Mpango huu (mbinu) uliahirisha mzozo huo kwa muda huo na Mu’awiyah alirudi (alirejea) Syria.

Hata hivyo, ilionekana wazi kwa Husein, na vivyo hivyo kwa Mu’awiyah, kwamba kugeukia kwenye matumizi ya silaha hakuwezi kukwepeka kwa muda mrefu. Husein, hata hivyo, hakuwa tayari kufungua (kuanzisha) vita kwa misingi ya kawaida na hata vile vile kutokana na mkataba wa amani kati ya Mu’awiyah na Hasan. Mu’awiyah pia aliona siyo wakati muafaka kuanza vita, hivyo hali ya wasiwasi kuhusu amani ilikuwepo kati ya pande zote. Urefu wa kipindi hicho ulifupishwa kutokana na kifo cha Mu’awiyah mnamo mwaka wa 60 A.H.

1. Kitabu: Tabari, Juz. 2, uk. 82
2. Kitabu: Al-kamil, Juz, 3 uk. 418, cha Ibn al-Athir

3. Kitabu: Tabari, uk. 174-175
4. Al-Kamil ya Al-Athir, Juz. 3, uk. 421-424
5. Kitabu: Al-Kamil, cha Ibn al-Athir, Juz. 2, uk. 25

# Sura Ya 11: Kifo Cha Mu'awiyah Na Kupanda Kwa Yazid Kwenye Ufalme

Katika mwaka wa 60 A.H. Mu'awiyah aliugua sana kiasi kwamba hakuweza kurudia afya (yake) njema katika kipindi kirefu cha maradhi yake. Ibn Hajr amesimulia kwamba siku moja Mu'awiyah alianza kulia. Katika kuulizwa sababu (ya kulia), Mu'awiyah alijibu kwamba kama upendo juu ya Yazid usingeshinda kabisa maamuzi yake, angejitafutia mwenyewe njia ya sawa.1

Akifafanua maelezo haya, Ibn Hajar anaandika kwamba Mu'awiyah kwa hiyo alikubali kabisa kwamba upendo kwa Yazid umemtia upofu kwenye njia ya uadilifu na kwamba amewatumbukiza Waislam, baada ya kufa kwake, kwenye mikono ya mtu mwenye dhambi kama Yazid ambaye angewaongoza kwenye kuangamia kabisa.2

Mwanzo wa maradhi yake ambayo yalikatisha uhai wake, Mu'awiyah ali- wahi kumwambia Yazid, "Nimewadhalilisha maadui zako wote, na nimewafanya Waarabu wote wanyenyekee kwenye mamlaka yako na wakubali urithi wako, lakini kuhusu suala la ukhalifa ambao takriban umekamilika, ninahofia kutokea matatizo kutoka kwa watu wanne: Husein bin Ali, Abdallah bin Umar, Abdallah bin Zubeir na Abd al-Rahman bin Abu Bakr."3

Wakati kifo kilipokuwa kinamkaribia kwa haraka sana, Mu'awiyah aliagizia Yazid aitwe ambaye alikuwa hata hivyo, akijifurahisha kwa uwindaji huko Huwwarin.4

Mu'awiyah, kwa hiyo alimpa al-Dahhak bin Qays al-Fihr, kiongozi wa *Shurta* yake, kuufikisha kwa Yazid ujumbe huu kama utokavyo kwake, "Watendee watu wa Hijaz kwa heshima inayostahili, wapokee hapo makao makuu kwa wema (ihsani) na heshima, watazame vyema watu wa heshima na maarufu miongoni mwao ambao huja mjini mara kwa mara katika wakati ufaao. Wategemee sana watu wa Syria kama viganja vyako na mikono yako ukichukua tahadhari kwamba hawabakii nje ya nchi ya Syria kwa muda mrefu wasije wakajifunza na kujua tabia za nchi nyingine. Na ujue kwamba ninahofia kukutokea wewe matatizo kuto- ka kwa watu wanne tu, nao ni Husein bin Ali, Abdallah bin Umar, Abd al- Rahman bin Abi Bakr na Abdallah bin Zubeir.5

Mu'awiyah alifariki dunia katika mwezi wa Rajab mwaka wa 60A.H.6 Alikuwa gavana wa Syria akiwa na umri wa miaka 38, akawa Khalifa huru akiwa na umri wa miaka 58 na akafariki dunia akiwa na umri wa miaka 78 au kati ya miaka 73 na 85 kwa mujibu wa baadhi ya wanahistoria.7

Yazid alirudi Damascus baada tu ya baba yake alipokwishazikwa. Alipanda kwenye ufalme na watu wa Syria waliapa kiapo cha utii kwake.

1. Kitabu: Al-Sawa'iq (pembezoni), uk. 56
2. Kitabu: Al-Sawa'iq (pembezoni), uk. 58
3. Kitabu: Tabari, Juz. 2, uk. 196-197
4. Kitabu: Tabari, Juz. 2, uk. 203
5. Kitabu: Tabari, Juz. 2, uk.197
6. Kitabu: Tabari, Juz. 2, uk. 198
7. Kitabu: Tabari, Juz. 2 uk. 19

# Sura Ya 12: Yazid

Mama yake Yazid, Maysum, alikuwa binti wa Bahdal bin Unayf al-Kalbi. Mu'awiyah alimwoa kutokana na uzuri wake wa kipekee. Alimjengea jumba kubwa la kifahari mkabala na Ghuta katika mazingira ya kupendeza na kuvutia sana na kupamba kwa fanicha za fahari ya Kifalme. Alimpatia mke wake huyo vito vya thamani aina mbalimbali na idadi kubwa ya mavazi yaliyotengeneza kwa vitambaa vya kuchaguliwa hasa, vinavyopendeza, na akaajiri vijakazi wengi kumtumkia katika anasa zake binafsi. Anasa zote alizopatiwa kwa matumizi yake na Mu'awiyah zilishindwa kumshawishi mke wake ambaye alikuwa mtoto wa jangwani, aliyezoea kwenye maisha magumu ya ardhi kame na isiyo na manufaa, na akiwa na mapenzi na maisha hayo.
Wakati mmoja kwa hiari yake mwenyewe aliangua kilio, alisema, *"Lile hema lisilokingwa dhidi ya dhoruba za upepo wenye nguvu lina thamani kubwa zaidi kwangu kuliko jumba hili la Kifalme. Gauni lile ovyo ovyo la sufu nililokuwa nikivaa lilikuwa lenye thamani zaidi kwangu kuliko nguo hizi nzuri zenye kupendeza. Niliona utamu zaidi kula nyama ya mkate mkavu kwenye pembe ya makazi yangu kuliko kula vipande vya mikate hii mieupe na mizuri na nilikuwa mwenye kupenda zaidi umbo la kijana aliye mwembamba, mrefu na asiyependeza machoni wa ukoo wangu na kabila langu kuliko bonge la mtu, katili mwenye tabia mbaya."*

Mu'awiyah alipoyasikia maneno haya, alikasirika sana, hasa katika utajo wa kushusha heshima ulioelekezwa kwake. Alimtaliki Maysam ambaye alikuwa amekwishakuwa mjamzito.

Alimhamisha kwenda kuishi na jamaa zake katika jangwa la Najd.[1] Yazid alizaliwa katika mwaka wa 22 A.H.,[2] na alipozipata habari hizi, Mu'awiyah aliagizia aletwe kwake.[3]

Toka mwanzoni mwa ujana wake Yazid alishikamana na njia za kiovu na aliishi maisha ya kifisadi. Mizaha ambayo kwamba alikuwa anaicheza na wanyama imehifadhiwa katika (kumbukumbu za) historia. Alikuwa mtu wa kwanza kumfanya chui mweusi kupanda farasi. Alifundisha nyani kupanda punda na kushindana katika mashindano ya farasi dhidi ya wapanda farasi wenye sifa kubwa. Yazid

alipata kuvuma kwa sifa mbaya kwa mazoea ya ulivi na Abdallah bin al-Zubeir alimpa jina la *Sakran*, yaani “mlevi.”4

Hakuweza kujizuia na kulewa wakati alipoutembelea mji wa Makka kwenda kutekeleza ibada ya Hijja ili akapate kuungwa mkono na watu kwa ajili ya uteuzi wake kama mrithi wa baba yake.5

Al-Waqid alimnukuu Abdallah bin Hanzala akisema “Wakati wa utawala wa Yazid tulihofia kwamba mawe yangetunyeshea juu yetu kwani hakuwaacha mama zake wa kambo, mabinti na dada zake kutokana na utongozaji wake wa kitamaa. Alikunywa vileo kwa uhuru kabisa na aka- puuza kusimamisha swala.6

Ilikuwa siyo kwamba Yazid alitenda dhambi tu kwa kwenda kinyume na amri za kisheria za Qur'ani na Sunna za Mtume, bali hata mawazo yake pia yalikuwa ya kidhambi vivyo hivyo. Ibara zake, kama zilivyotafsiriwa hapa chini, ambamo ndani yake anazichukulia kwa wepesi amri za kisheria za Qur'ani zinatoa ushuhuda kuhusu ukweli wa maelezo haya: “Sina muda wa kupoteza kutokana na kusikiliza gitaa na matuazi na nikawa nasikiliza *adhana* (wito) kwa ajili ya kwenda kusimamisha swala na nimechagua mwanamwali mzuri wa kikombe badala ya wanawake wa peponi (Mahurlain)”.

Aliikana pia imani ya kufufuliwa viumbe kama anavyosema katika ibara zilizotafsiriwa hapa chini: “Niimbie kuhusu matendo ya Abu Sufyan kule Uhud wakati alipoziingiza nyumba za maadui zake katika maombolezo.

Msiwe na matumaini ya kukutana kwetu baada ya kuachana ambako kunasababishwa na kifo. Mnaweza kuwa mmesikia kuhusu maisha ya mara ya pili, lakini hizi ni simulizi ndefu ambazo zinapotosha watu.”

Ibara hizi zinaonyesha wazi kabisa kwamba Yazid alitawaliwa na imani za kipindi cha giza cha kabla ya Uislamu, na kwamba alikuwa akiendekeza tamaa ambazo zilisababisha makafiri kupigana dhidi ya Mtume wa Uislamu. Ibara zake alizotoa baada ya kifo cha kishahidi cha Husein, na tena wakati watu wa familia ya Husein walipofika kama watumwa mbele yake kule Damascus zinadhihirisha hisia zile zile za upingaji mabadiliko dhidi ya Uislamu na Mtume wake.

Ilikuwa ni jambo la kinyume sana kwamba mtu kama huyu, sio tu aliweza kuitwaa kazi ya Ukhalifa wa Uislamu bali pia aliweza kukubaliwa kuwa hivyo na idadi kubwa ya Waislam. Matokeo yasiyoepukika yalikuwa kwamba mwelekeo wa jumla wa Waislam kuhusu imani yao uligeuka kuwa wa kutojali, na walibakia tu watazamaji wasiojali wa utafutaji wa starehe uliokuwepo na ukiukwaji wa amri za sheria za Qur'ani na sunna za Mtume.

1. Kitabu: Hayat al-Hayawan, Juz. 2 , uk. 207
2. Kitabu: Tabari, Juz. 4, uk. 259
3. Kitabu: Hayat al-Hayawan, Juz. 2, uk. 207
4. Kitabu: Al-Akhbar al-Tiwal, uk. 265
5. Kitabu: Kamil, Juz. 4 uk. 63
6. Kitabu: Al-Sawaiq, uk. 135

# Sura Ya 13: Tabia Njema Za Husein, Mafanikio Ya Hali Ya Juu Na Semi Za Thamani

Tabia huundwa na vipengele vingi mbalimbali ambavyo kwamba vilivyo vya muhimu zaidi ni sifa za kifamilia ikiwa ni pamoja na desturi za nasa ba, mazingira, malezi, elimu na uzoefu muhimu na wa wazi katika maisha.

Tabia sharifu zilizo bainifu za familia ya Husein zilikuwa hazifanani na za familia nyingine yoyote ile nchini Arabia na hata Yazidi wakati mmoja alikubali ndani ya baraza lake kwamba mama yake Husein alikuwa bora zaidi kuliko mama yake yeye mwenyewe, na kwamba babu mzaa mama yake Husein (yaani Mtume s.a.w.w) alikuwa bora zaidi kuliko babu mzaa mama yake yeye Yazidi.[1]

Alama tambulishi hizi za familia yake zilidumisha yale matumaini ya ubora wa moyo wa Husein, na malezi yake yalihakikisha utukufu wa mwenendo na usafi wa tabia. Alipitia pia katika mabadiliko mengi ya maisha na alijifunza kuongozwa zaidi na mantiki ya akili kuliko hisia.

Hili lilikuwa limepatia upevu wa busara katika mtazamo wake wa maisha na pia umadhubuti imara na werevu wa haraka.

Wakati wataalamu wa wasifu (maelezo ya maisha ya mtu) walipojaribu kutoa maelezo mafupi juu ya sifa za Husein na mafanikio mengi, iliwabidi watumie maelezo ya lugha ya kushawishi (fasaha). Ibn Abi Shayba, mtaalamu juu ya hadith, katika kumuelezea Husein alisema, "Alikuwa ametaalimika vyema katika Qur'an na alitenda kwa mujibu wa hicho.

Alikuwa mchamungu, mwenye kujizuia na kujinyima, mkarimu, mzuri wa muonekano, fasaha wa maneno, mwenye utambuzi juu ya Mwenyezi Mungu, hoja ya dhati tukufu sana ya Mungu." Akiyaona maelezo ya kawaida ya kusifia hayatoshi kutendea haki sifa nzuri sana za Husein, Ibn Abi Shayba aliongeza kifungu cha mwisho kwamba Husein alikuwa hoja ya dhati tukufu ya Mungu. Ibn al-Arabi, vile vile alisema kwamba Husein, mmoja wa wajukuu wa Mtume, alikuwa miongoni mwa alama za Mungu.

Ni kwa sababu ya Husein kwamba baadhi ya wale ambao wana mwelekeo wa Agnostiki (imani ya kusadiki kwamba hakuna habari za Mungu wala hazipatikani) wakati mwingine hujihisi kuvutika kwenye imani ya kumuamini Mungu. Kama vile Josh wa Malihabad, mtunga mashairi maarufu wa ki-Urdu, amesema hivi; "Ndiyo, yule Husein, ambaye uimara wake umeungana na umilele, mara moja moja huwaambia siri wanafalsafa ile iliyofichika katika usiri wenye rangi nyingi wa ulimwengu (kwamba) kuna Akili ambayo hufanya kazi na Dhati ambayo ina ujuzi. Huvuta uzingativu wetu kutoka kusujudu kwetu ndani ya swala kwenye lengo la kusujudu huku. Yeye pekee hutuonyesha yule Mmoja tu wa kuabudiwa."

Hata katika akili finyu ambayo kwayo ibada kwa kawaida hushirikishwa, kumwabudu Mwenyezi Mungu kwa Husein na swala zake hudumu katika kutofikiwa. Alienda Hijja safari 25 kwa miguu.

Mtu anaweza kupata mfano wa kweli wa moyo wa ibada za Mungu wa Husein kutokana na ombi alilolitoa wakati wa mchana wa tarehe 9 Muharam pake Karbala kwa kufanya makubalianao ya kusitisha vita kwa muda ili kwamba aweze kutumia muda wa msitisho huo wa vita katika kufanya ibada za swala na du'a (maombi) kwa Mwenyezi Mungu, kusoma Qur'an na ibada nyingine kama hizo zenye maombi. Ombi hili lilikubaliwa kwa shingo upande, na Husein na sahaba zake waliutumia usiku huo katika swala na maombi na mvumo wa sauti zao, katika ukimya ule wa usiku, ulifanana na mvumo wa nyuki. Halafu tena wakati wa mchana wa mwezi 10 Muharam, Husein alisimamisha swala zake za mchana pamoja na sahaba zake kwa nyakati zake, katikati kabisa ya uwanja wa mapigano wakati vita vilipokuwa katika hatua yake ya umwagaji damu mkubwa mno.

Wawili kati ya masahaba zake Husein walisimama mbele yake kuikinga mishale wakati yeye alipokuwa akitekeleza swala zake. Mmoja wao, Sa'id bin Abdillah al-Hanafi alianguka na kufa mara tu swala ilipofikia tamati.

Husein alikuwa mkarimu sana, na Mtume alipoitambua sifa hii ndani yake alisema: "Husein ana ukarimu na ujasiri wangu." Katika kugawanya mis- aada yake alitofautisha kati ya waombaji kwa kutumia msingi wa daraja za mafanikio yao na sifa nzuri na utambuzi wao juu ya Mungu. Bedui mmoja wakati mmoja alifika kwa Husein kuomba msaada. Alimwambia Husein kwamba Mtume aliwahi kumshauri kuomba msaada wakati wa haja, kutoka kwa mtu ambaye alikuwa aidha Mwarabu mwenye moyo mzuri, au chifu mkarimu, au mtu anayeiunga mkono na kuitetea Qur'ani au mtu aliye muungwana.

Kisha akamwambia Husein kwamba aliziona sifa hizi zote zikiwa zimewakilishwa ndani yake yeye, na akaomba msaada wake. Husein akamwelezea (bedui huyo) vigezo ambavyo kutokana navyo hivyo aliweza kuamulia madai ya wale ambao walimjia kumtaka msaada. Kisha akamwambia yule bedui kwamba angemuuliza maswali matatu, na kwam- ba kwa kila jawabu sahihi, zawadi yake ingekuwa ni theluthi moja (1/3) ya pesa alizokuwa nazo wakati huo ndani ya mkoba wake. Mazungumzo hayo ni yenye kuvutia vya kutosha kunukuliwa:

**Imam**: "Ni jambo gani bora mno la kufanya?"
**Bedui**: "Ni kumwamini Mwenyezi Mungu."
**Imam**:"Ni njia gani nzuri kabisa ya kuweza kumwokoa mtu kwenye maangamizi?"
**Bedui**: "Ni kumtegemea Mwenyezi Mungu."
**Imam**: "Ni nini pambo la mwanaadamu?"
**Bedui**: "Ni elimu iliyounganishwa na akili."
**Imam**: "Kama hii haipatikani, ni jambo gani tena?"
**Bedui**: "Ni utajiri (mali) ulioambatana na ukarimu."
**Imam**: "Itakuwaje basi kama hii haikupatikana?"
**Bedui**: "Ni umasikini ulioungana na subira (uvumilivu)."

**Imam:** “Je itakuwaje kama hili litakuwa pia haliwezi kutekelezeka?”
**Bedui:** “Basi wacha radi imtafune mtu huyo mpaka kuwa majivu.”

Husein kwa tabasamu pana kabisa aliukabidhi mkoba wake kwa Bedui huyo.[2]

Mkusanyiko (kitabu) wa baadhi ya du’a na maombi ya Husein kwa Mwenyezi Mungu, usiopitwa kwa maelezo ya uhusiano kati Mungu na viumbe Vyake, ufahamikao kama *al-Sahifa al-Husayniyya* upo mpaka leo hii. Idadi kubwa ya maelezo yake kuhusu sheria za Kiisilam, maarifa ya sheria na elimu ya dini vinapatikana katika mikusanyiko mbalimbali ya Hadith. Mbali na hizi, kiasi kidogo cha khutba zake na mashairi, akiwaagiza watu katika kupata elimu ya Mwenyezi Mungu na kuwasihi kufuata njia za uadilifu zote pia zinapatikana.

Ilikuwa ni kwa sababu ya nafasi inayowashinda wote ya Husein kuhusu elimu juu ya Mwenyezi Mungu, na uchamungu na ujuzi kwamba miongo- ni mwa masahaba zake pale Karbala, palikuwa na watu wenye uadilifu utambulikanao, na wenye mafanikio mazuri sana. Kwa kweli lilikuwa ni ua la jamii ya Kiislamu kama lilivyokuwa wakati huo na hazina ya elimu na matendo ambalo lilijitoa mhanga lenyewe pamoja na Husein. Masahaba zake walikuwa ni pamoja na watu ambao waliihifadhi Qur’ani kwa moyo, walikuwa na elimu yake ya kina na walikuwa ni wabebaji wa mwenendo wa Uislam. Watu kama hawa wangeweza kuvutwa tu na Husein ambaye ubora wake usio na upeo kwao, bila shaka kwa vyovyote vile ungeweza kukaribishwa.
Hata wale ambao walikuwa wameurithi uadui dhidi ya Husein walijua na kuikiri heshima yake kubwa na daraja lake la juu. Abdallah bin Amr al-Aas alikuwa maarufu miongoni mwa Bani Umayyah kwa kujizuia (kujinyima), uchamungu usalihina (udhari wa moyo) na kukubali kushikilia kazi za maadili mema. Alipigana akiwa upande mmoja na baba yake, Amr bin al-Aas dhidi ya Ali katika vita vya Siffin na Husein aliacha kuongea naye.

Siku moja, wakati Husein alipopita karibu na kundi la watu ambalo ndani yake Abdallah bin Amr bin al-Aas alikuwemo, yeye Abdullah aliwaambia wenzake aliokuwa nao kwamba miongoni mwa wakazi wa ardhini, aliye kipenzi kikubwa kwa wakaazi wa mbingu alikuwa Husein. Aliongeza kwa kusema kwamba kama kwa njia yoyote ile angeweza kupatanishwa na Husein, ingekuwa ni jambo lenye thamani zaidi kwake kuliko kuwa na Ngamia wekundu.[3]

Hata wakati wa utoto wake, Husein alikuwa na ujasiri wa kuongea ukweli. Alikatalia Khalifa wa pili, Umar, alipoivamia mimbari ya Mtume, na (Husein) akatoa amri kwa sauti akisema; “Shuka chini kutoka kwenye kiti cha baba yangu.” Khalifa alikubali, akasema, “Ni mimbari ya baba yako, kwa hakika, na siyo baba yangu mimi.”

Uthibitisho wa ukweli wa Husein mbele ya hatari kubwa sana unatolewa na ukweli kwamba hakufanya jaribio lolote kabisa la kufichua katika hatua yoyote ile ya safari yake kutoka Makka kwenda Karbala hatari zozote zile zilizokuwa zinawangoja mbele au vinavyovunja moyo na maafa (balaa) ambayo yalimpata.

Lakini kinyume chake, alirudia mara kwa mara kuwaonya masahaba zake kuhusu hatari zinazokaribia kuwazunguuka, na akawafahamisha ukweli. Kwa hiyo idadi ya watu wenye kumhurumia kwa sababu ya faida za kidunia, iliendelea kushuka. Aliendelea katika kutoa maonyo ya hatari mpaka kila uwezekano wa mtu yeyote aliyeshikamana naye kutokana na dhana potofu ukawa umetoweka.

Husein alipenda sana amani kiasi kwamba alijaribu kufanya amani na maadui zake mpaka dakika ya mwisho pale Karbala. Na bado alikuwa na ujasiri, uimara na subira na uvumilivu, kufidia kwa kichwa chake kwa ajili ya njia ya haki aliyoichagua kuiunga mkono.

Husein alikuwa mwamuzi (hakimu) wa watu asiyekosea. Ni kweli inayoshangaza kwamba hakuwa hata mmoja wa wale watu ambao alikuwa amewachagua kufuatana naye katika safari yake ya kwenda Karbala alikwepa kujitoa mhanga kwa ajli ya Husein. Alijionyesha vile vile kuwa yeye ni msimamizi wa watu mwenye kipaji sana, na alikiongoza kikundi chake kidogo cha masahaba vizuri sana kwamba, wakisaidiwa na nguvu za ajabu za moyo wa kujitoa mhanga na ujasiri, kikundi hicho kililiweka jeshi kubwa sana lililowazidi idadi la Yazid mapambano kwa sehemu kubwa zaidi ya siku hiyo ya mwezi 10 ya Muharam.

Maneno ya watu wengi walioko katika nafasi za juu mara nyingi ni yenye kuhitalifiana kwa dhahiri kabisa na vitendo vyao. Maneno yao kwa hiyo yanaelekea kuhifadhiwa vizuri kuliko kumbukumbu za matendo yao. Hivyo sivyo ilivyo kwa Husein. Tabia yake na kazi zake na mafanikio yake yalikuwa yenyewe katika mpangilio wa hali ya juu kwa kiasi kwamba ni zaidi ya kutosheleza kuikamata nathari ya waandishi na wasemaji wa ulimwengu.

Kwa hiyo, kulikuwa hakuna jitihada kubwa iliyotumika kati- ka kukusanya maneno yake ya kweli na hekima ambayo yanakutwa ndani ya vitabu mbalimbali, yote yakiwa katika nathari (insha) na beti. Baadhi yao yanafuata hapa chini:

1. Yule ambaye ni mkarimu, huwa kiongozi, yule aliye bakhili hupata fedheha.

2. Ni mkarimu mno miongoni mwa watu, yule ambaye hutoa misaada hata kwa wale ambao hawaitarajii.

3. Kuzipokea neema kutoka kwa Mungu huingiza wajibu wa kufanya fad- hila kwa wengine.

4. Kwamba watu wakujia wakati wakiwa katika haja, hilo lenyewe peke yake ni moja ya neema za Mungu.

5. Mfanye Muumba badala ya viumbe vyake kuwa kitovu (mahali pa) cha matumanini yako, na wewe utakuwa huru kutokana na mtu mwongo na yule mkweli halikadhalika.

Omba kwa ajili ya riziki yako ya kila siku ya Mungu Mwenye neema nyingi, kwani hakuna mwingine tena agawaye riziki za kila siku.

Yule ambaye hudhania kwamba watu wangeweza kumgawia mahitaji yake amepungukiwa na imani juu

ya Mwenyezi Mungu.

Yule ambaye hufikiria kwamba watu wangemtoshelezea anaelekea kwenye fedheha kubwa.

6. Yeyote yule aongezaye utajiri wake hujiongezea wasiwasi wake.

7. Kujiambatisha kwa Mungu huwatenganisha watu kutokana na mwingine yeyote yule.

8. Ibn Kathir anasimulia kutoka kwa Is'hak bin Ibrahim kwamba wakati mmoja, katika kuyazuru makaburi ya mashahidi yalioko eneo la al-Baqi, Husein alisoma mashairi yakiwa na maana ya:

"Niliwaita wakazi wa makaburini na wakanyamaza kimya, lakini vumbi la makaburi yao likatoa majibu kuhusu ukimya wao."
Likasema, "Je, unajua nimefanya nini kwa wale ambao wanakaa ndani yangu. Nimezipunguza nyama zao hadi kuwa vipande vidogo vidogo na ninezichana ngozi zao vipande vipande;
"Nimejaza macho yao kwa udongo ingawa huko nyuma kipande kidogo cha bua kiingiacho machoni mwao kiliwanyima raha ya kupumzika;
"Ama kuhusu mifupa yao, nimeipunguza na kuwa vipande vidogo vidogo kiasi kwamba maungio yao ni makano yanaonekana kwa wazi wazi kabisa;
"Nimevitenganisha viungo hivyo kimoja kutokana na kingine, ili kwamba vionyeshe alama zisizo na mashaka za kuoza na kuharibika."

9. Ibn Sabba al-Maliki ameyahusisha kwa Husein baadhi ya mashairi kati- ka kitabu kiitwacho *al-Fusul al-Muhimma*, ambayo yametafsiriwa hapa chini;

"Wakati meno ya zama yanapokujeruhi, kamwe usijinyenyekeze kwa watu.
Na isipokuwa kwa Mwenyezi Mungu ambaye hutoa namna ya kijikimu, kamwe usije kuomba riziki yako ya kila siku kutoka kwa yeyote yule.
Kwani hata kama utaizunguuka dunia kutoka Magharibi hadi Mashariki,
Hungekutana na mtu yeyote ambaye angeharibu au kutengeneza kile ambacho umepangiwa."

10. Hata kama ulimwengu ungekuwa ni mahali pa kupendeza na kuvutia, thawabu na malipo ya Mwenyezi Mungu yana daraja la juu zaidi.

Na kwa vile miili imezaliwa ili ife, ni vizuri zaidi kwa mwanadamu kuuawa kwa upanga katika njia ya Mwewnyezi Mungu.

Na kwa vile ni dhahiri kwamba fungu la kila mtu katika riziki ya kila siku limekwishapangwa mtu anapaswa ajizuie na ulafi juu yake.

Na wakati inapokuwa ni hakika kwamba mali (utajiri) imehodhiwa ili ije kuachwa nyuma, je isingekuwa sio jambo la busara kuwa kama mtu bakhili?

11. Wakati mmoja mtu fulani alimwomba Husein kumpatia kipande cha ushauri kwa maneno mafupi tu. Katika kumjibu, Husein alisema:

“Yeyote yule apendaye kulipata lengo lake kwa njia ya kumwasi Mwenyezi Mungu, atafedheheshwa katika matumaini yake na atajikuta mwenyewe karibu zaidi na hatari kubwa.”

Tafsiri ya baadhi ya tungo zake za kiuchamungu ambazo alikuwa akizitumia kwa kuzikariri katika Swala zake za kila siku na dua, ni kama zinavyoandikwa hapa chini:

1.) Ee Mwenyezi Mungu! Wewe ndiye Mwanzilishi wa ukarimu na upaji, na chochote kilichopo cha uwezo na nguvu ni Chako na nguvu Zako zimeenea kila mahali. Hali ikiwa ndivyo hivi ilivyo, natafuta hifadhi kwako Wewe, na ninategemea kwenye uwezo Wako na nguvu kwa msaada. Ninatii na kujiweka chini ya kile ambacho umekiamuru kwangu mimi tangu mwanzo. Nitatembea juu ya njia ambayo Wewe umeniweka na ninadhamiria tu kwenye kile ambacho kinakubaliana na radhi Yako. Siachi kujibidisha hata kidogo wala sikubali uzembe wowote ule katika jitihada zangu za kutii amri Zako. Kinyume chake natembea kwa wepesi na hima juu ya njia ambayo Wewe umenichagulia. Napenda kutekeleza kikamilifu majukumu ambayo Wewe umeyakabidhi kwangu.

Unaweza sasa, Wewe Mwenyewe kunisaidia kwa msaada Wako, na usininyime neema Zako au uwezo Wako, wala usinitenganishe kutoka kwenye lengo ambalo kwa kupitia hilo napenda kutimiza radhi Zako. Ifanye tabia yangu itengemezwe juu ya busara na kanuni ya mwenendo Wangu (itegemezwe) juu ya mwongozo wa kweli na sahihi. Ifanye njia yangu ielekezwe kwenye makusudio sahihi ili kuweza kuniongoza kwenye ukamilishaji wa matakwa yangu, na kunifikisha mwisho wa safari ambao Wewe umeikusudia kwa ajili yangu mimi na ambao kwawo Wewe umeniumba, na ambao kwa huo Umeelekeza nia yangu.

Maneno ya du’a hii yanaashiria kwamba Husein alikuwa ameyatoa maisha yake kwa lengo fulani maalum na kwamba muda wote wa maisha yake ul tumika katika kuyatii maelekezo ya Mwenyezi Mungu. Katika mwaka wa 61 A.H maneno (semi hizi) haya yalipata sura ya kujitoa kwake mhanga kusikolinganishika huko Karbala.4

2.) Ee Mwenyezi Mungu! Kama mtu yeyote atachukua hifadhi kwa mtu mwingine zaidi mbali na kwako Wewe, basi mwache afanye hivyo. Wewe ndiyo kimbilio langu, na kimbilio langu pekee. Kama mtu ataelekea kwa mwingine yeyote mbali na Wewe kwa kutaka msaada, yuko huru kufanya hivyo, bali Wewe ndiyo msaada wangu, na msaada wangu pekee. Ufanye ukubwa Wako, ambao hauwezi kuathiriwa na tamaa potovu yoyote ile au madhara, na ambao ndani yake chuki ya kawaida haiwezi kuwa na sauti, nilinde katika mtihani wangu kutokana na kuhusishwa katika fitina yoyote ile, au kufadhaishwa na kundi lolote lile la kishetani mpaka nitakaporejea Kwako, nikiwa mtiifu kwenye utashi Wako, moyo wangu ukiwa huru kutokana na mawazo mabaya, watu wengine wakiwa hawanifikirii mawazo mabaya, wala mimi kuwatilia watu wengine mashaka, wala wengine wakiwa katika hali ya kutokuwa na yakini kuhusu mimi.5

3.) Husein alikuwa akitumia kurudia rudia kuisoma dua ifuatayo wakati wa asubuhi na jioni:
“Ewe Mwenyezi Mungu! Mimi nimenyenyekea Kwako, na nimegeukia Kwako, na nimeweka mikono yangu mkononi Mwako. Ee Mwenyezi Mungu! Wewe pekee unaweza kunilinda kutokana na fitina za kila mtu mwingine, lakini hakuna mwingine yeyote isipokuwa Wewe awezaye kuniokoa na ghadhabu Yako.”

Je, ilikuwa inawezekana kwa mtu wa namna hii, kama inavyodhihirishwa na semi na du’a za Husein kukubali kunywea kwenye nguvu za ukaidi kwa Mungu, kutoa kiapo cha utii kwa mtu muovu kama Yazid? Jibu ni lazima liwe ni hapana yenye nguvu.

Hata wakati akiwa peke yake, na akiwa amezunguukwa na jeshi kubwa pale Karbala, Husein alisimama imara katika imani yake na itikadi zake. Kweli, Husein na sahaba zake walichinjwa. Lakini wakati matokeo ya vita vya Karbala yalipoanza kujitokeza ilionekana kwamba katika hali halisi alikuwa ni Husein ambaye aliibuka kuwa mshindi.

Falsafa ya maisha ya Husein kama ilivyofundishwa na baba yake, Ali ilikuwa ‘Shikamana na haki, hata kama ikiwa chungu.”

1. Tabari, juz. 6, uk. 266.
2. Al-Tafsir al-Kabir, uk. 272 cha Al-Razi. (Tabari, juz. 6, uk. 266 tanbihi ya kwanza)
3. Usudul-Ghaba, juz. III, uk. 235 cha Ibn al-Athir.
4. Majmu Du’at, uk. 71-72.
5. Ibid, uk. 73.

# Sura Ya 14: Msisitizo Wa Yazid Juu Ya Kiapo Cha Utii Cha Husein Na Kukataa Kwa Husein.

Kwa kuwa mfalme, Yazid alijikuta katika kumiliki utajiri mwingi usioelezeka madaraka yasiyo na mipaka. Kitu kimoja ambacho baba yake alimwonya nacho akiwa kwenye kitanda chake alichofia, hata hivyo kilimweka na wasiwasi uliomhuzunisha sana. Lilikuwa kwamba watu wachache maarufu miongoni mwa Maquraishi wamekaidi kutoa viapo vyao vya utii kwake. Muhimu miongoni mwa waliopinga ambao idadi yao iliwajumlisha Abdalla bin Zubairi, Abdillahi bin Umar na Husein bin Ali.

Yazid hakupoteza muda katika kumwandikia barua binamu yake, al-Walid bin Utbah bin Abi Sufyani, gavana wa Madina, kuhusu kifo cha Mu’awiyah na kumwelekeza kuwalazimisha Husein bin Ali na Abdullah bin al-Zubeir kutoa kiapo cha utii kwake, na asiwaachie kabla hawajafanya hivyo.

Mbali ya kuwa na uhusiano wa karibu sana na Yazid, al-Walid alikuwa na hisia za heshima kubwa kwa Husein kutokana na kunyanyuka kwa daraja lake tukufu. Maelekezo yaliyopokelewa toka kwa Yazid, kwa hiyo yalimtingisha na kumtia wasiwasi sana. Ingawaje hakuwa katika hali ya mahusianao mazuri

sana na Marwan kwa wakati fulani, alimtaka ushauri Marwan kuhusiana na jambo hili ili kujizoesha na mwelekeo wa sasa wa fikra za Bani Umayyah. Inaweza pia kutajwa kwamba Marwan aliishi kwa kufanya hizaya na dharau wakati wa uhai wa Mtume kwa kiasi kwamba alifukuzwa pamoja na baba yake kutoka Madina na Mtume mwenyewe.

Marwan alimwambia al-Walid ondoa wasiwasi wote kuhusu Abdallah bin Umar kwani yeye hataudai Ukhalifa. Alisisitiza sana kwamba kiapo cha utii kwa Yazid kichukuliwe kutoka kwa Husein bin Ali na Abdullah bin Zubeir, na kwamba endapo wataweka vipingamizi, basi wauawe kabla taarifa za kifo cha Mu'awiyah hazijatangazwa, kwani kama itakuwa hivyo, yeye alidhani, wote wawili wangejitahidi kukusanya waunga mkono kuhusu madai yao, na kwa wazi wangemkataa Yazid.[1]

Al-Walid aliwaita Husein na Abdillaha bin Zubeir ambao wote wawili walikuwa katika msikiti wa Mtume. Ilikuwa ni saa zisizokuwa za kawaida kwa Al-Walid kuwaita watu katika wakati kama huo na wangeweza kudhania kwamba Mu'awiyah amekufa na kwamba walikuwa wameitwa kutoa kiapo cha utii kwa Yazid. Husein aliwakusanya ndugu na marafiki zake na kwenda nao kwenye jumba la gavana. Aliwaambia wamngojee mlangoni kwa al-Walid wakati yeye alipokwenda ndani kumwona gavana, lakini waingie ndani ya nyumba hiyo endapo angewaita au al-Walid atakapopandisha juu sauti yake.

Al-Walid alizitangaza habari za kifo cha Mu'awiyah na baada ya taratibu za kawaida za rambirambi zilipokwishafanyika, alimtaka Husein kutoa kiapo cha utii kwa Yazid. Husein alijibu kwamba labda ingefikiriwa haitoshi kwamba mtu kama yeye angetoa kiapo cha utii kwa siri badala ya kufanya hivyo mbele ya halaiki ya watu.

Al-Walid alikubali kuchukua kiapo cha utii cha Husein wakati atapokuja kutangaza hadharani kuhusu kifo cha Mu'awiyah, na akawataka wengine wote kutoa kiapo cha utii kwa Yazid, kwani huo ndio ungekuwa wakati mwafaka kwa suala hili kuweza kupatiwa ufumbuzi wa mwisho kabisa.

Marwan, ambaye alikuwa anaangalia maendeleo ya shughuli zote hizi hakuupendelea mwelekeo wa hisani wa al-Walid juu ya Husein, akiipandisha juu sauti yake alisema, “Kama Husein ataondoka sasa, bila kutoa kiapo, kamwe hutaweza tena kupata nafasi kama hii, labda iwe hivyo baada ya kumwagika damu nyingi. Ni bora zaidi kumkamata hapa na sasa hivi, na kumzuia kurudi nyumbani kwake mpaka labda atoe kiapo cha utii au vinginevyo kumuua.”

Hili lilimkasirisha sana Husein ambaye alisimama na kusema; “Marwan, vipi unaweza kuthubutu kuniua? Wallahi umetamka kimakosa na umetenda dhambi.” Husein kisha akaondoka kwenda nyumbani kwake (**Tabarim uk.218**)

Kwa nini Yazid awe alisisitiza sana kwa jitihada zisizokuwa na mwisho juu ya kupata kiapo cha utii cha Husein juu yake yeye? Inapaswa iwe dhahiri kwamba hata liwe kundi la watu kubwa namna gani ambalo Mu'awiyah angeweza kulikusanya Makka na Madina ili waape kumuunga mkono Yazid, lazima kutakuwepo mamia ya watu katika sehemu zote mbili ambao wanaweza kuwa walibakia majumbani mwao na hawakutoa kiapo.

Tena, hakuna mtu mwingine zaidi ya Husein, ambaye alitokana na familia ya Mtume, au aliyetokana na kizazi cha Ali, aliyetakiwa kuchukua kiapo cha utii kwa Yazid, hata ingawaje Muhammad ibn al-Hanafiyya Abdallah bin Ja'afar na Abbas ibn Ali walikuwepo hapo.

Katika demokrasia kukubalika na watu wengi juu ya uhalali wa serikali kunatosha, na maoni ya wachache wasiokubaliana hutupiliwa mbali kabisa. Kundi hilo dogo halilazimishwi kuacha maoni yao, wala yeyote kati ya watu wake kutishiwa kwa kufanyiwa vurugu, au kuteswa kwa hilo.

Katika vipindi vyote vya ukhalifa vilivyopita kulikuwepo na watu ambao hawakutoa viapo vya utii kwa khalifa. Wakati wa Ukhalifa wa Ali mwenyewe, Hassan bin Thabit, Ka'b bin Malik na Zayd bin Thabit, miongoni mwa wengine wengi, hawakutoa kiapo cha utii kwake, bila ya kufikwa na matokeo yoyote yale mabaya, yasiyopendeza. Kwa nini, basi utaratibu mzima wa serikali ya Syria utake kwa nguvu kiapo cha utii kutoka kwa Husein pekee?

Ilikuwa hivyo kwa sababu Yazid alitaka akubalike kama Khalifa wa Uislam, licha ya ukiukaji mwingi wa amri za sheria za Qur'an na Sunna za Mtume, siyo na watu wa kawaida, bali akubaliwe na Husein ambaye juu yake yeye, akiwa kama mkubwa kabisa wa familia ya Mtume, na mrithi wake wa haki kabisa, alikuwa ndiyo mwenye wajibu pekee wa kuusaidia Uislamu na kuitetea haki.

Yazid angeweza kufanya hivyo bila ya kiapo cha Husein kama masingizio yake yangevutika kwenye madaraka ya kidunia tu, bali kwa vile alipenda kuidhibiti dini pia, na kuifanya iwe ya kutumikia utashi wake na matakwa yake, ilibidi apate kiapo cha utii cha Husein. Hata hivyo Husein aliuzuia mkono wake (kwa kutokutoa kiapo cha utii) na akakitoa kichwa chake katika muhanga kwa ajili ya Uislamu.

1. Tabari, uk. 217.

# Sura Ya 15: Utulivu Wa Hasan Na Shughuli Za Husein.

Swali, ambalo wakati mwingine hujadiliwa, ni kwa nini Husein hakuchagua kukubaliana na Yazid kama vile ndugu yake mkubwa al-Hasan, alivyofanya huko nyuma wakati akishughulika na Mu'awiyah. Swali hili hal- izingatii tofauti katika hali ya ndugu wawili hawa ambayo hukua katika umuhimu pamoja na uzito ulioambatana na hali za nje.

Kwani kwa mujibu wa imani ya Shi'a Hasan alimrithi Ali kama Imam, na Husein alimrithi Hasan katika wadhifa huo huo kama ilivyoamriwa na Mwenyezi Mungu. Kwa hiyo, ndugu wawili hawa, walikuwa na hadhi moja hiyo hiyo mbele ya macho ya Mtume na mbele ya Mwenyezi Mungu. Lakini Hasan alikuwa amewekwa pia kama khalifa.

Alipoona kwamba Mu’awiyah amefaulu katika kupanda kwa siri mbegu za kutofuatiana na kufarakana miongoni mwa Waislamu, na alikuwa ameingiza hisia za ukosefu mkubwa wa usalama kwa kudhoofisha utaratibu wa udumishaji wa amani, sheria na taratibu, Hasan aliona inafaa kuingia katika mkataba wa amani naye ambao chini yake huo alijiuzulu kwa manufaa ya mpinzani wake kwenye zile nyongeza tu, za mamlaka ya kidunia.

Hakujitenga kabisa kutoka kwenye ubora wa kiroho hata kidogo, na akaendelea kuwa kiongozi wa kiroho wa Waslamu. Mu’awiyah aliyavunja masharti ya mkataba wakati wa uhai wa Hasan, na ulipunguzwa kuwa makubaliano tu ya Hasan kutomwingilia Mu’awiyah.

Baada ya hitimisho la mkataba, Mu’awiyah alijaribu kwa uwezo wake wote kutaka kumvua Hasan ule ubora wa kiroho, na kwa kipindi cha miaka ishirini Husein alibakia amefungwa na masharti ya mkataba uliofanywa na ndugu yake. Baada ya watia sahihi kwenye mkataba walipokuwa wamekwishakufa, Husein hakufungua mazungumzo yoyote yale kwa ajili ya amani, akijua vyema kwamba sera kama ilivyodhihirishwa na mkataba na Hasan wa kumnyima uongozi wa kiroho wa mamlaka ya kidunia umebadilishwa na ule wa kuteka au utwaaji wa uongozi wa kiroho na mtawala mwenyewe.

Viunganisho katika nyororo hii ya utekelezaji wa sera hii vilikuwa ni uvunjaji wa dhahiri wa masharti ya mkataba na Hasan, na mauaji ya Hasan yaliyifanywa na mmoja wa wake zake, aliyeitwa Ju’da, ambaye alimtilia sumu kwa maelekezo ya siri ya Mu’awiyah.

Kielekezo kingine katika welekeo uliotajwa katika ibara iliyotangulia kimetolewa na khitilafu au tofauti katika namna na taratibu ambamo Yazid aliwafanya watu watoe kiapo cha utii kwake kutokana na njia na mitindo ambayo ilikuwepo na kutumika katika siku za Makhalifa waliotangulia. Katika matukio kama hayo walikuwa wakiahidi kuzitetea amri za Qur’an na Sunna za Mtume.

Ufidhuli wa Yazid na kiburi ulikifanya kiapo kuwa ni utambuzi wa unyonge kwa mwenye kuapa kwamba alikuwa ni mtumwa wa Khalifa ambaye angeweza kuangamiza maisha yake, mali yake na kizazi chake katika namna yoyote ile aionayo inafaa. Yazid ibn Abdallah ibn Rabia alikuwa tayari kutoa kiapo cha utii kwa mujibu wa taratibu ya zamani lakini alisita kuapa kumtii Yazid kwa mtindo uliopendekezwa. Akauawa. Haya yalifanyika Madina.

Wapi, basi palipokuwa na haja yoyote ile kwa Husein kujaribu kujipendekeza kwa Yazid? Husein alikuwa akishirikiana kwa ukaribu mno na Hasan wakati wa miaka yote iliyopitiwa na mkataba wa Hasan na Mu’awiyah, na alikuwa ameona upotofu uliokuwa umejitokeza wa mielekeo iliyoenea inayoelekezwa kwenye dini (imani) na kukosekana majibu ya malalamiko yake ya mdomo na maandishi dhidi ya kile kilichokuwa kinatokea katika nchi za Kiislamu.

Lazima atakuwa ameona ya mbele kwamba upinzani wa namna ya mfano, kama ni lazima, mpaka mwisho mchungu, ulikuwa utolewe ili kuuokoa Uislam. Hata hivyo, hakufanya haraka katika kulifanya hilo. Alipochukua madaraka, hatua ya kwanza ya kisiasa ambayo Yazid aliichukua ilikuwa ni kutaka kiapo cha utii cha Husein cha kumtii yeye chini ya vitisho vya kutumia nguvu.

Hapa ndipo ambapo Husein alipojiona amewekwa katika mazingira ambayo yalikuwa kwa dhahiri kabisa tofauti na yale ambayo yalimkabili Hasan ambaye aliachia madaraka yake ya kidunia tu kwa manufaa ya Mu'awiyah kwa ajili ya kuiweka amani na utulivu katika milki yake.

Alikuwa, hata hivyo, ameshikilia ubora wake wa kiroho na uongozi wa Waislamu. Husein alishurutishwa siyo tu kujivua ubora wa kiroho, bali pia kutoa kiapo cha utii kwa Yazid ambaye alichukua amri za Qur'an na Sunna za Mtume kwa thamani ndogo sana. Ilikuwa ni kwa sababu hii kwamba hakuna hata mmoja wa marafiki na ndugu zake Husein, hali wakiwa wanamshawishi asiondoke kwenda Kufa, na wakimshauri kubakia Madina, au kukaa Makka au kwenda Ta'if au Yemen, aliyependekeza kwake kukubaliana na kuchukua kiapo cha utii kwa Yazid.

Ilikuwa inafahamika kwao wote kwamba aina hii ya kiapo cha utii ilikuwa nje kabisa ya suala hili kwa kiasi ambacho Husein alikuwa anahusika, ikiwa yenye kubomoa yale yote yaliyokuwa matukufu na ya hali ya fikira za kiungwana, na kufikia kubadilishana haki mbalimbali za Waislamu, na madai yake mwenyewe ya haki.

# Sura Ya 16: Msimamo Wa Husein – Fasiri

Suluhu na Yazid ikiwa haiwezekani kabisa, njia mbadala pekee iliyo ya wazi kwa Husein ilikuwa ni kumpinga Yazid ili kuyaokoa maadili mema ya Uislam kutokana na kushuka zaidi chini na kuilinda dini yenyewe kutokana na mashambulio yenye kuangamiza ya uhuishaji wa hali ya kabla ya Uislam.

Asingeweza, hata hivyo, kulea ndoto au fikra za uwongo kuhusu aina ya msaada ambao angeweza kuutumainia kujiorodheshea katika mzozo wowote ule na Yazid.

Hali iliyokithiri ya kutofurahisha ambamo ndugu yake, Hasan, alijikuta nayo mwenyewe, kupitia kule kuondoshwa kisaliti kwa msaada aliokuwa amepewa katika kukabiliana kwake na Mu'awiyah, na vile alivyoacha Hasan, chini ya vikwazo, yale madaraka ya kidunia kwa manufaa ya Mu'awiyah, na uvunjaji wa Mu'awiyah wa masharti yote ya mkataba wake na Hasan bila kupata adhabu yoyote juu ya hilo, yote haya yalikuwa ni historia tu ya siku za karibuni, na umuhimu wake usingeweza kupotea (akilini) kwa Hasan.

Kwa hiyo, yeye alifikiria mkakati mpya kabisa wa vita na Yazid, kwani, kwa hali yoyote ile, vita ilikuwa lazima iwepo. Hakufanya jaribio la kukutana na nguvu za kijeshi za Yazid kwa uwezo wake mwenyewe wa kijeshi. Hakujenga matumaini juu ya nguvu za idadi (kubwa ya watu) kwa mafanikio ya jambo lake (la haki) au juu ya njia zozote zile za kimaada. Husein aliamua kupigana vita na Yazid kwenye uwanja wa kiroho, kupinga maguvu ya Yazid kwa nji ya utukufu wa tabia yake, kuikabili nguvu kwa kutokuwa na maguvu, kukutana na makundi pamoja na ukosefu wa msaada wa nyenzo na kupinga dhulma kwa

(kukubali) kuteseka na kufa kishahidi.

Utajiri mkubwa ambao ulimiminika katika nchi za Waislamu ukiwa kama matokeo ya kutekwa nchi kulikofanywa na Waislamu na namna za maisha ya anasa ya watawala na matajiri, ziliwafanya wapuuze wajibu wao kwa Mwenyezi Mungu na wanadamu wenzao. Ilikuwa ni hatua fupi, rahisi tu kwa watu kwa kawaida kutwaa mielekeo ya wakubwa wao wa kijamii.

Mbali na kutoa huduma za maneno matupu kwenye itikadi fulani fulani za kiislamu, na utekelezaji wa kijuujuu tu wa baadhi ya matendo ya Kiislamu, ule moyo wa Kiislam kwa kweli ulikuwa umelala bwete katika jamii ya Waislamu.

Ili kuendeleza mamlaka yao, watawala wa Bani Umayyah walitafuta kuto- ka kwa Waislamu utii mkubwa kwa watawala wao. Hili lingeweza kufanikishwa kimya kimya bila kujitokeza kwa kuingiza ugoigoi katika welekevu wa akili na kuwanyima watu hamu na ujasiri wa kuzungumza.

Baadhi ya watu maarufu ambao hawakujitolea kuusaidia utaratibu uliowekwa katika kuendeleza njama hii ya ukimya, huu ufishaji wa uwezo wa kuhisi wa umma na huku kusimamishwa kwa muda kwa uhuru na ukweli wa kuelezea maoni, walipatikana wakifanya hivyo kwa kupewa misaada au kwa vitisho vya matokeo ya kuuawa kwao, na kampeni za kitaifa za kuwaondolea watu uwezo wa kufikiri kwa uhuru kabisa na ujasiri wa kuongea zilishamiri.

Mbinu kubwa ya al-Huseun ya kupinga utawala wa Yazid ilikuwa ni kuhuisha uwezo wa watu wa kuhisi, kuamsha ndani yao uwezo wa kujifikiria wenyewe kwa hali ya kuwa huru kabisa, na kuwarudishia ujasiri wa kutoa maoni kwa uhuru kwa uamuzi wa dhamira zao.

Bani Umayyah ambao kwa nje waliukubali Uislam, walijaribu kuuangamiza Uislam kutokea ndani kwa kupotosha mafundisho yake, na kuwanyima Waislamu uwezo wao wa kuhisi, na ujasiri wa kuongea. Husein, kwa hiyo alikusudia kuipasua barakoa ya Uislamu kutoka kwenye uso wa watawala wa Bani Umayyah ili kudhihirishia ulimwengu walikuwa mbali kiasi gani kutokana na kuzionyesha alama halisi za Uislam, na kuwatenganisha Waislamu kutokana na washauri wao waliopotoka ili kuviokoa vizazi vijavyo vya Kiislamu kutokana na kuitukuza mifano iliyowekwa na wao kwa jina la Uislam ili kwamba wakati wowote njia mbaya au ovu za Bani Umayyah zilipotajwa kwa kuushushia hadhi Uislam, tabia yake mwenyewe (Husein) na mwenendo vingeweza kutajwa mara moja kwa kuwaokoa Waislamu kutokana na fedheha.

Malengo ya Husein aliyokuwa nayo katika fikra yasingeweza kupatikana kama angepigana kwa msaada wa nyenzo. Vita vya namna hiyo hus- ababisha vifo vya watu na uharibifu wa mali, lakini siyo kuangamia kwa itikadi. Kuchinjwa kwa watu na kuangamizwa kwa mali vilikuwa siyo sehemu ya lengo la Husein, na kuangamia kwa itikadi ambako kulikuwa kunadhoofisha dini kusingeweza kupatikana kwa vita katika uwanda wa nyenzo na zana.

Aidha, vita inayopiganwa kwa msingi wa nguvu za kijeshi vingeweza pia kuchanganywa, kwa

kufananishwa na vita kati ya washindani wawili wanaogombea madaraka ambavyo vilikuwa mbali na ukweli kulingana na Husein alivyokuwa amehusika. Vita kama hivyo, kwa hali yoyote ile, vingekomea katika mafanikio kwa Yazid na huenda vingemwacha Yazid akiwa bado amefunikwa katika vazi la Kiislam, wakati vita vya Husein vilivyopiganwa katika uwanda wa kiroho, kwa kiasi vilimfedhehesha mtawala kiasi kwamba alipoteza huruma zote juu yake kutoka kwa wanadamu.

# Sura Ya 17: Kuondoka Husein Madina Na Kuchukua Hifadhi Huko Makkah

Husein aliondoka Madina mwezi 28 Rajab, mwaka wa 60 A.H, na akafika Makkah ndani ya juma moja tarehe 3 mwezi wa Shaaban.

Ingekuwa kinyume cha ushuhuda wa ukweli, ambao Husein lazima awe mwenyewe ameuona kufikiria kwamba kama angebakia kukaa Madina wenyeji wa mji huo wangemweka mbali asifikiwe na maadui zake, au wangetoka kuja kumpa msaada. Kwani baada ya kifo cha Mtume watu fulani wenye ushawishi, ambao walikuwa hawana mapenzi kwa Ahlul Bait wa Mtume (watu wa nyumba ya Mtume), walikuwa wamepata madaraka.

Hivyo ilikuwa kwamba wakati Mtume alipokuwa amefariki, binti yake, Fatimah, alihatarishwa kwa ufidhuli mwingi, madhara na kunyang'anywa mali yake mjini Madina. Ilikuwa tena ni hapo hapo Madina ambapo kwa kipindi cha robo karne (miaka 25) ilibidi Ali avumilie na kustahimili uchungu mkubwa sana wa masikitiko yake makali na kuzimwa kwa madai yake ya haki juu ya kumrithi Mtume, na pia kuvumilia kupuuzwa na kud- halilishwa. Hakuna faraja, hakuna msaada na hakuna neno la kutia moyo lililotolewa imma kwa Fatimah au kwa Ali, na mkazi yeyote yule wa Madina katika msiba wao.

Na halafu ilikuwa ni hapo hapo Madina ambapo Bani Umayyah walikuwa wametumia vurugu kuuzuia mwili wa Hasan usichukuliwe kwenda kuzikwa karibu na kaburi la Mtume. Hakuna mkazi wa Madina aliyenyanyua sauti yake katika kupinga dhidi ya udhalimu huu.

Ukweli huu na yaliyokuja kujiri baadaye yalionyesha kwamba kama Husein asingetazamia matatizo mjini Madina, na akaondoka kwenda Makkah, Marwan angemchochea Yazidi kuchukua hatua kali zaidi dhidi yake (Husein), ili kwamba damu ya Husein iweze kumwagwa katika mji wa Madina wenyewe. Barua zilizoandikwa kati ya al-Walid, gavana wa Madina, na Yazid zinaonyesha kwamnba jukwaa lilikuwa limekwisha andaliwa kwa ajili ya mauaji ya Husein. Al-Walid alikuwa ametoa taarifa kwamba: "… Husein haukubali Ukhalifa wako… sasa yote yanategemea juu ya ridhaa yako." Yazid alijibu, "Nitumie orodha kamili ya watu wote walio maarufu ambao wamekula kiapo cha utii kwangu, na pia ya wale ambao hawakufanya hivyo. Kichwa cha Husein bin Ali ni vizuri kifuatane na jibu lako." Jibu hili lilimfikia al-Walid

baada ya Husein alipokuwa amekwishaondoka Madina.

Kama Husein angeuawa mjini Madina, Bani Umayyah wangeliwasilisha tukio hili kama kadhia ya kawaida. Muhanga wa Husein ungewasilishwa katika hali isiyo na maana yoyote.

Muuaji wa kudharaulika kama Ju'da, bint ya al-Ash'ath au waasi fulani walioritadi kutoka kwenye Uislamu kama Ibnu Muljam, wangeweza kukodiwa kumuua Husein, ili kwamba lawama kwa kosa hilo isingeweza kuwekwa mlangoni mwa serikali ya Syria. Muhanga wa Husein pale Karbala, kama hali ilivyokuwa, ulimweka Yazid kizimbani, kama adui wa Uislamu, na kumfanya Husein kuwa mwokozi wa Uislamu huo.

Husein aliwachukua pamoja naye dhuria wote wa babu yake Abu Talib, na dada zake, Zainab na Umm Kulthumu. Muhammad bin al-Hanafiyya hakuambatana na Husein kwa sababu ya matatizo fulani, na Umm Hani, dada ya baba yake (shangazi yake), aliachwa nyuma kutokana na umri wake mkubwa (mzee). Mbali na kizazi cha Abu Talib, hapakuwepo na dhuria wengine wa Bani Hashim waliokuwa pamoja na Husein hapo Karbala.
Ukweli kwamba Husein alikuwa amewachukua pamoja naye wale ndugu tu, waliokuwa karibu naye mno ulidhihirisha kwamba yeye hakutiwa hamasa na shauku yoyote ya kivita wakati alipoondoka Madina. Kituo chake Makkah, kilikuwa pia kielekezi chenye nguvu sana kwenye upande huohuo, kwani Makkah kwa desturi ni mahali pa amani ambapo haparuhusiwi kutoa uhai wa kiumbe chochote kile cha Mwenyezi Mungu.

Hapo Makkah Husein aliishi *Shi'b-Ali* katika hali ya ukimya wa amani. Hakuwa na shauku ya kushughulikia na utawala wa masuala ya kila siku yahusianayo na sera za taifa. Hakujiingiza katika kufanya mawasiliano na mtu yeyote yule na hakuwashawishi watu kutoa misaada yao kwake.

Abdallah bin Zubeir ambaye alikuwa amewasili Makkah siku chache mapema zaidi kabla ya Husein alikwishaanza kuwavutia wageni kutokana na kule kujitokeza kwake kwa ghafla hapo (Makkah), na kwa hiyo alikuwa amepata nafasi ya umaarufu, ambayo aliipoteza mara tu kwa Husein wakati alipowasili mjini hapo. Abdallah bin Zubeir alizitambua sifa za daraja la juu sana za Husein na cheo chake kikubwa na akaona inafaa kumtembelea (Husein) kila wakati.

Husein alifanya makazi Makkah kama sehemu ya hifadhi. Kwa sura ya nje, kukaa kwake hapo kulikuwa kama kwa kudumu. Alikuwa hana lengo maalumu mbele yake. Ilikuwa ni ile fursa ya hifadhi tu ambayo Makkah ilikuwa inatoa kwake katika wakati uliomchukua Husein kwenda huko.

Na hili liliafikiana na ushauri uliotolewa kwake na Muhammad ibn Hanafiyya kwamba kama mambo yatageuka na kutoridhisha, basi aende Makkah au maeneo ya jangwani na maeneo mapana yasiyo na rutuba na maeneo makubwa ya milimani na kuhama kutoka mji hadi mji mpaka atakapoweza kuunda mawazo ya wazi juu ya mwelekeo wa watu ili kuweza kufikia uamuzi wa mwisho.

# Sura Ya 18: Mialiko Kutoka Kufa Na Ujumbe Wa Muslim Bin Aqil

Baada ya mafanikio ya Waislamu pale al-Qadisiyya, na katika viwanja vingine vya mapambano ilionekana kuwa ni muhimu kuliweka jeshi la Kiislamu katika makazi ya kudumu ndani ya Iraq. Mji wa Kufa ulichaguliwa kama sehemu ifaayo kwa ajili ya lengo hilo na msikiti na nyumba za kuishi watu zilitayarishwa hapo.[1] Katika mwaka wa 17 A.H Sa'd bin Abi Waqqas aliyahamisha makao yake makuu kutoka Madaini kuyapeleka Kufa ambayo kwa kuanzia yalikuwa na idadi ya askari wapatao laki moja.

Wakati Ali alipotawalishwa kuwa khalifa, na Aisha alipochochewa na Talha na al-Zubeir, yeye (Aisha) alisimama kupigana dhidi ya Ali katika yale maasi ya Basra. Alishindwa katika vita vilivyojukana kama 'Vita vya Ngamia.' Ilikuwa ni baada ya tukio hili ndipo alipoufanya mji wa Kufa kuwa makao ya serikali yake, katika mwaka wa 36 A.H.

Baadaye katika Vita vya Siffin dhidi ya Mu'awiyah, na katika Vita vya Nahrawan dhidi ya Makhawarij (wale waliojitenga naye), wenyeji wa Kufa kwa sehemu kubwa sana walipigana wakiwa katika upande wa Ali hivyo kwamba walikuja kufahamika kama Shia wa Ali.

Ilikuwa siyo kwamba wote katika wao walikuwa katika imani ya Kishia kwamba hakuna mtu yeyote aliyeingilia katika suala la Ukhalifa kati ya Mtume na Ali, bali wao walipendelea kuitwa Shia (wafuasi) wa Ali kuliko kuitwa Shia wa Bani Umayyah.

Hata hivyo, mara tu Mu'awiyah alipopata udhibiti wa nchi za Kiislamu na Ziyad bin Abihi alipoteuliwa kuwa gavana wa Kufa, enzi ya hofu kubwa ilianzishwa dhidi ya Shi'a; hakukuwa na nafasi kwa ajili yao katika Iraki, na kwa kweli ilionekana kila pumzi waliyoivuta iliwezekana kwao kuwa ni pumzi yao ya mwisho. Na maisha haya ya dhiki kubwa yalidumishwa kwa kipindi ambacho si chini ya miaka ishirini.

Katika hali hizi za mtihani mgumu mno, imani (itikadi) ya Kishia ilikuja kufungika kwa siri ndani ya kikundi kidogo sana cha watu ambacho kilikuwa kinapitisha siku zake katika hatari kubwa sana katika miji mbalimbali ya Iraki na Hijaz katika hali ya kutokuwa na jina kabisa.

Katika mwezi wa Rajab mwaka wa 60 A.H, Mu'awiyah alifariki dunia, na alirithiwa katika nafasi ya Ukhalifa na mwanawe Yazid, ambaye tabia zake za kiuovu, ubobeaji kwenye ulevi, tamaa ya uzinifu, kutojali kabisa makatazo ya dini na staha zake vilikuwa vinafahamika sana miongoni mwa watu. Hisia ya jumla ya chuki kubwa na maudhi iliwashika watu wote, na usakaji wa kutumia akili unaelekea kuwa ulikwishaanza kwa ajili ya mtu ambaye angeweza kuwaokoa waumini kutokana na khalifa huyu wa sifa mbaya na tabia ya kuchukiza.

Msako huu lazima utakukwa umepata mwelekeo wa uhakika kutokana na kile ambacho lazima

kingekuwa ni ufahamu wa kawaida kwa wote kwa wakati huo, kwamba mjukuu wa Mtume alikataa kutoa kiapo cha utii kwa Yazid, na alikuwa ameondoka kwenda Makkah.

Ilikuwa ni katika mazingira ya namna hii kwamba baadhi ya marafiki wa Ali, wakiuona mwanga wa matumaini ya nusura yao kutoka kwa madhalimu wao, walikutana katika nyumba ya Suleimani bin Surad, sahaba wa Mtume, mtu mwenye uzoefu mwingi na mkongwe aliyepigana vita vingi akiwa pamoja na Ali.

Akitoa maoni yake kwa mpangilio mzuri sana, alitaja habari za kifo cha Mu'awiyah, na kukataa kwa Husein kutoa kiapo cha utii kwa Yazid kama mrithi wa Mu'awiyah kwenye Ukhalifa. Aliongeza kwamba Husein alikuwa ameondoka kwenda Makkah.

Aliwaambia marafiki zake kwamba kama wangekuwa na uhakika kwamba katika mazingira ya namna yoyote watakayokuwa wasingezembea katika kumsaidia Husein, na katika kupigana dhidi ya maadui zake, wangeweza kuwasiliana naye. Aliwaonya kwamba kama wanatambua ugoigoi wowote wa jitihada au udhaifu wa lengo kwa upande wao, wasije kwa hali yoyote ile, wakahatarisha maisha ya Husein kwa kuzua matumaini ya uwongo.[2]

Wakati muda ulivyozidi kupita baadhi ya wale waliokuwepo walionekana kukadiria kupita kiasi uwezo wao wa kutenda kwa maneno yao, kwani wote kwa pamoja kwa kauli moja walitamka dhamira yao ya kuwapiga maadui wa Husein mpaka wao wenyewe wawe wamekufa kwa kutoa muhanga maisha yao kwa ajili ya Husein.[3] Barua ilipelekwa kwa Husein ikisema:

"Barua hii imeandikwa kwa Husein bin Ali kwa niaba ya Suleiman bin Surad, al-Musayyab bin Najaba, Rifa'a bin Shaddad, na Habib bin Muzahir, na marafiki wengine kutoka miongoni mwa Waislamu na waumini wa Kufa."

Kisha ilishughulika na kifo cha Mu'awiyah na urithi wa Yazid na ikaendelea kusema; "Hakuna Imam juu yetu. Tafadhali njoo, kwa kupitia kwako Mungu anaweza kutuunganisha kwenye haki."

Barua hii ilikuwa ya kwanza kupokewa na Husein ambaye aliipata tarehe 10 mwezi wa Ramadhani. Wale ambao kwanza walikuwa wamekutana Kufa nyumbani kwa Suleiman bin Surad ndipo kwa siri walilitangaza vuguvugu lao kiasi kwamba ndani ya siku kadhaa si chini ya maombi ham- sini yaliandikwa. Kila moja lilitiwa sahihi na watu kati ya mmoja hadi wanne.

Mfadhaiko wa kiroho ulioingia kwa wote kwa ujumla, bila kujali dini au madhehebu ambayo mtu alihusika nayo, juu ya urithi wa Yazid kwenye Ukhalifa ulilifanya pendekezo la Suleiman bin Surad na marafiki zake likubalike kwa kila mtu.

Hata wale ambao hawakuwa na itikadi za Kishia waliliunga mkono pendekezo hilo kwa bidii sana, siyo kwa sababu ya imani yoyote ile juu ya uongozi wa Husein, bali kwa sababu ya kuamini kwamba bila shaka yoyote ile yeye (Husein) alikuwa bora zaidi kuliko mtu mlevi kama Yazid.

Al-Dinawar anasimulia kwamba maombi yote haya na barua na wachukuaji wao zilimfikia Husein moja baada ya nyingine ndani ya siku mbili, na baada ya siku chache wingi wa mawasiliamo ya kuandikiana ulizidi sana kiasi cha kujaza mifuko miwili ya shogi.[4]

Khutba ya Suleimani bin Surad na uchunguzi wa yale yaliyojiri baadaye humfanya mtu kuhitimisha kwamba Husein:

i) Hakukataa kutoa kiapo cha utii kwa Yazid na baadaye akaondoka kwenda Makkah kutokana na vichocheo vyovyote vile kutoka nje au uelewa wa mapema sana ulio wa siri na wakazi wa Kufa;

ii) Alikuwa wala hakufikiria kwenda Kufa wakati alipokuwa anaondoka Madina; na

iii) Hakuanzisha vuguvugu lolote lile kwa ajili yake miongoni mwa wenyeji wa Kufa, na hakufanya mawasiliano na mtu yeyote hapo kueneza maoini yake.

Ni njia ipi Husein angeichukua wakati alipopata idadi kubwa ya maombi kutoka Kufa yakimtaka kwenda kwenye mji ule ili kuwaongoza? Bila shaka kulikuwepo na baadhi ya watu kama Abdalla bin Abbas, ambaye alijaribu kumshawishi asijitolee kufanya safari hiyo ya kwenda Kufa kwa sababu ya kwamba hakuna matumaini yanayoweza kutarajiwa juu ya ahadi zilizofanywa na watu wa Iraq. Husein alikuwa amedhamiria kutotoa kiapo cha utii kwa Yazid. Hili lilihatarisha maisha yake hapo Madina ambapo yeye aliondoka na kwenda Makkah.

Kukaa kwake Makkah kungeweza kumpatia angalau kuahirishwa kwa madhara kwa muda kiasi, kwani Yazid asingeweza kwa njia yoyote ile kutegemewa kuacha kutumia nguvu dhidi yake ndani ya Makkah yenyewe. Aidha, mbali na ukweli kwamba kuondoka kwake kutoka Madina lazima kuwe kumefahamika sana hakupata ahadi yoyote ya kupata msaada, au mwaliko wowote ule kutoka at-Taif au Yemen, Basra au Yamama. Ule mwaliko kutoka Kufa ulichukua umuhimu maalum kwa ajili ya Husein katika wakati huu wa hali ya hatari kwake yeye.

Lilikuwa ni jambo la hiari na limekuja kutoka kwa marafiki na maadui pia na liliungwa mkono na maombi si chini ya hamsini na tano na mifuko miwili ya shogi iliyojaa barua. Lilianzia Kufa, kituo muhimu sana katika eneo lenye kukaliwa na watu wengi mno la Uarabuni, na ombi la kwanza kumfikia yeye lilikuwa na sahihi za akina Habiba bin Muzahir, Suleiman bin Surad na Rifa'a bin Shaddad watu ambao kwao yeye Husein alikuwa na imani thabiti juu yao. Wakazi wa Kufa pia walimsaidia baba yake, Ali, katika Vita vyake.

Katika majibu kwa wale ambao walisisitiza juu ya kutokutegemeka kwa watu wa Kufa ili kumshawishi kuacha kujitolea kufanya safari kwenda Kufa, Husein kamwe hakusema kwamba aliweka matumaini katika ahadi zilifanywa na watu wa Iraq, au kwamba wao kwa hakika wengemsaidia kama angekwenda Kufa. Kwa kawaida alidumisha ukimya juu ya jambo hili.

Wakati mwingine alidokezea kwa uwazi kabisa kwamba hata kama angerefusha ukaaji wake mjini

Makkah kwa hakika atakuja kuuawa, na kwamba hapo basi ingekuwa ni kwa sababu yake yeye kwamba Ka'aba ingekuwa imenajisiwa, kama wakati alipomwambia Abdallah bin Zubeir, "Baba yangu aliniambia kwamba kutakujakuwepo na mtu kama kondoo dume ambaye atakuja kusababisha kunajisiwa Ka'aba.

Mimi sipendi kuwa kondoo dume huyo."[5] Katika wakati mwingine alisema, "Naapa kwa Mwenyezi Mungu kwamba inaridhiana nami zaidi kuuawa katika kipimo cha shubiri moja nje kuliko shubiri moja ndani ya eneo la Ka'abah, na Wallahi, kama ningekuwa niishi ndani ya kishimo cha mdudu mharibifu, watu hawa watanitoa ili waweze kunifanyia mimi lile wanalolitaka. Naapa kwa Mwenyezi Mungu kwamba watu watatenda mengi zaidi dhidi yangu kama vile Mayahudi walivyovuka mipaka dhidi ya Sabato."[6] Katika hali ambayo ndani yake mambo kwa sura ya nje yalijidhihirisha yenyewe ilionekana kuwepo nafasi ndogo kwa Husein isipokuwa kukubali maombi yaliyoandikwa kwake na miito iliyotolewa kwake kutoka Kufa, kwa ajili ya lengo lile lile lililosifika la kuwaongoza wakazi wa mji huo kiroho, kimaadili na kidini.

Hata hivyo, hakuonyesha haraka isiyostahili katika kujitolea kuutekeleza ujumbe huu. Alichukua hatua za tahadhari za kumpeleka binamu yake, Muslim bin Aqil, ambaye alikuwa amefuatana naye kutoka Madina, kama mwakilishi wake kuichunguza hali ilivyo[7] huko na kumtaarifu makadirio yake mwenyewe kuhusu hilo.

Husein, hata hivyo alipeleka barua kwa wakazi wa Kufa kupitia kwa Hani ibn Hani na Sa'id bin Abdallah, kabla hajatoka kuuendea mji ule. Ilisema; "Hani na Sa'id wameleta barua zenu kwangu, na watu wote wawili hawa waliotumwa nanyi ndiyo wajumbe wenu wa mwisho kuja kwangu. Nimezisoma kwa makini sana na kuelewa yale mliyoniandikia.

Wengi wenu mnaniita nije kwenu mwenyewe kwa vile hamna Imam wa kukuongozeni, ili kwamba Mwenyezi Mungu aweze kuwaunganisheni kupitia kwangu.

Kwa hiyo, ninamtuma kwenu binamu yangu mtoto wa ami yangu, kama mtu ambaye kwake yeye naweka dhamana yangu maalumu ili kuniarifu juu ya masuala yenu. Kama atanitumia neno la kwamba safu zenu na wale walioko kwenye uongozi wa mambo yenu zimeungana kuhusu yale mliyoyasema ndani ya barua zenu, basi nitajiunga nanyi hivi punde ..."[8]

Inaonekana kwamba balaa ilizikumba hata zile hatua za mwanzo za safari ya Muslim kwenda Kufa. Alikuwa amewakodi watu wawili kama waongoza njia wake na walikuwa wameizoea sana njia hiyo ya kwendea Kufa. Wote hawa waliipoteza njia yao, na wakatangatanga ndani ya jangwa na angalau mmoja katika wao,[9] kama si wote wawili,[10] alikufa kwa kiu.

Ilikuwa ni kwa taabu kubwa kwamba Muslim na sahaba zake walikuta kijito ambapo hapo alielezea bahati yake mbaya kwa Husein, akiongezea kusema kwamba hakuwa na moyo wa kuendelea na safari yake zaidi ya hapo. Hata hivyo, ilibidi aendelee katika safari yake yenye mkosi kwa maelekezo ya Husein. Alipofika Kufa, ilimbidi Muslim akae nyumbani kwa al-Mukhtar bin Abi Ubayd al-Thaqafi[11] kwa vile Suleiman bin Surad alikuwa ametoka nje ya mji.

Habari za kuwasili kwa Muslim zilienea na zikapokelewa vizuri kila mahali. Wageni walimiminika kuja kumwona, na Muslim aliisoma barua ya Husein kwenye mkusanyiko wa kundi kubwa la wale ambao walikuja kuonana naye.

Hii ilisababisha kudhihiri kwa ari yenye hamasa nyingi kwa wasikilizaji waliokuwa wakihutubiwa na Abis bin Abi Shabib al– Shakir, Habib bin Muzahir na Sa'id bin Abdallah al–Hanafi. Wazungumzaji, kila mmoja akitoa maoni yake binafsi walimhakikishia Muslim dhamira yao ya kupigana katika upande wake dhidi ya maadui wake, na kushambulia kwa panga zao mpaka wote wawe wamekufa, lengo lao likiwa tu ni kutafuta radhi za Mwenyezi Mungu. Kisha mkusanyiko huo ulitawanyika.

Mfarakano wa watu na Yazid kutokana na tabia zake za kiovu, umaarufu wa Husein kwa sababu ya utukufu wa familia yake na ubora wake mwenyewe wa tabia na elimu, maarifa na ujuzi, na jina zuri na nafasi yenye mvuto na ushawishi katika jamii ya wanaoendeleza harakati kwa upande wake zilikuwa miongoni mwa sababu kubwa ambazo ziliwavutia wakazi wa Kufa wapatao 12,000[12] au 18,000[13] ndani ya kipindi cha wiki moja kuja kutoa kiapo cha utii kwake katika mikono ya Muslim.

Je, watu wote hawa walikuwa marafiki wa Ali? Je, idadi kubwa kama hii ya marafiki wa kweli wa Ali wangeweza kubakizwa mjini Kufa wakati wa utawala uliochukuwa zaidi ya miaka ishirini ya Ziyad na kizazi chake wakati watu walikuwa wanauawa kwa upanga bila haya kwa kuonyesha dalili japo ndogo tu za upendo kwa Ali? Jibu lazima liwe la wazi la kukataa kwa nguvu.

Shi'a wa kweli walikuwa wachache kwa idadi hata huko nyuma zaidi na walikuwa takriban wameangamizwa na Mu'awiyah na Ziyad. Wale tu Shi'a wachache kabisa ambao walifanikiwa kujificha wenyewe ndio waliokwepa kufa. Wengine wote ambao walimfanya Ali kama Khalifa wa nne pia walionekana kuwa ni Shi'a kwa maana halisi tu ya neno hilo kwa sababu ya ushirikiano wao naye. Kwa kawaida, uungaji mkono wa watu wa namna hii, na wengineo ambao, wanaweza kuwa wamevutiwa tu na harakati hizi kwa sababu ya kuanzisha kwake jambo mpya, ulikosa umadhubuti.

Haishangazi kwamba wakati waendelezaji wa harakati hizi, waliozaliwa kulelewa mjini Kufa, walishindwa kugundua udhaifu wa msingi ambao juu yake uungaji mkono wa sehemu kubwa ya watu wa mji wao uliegemea, Muslim naye pia alikuwa amechukuliwa na vuguvugu la mapokezi mazuri aliyofanyiwa na watu wote wa mji huo. Viongozi watangazaji wa harakati hizi kwa ajili ya Husein, hata hivyo walisimama imara kwa neno lao la ahadi, na wakalipa kishujaa kwa maisha yao kwa ajili ya kumuunga mkono yeye.

Alipoona kwamba watu wa Kufa walitenda kwa mujibu wa ahadi zao, Muslim alimwandikia Husein akimwomba aharakishe uondokaji wake kuja Kufa.[14] Gavana wa mji huo, al–Nu'man bin Bashir, alifanya uvu– milivu na akatangaza kutoka kwenye mimbari kwamba asingechukuwa hatua yoyote mradi tu hapingwi kwa ushari na uchokozi.[15]

Mshirika mmoja wa Bani Umayyah hakuupenda msimamo huu wa gavana wenye hisani juu ya Muslim, na aliandika kwa Yazid akilalamika dhidi ya ushuhu– likiaji wa kinyonge wa gavana kuhusu hali ya Kufa ambako Muslim bin Aqil alikuwa amefika na wafuasi wake wenye kumuunga mkono wametoa kiapo cha

utii kwa Husein. Alipendekeza kwamba al-Nu'man bin Bashir abadilishwe na mtu shupavu mwenye mabavu, kama Yazid alikuwa anataka kuubakiza (mji wa) Kufa katika milki yake.

Umara bin Uqba na Umar bin Sa'd pia waliandika kwa Yazid kuhusu jambo hilo hilo na matokeo yake yakawa kwamba Yazid aiandike barua kwa Ubaydullah bin Ziyad akisema; "................Muslim bin Aqil amefika Kufa na anaunda jeshi ili kuchochea mfarakano na kutokuelewana miongoni mwa Waislamu. Nenda Kufa haraka sana mara tu uipatapo barua hii na ukisha mkamata Muslim, ama umfunge, umkate kichwa au mhamishe."16

Barua hii ilipelekwa pamoja na amri ya kumteua Ubaydullah bin Ziyad kama gavana wa Kufa. Ubaydullah aliondoka Basra, ambako alikuwa kazini kama gavana akaenda Kufa haraka sana.

Alizifanya nyendo zake kwa hali ya siri sana, ili kwamba kuwasili kwake mjini Kufa kuwe kwa yote mawili; kwa kutotegemewa na kwa ghafla. Ili kuweza kusafiri kupitia jangwani, alikuwa amezungusha kipande cha kitambaa usoni mwake kuulinda na mchanga. Alionekana mwenye kupendeza kiasi, akiwa amepanda juu ya farasi ya Kiarabu, aliyevaa vazi jeusi kichwani la Mwarabu muungwana, na akifuatiwa na msafara.

Kwa vile watu wakati huo walikuwa wanasubiri kuwasili kwa Husein, walifikiri kwamba alikuwa ni mjukuu wa Mtume ambaye alikuwa amewasili mjini hapo, na watu walikuwa wamemiminika kutoka pande zote kuja kumsalimia kwa wingi kama hivyo.
Ubaydullah aliendelea na njia yake bila ya kuitikia salamu hizo. Ummati wa wale ambao walikuja kumkaribisha yule ambaye walikosea wakamdhania ni Husein, walizuia kuendelea mbele kwa Ubaydullah na Muslim bin Amr al-Bahili ambaye alifuatana naye alisema kwa sauti kubwa, "Pisheni njia, yeye ni Ubaydullah bin Ziyad."

Fazaa ikabadilisha haraka sana ile hali ya furaha ya watu. Kumbukumbu za ukatili wa kinyama wa Ziyad ulioendelea kwa kipindi cha zaidi ya miaka ishirini lazima itakuwa imehuishwa kwa kutokea mtoto wake na mamlaka ya baba yake. Ubaydullah alitangaza kuteuliwa kwake kama gavana wa Kufa mbele ya mkusanyiko wa watu ndani ya msikiti wa Jamaa.

Kisha aliwataka watu wote wenye kuwajibika na sehemu mbalimbali za makazi katika Kufa kumpatia orodha ya wakazi wote wa sehemu zao husika wakitaja na kueleza bayana majina ya wageni na ya wale ambao waliweka tishio kwa serikali ya Syria.

Kama wasingeweza kumpatia orodha hizo kwa maelezo ya kina, basi walitakiwa watoe ahadi kwamba hakuna mtu yeyote katika sehemu yao ya Kufa ambaye angejiingiza katika shughuli yoyote ile ya uchochezi. Endapo utatokea uvunjaji wa ahadi hii, mkuu wa sehemu hiyo ya mji inayohusika atanyongwa mbele ya nyumba yake mwenyewe.17

Hatua hii kali ilileta ndani ya mfuatano wake wingi kupita kiasi wa wapelelezi na watoa habari, na maisha mjini Kufa yakawa hayana usalama kabisa. Watu walikuwa wanaogopa kutoka nje ya nyumba zao na

kuwa– tembelea marafiki. Mikutano na majadiliano hata katika vikundi vidogo vidogo sana juu ya suala lolote lile havikuwezekana hata kufikiriwa.

Akiwa ni mwenye wasi wasi juu ya usalama wa maisha yake na kudumu kwa ujumbe wake, Muslim aliacha kuendelea kukaa nyumbani kwa al–Mukhtar bin Abi Ubayd al–Thakafi, ambaye mbali na kuwa nje ya Kufa, hakuwa tena na nguvu kubwa ya ushawishi wa kutosha. Alihamia kwa Hani bin Urwa, mkuu wa kabila lake. Hani alifanya kukaa kwake na Muslim kuwa na ulinzi wa karibu sana na wa siri, akikushirikisha tu na watu wake wanaoaminika sana.

Kwa kuzingatia hatari inayoweza kutokea karibuni ya matumizi ya nguvu dhidi ya Muslim bin Aqil, wasimamizi wa harakati za kumwita Husein kuja Kufa kwa ghafla walibadilisha lengo lao la kutoa msaada wote uwezekanao kwa Muslim ili kupata kutoka kwa watu wa Kufa lile neno lao la ahadi kwa ajili ya Husein ili waweze kuchukua hatua za kumlinda Muslim kutokana na hatari ambayo ilitishia maisha yake. Muslim bin Awsaja aliyejishughulisha katika kupata ahadi kutoka kwa watu kwa ajili ya msaada na ulinzi wa Muslim bin Aqil na Abu Thumama al–Sa'di alichukua wajibu juu yake mwenyewe wa kukusanya silaha na fedha kwa ajili ya lengo hilo.[18]

Ubaydullah bin Ziyad alikuwa na shauku sana ya kugundua mahali ambapo Muslim bin Aqil alipokuwa amejificha, na akamtuma mtumwa wake, Ma'qil kutafuta mahali gani Muslim alikokwenda kujificha. Ma'qil alikwenda kwenye msikiti wa jamaa kubwa na, kwa bahati nzuri tu, alimwona Muslim bin Awsaja akisali pia.

Kwa vile Muslim bin Awsaja alichukua muda mrefu kumaliza swala zake, Ma'qil alimsubiri, na akamwambia kwamba yeye alikuwa ni Msyria mwenye kuwapenda sana watu wa Nyumba ya Mtume, na amesikia kwamba mtu mmoja atokanaye na familia ya Mtume amewasili mjini hapo na kwamba alikuwa anachukuwa viapo vya utii kwa ajili ya Husein.

Alitoa dirham 3,000 na akasema alipenda kuzitoa pesa hizo kwa mwakilishi wa Husein kama atajua mahali alipokuwa. Yote haya yalisemwa na Ma'qil katika namna ambayo ilipandikiza imani kamili katika unyenyekevu wake na alifanikiwa kumdanganya Muslim bin Awsaja katika kumchukua yeye na kumpeleka kwa Muslim bin Aqil. Ma'qil, katika matembezi yake ya kirefu mara kwa mara kwa Muslim bin Aqil, alikusanya taarifa kamili kuhusu lengo la Muslim bin Aqil kutembelea Kufa. Alizifikisha habari zote alizozikusanya kwa Ubaydullah bin Ziyad.[19]

Hani bin Urwa kwa muda mrefu alikuwa amezoeana na Ubaydullah bin Ziyad, lakini siku za karibuni alikuwa anakwepa kumwona kwa kisingizio cha ugonjwa isijekuwa Ubaydullah bin Ziyad akapata fununu ya ukaaji wa Muslim bin Aqil pamoja naye. Katika kupata habari hizi kupitia kwa Ma'qil, Ubaydullah aliamua kumwita Hani kuja kwenye kasiri la gavana.

Bila ya kutambua hatari yoyote ile, Hani alikwenda kumwona Ubaidullah akiwa peke yake bila kufuatana na askari wake, na bila ya kumwarifu mtu yeyote yule kuhusu wito wa Ubaydullah.

Aligundua kwamba msimamo wa Ubaydullah kuhusu yeye ulikuwa umebadilika kabisa wakati alipomwambia Hani, “Ni fedheha kiasi gani hii kwamba wewe umeifanya nyumba yako kuwa mahali pa fitna ya njama dhidi ya Khalifa wa wakati huu na dhidi ya Waislam wote.

Umemwita Muslim bin Aqil na umekuwa ukimkirimu nyumbani kwako, ukimkusanyia silaha, ukiandikisha watu kwa ajili ya msaada wake na kuwaweka kwenye nyumba zilizoko kwenye ujirani wako. Je, unafikiri mambo haya yangebakia kufichika kwangu?”[20]

Hani baada ya hapo mwanzo kuukana ukweli wa madai haya, alitambua, wakati Marqi alipoletwa, kwamba alikuwa akipelelezwa na akasema, “Sasa sikiliza ukweli na uniamini.

Namwomba Mungu awe shahidi yangu kwamba sikumwita Muslim bin Aqil, wala sikuwa nikitambua harakati yoyote ile kwa upande wake, alikuja kwangu kwa uchaguzi wake mwenyewe, na akaelezea hamu ya kukaa nami. Sikuweza kwa heshima kukataa kumkaribisha nyumbani kwangu. Kwa hiyo, mimi nilimpokea kama mgeni kuja kukaa chini ya paa langu.

Hata hivyo, ninaahidi, sitotenda tendo lolote la uchokozi dhidi yako; na nitajiweka chini yako kwa sasa. Hata hivyo, kabla sijafanya hivyo, nataka ruhusa kwako ili nimwambie Muslim atoke nyumbani kwangu na aende popote pale atakapofikiria kwenda, ili kwamba niweze kujitoa kwenye wajibu wangu wa kumpatia hifadhi. Hapo tena nitakuwa sina la kuhusiana naye.”[21]

Ubaydullah, hata hivyo, alisisitiza kwamba Muslim bin Aqil akabidhiwe kwake na akapendekeza kumtia Hani mbaroni na azuiliwe mpaka wakati huo. Hani alielezea wazi kwamba ilikuwa haiwezekani kwake kumtoa mgeni wake kwenye kifo cha dhahiri. Mabishano kati ya wawili hawa yali- pamba moto kiasi kwamba Ubaydullah alimpiga Hani usoni kwa fimbo, na damu ilitiririka kutoka mahali palipojeruhiwa. Kisha Hani alitupwa gerezani.[22]

Amr bin Hajjaj, shemeji yake Hani bin Urwa na mkuu wa kabila la Zubayda alilizunguuka jumba la gavana na kundi kubwa lenye kumfuata la wapanda farasi waliposikia uvumi kwamba Hani alikuwa ameuawa. Waliondoka tu pale kadhi Shuraydi alitangaza kwamba Hani alikuwa amewekwa kizuizini kwa muda tu.[23]

Je, ingekuwa inafaa kwa Muslim bin Aqil kubakia mafichoni hata katika hatua hii, au kuhatarisha zaidi usalama wa rafiki yake mwingine mwamini- fu kwa kutafuta hifadhi kwake? Njia zote mbili hizi zilikuwa hazikubaliki kwa mujibu wa kanuni za uungwana wa Bani Hashim. Tabari ameeleza kwa uwazi kabisa kwamba Muslim alitoka kwenda kupigana na maadui zake bila ya kuwataarifu marafiki zake au bila ya kuwepo hapo mata- yarisho yoyote yale.

Wakati Ubaydullah bin Ziyad alipokuwa anatoa hotuba ya vitisho huko msikitini, watu walimiminika kuingia ndani na kutangaza kwamba Muslim bin Aqil amewasili. Ubaydullah kwa haraka sana aliteremka chini kutoka kwenye mimbari na akajifungia ndani ya kasiri lake.

Akiufikiria mgeuko wa ghafla na usiotegemewa ambao matukio yalichukua hapo Kufa, isingeweza kutumainiwa kwamba watu 18,000 ambao walikuwa wametoa ahadi ya kiapo cha utii kwa Husein mikononi mwa Muslim bin Aqil wangeweza kukusanyika kumzunguuka katika wakati huu wa hatari kubwa ya kutisha. Wafuasi hawa walikuja kutoka sehemu mbalimbali za mji.

Sehemu hizi zilikuwa na umbali kidogo kuto- ka sehemu moja hadi nyingine na habari za yanayotokea katika sehemu moja zilichukua muda kuzifikia zile sehemu za mbali zaidi.

Wengi wa wafuasi hawa walikuwa si watu wenye kufikiri, na walikosa unyofu wa imani na upendo wao kwa watu wa nyumba ya Mtume ulikuwa haujapata mtihani. Katika eneo ambalo ndani yake Muslim bin Aqil amepata hifadhi, watu 4,000 kati ya hawa wenye kuwaonea huruma waliishi, na waliposikia ukelele wa vita wa Mtume walijitokeza. Wakiwa hawakujiandaa na hawakupata mafunzo yoyote hawakuweza kukabiliana na majeshi ya kawaida ya serikali. Wakati Muslim alipowaongoza kushambulia makazi ya gavana alikuwa na watu 300 tu, na kati ya hao hakuna aliyebaki naye alipofika mwisho wa safari yake.

Ubaydullah ibn Ziyad alikuwa tangu asubuhi amewazuilia wakuu (watemi) wa kikabila na watu wengine mashuhuri pamoja naye kama hatua za tahadhari. Alifunga pia vituo vyote vya njia ziingiazo mjini na iendayo kwa Muslim bin Aqil, ili kuzuia msaada kutoka nje kumfikia na kuwaweka wale walioko mjini katika hali ya kushindwa kuungana naye. Msaada wote ulikuwa umekatwa usimfikie ili kwamba hata wale watu watiifu wakuu wenye uthabiti usio na wasiwasi kama vile Habib bin Muzahir, Muslim bin Awsaja na Abu Thumama al-Sa'idi wasiweze kufanya mawasiliano na Muslim bin Aqil katika siku ile ya msiba.

Watemi mbalimbali wa kikabila walipanda juu kwenye mapaa ya makazi ya gavana na wakawasihi wenye kumuunga mkono Muslim bin Aqil kutawanyika, wakitangaza juu ya viapo vyao kwamba jeshi kubwa karibuni lingefika kutoka Syria na lingewasagasaga na kuwaangamiza waunga mkono wote wa Muslim bin Aqil. Matokeo yalikuwa kwamba ni watu 30 tu walibaki na Muslim ulipofika wakati wa jioni. Hata watu hawa walimwacha wakati alipoondoka kwenda kwenye swala ya jioni msikitini.[24]

Akitangatanga peke yake, na akiwa anatafuta mahali pa kujipatia hifadhi, Muslim alifika baada ya kuingia usiku kwenye nyumba ya Taw'a, kijakazi mwachwa huru wa Muhammad bin al-Ash'ath, ambaye alikuwa na mtoto wa kiume, Bilal. Alimpatia Muslim chumba nyumbani mwake baada ya kuyapata maelezo ya kuhuzunisha. Wakati mtoto wake alipofika wakati wa usiku wa manane, alilazimika bila kupenda kuelezea utambulisho wa Muslim kwake. Alimsihi mwanawe aitunze siri hiyo mwenyewe kwa makini kabisa.

Wakati Ubaydullah bin Ziyad alipoona kwamba hatari imepungua nguvu, alituma itangazwe kwamba kila mtu lazima awepo msikitini, akiongeza kwamba kutoitekeleza amri hii kutaindolea serikali wajibu kwa ajili ya usalama wa mtu anayehusika. Amri hii ilisababisha kujaa sana msikiti hata kabla ya kufika wakati wa swala za usiku (Magharibi na Isha).

Baada ya swala hizo Ubaydulah alitangaza kwamba asingewajibika na usalama wa mtu yeyote yule

ambaye nyumbani mwake atakutwa Muslim bin Aqil akiwa amejificha humo, na kisha akaanzisha msako wa kumtafuta Muslim kutoka nyumba hadi nyumba.

Mtoto wa Taw'a, Bilal, alikwenda kumwona Abd al-Rahman, kijana wa Muhamad bin al-Ash'ath wakati wa alfajir na akamwambia kuhusu kuwe- po Muslim nyumbani kwake. Abd al-Rahman aliwasiliana na baba yake na huyo baba yake akazitoa habari hizi kwa Ubaydullah bin Ziyad ambaye alipeleka kikosi chini ya Muhamad bin al-Ash'ath kwenda kumkamata Muslim na kumfanya mateka.

Akiwa anapigana peke yake, Muslim alifanikiwa mara mbili katika kuwatupa askari hao nje ya nyumba ya Taw'a. Katika harakati hizo za kupigana mmoja wa midomo yake ulikatwa na ule mwingine ukajeruhiwa, na meno yake mawili yakang'olewa.

Walipoona kwamba mitindo ya kawaida ya kupigana ilikuwa haina matokeo mazuri, watu walipanda juu ya paa la nyumba na kumtupia mawe Muslim. Walimtupia pia vitita vya matete yaliyowashwa moto kumfanya apate majeraha ya kuungua.

Akishambuliwa kwa njia hii, Muslim alitoka nje ya nyumba kupigana kwa upanga wake. Muhamad bin al-Ash'ath alimwita akisema kwamba angepata ulinzi na usalama na akamtaka aache kupigana. Muslim, hata hivyo hakuisimamisha vita na alisoma beti zinazomaanisha ya kwamba, "Nimekula kiapo nisiuawe kwa upanga isipokuwa nikiwa kama mtu huru. Kifo, kwa kweli, ni kitu kisichopendeza, lakini kwa kila mtu lazima siku moja kitamjia. Nahofia nisije nikaambiwa uwongo na kulaghaiwa."

Akiwa amechokeshwa na mapigano kama alivyoonekana Muslim aliuliza kama kweli ulinzi na usalama ungeweza kutolewa. Muhamad bin al-Ash'ath na washirika wake wote, isipokuwa mmoja tu ambaye alikataa, walimhakikishia Muslim kwamba alikuwa salama, Muslim aliwaambia tena wakumbuke kwamba alikuwa anaweka upanga wake ndani ya ala yake kwa sababu tu amepewa usalama, vinginevyo asingejitoa mwenyewe kwao. Muslim alipewa farasi wa kumpanda. Kisha askari wakamzunguuka na kumpokonya upanga wake.

Kitendo hiki kilimvunja moyo Muslim kikiwa kama usaliti wa kwanza wa dhamana yake (aliyoahidiwa). Halafu alianza kulia, na alipoulizwa sababu ya kulia alisema, "Naapa kwa Allah, sijililii mimi binafsi, bali moyo wangu unayeyuka kwa ajili ya Husein na sahaba zake ambao watatoka kuja Kufa baada ya kupata barua yangu."

Kisha alimtaka Muhammad bin al-Ash'ath kumwarifu Husein kwamba Muslim amechukuliwa mateka na maadui zake na alitegemewa kuuawa jioni hiyo, na kumwomba asifikirie juu ya kuja Kufa, na asidanganywe na ahadi zili- zofanywa na wakazi wa mji huo kwani zote zilikuwa za uwongo, na map- atano yao na shughuli zao vyote hivyo vilikuwa siyo vya kutegemewa tena.

Kisha Muhamad bin al-Ash'ath akamwambia Ubaydullah bin Ziyad kwamba ametoa usalama kwa Muslim, lakini Ubaydullah alikataa kuutambua uwezo wa Muahamad bin al-Ash'ath kufanya hivyo. Alimwambia Muslim kwamba angeuawa wakati huo huo. Muslim alijibu kwamba alikuwa tayari kuufikia

mwisho huo.

Ombi lake la kuwasilisha matakwa yake ya mwisho kwa mtu fulani aliyekuwapo hapo lilikubaliwa, na Muslim alimchagua Umar bin Sa'd kwa lengo hilo. Alikataa kumlazimisha Muslim ili asije akamkosea Ubaydullah, ambaye alimlaumu Umar bin Sa'ad kwa kutoridhika kwake kuyasikiliza matakwa (maneno) ya mwisho ya Muslim. Kisha Muslim akamwambia kwamba maneno yake ya mwisho yalikuwa kwamba:

(a). Deni la dirmah mia saba (700) alilopata wakati wa kukaa kwake Kufa lilipwe kwa thamani ya upanga wake na deraya. (b). Kwamba mwili wake uzikwe; na (c). Mjumbe atumwe kwa Husein kumjulisha hatma ya Muslim ili kwamba aweze kurudi alikotoka na asidanganywe na ahadi zilizofanywa na wenyeji wa Kufa.

Baada ya kuisikia haja ya mwisho (wosia) ya Muslim, Umar bin Sa'd alik- wenda kwa Ubaydullah bin Ziyad na kumwambia yale yote ambayo Muslim alimwambia. Tabia hii ya kufedhehesha ilimuudhi hata Ubaydullah mwenyewe na aliurudia msemo wa Kiarabu, wenye maana ya kwamba;
"Mtu mwaminifu hawezi kukusaliti lakini wakati mwingine mtu asiyemwaminifu huamimiwa."25
Halafu alitoa maamuzi mwenyewe juu ya maombi ya Muslim; "Sina haja yoyote katika vitu vyako ambavyo vitauzwa kulipia madeni yako.

Sina lolote la kufanya kuhusiana na Husein, kama hatakuja upande huu. Ninashindwa kutoa ahadi yoyote ile ya kuwa mwenye huruma kuhusu utupaji wa mwili wako kwa vile wewe ulifanya uasi dhidi yangu na uliwatia moyo watu ili kusababisha mfarakano na kutokuelewana miongoni mwao.26
Muslim alijibu shutuma zote hizi na akafichua kabisa uwongo wa madai yaliyoelekezwa dhidi yake. Kisha Ubaydullah bin Ziyad aliamuru Muslim bin Aqil kuchukuliwa juu gorofani mwa kasri lake na auawe hapo. Halafu mwili wake utupwe chini ardhini. Muslim alipanda kwenye gorofani la jumba hilo kwa utulivu mkubwa, huku akimtukuza Mungu na kumwomba baraka Zake.

Bakr bin Humran al-Ahmari ambaye ndiye aliyekuwa amejeruhi midomo ya Muslim na kinywa chake alimnyonga na kuutupa huo mwili wake chini kwenye sakafu ya kasri hilo.27 Muslim alianza mapambano yake hayo tarehe 8 Dhil-Hijja mwaka wa 60 A.H.28 na aliuawa kishahidi katika siku iliyofuatia.

Baada ya tukio hili, hofu iliigubika Kufa, na watu waliacha kutoka nje ya nyumba zao kwa muda mrefu kidogo. Bado tukio jingine kubwa la kusikitisha katika muktadha huo huo ilikuwa ni kwamba Hani ibn Urwa aliburuzwa mpaka sehemu ya sokoni, akiwa amefungwa kamba na akauawa kwa upanga na mtumwa wa ki-Turuki wa Ubaydullah bin Ziyad29 bila ya kuvutia ujulikanaji wake wowote ule makhususi.

1. Tabari, Juz. I, uk. 2389
2. Tabari, Juz. II, uk. 234, Irishad.
3. Ibid
4. Al-Akhbar al-Tiwar, uk. 229.
5. Tabari, Juz. II, uk. 272.
6. Ibid
7. Tabari, Juz. II, uk. 236.

8. Tabari, Juz. II, uk. 235.
9. Tabari, Juz II, uk. 228.
10. Tabari, Juz. II, uk. 237.
11. Ibid
12. Tabari, Juz. II, uk. 220.
13. Tabari, Juz. II, uk. 264.
14. Tabari, Juz. II, uk. 264.
15. Tabari, Juz. II, uk. 228
16. Irishad, uk. 308; Tabari, Juz. II, uk. 240.
17. Tabari, Juz. II, uk. 241.
18. Tabari, Juz. II, uk. 249; Irishad, uk. 311
19. Tabari, Juz. II, uk. 249; Irshad, uk. 311
20. Tabari, Juz. II, uk. 201; Irshad, uk. 312.
21. Tabari, Juz. II, uk. 251-252; al-Irshad, uk. 312-313.
22. Tabari, Juz. II, uk.253; Irshad; 313-314.
23. Tabari, Juz. II, uk. 255; Irshad, uk. 315.
24. Tabari, Juz. II, uk. 258; Irshad, uk. 317.
25. Tabari, Juz. II, uk. 266
26. Ibid
27. Tabari, Juz. II, uk. 267.
28. Tabari, Juz. II, uk. 271.
29. Tabari, Juz. II, uk. 268; Irshad, uk. 325.

# Sura Ya 19:Safari Ya Husein Kwenda Karbala Na Vituo Vyake

Taarifa katika siku hizo za kale na njia za mawasiliano zilikwenda pole pole sana kiasi cha kuwafanya watu wa Makkah kutoyasikia mabadiliko ya msingi ambayo yalikuwa yameathiri mpango wa kisiasa mjini Kufa na kifo cha kishahidi cha Muslim bin Aqil na Hani bin Urwa kabla ya kuondoka kwa Husein miongoni mwao.

Kwa nini Husein aliondoka Makkah? Barua ya Muslim iliyopelekwa mwezi 12 ya Dhil Qadi[1] yaani siku 27 kabla ya mwisho wake wenye kuhuzunisha, ikimwomba Husein kuendelea kwenda Kufa katika kuitikia mialiko iliyopokelewa kutoka huko, na ikitaja mapokezi ya shauku kubwa aliyofanyiwa, haikuarifu kabisa kile kiwango cha umuhimu wa kuondoka kwake kwenda Kufa ambacho kingemshawishi Husein, hususan hasa kuhusu utekelezaji wa matendo yote yaliyoamriwa na Uislamu, kuondoka Makkah bila ya kutekeleza

Hijja kamili ambayo ingefanywa siku chache tu zijazo, na ambayo kwayo (hija) Waislamu hata kutoka sehemu za mbali ulimwengu mzima walikuwa wanakuja Makkah. Husein, hata hivyo, aliridhika

mwenyewe kwa nafsi yake na utekelezaji wa ibada ya *Umra*, yaani hija ndogo. Sababu ya uondokaji wa haraka wa Husein kutoka Makkah ilikuwa kwamnba aligundua kuwasili kwa askari wakiwa katika mavazi ya mahujaji kwa uwazi kabisa kuja kumchukua yeye mateka hapo Makkah.

Husein alikuwa anatambua vyema kabisa mwisho wake wa msingi, yaani kifo cha kishahidi, na hili limeonyeshwa kwenye hotuba aliyoitoa wakati anaondoka Makkah, alisema: "Kifo ni kama shada la maua kwenye shingo ya mtu na ninatamani kukutana na wahenga wangu (mababu) kwa hamu kubwa sana kama vile Yaqub alivyokuwa na hamu kumuona Yusufu (mwanawe).

Ninaona kwa wazi kabisa kwa jicho langu la akili mandhari ya mahali pa tukio wakati maadui wa silika njema za kibinadamu, wakiwa kama wanyama wa mawindo watakapokuwa wanauchana vipande vipande mwili wangu. Hakuna ponyo dhidi ya hatima.

Sisi, watu wa nyumba ya Mtume, tunaridhia kimya kimya mapenzi ya Mwenyezi Mungu, tunakuwa wenye subira katika mitihani iliyoamriwa na Yeye, na tunapata ujira wa wale wanaojijanibu katika utashi Wake. Vipande vya nyama yake haviwezi kutenganishwa na Mtume. Yeyote yule ambaye yuko tayari kujitoa muhanga maisha yake pamoja nami na kukutana na Mungu wake anaweza kufuatana nami katika safari yangu."

Katika kila kituo cha safari yake alikuwa mara kwa mara akikumbuka kifo cha kishahidi cha Yahya bin Zakariyya (Yohana mbatizaji) akisema kwam- ba mbele ya macho ya Mwenyezi Mungu ilikuwa inatosha kuonyesha kotokuwa na thamani kwa ulimwengu huu kwamba kichwa cha Yahya kilikatwa kutoka mwilini mwake ili kikabidhiwe kama zawadi kwa kaha- ba miongoni mwa Waisraeli.[2]

Sababu ya kwa nini Husein alichagua kwenda Kufa ingawa alishawishiwa kuacha kufanya hivyo na watakiaheri wa kweli, imeelezewa katika sura iliyopita nyuma na hakuna haja ya kurudia kuitaja tena hapa.

Mbali na wale jamaa na ndugu zake wakuu ambao walifuatana naye kutoka Madina, wachache kati ya marafiki zake kutoka Hijaz na Basra pia walikwenda pamoja na Husein katika safari hiyo ya majaaliwa.[3]

Kwa kiasi kinachoweza kuyakinishwa, vituo mbalimbali vya safari ya Husein kwenda Karbala vinaweza kupangwa kwa utaratibu wa kituo na matukio katika mpango ufuatao:

**Safah**: Alipitia Safah bila ya kukaa hapo hasa. Hapa alikutana na al- Farazdaq,[4] mshairi ambaye akitoa makisio yake ya hali iliyokuwepo hapo Kufa, alisema; "Nyoyo za wakazi wa Kufa ziko katika upande wako, na panga zao ziko upande wa Bani Umayyah." Husein alikubaliana na maoini ya al-Farazdaq na akasema kwamba angeshukuru kama amri ya Mwenyezi Mungu ingekubaliana na matakwa yake na kwamba kama mapenzi ya Mungu yalimzuia, ingekuwa si mafanikio haba kwa mtu yeyote yule ambaye nia zake zilikuwa halisi na dhamira safi.[5]

**Tan'im:** Husein alikodisha kiasi fulani cha ngamia hapa kutoka kwenye msafara wa watu wa Yemen kwa

ajili ya usafiri wa vyombo vyake na baadhi ya sahaba zake. Hii inaonyesha kwamba alikuwa ameondoka Makkah bila ya maandalizi ya sawa sawa kwani wakati ulimtupa mkono. Ilikuwa ni katika hali hii kwamba Abdallah bin Ja'far, na Yahya bin Sa'id ibn al-Aas, ndugu yake gavana wa Madina na Makkah walimwona Husein ili kumshawishi asiendelee na safari ya kwenda Kufa. Abdallah alikuwa ni binamu yake Husein na hapo nyuma pia alijaribu kumshawishi kwa kumwandikia barua asiende Kufa.

Sasa, alipata hati ya maandishi kutoka kwa gavana wa Madina akitoa usalama kwa Husein, na ili kuupa nguvu zaidi na ustahili wa kusadikika utoaji huu wa usalama, alikuwa pia ameku- ja na ndugu wa gavana Yahya. Husein alijua thamani ya usalama aliopewa na mamlaka ya serikali za mitaa dhidi ya sera ya serikali kuu.

Hakukubaliana na mawazo ya Abdallah bin Ja'far kama hapo mwanzo. Akiwaacha watoto wake, Awn na Muhammad ili wafuatane na Husein, Abdallah bin Ja'far alirudi Madina.[6]

**Dhat 'Irq**: Baada ya kuondoka Abdallah bin Ja'afar, Husein alisimama hapa.[7]

**Al-Hajir in Batn al-Rumma**: Kutoka hapa Husein alipeleka barua kwa wakazi wa Kufa akiwaambia kuhusu kupata barua ya Muslim bin Aqil, kuondoka kwake mwenyewe kutoka Makkah tarehe 8 ya Dhil Hijja, na juu ya kuwasili kwake Kufa muda mfupi ujao, na kuwataka wao wafanye maandalizi yote muhimu.[8]

Mjumbe ambaye alikuwa anaichukua barua hii kuipeleka Kufa, Qays bin Mushir, alikamatwa katika sehemu iitwayo al-Qadisiyya na watu wa Ubaydullah bin Ziyad na alipelekwa kwa Ubaydullah (mwenyewe) ambaye alimtaka amnenee mabaya Ali bin Abi Talib kama alikuwa anataka kweli kuokoa maisha yake.
Qays alipanda juu ya mimbari na akamsifu sana Husein, na akamtaka kila mtu kuitikia wito wake. Hapa bila shaka kabisa alipoteza maisha yake.[9]

Wakati akiondoka kwenye kituo hiki, Husein alikutana na Abdallah bin Muti' ambaye alikuwa akitokea Iraq. Yeye pia hakukubaliana na mpango wake wa kwenda Kufa.

**Zarud**: Ilikuwa ni katika kituo hiki ambapo Husein alijipatia rafiki kutoka miongoni mwa watu wale ambao walikuwa kwao ni mamoja tu katika kuhusiana na jambo la watu wa nyumba ya Mtume. Zuhayr bin al-Qays alikuwa mmoja wa Waislamu wa namna hiyo, akiunga mkono lile kundi ambalo lilikuwa wakati huo likifahamika kama kundi la Uthman. Alikuwa njiani akielekea Kufa baada ya kutekeleza ibada ya Hijja, na alikuwa amepiga kambi karibu na sehemu inayoitwa Zarud. Imam Husein alimpelekea ujumbe akielezea haja ya kutaka kumwona.

Aliposikia ombi hili likikataliwa, mke wa Zuhayr alimkemea kwa ukali sana kwa ukosefu wake wa unyenyekevu kwa mjukuu wa Mtume kiasi kwamba (Zuhayr) alikwenda kwa Husein mwenyewe, na alivutiwa sana na uwazi wa hoja zake kiasi kwamba alielekeza kwamba mahema yake yapigiliwe karibu na mahema ya Husein. Alimtaliki mkewe na kumwambia kwamba yeye ameamua kufa kwa ajili ya

Husein. Kisha kila mtu aliyefuatana naye pia aliondoka na kumwacha.[10]

Ilikuwa ni mahali hapa ambapo watu wawili wa kabali la Asad walimwona mtu anamkaribia Husein kutoka upande wa Kufa. Alipomwona mtu huyo Husein alimsimamisha ili kupata habari kutoka kwake juu ya vipi mambo yalivyokuwa yakiendelea huko Kufa. Mtu huyo, alipouona msafara wa Husein, alibadilisha njia ya safari yake, ambayo kwayo Husein aliendelea na safari yake. Watu wawili hao wa kabila la Asad, hata hivyo, walimfua- ta na kumkuta mtu yule ambaye aliwaambia kwamba wote Muslim bin Aqil na Hani bin Urwa walikwishauawa.[11] Walibakia kimya na taarifa hiyo na kuifikisha kwa Husein jioni iliyofuatia.

**Tha'labiyya**: Ilikuwa mahali ambapo watu wale wawili wa kabila la Asad walimwambia Husein, kwa idhini yake, mbele ya wengine wote waliokuwepo hapo wakati huo, habari za kuhuzunisha sana za kifo cha kishahidi cha Muslim bin Aqil na kile cha Hani bin Urwa.

Viongozi wa watu kwa kawaida huficha misiba ya hasara kama hii ya wanajeshi na wafanyakazi ili kudumisha ari ya wafuasi wao. Hapa Husein alikwisha tambua mapema mno kwamba ushindi wa kimaada usingekuwa (upande) wake, na alikuwa hajali kabisa kuhusu idadi ya wafuasi wake. Kwa kweli, kiakili alikuwa tayari kuwaruhusu wote waondoke na kumwacha akutane na majaaliwa (ajali) yake, kwani alijua vyema kabisa kwamba ilikuwa ni damu yake tu (ndiyo) ambayo Yazid alikuwa anataka kuimwaga.

Kwa hiyo, alizipokea habari hizo za kuhuzunisha kwa kurudia rudia virai vya mazungumzo ya kawaida, "**Hakika sisi tu wa Mwenyezi Mungu na Kwake tutarejea,**" Na "**Huruma za Mwenyezi Mungu ziwe juu yao**." Kisha aliendelea kunyamaza kimya.[12] Al-Dinawari anasema kwamba Husein alisema, "Tunatoa hesabu za maisha yetu kwa Mwenyezi Mungu," akikusudia kwamba 'tunatoa muhanga maisha yetu katika njia Yake na ni Yeye ambaye hutulipa ujira."

Wale watu wawili wa kabila la Asad ambao walikuwa wameguswa sana na maendeleo ya kuhuzunisha waliona vigumu kuzishinda hisia zao zaidi. Walimwambia Husein: "Kwa ajili ya Mwenyezi Mungu, tafadhali sana usiyaache maisha ya familia yako nzima yote katika hatari na urudi nyuma kutokea kituo hiki hasa kwani hakuna mtu hata mmoja huko Kufa wa kukusaidia au kufanya nawe urafiki.

Kinyume chake tunahofia kwamba Kufa yote itakuwa ni yenye uadui juu yako." Ushauri kama huu wenye uaminifu na huruma za dhahiri, pengine usingeweza kukataliwa vya kuridhisha kwa kutumia akili pekee.
Husein, tokea mwanzoni kabisa, alikuwa ameutambua mwisho wa kuhuzunisha wa safari yake ambayo alikuwa amekwishaianza, na zile habari za kusikitisha ambazo zilikuwa zimekwisha pokelewa hazikuleta tofauti yoyote ile kwake binafsi. Yeye, kwa hiyo alifikiria kwamba ingekuwa inafaa kwa ubora sana kuona vipi habari hizi zimepokelewa, kutoka kwenye kundi la watu wengine kabisa miongoni mwa sahaba zake. Akiwahutubia watoto wa Aqil, aliwauliza, "Ninyi mnafikiria nini sasa ambapo Muslim ameuawa kishahidi?"

Wote waliruka na kusimama kwa miguu yao na kusema kwa sauti kubwa, "Tunaapa kwa Mwenyezi

Mungu, hatutarudi mpaka tuwe tumelipiza kisasi kwa kifo cha Muslim au sisi wenyewe tuwe tumekunywa kikombe cha mauti kama ambavyo Muslim amefanya." Kisha Husein aliwaambia wale watu wa kabila la Bani Asad, "Kama hawa wanayatoa maisha yao, kuishi kwangu kutahudumia lengo gani?"[13] Miongoni mwa wale ambao walikuwepo, mmoja wapo alisema kwamba Husein alikuwa na cheo kikubwa (hadhi) zaidi kuliko Muslim bin Aqil, na kwamba wakazi wa Kufa wangekimbilia kutoa msaada kwa Husein.

Husein hakuiunga mkono rai hii na aliamua kunyamaza.[14]Baada ya kuupitisha usiku ule hapa, na kujichukulia pamoja naye maji ya kutosha asubuhi na mapema, Husein alianza safari yake na aliwasili mahali paitwapo Zubala.[15]

**Zubala**: Ilikuwa ni mahali hapa ambapo Husein alipokea ujumbe[16]kutoka kwa Muhammad bin al-Ash'ath uliotumwa katika kutekeleza moja ya matakwa yake ya mwisho (wosia) ya Muslim bin Aqil kumwonya asiendelee na safari ya Kufa ambako asingeweza kupata msaada. Mjumbe huyo pia alileta habari kwamba Qays bin Mushir naye pia amekwisha uawa kwa upanga.

Inaonekana kwamba wale masahaba wa Husein ambao walisikia habari za kifo cha kishahidi cha Muslim bin Aqil hapo Tha'labiyya walizihifadhi bila kusema.

Husein hakufikiria kwamba ni sahihi kuzuia taarifa hizi kwa jamaa wengine wa msafara wake ambao umekuwa katika mwelekeo wake umewavutia watu wengi ambao walifikiria kwamba Husein alikuwa anakwenda katika nchi ambako kwa uhakika angefanywa kuwa mtawala, na wangezawadiwa vizuri sana kwa kule kufuatana naye. Yeye alitaka kuziweka sawa fikra za watu hawa waliokuwa na mawazo potovu kama haya.

Akiwahutubia, akisema; "Nimepokea habari zenye kuumiza sana moyo kwamba Muslim bin Aqil na Hani bin Urwa wameuawa. Wale ambao waliotamka kwamba walikuwa tayari kutusaidia wamevunja ahadi zao. Kwa hiyo, yeyote yule awaye katika ninyi, anayependa kurudi atokako anaweza kufanya hivyo, sitamtaka kutoa maelezo kwangu." Walipoyasikia maneno haya wengi katika kundi lake sasa waliondoka hivyo kwamba kundi hilo likabaki na watu wale tu ambao walifuatana naye kutoka Madina.[17]

**Batn al-Aqaba**: Husein alipata taarifa hapa kwamba Ubaydullah bin Ziyad amepeleka askari walinzi katika njia yote kati ya al-Qadisiyya na Udhayb. Alikuwa pia ameombwa kwa dhati kabisa na mtoa taarifa kwamba asiende Kufa bali arudi alikotoka. Husein alifanya mabadiliko kidogo katika mwelekeo wa safari yake, ili kuweza kuikwepa al-Qadisiya na akaendelea na safari yake.

**Sharaf**: At-Tabari na Shaykh al-Mufid wote wawili wameeleza kwamba Husein alihakikisha kwamba ngozi zote za maji na chupa za ngozi zilikuwa zimejazwa maji kabla yeye hajaondoka hapa.[18]Mwezi wa Muharam ulikuwa ndiyo kwanza umeonekana kwa mwaka wa 61 A.H, wakati Husein alipoanza safari yake. Walikuwa wamefika mahali karibu na al-Qadisiyya, wakati farasi fulani walionekana kwa mbali sana wakija kuwaelekea wao.
**Dhu' Husum**: Husein kwa haraka sana alikwenda kwenye mlima Dhu' Husum uliokuwa karibu ili kujilinda kutokana na kushambuliwa kutoka upande wa nyuma au kuzungukwa na maadui. Ilitangaa

kwamba al-Hurr bin Yazid akiliongoza jeshi la askari elfu moja ametumwa kuja kumzuia Husein asiendelee mbele, kwani alijua yale mabadiliko ya njia ya Husein kupitia nje ya al-Qadisiyya ili kukwepa kukabiliana na jeshi hilo hapo. Ili kumfikia Husein, al-Hurr na watu wake walilazimika kufanya bidii sana katika joto la jangwani kiasi kwamba walipatwa na kiu kali sana yenye kuondoa nguvu na uwezo wa mwili. Farasi wao hawakuwa katika hali nzuri pia. Ilikuwa ni katika hali hii ya dhiki kubwa mno ambapo al-Hurr, watu wake na farasi zao walitokea mbele ya Husein ambaye kwa tabia ya kiungwana na huruma aliwapatia maji watu na wanyama pia, kiasi kwam- ba kiu yao ilikatwa kabisa. Swala za mchana ziliongozwa na Husein, na al-Hurr na watu wake walijiunga nao.[19]

Kabla ya swala Husein alimhutubia al-Hurr na wanajeshi wake akisema, "Sikuwajieni ninyi mpaka pale barua ziliponifikia zikiniita kuja kukuongozeni ili kwamba nyinyi labda mungeweza kuungana katika njia ya sawa na haki kwa kupitia kwangu mimi. Kama mtatimiza ahadi zenu mimi niko hapa tayari kulitimiza lengo langu. Hata hivyo, kama hamfurahii kuja kwangu kwenu mimi nitarudi kule nilikotoka." Hakuna aliyetoa jibu lolote lile kuhusu maelezo haya.[20]

Wakati wa jioni hali kadhalika aliziongoza swala. Husein alimwambia tena al-Hurr na watu wake kwamba kama walikuwa na maoni tofauti na yale ambayo waliwasilisha kwake katika barua zao na kupitia kwa wajumbe wao, angeweza kurudi alikotoka. Al-Hurr alithibitisha kwa dhati kwamba alikuwa hatambui kabisa kuhusu barua hizo anazozizungumzia. Husein hapo hapo alitoa mifuko miwili ya shogi iliyojaa barua zikimwita Kufa kama alivyokwishaeleza.

Al-Hurr alijibu kwamba hakuwahi kutuma barua yoyote katika hizo, na vile vile aliweka wazi kwamba yeye alipewa jukumu kumwandama Husein ili kumpeleka kwa Ubaydullah bin Ziyad. Alipoyasikia haya, Husein alimwambia kwa sauti kubwa, "Kifo kitakuwa karibu zaidi na wewe."[21]

Kisha Husein aliliacha wazo la kwenda Kufa na akiwahutubia sahaba zake, alisema sana juu ya mabadiliko ambayo yametokea na jinsi gani nyakati zilivyoteguka juu ya watu wema na waadilifu, na akasema kwamba ilikuwa ni laana kuishi katikati ya dhulma hizi.

Kisha Zuhayr bin al-Qays alismama ili kumhakikishia Husein kuhusu utiifu wake kwake, akisema, "Hata kama ulimwengu ungekuwa umemalizika kwetu sisi, na kuachana nao kumejitokeza tu kutokana na kutoa msaada wetu na kukuonea huruma wewe, tungechagua kukupa msaada wewe zaidi kuliko kubakia kuishi katika ulimwengu huu."

Naf'i bin Hilal akitaja usaliti na utovu wa uaminifu wa baadhi ya marafiki wa babu mzaa mama wa Husein, yaani Mtume, na wa baba yake, Ali bin Abi Talib, alisema kwamba ilikuwa sasa ni zamu yake kukabiliwa na hali hizo hizo. Kisha alimhakikishia Husein kuhusu upendo wake kwake usiobadilika na uamuzi wake kumfuata yeye popote pale ambako angetaka kumchukua. Burayr bin Budayr al-Hamadan pia alizungumzia katika mkazo huo huo.

Kisha Husein aliamuru kwamba, kila mtu aliyekuwa pamoja naye apande mnyama na kwamba warudi kupitia njia ile ile ambayo wamejia. Al-Hurr aliwazuia wasifanye hivyo, kwani alitaka kumchukua

(Husein) kumpaleka kwa Ubaydullah bin Ziyad. Husein aliapa kwa jina la Mwenyezi Mungu kwamba ilikuwa haiwezekani kwa matakwa yake haya kutekelezwa.

Baada ya mabishano makali iliamuliwa kwamba kwa vile al-Hurr alikuwa ameelekezwa kumfuata Husein mpaka atakapofika Kufa ambako sasa kulikuwa kumekoma kuwa mwisho wa safari ya Husein, Husein anapaswa achukue njia ambayo ilikuwa haielekei imma Madina wala kwenda Kufa, na kwamba al-Hurr angekuwa anamfuata tu kama alivyoagizwa.

**Al-Bayda**: Katika hotuba iliyotolewa kwa watu wa jeshi la al-Hurr na sahaba zake mwenyewe, Husein aliwakumbusha hadithi ya Mtume kwamba yeyote yule amwonaye mtawala ambaye anawakandamiza na kuwatesa raia zake, akahalalisha ambayo Mungu ameharamisha, anavunja viapo vyake kwa Mwenyezi Mungu, anapinga mafundisho na matendo ya Mtume na anawatendea uovu viumbe wa Mwenyezi Mungu, na anaruhusu mambo haya yafanyike bila ya kupingwa kwa maneno yake na vitendo vyake na hakufanya jaribio lolote la kurekebisha mambo hayo, basi huyo anastahili kuhesabiwa na Mwenyezi Mungu kwa namna ile ile kama ya mtawala huyo.

Akielezea juu ya hali katika nchi, Husein alisema, “Bani Umayyah wamechukua njia za shetani, wamekana kusalimu amri kwenye maamrisho ya Mwenyezi Mungu, wanatumia vibaya kile kinachowahusu Waislamu, wamehalalisha kile ambacho Mwenyezi Mungu ameharamisha, na wameharamisha kile ambacho Mwenyezi Mungu amekihalalisha. Katika mazingira haya, ni juu ya nani wajibu wa kutengeneza mambo haya upo zaidi kuliko juu yangu mimi?”[22]

**Udhayb al-Hijarat**: Watu watano, yaani Amr bin Khalid al-Saydawi, mtumwa wake Sa’d, Mujammi‘ bin Abdallah al-Aidhi, mtoto wake Aidh, na Janada bin Harith al-Salmani walifika kutoka Kufa wakiwa wamepanda juu ya farasi na pia wakiwa wameleta pamoja nao farasi mmoja. Al- Hurr alitishia kuwakamata kwani wao hawakuwa miongoni mwa kundi la masahaba wa Husein. Husein, hata hivyo, alisihi sana kwamba walikuwa marafiki zake na washirika na walikuwa chini ya ulinzi wake. Al-Hurr hakuleta matatizo baada ya hapo.

Mujammi bin Abdillah alimwarifu Husein kwamba watu muhimu wa Kufa wamehongwa sana ili kumpinga yeye, na kwamba wakati nyoyo za watu wengine zilikuwa bado ziko katika kumsaidia yeye, mikono yao na panga zao zingeamshwa dhidi yake. Al-Tirimma alimwambia Husein kwamba ameona jeshi kubwa mjini Kufa kiasi kwamba kamwe hajawahi kuona mfano wake kabla, na kwamba kwa vile ingekuwa ni kitu kisichowezekana kupigana vita na jeshi kubwa namna hiyo, alimshauri Husein kufuatana naye kuenda kwenye mlima Aja ambako watu 20,000 wa kabila la Tayyi wangekuwa katika huduma yake (kumhudumia) katika nchi ambayo wafalme wenye nguvu sana katika nyakati zilizopita walishindwa kuwashinda. Husein alikataa kulikubali ombi hilo.[23]

**Qasr Bani Muqatil**: Husein alimuona Abdallah bin al-Hurr al-Jufi, mpandafarasi shujaa na maarufu sana wa Kufa akiwa anaishi hapa, na akamwomba msaada wake. Abdallah bin al-Hurr alikataa kumsaidia, laki- ni akajutia sana kukataa kusaidia kwake huku kwa kipindi chote cha maisha yake

yaliobakia. Mwishowe aliungana na wale ambao walisimama kulipiza kisasi cha mauaji ya Husein.

Katika kuondoka sehemu hii, Husein alikuwa bado hajakwenda mbali wakati alipojisikia ni mwenye usingizi na akaota kwamba alimwona mpanda farasi akisema, "Watu hawa wanaendelea na safari yao, na mauti yanawakaribia." Hapo hapo aliurudia msemo wa kawaida, "**Hakika sisi tu wa Mwenyezi Mungu na kwa hakika kwake tutarejea**."

Aliisimulia ndoto yake kwa mwanawe, Ali Akbar ambaye alidadisi kama pengine walikuwa hawafuati njia ya sawa. Husein alimwambia kwamba kulikuwa hakuna shaka yoyote juu ya hilo. Ali Akbar kisha alisema kwamba katika hali hiyo hawana haja ya kujali kuhusu mauti.

**Nineveh**: Mpanda farasi mwenye silaha alileta barua kutoka Kufa itokayo kwa Ubaydullah bin Ziyad kuletwa kwa al-Hurr katika kituo hiki. Ilimwelekeza al-Hurr kumzuia Husein asiendelee zaidi na safari yake, popote ambapo barua hii ingemfikia. Iliendelea kusema kwamba mjumbe alikuwa amedhaminishwa kuambatana na al-Hurr na kumtaarifu Ubaydullah bin Ziyad juu ya hatua zinazochukuliwa na al-Hurr, na asimwache mpaka amri hiyo iwe imetekelezwa kikamilifu.[24]

Yawezekana Ubaydullah alikuwa amesikia tabia ya huruma ya al-Hurr kuhusu Husein, na amekuja kuonyesha wasiwasi kuhusu uaminifu wake. Al-Hurr alimzoesha Husein kwa ukamilifu yale yote yaliyomo ndani ya barua na, kwa hiyo, alilikataa ombi la Husein la kushuka kwenye kituo chochote kile zaidi ya mahali alipokwishafika.
**Karbala**: Husein alizuiwa na Al-Hurr hapo Karbala ili asiendelee mbele zaidi, na kwa hiyo aliweka kambi yake hapa. Ilikuwa ni siku ya pili ya mwezi wa Muharam mwaka wa 61 A.H, wakati Husein alipofika hapa.

Ile inayoitwa Karbala sasa hapo nyuma ilikuwa kwa kweli ni mkusanyiko wa vitongoji vingi mbalimbali, majina ya baadhi yao kama vile Nineveh na Ghadariyya bado yanasikika katika muktadha wa matukio ya Karbala. Mto wenyewe hasa wa Furati hauhusiki moja kwa moja na eneo la Karbala.

Tawi dogo la mto huo limejitenga lenyewe kutoka mto wenyewe katika sehemu iitwayo Ridhwaniyya na kupindapinda kuelekea eneo ambako kuna kaburi la Abbas, ndugu yake Husein na mshika bendera wake. Tawi hili la mto linaitwa Alqama, na kwa sababu ya chanzo chake wakati mwingine huitwa Furati pia.

Linakutana na mto wenyewe upande wa Magharibi wa Dhu Kifli. 'Taff' maana yake ni ufukwe wa mto, na neno hilo lilitumiwa kwa ufukwe ule wa Furati ambao ulipanuka katika upande wa Kusini kutoka Basra mpaka Hit, na kwa hiyo lilitumika kwa ufukwe ule wa Al-qama ambapo Karbala ndipo ilipojengwa. Karbala pia inaitwa *Shatt al-Furat.* Pengine, ingefaa kueleza tena kwa muhtarasi baadhi ya vipengele vya safari ya Husein kama ifuatavyo hapa chini:

Husein kamwe hakukusudia kufanya vita dhidi ya Yazid kwa kutumia nguvu za kizana ili kujipatia mamlaka ya kidunia. Alikusudia tu kuwatia nguvu Waislamu kutokana na hali ya utepetevu na kutojali

kujihusisha na amri za sheria za Qur'an, na mafundisho ya Mtume, na kuleta mapinduzi ya kiroho ili kuwawezesha kuliona tishio baya sana ambalo kupanda cheo kwa Yazid kwenye ukhalifa kumelishikilia juu ya Uislam.

Kwa hiyo alikataa kula kiapo cha utii kwa Yazid ambaye aliagiza kwamba Husein auawe. Husein hakupenda kujitoa mhanga mjini Madina, kwani mtu angeweza kukodishwa kama Ju'da, mke wa Hasan ambaye alimtilia sumu mume wake, kumuua yeye pia, akiachwa mchochezi wa kosa hilo, Mu'awiyah, akiwa hafahamiki kabisa.

Hili lingeunyima mhanga wa Husein moja ya malengo yake makuu, ambayo ni kumweka wazi khalifa asiyefaa kwenye kutokukubalika kwa ulimwengu wote.

Kisha Husein alikwenda Makkah ambako alitumia muda wake kwa amani. Kwa ujio wa msimu wa Hijja, Husein aliona miongoni mwa makundi yanayokusanyika ya mahujaji, wauaji waliovaa kama mahujaji waliokuja ili kumchukua kama mateka au kumuua.

Tishio juu ya maisha yake lilizidi kukua kwa kiasi kikubwa kwamba ingawa ni siku chache tu zilizokuwa zimebaki kwa ajili ya ibada ya Hijja Husein aliridhika yeye mwenyewe binafsi na utekelezaji wa Umra (hija ndogo) na aliondoka Makkah na watu wa familia yake na marafiki.

Husein hakupenda kujitoa mhanga mjini Makkah kwani kufanya hivi kungevunja utakatifu wa Ka'abah. Aidha, katika mkusanyiko mkubwa wa mahujaji, muuaji angeweza kutoweka kwa urahisi, na kufanya utambulisho wake kama wakala wa serikali usiwezekane.

Kwa hali yoyote ile uondokaji wake kutoka Makkah wakati ambao haswa Waislamu kutoka nchi zote za Kiislamu walikuwa wanaingia, kulipata utangazwaji mkubwa katika rasi (peninsula) hiyo ya Uarabuni, na maelfu ya watu kutoka nchi za mbali na karibu watakuwa wamelazimika kujadiliana na kufanya midahalo kuhusu sababu za kuondoka kwa Husein, na kusalia kwa maoni ya umma lazima yalikuwa yameelekea kwenye upande wake.

Ilikuwa itegemewe tu kwamba Husein angekuwa lazima sasa aende huko Kufa ambako kutoka huko alikuwa amepokea mialiko yenye msisitizo kwa ajili ya kwenda huko kuwaongoza watu kwenye umoja wa kidini. Asingeweza kukataa kulichukua jukumu hili la kusifika na kuyakataa maombi ya watu wa Kufa kwa sababu ya utovu wao wa uaminifu uliokisiwa. Au basi ndio ingekuwa Husein aende mahali penginepo pale kama mgeni asiyealikwa?

Inaweza ikaonekana kwamba baadhi ya ndugu zake na wale marafiki zake watiifu na wale wote ambao walikutana katika vituo mbalimbali vya safari yake kuelekea Kufa walikuwa wakijaribu kumshawishi Husein asiende Kufa; katika kuunga kwao mkono, baadhi yao waliukiri utovu wa uwaminifu wa wakazi wa mji ule, wengine walithibitisha kudhihiri kwa uadui kwa watu pale (mjini Kufa), na wengine walisisitiza sana kutokuwezekana kulikabili kwa mafanikio lile jeshi kubwa lililojikusanya Kufa ili kupigana naye.

Lakini kwa vile Husein hakufanya safari hii kwa matumaini yoyote yale ya kufanikiwa katika kiwango cha kimaada, hata zile habari hasa zenye kuhuzunisha za kifo cha kishahidi cha Muslim bin Aqil zilishindwa kumshawishi kufanya mabadiliko yoyote yale katika azimio lake.

1. Tabari, cha II, uk. 289.
2. Al-Irshad, cha II, uk. 377.
3. Tabari, cha II, uk. 278, Irshad cha I uk. 327.
4. ?
5. Tabari, cha II, uk.277-278.
6. Tabari, cha II, uk. 278.
7. . Al-Irshad, kur. 328-329.
8. Al-Irshad, uk. 329
9. Tabari, cha II, uk. 288-289.
10. Tabari, cha II, uk. 289.
11. Tabari, cha II, uk. 290; Irshad, 330-331.
12. Tabari, cha II, uk. Irshad, 332-333.
13. Tabari, cha II, uk. 292-293.
14. Tabari, cha II, uk. 292-293; Irshad, uk. 333.
15. Ibid
16. Tabari, cha II, uk. 293.
17. Tabari, cha II, uk. 264.
18. Tabari, cha II, uk. 294; Irshad, 333-334.
19. Tabari, cha II, uk. 295; Irishad, 334.
20. Tabari, cha II, uk. 297; Irishad, 335-336.
21. Tabari, cha II, uk. 297; Irishad, uk. 336.
22. Tabari, cha II, uk. 300.
23. Tabari, cha II, uk. 304
24. Tabari, II uk. 306-307 na Irshad, uk. 339-340.

# Sura Ya 20: Majeshi Yakusanyika Dhidi Ya Husein.

Baada ya mauaji ya Muslim bin Aqil kule Kufa, Ubaydullah bin Ziyad alichukua hatua za ukali usio na ukomo kuondoa kutoka kwenye mawazo ya watu zile fikra zote za uaminifu na utii kwa Husein ambaye kwake yeye idadi kubwa ya wao wametoa kiapo cha utii mikononi mwa Muslim. Wale ambao dhidi yao hata shaka ndogo sana kiasi gani waliyoweza kuwa nayo ya uaminifu na utiifu kwa Husein waliuawa au walitupwa gerezani bila ya kufanyiwa uchunguzi wowote.

Mitham, ambaye alikuwa akiuza tende na Rashid al-Hajri waliuawa wakati wa utawala huu wa hofu. Al-Mukhtar bin Abi Ubayd al-Thaqaf pia alifungwa, ingawa alikuwa hayupo mjini Kufa wakati Muslim alipouawa, na alikuwa, kama suala la uangalifu, alikubali hifadhi ya maisha na mali iliyotangazwa hapo

Kufa kwa wale ambao wali- itafuta chini ya bendera iliyopandishwa na Amr bin Hurayth.

Baada ya kwisha kutokomeza upinzani wote kwa mtawala, Yazid, hapo mjini, Ubaydullah bin Ziyad alichukua hatua za kuzuia hatari kwa serikali iliyoanzishwa iliyokuwa ikiibuka kutokea katika maeneo yapakanayo na Kufa, ambayo alipanga iweze kulindwa kwa ulinzi mkali sana. Kamanda wa shurta, Husein bin Tamim, alitolewa akiwaongoza watu 4000 kwenda Qadisiyya ambako njia kuu kutoka Hijaz, Iraq na Syria zilikutana. Vikosi vilisambazwa katika pande zote za njia kuu zinazokuja kutokea Basra na Syria na katika vituo vingine nyeti na dhaifu ili kuwazuia wale wote wenye kumwonea huruma Husein na kuwazuia wasiingie Kufa kusababisha matatizo hapo.

Basi wakati huo huo kabila la Dailam liliasi na kuushika mji wa Dastaba, ambao ulikuwa nje ya eneo la Kiarabu. Umar bin Sa'ad alipelekwa na watu 4000 kwenda kuwazimisha waasi, na malipo kwa huduma hizo, alipewa hati ya maandishi akiteuliwa kuwa mtawala wa Rayy, Dastaba na Dailam.
Jeshi hilo lilikuwa limeondoka kuelekea Iran, na yeye mwenyewe alikuwa katika hatua za kuondoka wakati suala la kumshughulikia Husein lilipochukua umuhimu tena. Ubaydallah bin Ziyad alimtaka Umar bin Sa'd kuzifikisha kampeni dhidi ya Husein kwenye mwisho wenye kufuzu, na kisha ndiyo aende Iran.[1]

Umar bin Sa'd alizaliwa ile siku ambayo Umar, khalifa wa pili aliyokufa. Kwa hiyo, ni lazima atakuwa amewaona masahaba wengi wa Mtume, na kuzisikia kutoka kwao zile hadith za Mtume ambazo zilionyesha upendo mwingi aliokuwa nao kwa wajukuu zake, Hasan na Husein. Atakuwa pia amemuona binafsi yeye Husein, na kumwona ni mtu mwenye tabia tukufu. Akihusishwa kwa kulinganisha ukaaji wake wa hivi karibuni mjini Makkah, maelezo kuhusu kujinyima kwa Husein, ucha-Mungu wake na utukufu wa tabia yake lazima hayo nayo pia atakuwa ameyasikia.

Kwa sababu zilizotajwa katika ibara ilitoyangulia Umar bin Sa'd hakupenda kupigana dhidi ya Husein akiona kwamba ni dhambi kufanya hivyo. Alipendelea kuachwa huru kutokana na kuchukua jukumu la kufanya kam- peni dhidi ya Husein. Ubaydullah bin Ziyad hapo hapo akataka irudishwe kwake ile amri ya kuteuliwa yeye kuwa mtawala wa Rayy, na hili lilimkabili Umar bin Sa'd kwa mgongano katika mapendeleo yake. Aliomba apewe siku moja ili afikirie na kutafakari juu ya jambo hili. Rafiki zake walimshauri asipigane dhidi ya Husein.
Mmoja wao alisema, "Naapa kwa Mwenyezi Mungu, kama utajiri wote na serikali zote vingekuwa katika milki yako, na ungekuwa upotee kwako ingekuwa ni vizuri zaidi kuliko kujichukulia jukumu la kumwaga damu ya Husein."[2]Tamaa ya kuwa na cheo kikubwa ilimvuta kuelekea upande tofauti na kiakili akawa katika huzuni na fadhaa kubwa.

Mwishowe hata hivyo aliruhusu mvuto (ubembe) unaopita wa madaraka ya kilimwengu kupotosha uamuzi wake, na akakubali kupigana dhidi ya Husein; na akaondoka kwenda Karbala na jeshi lake. Alifika Karbala mnamo mwezi 3 Muharram.[3]Pamoja na askari elfu moja chini ya Hurr, nguvu ya jeshi la Umar bin Sa'd ilipanda na kufikia watu elfu tano (5000), lakini Ubaydullah bin Ziyad, akielewa vyema ushujaa wa asili wa familia ya Husein aliwapeleka askari 3000 waliobakia wa ngome ya al-Qadisiyya kwenda Karbala pia.

Uandikishaji wa jumla wa askari kwa ajili ya jeshi ulitangazwa hapo Kufa, na Ubaydullah bin Ziyad alikwenda Nukhayla ambao uko katika njia iendayo Karbala kwenda kuyakagua majeshi na kuyapeleka Karbala bila mkatizo wowote ule. Viongozi muhimu wa Kufa walielekezwa kwenda Karbala na wafuasi wao. Kila mmoja katika wao ilibidi aondoke na jeshi kubwa, na kutokukubaliana na amri hii ilikuwa haisameheki kwa sababu yoyote ile. Hofu kuu iliingia katika nyoyo za wale ambao walirudi Kufa mara moja tu baada ya kutokea mbele ya Ubaydullah bin Ziyad.

Alipojua jambo hili, alimpeleka Suwayd bin Abd al-Rahman Minqar na kiasi cha askari wapanda farasi kwenda Kufa kumkamata kila mtu pale ambaye hajaondoka bado mpaka wakati huo hapo mjini kwenda kuungana na wenzie katika vita dhidi ya Husein. Suwayd alimkuta Msyria mmoja ambaye alikuwa katika ziara mjini Kufa kwa jambo lenye kuhusiana na mgogoro wa urithi wa mali. Mtu huyo alipelekwa kwa Ubaydullah bin Ziyad alihukumiwa akatwe kichwa chake mara moja. Kisha kila mtu alikwenda Karbala kupigana dhidi ya Husein.

Kwa hiyo, ilikuwa siyo muhimu kuzithibitisha takwimu zilizotolewa na wanahistoria mbali mbali- 20,000 za Ibn Tawus; 30,000 za al-Majlis; 35,000 za Ibn Shahrashub na 100,000 na wengine kama idadi ya watu ambao walijitokeza kupigana dhidi ya Husein.

Hatua zilizochukuliwa kuliongeza jeshi kupigana dhidi ya al-Husein yatosha kuoinyesha kwamba wakazi wote wa Jiji kubwa la Kufa, wafaao kwa kazi za kijeshi, kwa kweli walimiminwa mjini Karbala wakiwa katika muundo wa majeshi ya Yazid.

1. Tabari, II uk. 308.
2. Tabari, cha II, uk. 308-309.
3. Tabari, cha II, uk. 309.

# Sura Ya 21: Marafiki Wa Husein, Udhaifu Wao Katika Idadi Na Sababu Zake

Mauaji ya jumla ya kikatili na kufungwa jela, hapo Kufa, kwa kila mtu aliyetiliwa shaka ya kuwa na huruma na Husein, chini ya maelekezo ya Ubaydullah bin Ziyad, yasingeweza kuacha nyuma hata kidogo bila kuumiza mtu yeyote yule isipokuwa idadi ndogo sana ya wale watu ambao kwa kweli wangeweza kuelewa wajibu wao wa kumpa msaada.

Marafiki kama hao kutoka Kufa au maeneo mengine lazima, hata hivyo, wawe wameona ni vigumu sana kujiunga na Husein ili kumsaidia, kwani njia zote za kumfikia yeye hapo Karbala kwenye sehemu zote muhimu na za kimikakati kama vile al-Qadisiyya, Khattan, Qutqutana na La’la, zimewekwa chini ya askari doria wa kijeshi pamoja na amri za kuwakamata wale wote ambao walipenda kuendelea kwenda

kumsaidia Husein.

Sababu nyingine kwa kuwepo idadi ndogo sana ya watu ambao walijitokeza kumsaidia Husein hapo Karbala ilikuwa kwamba kuwasili kwake pale hakukutegemewa na kulikuwa kwa ghafla na kulikuwa hakujulikani katika viunga vya Kufa, hivyo kwamba hata baada ya siku kupita baada ya matukio haya ya masaibu kutokea pale Karbala, watu wengi walikuwa hawayatambui.

Hata hivyo wale wa upande wa kundi la Shia ambao walianzisha harakati za kumwita Husein kuja Kufa, na kwa kuwasili kwa Muslim bin Aqil huko Kufa, walikula kiapo cha utii kwake katika mkutano wa kwanza na wakaapa kujitoa mhanga katika kumsaidia Husein, na walifika Karbala na walijitoa mhanga kwa ajili ya Husein. Na hakuna hata mmoja katika wao, ambaye hakuweza kwenda kumsaidia Husein ameonekana akipigana dhidi yake.

Jeshi la Umar bin Sa'd liliundwa na watu wa kawaida wa Kufa na jamaa wa makabila wanaoishi katika viunga vya mji. Hawakuweza kutegemewa kuwa na nguvu ya utashi, moyo, ari na uthabiti wa marafiki wa Husein. Watu hawa hawakuwa bora zaidi kuliko watu waliofundishwa kutii kibubusa tu kiongozi wa kikabila, wasiojali au hata kuwa wajinga wa kutojua masuala yaliyowaingiza katika vita ambavyo walikuwa wanapigana.

Baadhi yao hawakuwa tayari kupigana dhidi ya Husein, lakini walikosa nguvu za kiuadilifu kutenda kwa mujibu wa yale yanayoamriwa na dhamira zao wenyewe. Kwa sehemu kubwa walishirikiana pamoja kuunda sifa njema mbele ya macho ya wakuu wao wa kijamii, na zawadi na vyeo walivyoahidiwa na serikali.

Kinyume chake, watu wote wa Kufa ambao walikuwa pamoja na Husein walifanya tabaka la watu wa kiroho wa mjini pale, na walikuwa ni mabwana wadhibiti wa utashi wao na matendo yao mbele ya mitihani mikubwa. Wengi katika wao walikuwa ni watu wenye kufahamika sana wa Kufa, na walifaidi ushawishi na mvuto mkubwa kiasi katika mji.

Watu wa Kufa, kwa ujumla, hawakuweza kuelewa kwa nini watu kama hawa wenye kudumu katika sala kwa utiifu kabisa na wenye kujinyima wamejiingiza katika vita. Watu hawa wakati mwingine huonesha athari yenye nguvu kwa maadui zao kiasi cha kuwaogopesha.

Katika maelezo ya vita vya Karbala mtu mara kwa mara hukutana maelezo ya maadui wanaokimbia mbele ya wapiganaji wa Husein. Kuondoka huku kwa ghafla ghafla kulikuwa ni matokeo tu ya misuto ya dhamira iliyohisiwa na maadui mbele ya watu wenye tabia njema kama hizi kama wafuasi marafiki wa Husein.

# Sura Ya 22: Mazungumzo Ya Amani

Tamaa ya mamlaka ya kidunia na utukufu vilimfanya Umar bin Sa'd kukubali mapatano na Ubaydullah bin Ziyad, ambayo aliyajua kuwa ni mabaya, ya kuliongoza jeshi lake kwenda Karbala kumwaga damu ya Husein kwa malipo ya kuupata utawala wa eneo la Rayy. Alitamani sana kujiokoa kwa njia ya kiwerevu kutokana na shughuli hii chafu na alipofika Karbala, alijaribu kugundua uwezekano wa kuwepo ufumbuzi wa amani kuhusu mgogoro uliopo kati ya pande husika.

Alimtuma Qurra bin Qays al-Hanzali kwa Husein kwenda kujua kutoka kwake lengo la jambo lililomfanya kuitembelea Iraq, kwa kutokea mbali kote huko katika nchi ya Hijaz.

Husein alimwambia Qurra kwamba wenyeji wa Kufa walimwita kuja katika mji wao, na kwamba kwa vile walionekana kutokupenda kuwepo kwake hapo mjini, alikuwa yuko tayari kurudi alikotoka. Qurra alilifikisha jibu hili la wazi kwa Umar bin Sa'd ambaye aliliona ndani yake kuwepo mwanzo ya kuleta amani.

Alimwandikia Ubayddullah bin Ziyad yale yote ambayo yametokea kati yake na Husein. Alipokwishaipata barua hii Ubaydullah alisoma shairi, linalomaanisha "Sasa kwa vile wako katika makucha ya mikono yetu, wanaomba waachiliwe. Hawawezi kutukimbia."

Alimwandikia Umar bin Sa'd majibu, akisema, "... unaweza sasa ukamshauri Husein kwamba yeye na sahaba zake wote lazima watoe kiapo cha utii kwa Yazid. Nitalifikiria suala hili tena wakati hili (la kiapo) limekwisha tendeka."[1]

Barua hii ilivunja matumaini ya Umar bin Sa'd ya amani kati ya makundi haya. Kuleta suala la Husein kutoa kiapo cha utii kwa Yazid lilikuwa jambo lisilo la haki kabisa. Pia, hata kama ni kwa ajili ya hoja tu, mtu angekubali kwamba jambo lisilowezekana lingetokea, hakuna ahadi kwa tendo lolote lile lipendezalo lilionekana limeshikwa kwa ajili ya Husein serikali ingeweza hata hapo kumpa aina ya adhabu ambayo wangeiona ni yenye kufaa.

Ubaydullah bin Ziyad alishindwa kabisa kuelewa maana ya jibu la Husein kwa Umar bin Sa'd. Lilikuwa tu limetegemezwa juu ya jaribio la kumaliza mabishano yote na kuondoa uwezekano wa kutokea vita kati ya makundi haya. Ubaydullah alifikiria kwamba labda Husein alikuwa ametishwa na majeshi makubwa yaliyotumwa na yeye kwenda Karbala, na kwa hiyo, akaamua kurudi alikotoka. Umar bin Sa'd, ambaye alikuwa akimchunguza Husein kwa ukaribu zaidi katika sehemu za makazi yake alijua vizuri zaidi, na akasema, "Nilijua kwamba Ubaydullah bin Ziyad hataki amani."[2]

Aliipeleka barua yake kwa Husein ambaye alitengeneza jibu hili tu, "Hili haliwezi kamwe kuwa. Lililo kubwa kabisa ambalo laweza kuni- angukia ni kifo na mimi niko tayari kukikaribisha."[3]

1. Tabari, uk. 311.
2. Ibid.

3. Al-Akhbar al-Tiwal, uk. 254.

# Sura Ya 23: Huduma Ya Maji Kwa Husein Yasimamishwa. Kiu Ya Kupita Kiasi Yaathiri Kundi Lake.

Mpango wa kuzuia maji yasimfikie Husein na watu wa kundi lake pamoja na watoto wadogo lazima ulikuwa unaunda picha hiyo ndani ya fikira za Ubaydullah bin Ziyad kwa kipindi fulani wakati alipoandika barua kwa al-Hurr bin Yazid al-Riyahi ambaye al-Hurr aliipata akiwa Karbala katika siku ya pili ya mwezi wa Muhamrram mwaka wa 61 A.H. Aliagiza katika barua hii kwamba Husein lazima alazimishwe kukaa mahali ambapo huduma ya maji ni haba.

Katika kuafikiana na amri zilizopokelewa na al-Hurr, kambi ya Husein iliwekwa katika kiwanja cha mchanga chenye ardhi isiyo na kivuli iliyoondolewa kutoka kwenye mto, na joto la jua wakati wa mchana lilikuwa ni chanzo cha shida kubwa kwa wote, na hasa zaidi kwa watoto.

Inaonekana kwamba amri za Ubaydullah bin Ziyad zilikuwa kwa ujumla zimefahamika ndani ya jeshi, na baadhi ya watu katika kujaribu kujipendekeza na kujikomba kwa wakuu wao walifanya kazi ya kugawa maji kwa Husein, kuwa ngumu, kama ilivyokuwa na hatari vilevile.

Tarehe 7 Muharam Umar bin Sa'd alipata barua nyingine tena kutoka kwa Ibn Ziyad akimwelekeza asimamishe ugavi wa maji kwa Husein na sahaba zake ili kwamba wasipate hata tone la maji kama alivyonyimwa maji Uthman bin Affan, Khalifa wa tatu.[1]

Umar bin Sa'd alimdhaminisha Amr bin Hajjaj al-Zubaydi kwa kazi ya kuweka uangalizi mkali sana katika kingo za mto na kulinda lisipatikane hata tone moja la maji kumfikia Husein. Alimpa Amr bin Hajjaj askari 500 kumsaidia katika kuitekeleza kazi hii. Uzuiaji wa ugavi huu wa maji ulisababisha ukali zaidi wa kiu iliyohisiwa na Husein na watu wa kundi lake.

Kuongezea fedheha kwenye jeraha hili, maadui wakati mwingine wakimhutubia Husein, wakisema, "Hapa pana maji, mbwa na nguruwe wanayanywa, punda na hata mbwa mwitu wanayatumia, lakini wewe na wenzio hamtapata hata tone moja la maji hayo."

Huenda pia kwamba baadhi ya maadui wa Husein angalau wangefikiria kwamba kiu tu yenyewe ingemuua yeye na sahaba zake, na kwamba hatua ya vita iliyokuwa ikiandaliwa kamwe isingefika. Marafiki wa Husein, hata hivyo, wakati mwingine waliweza kuyachota maji kwa ajili ya Husein kutoka kwenye mto kwa kutumia nguvu.

Jaribio la mwisho la namna hiyo lililokuwa na mafanikio lilifanywa na ndugu yake Husein, Abbas, katika usiku kabla ya mwezi 8 Muharam.
Ni mfano wa uaminifu na utii usio na kifani wa idadi kubwa ya watu kwa kiongozi wao, kwamba hata kama baadhi ya ndugu wa Husein na maraf ki wakati mwingine walifaulu kuufikia mto, hakuna hata mmoja katika wao alijali hata kuilowesha tu midomo yake kwa maji ambayo yalikuwa hayapatikani kwa ajili ya kukata kiu ya Husein.

Husein hakutumia nguvu ili aweze kuyapata maji. Alijaribu katika siku zote tatu alizokaa akiwa amenyimwa maji kuziamsha dhamira za maadui zake ili kwamba waweze kukubaliana na ombi lake la mara kwa mara la kupewa maji. Aliwaruhusu marafiki zake pia wafanye maombi kama hayo.

Burayr al-Hamadani alikutana na Umar bin Sad na akasema; "Wewe ni mwislamu wa namna gani uliyejiandaa kukichinja kizazi cha Mtume na pia unalikuza zaidi kosa kwa kumzuia Husein, na watu wa familia yake na marafiki zake, wanaokufa sasa kwa kiu, (unawazuia) kuyapata maji ya Mto Furat kwa matumizi yao, ambayo yananywewa bure na kwa uhuru kabisa na mbwa na nguruwe?"

Umari bin Sa'd alikiri udhaifu wake vinginevyo mpaka labda auachie uongozi wake wa eneo la Rayy, jambo ambalo hangeweza kulifanya kwa hali yoyote na kwa gharama yoyote ile.

Katika tarehe 10 Muharam wakati al-Hurr alipolitelekeza jeshi la Umar bin Sa'd, na kwenda kujiunga na kundi la Husein alielezea majuto makubwa pamoja na mambo mengine, kwa kusababisha Husein kuwekwa kambi yake mbali na mto.

Ni lazima awe ameteswa na kumbukumbu za tabia ya ukarimu ambayo Husein hapo nyuma kidogo alimfariji nayo kwa kumtuliza yeye na watu waliokuwa chini yake na farasi wao kutokana na kiu yao iliyowazidi nguvu na yenye kudhikisha.

Baada ya kujasiria shida kubwa ya kiu kali kwa muda wa siku tatu, na kutekeleza wajibu wao wa kupigana vita takatifu kwa ujasiri mkubwa, Husein na sahaba zake walikutana na vifo vyao vya kishahidi.

1. Tabari, cha II, uk. 312.

# Sura Ya 24: Jaribio La Mwisho La Kuleta Amani Na Jinsi Lilivyofikia Mwisho.

Ili kuepusha vita na kuwazuia Waislamu kujiingiza katika umwagaji damu kwa pande zote, Husein alijaribu kufungua mazungumzo kwa ajili ya kuwepo amani na Umar bin Sa'd hapo Karbala na

akamwalika Umar bin Sa’d kwa kumtumia Quraza bin Ka’b al-Ansar kukutana naye katika ardhi ambayo iko katikati ya sehemu zenye majeshi yao. Mazungumzo yalirefushwa mpaka ukaingia usiku. Kisha washiriki (katika mazungumzo hayo) wakarudi kwenye kambi zao.[1]

Uendeshaji wa mkutano ule ulikuwa ni siri, lakini ilitangaa kuhusu Husein kuwa alikuwa amejiandaa kuondoka Iraq, na hata kuihama Bara Arabu yote na kwenda sehemu ya mbali sana katika ulimwengu huu.[2] Kwa ukweli hili nalo pia lilikuwa sawa na ufanikishaji wa lengo la Husein ambalo kwalo ameyatoa maisha yake, nalo ni kutotoa kiapo cha utii kwa Yazid kama khalifa.

Tabia za Husein zilikuwa ni za upole sana na za kiungwana zenye kutoa fursa kiasi kwamba Umar bin Sa’d mara moja alikiri kwamba alitaka kupita katika njia ya amani na kwa kweli alikuwa anachukizwa sana na kujiingiza katika vurugu.

Alimjulisha Ubaydullah bin Ziyad juu ya masharti ya amani yaliyokubaliwa na Husein, na akasema, “Mungu atukuzwe na kushukuriwa kwamba moto wa fitina umezimishwa, ule uwezekano wa Waislamu kubakia wameshikamana pamoja umejitokeza na mambo ya wafuasi wa Uislamu yako katika mwelekeo wa kuboreka.” Aliongeza kusema kwamba hakuna sababu nyingine zaidi iliyobakia kuleta mzozo, na kwamba jambo hili sasa lingeweza kufungwa.[3]

Imeelezewa kwamba Ibn Ziyad alielekea kukubaliana na rai ya Umar bin Sa’d ambayo ilikuwa ikipingwa kwa nguvu sana na Shimr[4] ambaye alihoji kwamba ikiwa Husein angeruhusiwa kutoroka wakati huo, angedai kwa haki kabisa madaraka na heshima. Kuyakubali mapendekezo ya Husein kulikuwa machoni ni alama ya unyonge ambayo ingeleta aibu tupu na fedheha.

Alishauri kwamba Husein lazima aambiwe asalimishe silaha zake bila ya masharti yoyote, na akubali kumtii Ibn Ziyad, ambaye angeweza wakati huo kumuua Husein kwa upanga jambo ambalo lingekuwa halali kabisa, au kumpa msamaha. Alilalamika dhidi ya Umar bin Sa’d, akisema kwamba alitumia mikesha mizima kwa kuongea na Husein.

Kwa maneno haya, ambayo mara ni yenye kutisha na mara ni yenye kusifu sana, Ibnu Ziyad alivutiwa sana na akamwona Shimr kuwa mshauri wake mwaminifu na mwenye kumtakia mema. Alitilia shaka juu ya uaminifu wa Umar bin Sa’d ambaye kwake aliandika barua akisema, “Sikukupeleka wewe kwa Husein, ukamsikilize na kuzingatia maneno yake, au kurefusha sana mazungumzo yenu au kumpa matumaini ya kuishi au kufanya mapendekezo kwangu yenye manufaa kwake.

Angalia kwa makini sana kwamba kama Husein na marafiki zake (wafuasi) watanyenyekea kwangu na watataka huruma yangu, basi walete kwangu upesi sana, na kama wakikataa kufanya hivyo, waue, na wakate vipande vipande kwani haya ndiyo wanayoyastahili kuyapata.”

Kwa aibu yake ya milele aliongeza kusema, “Kama Husein atauawa, kifua chake na mgongo vikanyagwe chini ya kwato za farasi kwa sababu yeye ni muasi ninaongeza hili kwa sababu nimesema kwamba ningemshugulikia Husein katika namna hii kama ningempata kwa kuuawa kwa upanga. Kama

utatekeleza maagizo hayo utalipwa ipasavyo. Kama hupendi kufanya kama ulivyoamriwa hapa, kabidhi madaraka yako kwa Shimr."

Ubaydullah bin Ziyad baada ya hapo alimpa Shimr barua na akamuambia kwa mdomo kwamba kama Umar bin Sa'd hakutekeleza maagizo yake haraka vya kutosha, lazima achukuliwe kwamba ameondolewa katika wadhifa wake na kwamba Shimr angefanywa kuwa mrithi wake. Kisha alimwambia Shimr kupigana na Husein, amue Umar bin Sa'd na apeleke kwake kichwa chake pia.[5]

Umar bin Sa'd alikuwa na uhakika kabisa kwamba Husein kamwe asingetoa kiapo cha utii kwa Yazid, wala kujisalimisha yeye na sahaba zake bila ya masharti yoyote kwa Ibn Ziyad, lakini kuwepo kwa Shimr ubavuni pake kulifanya tishio katika kuendelea katika wadhifa wake wa juu, na hatari kwa maisha yake kuwa karibu sana, kiasi kwamba aliagiza maandalizi yafanywe juu ya kumshambulia Husein mara tu baada ya kupata barua ya Ibnu Ziyad.

Ilikuwa tarerhe 9 Muharam kabla ya jioni ambapo mashambulizi kwa kweli yalielekezwa dhidi ya Husein bila ya kumtangulizia taarifa kabla. Husein alikuwa amekaa karibu na mlango wa hema lake, wakati alipotiwa wasiwasi na vishindo vya majeshi yanayokuja, dada yake, Zainab, alimtahadharisha juu ya mvumo huo. Husein alimwambia dada yake katika kumjibu kwamba aliota ndoto Mtume anamwambia kwamba wangeonana naye muda mfupi baadaye.

Wakati huo huo Abbas alimletea Husein habari za mashambulizi, na habari za maagizo kutoka kwa Ubaydullah bin Ziyad. Husein alipendekeza kwamnba adui aombwe kuakhirisha vita kwa usiku ule ili kwamba aweze kuutumia katika du'a na maombi kwa Mwenyezi Mungu, kusoma Qur'an Tukufu, kuomba msamaha Wake na kumwomba Yeye rehema Zake.

Umar bin Sa'd alihisi haja ya kuchukua tahadhari katika uamuzi juu ya ombi la Husein kwa vile Shimr alikuwa yupo pale, alimtaka maoni yake juu ya jambo hili.

Shimr hakutaka kumlazimisha, akasema kwamba kwa vile yeye (Umar) alikuwa katika madaraka, ilikuwa ni juu yake kuliamulia jambo hilo. Kisha aligeukia kwa maafisa wengine kwa maoni yao.
Amr bin Hajjaj al-Zubaydi alisema, "Hata kama watu hawa wangetoka makabila ya Turk na Dailan, kisha wangeomba tahafifu hiyo ndogo, ungepaswa kulikubali hilo."[6] Angalau vita viliakhirishwa kwa usiku huo.

1. Tabari, cha II, uk. 313-314.
2. Ibid.
3. Tabari, cha II, uk. 315 Irshad uk. 343.
4. Jina la Shirm lilikuwa Shurahbil bin Amr bin Muawiya, wa uzao wa al- Walid wa kabila la Bani Amr, kutoka kitabu; al-Akhbar al-Tiwal, uk. wa 267.
5. Tabari, II uk. 315-316 Irshad, 344.
6. Tabari, II uk. 319-320.

# Sura Ya 25: Mkesha Wa Mwezi 10 Muharam.

Lengo kuu la msingi alilolitamani sana Husein ambalo kwalo aliomba kusimamishwa mapigano kwa muda, lilikuwa kumwezesha yeye na sahaba zake kuutumia usiku huo wa mwisho wa uhai wao katika Sala na du'a kwa Mwenyezi Mungu, kusoma Qur'ani Tukufu na kumwomba Allah Mwenye Nguvu zote kwa ajili ya rehema Zake.

Moja ya malengo mengine muhimu ya kutaka uakhirisho huu mfupi ni kwamba alipenda kuwapa marafiki na maadui pia, fursa nyingine ya kuchunguza usawa wa msimamo waliochukua katika vita hii, kuchagua, bila hofu au upendeleo, njia iliyo bora zaidi, kwa vile sasa mauti yanaonekana kuwa dhahiri kwa marafiki zake, na sio kwa uhakika kabisa kwa wengi wa maadui zake. Kuingia kwa jioni ya siku ya 9 ya Muharam Husein, aliwaita ndugu na marafiki zake, na baada ya kuwatolea heshima za juu kwa uaminifu wao kwake na sifa nyingine zilizo bora, alisema:

"Vita ni hakika mno vitapiganwa kesho. Ninavifungua viapo vyenu vyote vya utii kwangu na ninakupeni ruhusa kamili kuondoka na kwenda popote pale ambapo mngependa kwenda. Litumieni giza la usiku na muondoke. Kila mmoja wenu anaweza pia kuushika mkono wa mmoja wa ndugu zangu na kuon- doka naye pia. Kwani maadui wana kiu ya damu yangu tu, na mara watakapokuwa wameshaniua hawatamtafuta mwingine yeyote yule.[1]

Abbas bin Ali, ndugu yake Husein alisimama na akasema, "Kwa nini tufanye kama ilivyopendekezwa? Kuishi baada yako wewe hakuna faida. Hapana, Mwenyezi Mungu atuweke mbali na siku nyeusi kama hiyo!" Hisia za namna hii zilielezwa pia na kizazi cha Aqil.

Kisha Muslim bin Awsaja alisimama, na alisema: "Hatuna uwezo wa kukutelekeza wewe. Nitapigana kwa mkuki…kwa upanga wangu na kama nikikosehswa silaha, nitawashambulia kwa kuwatupia mawe mpaka niwe nimejitoa mhanga maisha yangu miguuni mwako."

Saidi bin Abdillah al-Hanafi alisema, "…Naapa kwa Mwenyezi Mungu kwamba kama nikitambua kwamba nitauawa kwa upanga, na nikarudishwa tena kuwa hai, na kisha ningeunguzwa nikiwa hai, na majivu yangu yakatawanywa hewani na kwamba ningetendewa vivyo hivyo mara sabini, sitakuwacha mpaka wakati wa mwisho nifie miguuni mwako."

Zuhair bin Qayn alisema: "Naapa kwa Mwenyezi Mungu, ni hamu yangu ya dhati kuuawa kwa upanga, nifufuliwe na halafu tena niuawe. Hivi inaweza kurudiwa mara elfu moja kama msiba unaokaribia kutokea unaweza kuepushwa kutokana na kukupata wewe na watu hawa mashujaa wa familia yako."

Hisia kama hizi za uaminifu thabiti na utiifu kwa Husein zilielezwa na masahaba wengine wa Husein. Husein hakufanya jitihada zozote kuwaweka watu pamoja naye kwa kuamsha hisia zao au kuyalea matumaini ya uwongo au hamu kubwa ya kupata kitu. Badala yake aliwataka wafuasi wake waende

kwenye usalama kama nafasi yoyote ile ya kufanya hivyo itapatikana.

Siku ya mwezi 10 Muharram, ilitangaa kwamba Amr, mtoto wa Bishr bin Amr al-Hadramin, alikuwa amekamatwa katika mipaka ya Rayy. Bishr alisema kwamba alim- toa mtoto wake na yeye mwenyewe kwa ajili ya Mwenyezi Mungu na kwamba kama ataishi asingependa kuona mtoto wake anakuwa kizuizini. Husein aliyasikia haya na akamwita Bishr kwake akamwambia kwamba amemfungulia na kumwacha huru kutokana na kiapo chake cha utii na anaweza kwenda kumtoa mtoto wake kizuizini. Bishr alijibu: "Wanyama wakali walao nyama wanimeze nikiwa ningali hai, kama ningekuwa mimi ni mwenye kukuacha wewe. Mambo haya yatawezekana vipi?".
Kisha Husein alimtaka ampeleke mmoja wa wanawe mwingine, aitwaye Muhammad, aende kwa nduguye na akampatia nguo zenye thamani kiasi cha dirham 1000."

Kama ilivyokwishatajwa, lengo la Husein katika kuomba kusitishwa vita kwa muda wa usiku mmoja lingewezekana vile vile kukusudiwa kuwapa adui zake muda wa kufikiria sifa stahilifu za dhuria wahusikao katika vita hivi na kupata uamuzi wao wa mwisho kuwahusu hao.

Kukimbia kwa Hur na wanajeshi wachache wa jeshi la Umar bin Sa'd kwenda kujiunga na jeshi la Husein katika siku ya 10 ya Muharam huonyesha mafanikio aliyoyapata Husein katika kuudhihirisha ukweli wa njia yake kwa wale ambao walikuwa tayari kumsikiliza na kufikiria kwa uhuru.

Husein na jamaa zake aliutumia usiku huu katika maombi na Sala kwa Mwenyezi Mungu kumwomba na kumsihi sana, waliutumia pia katika kusoma Qur'an na kufanya matendo mengine yafananayo na haya, huku mrindimo wa sauti zao ukiuvunja ukimya wa usiku kama nyuki wavumao.

Hatua za kuhakikisha usalama zaidi kwa taratibu zilizokuwepo wakati wa vita zilichukuliwa. Mahema yalikitwa karibu zaidi kila moja na lingine na kamba za kila hema ziliimarishwa kwa kuzifunga pamoja na zile za mahe- ma yaliyo karibu. Mwinamo wa nyuma wa mahema ulifanywa kuwa na kina zaidi ili kufanya handaki. Kuni zilipangwa ndani yake ili kwamba wakati lilipowashwa moto, kusingekuwa na shambulizi la adui ambalo lingekuwa rahisi kuongozwa dhidi ya mahema kutoka upande wa nyuma.

1. Tabari, cha II, uk. 320-321.

# Sura Ya 26: Kumalizika Kwa Mazungumzo Na Kuanza Kwa Vita.

Wakati wa asubuhi na mapema katika siku ya 10 Muharam, 61 A.H, Husein aliongoza idadi ndogo ya wafuasi wake waliokusanyika kwa Sala ya jamaa.

Waliliona lile jeshi kubwa la Umar bin Sa'd, likiwa bila upungufu japo kidogo, kwa maana ya mahitaji ya kimaada, likija kukabiliana na kikundi chao kidogo, kilichoteseka kwa kiu kali kupindukia. Nyuso zao, hata hivyo, hazikuonyesha ishara za kuvunjika moyo, sembuze za kukata tamaa. Kinyume chake, ule uhakika wa kukutana kwao na mauti karibuni sana kulizifanya nyuso zao zikichangamka kwa furaha.

Kwa kweli, mmoja wao, Burayr bin Hudayr al-Hamadan, alikengeuka kwenye umakini wa kawaida wa uzungumzaji wake na alielekea kupamba maneno yake kwa ucheshi wenye mahoka kidogo. Wakati upinzani ulipoingia juu ya mwelekeo usio wa wakati muafaka wa mazungumzo yake alisema, "Naapa kwa jina la Mwenyezi Mungu, kitu ambacho kinatutenganisha kutokana na furaha kuu ya milele hasa ni kutokana na kuchelewa ambako maadui wanakufanya katika kutushambulia kwa panga zao. Kwa kweli naitamani hiyo saa wakati panga zao zitakapoanza kutupiga."1

Wakati huo huo Umar bin Sa'd alilipanga jeshi lake, lenye askari wapatao karibu 20,000 katika uwanja wa vita. Kwenye kikosi cha Amr bin Hajjaj al-Zubayd alipangiwa kusimamia upande wa kulia wa jeshi na Shimr alipangiwa kuongoza upande wa kushoto wa jeshi. Azra bin Qays al-Ahmasi aliwekwa kuliuongoza jeshi la askari waendao kwa miguu na Shabath bin Ribii alikuwa aongoze jeshi la askari wapandao farasi. Durayd, mtumwa wa Umar bin Sa'd, alipewa bendera ya jeshi.2

Husein pia naye aliongoza jeshi lake dogo kwenye uwanja wa vita. Lilikuwa limekadiriwa kuwa na watu 72, askari 32 wakiwa ni wapanda farasi na 40 ni askari waendao kwa miguu.3 Ni kwa sababu hii kwamba idadi ya wale ambao walijitolea mhanga maisha yao hapo Karbala kwa kawaida inachukuliwa kuwa ni 72.

Kutokana na vyanzo mbalimbali ambavyo vinapatikana, inaonekana kwamba idadi ya wale ambao walipigana upande wa Husein walikuwa kati ya mia moja na mia mbili.
Katika wakati wa kuingia kwenye uwanja wa vita, Husein aliomba dua kwa Mwenyezi Mungu ambayo maneno yake yanaonyesha imani thabiti isiyotikisika katika kumtegemea na kumtumainia Mwenyezi Mungu.

Kwa dua hii maneno ya Yesu Kristo pale Msalabani (kama wanavyodai wakristo kwamba kasulubiwa); "Mungu wangu, Mungu wangu, mbona umeni- acha (umenitelekeza)?" Kama ilivyotajwa katika Agano Jipya, yasingekuwa na ulinganisho hata kidogo. Katika upeo wa mateso yake Husein aliomba, "Ee Mwenyezi Mungu, hakika Wewe ndio msaidizi wangu katika dhiki na shida zote, na Kwako Wewe ndio nageukia kwa matumaini katika matatizo yangu yote ..."

Husein kisha alilipanga jeshi lake dogo akiukabidhi upande wa kulia wa jeshi hilo kwa Zuhayr bin Qayn, na kwa upande wake wa kushoto ukawekwa chini ya maamrisho ya Habib bin Muzahir na bendera ya jeshi akaikabidhi kwa ndugu yake, Abbas.4

Bani Umayyah walieneza kwa utaratibu maalum, propaganda katika nchi ambazo zilikuwa chini ya mamlaka yao kwamba wao ndio waliokuwa warithi pekee wa Mtume ambaye alikufa bila ya kuwa na watoto.

Kwa hiyo, ilikuwa ni muhimu kwa Husein kwamba afanye jina lake, majina ya mahenga (mababu) wake, sifa njema za familia yake na hadithi za Mtume juu ya tabia njema kumhusu yeye mwenyewe zifahamike kwa mapana sana na bila makosa kiasi kwamba kusingekuwa na hata mtu mmoja aliyebaki kuwa na nafasi yoyote ile ya kudai kutojua ukweli kuhusu yeye, familia yake, na hadithi zilizopo katika Uislam kuhusu yeye.

Kufanya hivi kulikuwa na umuhimu mkubwa ili kuufanya uovu na ukatili wa wakandamizaji wake kujidhihirisha wenyewe kwa kila mtu.

Ilikuwa ni pamoja na lengo lililotajwa katika ibara iliyotangulia kwamba kabla ya kuanza kwa vita, Husein alimpanda ngamia, akaiweka Qur'an mbele yake[5] na akiwahutubia wakuu wa jeshi la Umar bin Sa'd, alitoa hotuba akasema, "… msiwe na haraka, Acheni nitekeleze wajibu wa kuku- peni onyo na mwongozo nilio na deni kwenu, na kukuwekeeni mbele yenu ule ukweli wote kuhusu kuja kwangu kwenu ninyi.

Kama mtayaamini maneno yangu na mkanitendea haki mimi, itakuwa hiyo ni bahati kwenu, na mtatambua na kujua kwamba hamuwezi kuwa na sababu ya kunipinga mimi. Kama hamtaamini yale ambayo nitayasema kwenu, na mkaacha kunitendea kwa haki, basi mnakaribishwa kukusanya majeshi yenu… na kuukomesha uhai wangu… Muumba wangu ananitosha …

Fikirini sana kuhusu jina langu na jadi yangu, na jaribuni kuelewa na kutambua mimi ni nani na jaribuni kuwa na haya. Fikirieni kama ni halali kwenu kuimwaga damu yangu au kulishusha daraja langu la juu. Je, mimi siyo mjukuu wa Mtume wenu Muhammad, na mtoto wa binamu yake ambaye alikuwa ndiye mtekelezaji wa wosia wake, aliyekuwa wa kwanza kuukubali, kuuamimi na kula kiapo kwa ajili ya Uislamu?

Je, hamkuisikia ile hadith maarufu sana ya Mtume kumhusu ndugu yangu (Hasan) na mimi kwamba sisi ni mabwana wa vijana wa peponi? Je, Hamza hakuwa kiongozi wa mashahidi, ami yake baba yangu, na Ja'far al-Tayyar ami yangu mwenyewe?

Kama mkikubali ninayokuelezeni kuwa ni kweli, na bila shaka hii ni kweli, kwa vile kamwe sijatamka au sijaongea uwongo, hakuna kinachobakia kwangu cha kuongeza au kueleza. Hata hivyo, kama mngeyafanya maele- zo haya kuwa ya uwongo, bado kuna watu wanaoweza kupatikana ambao watakuelezeni ukweli huu kama mtawauliza. Waulizeni Jabir bin Abdillah al-Ansar, Zayd bin Arqam na Anas bin Malik. Je sasa basi haitoshi hii kukuzuieni kuimwaga damu yangu."

Baaada ya kukatishwa na baadhi ya watu, aliendela na hotuba yake akisema, "Kama mnatia shaka juu ya ukweli na usahihi wa hadithi hizi za Mtume kunihusu mimi, je mnafanya namna yoyote ya mashaka kuhusu mimi kuwa mjukuu wake? Naapa kwa Allah, kamwe katika Magharibi wala katika Mashariki, hakuna mjukuu wa Mtume zaidi yangu mimi anaishi, kamwe siyo miongoni mwenu nyinyi wala katika kabila lingine lolote lile. Mimi ni Mjukuu wa Mtume wenu Muhammad. Niambieni mumeniinamia mnataka kuniua? Je, mnataka kulipa kisasi cha mauaji ya yeyote yule miongoni mwenu ambaye kwake yeye huyo

labda nimeyafanya? Je, mnataka malipo ya mali yenu yoyote ile ambayo labda nimeyasababisha kwa yeyote yule kati yenu?"

Kimya kizito kuligubika jeshi lote la maadui wa Husein, na hakuna hata mtu mmoja aliyethubutu kujibu. Husein kisha akaanza kutaja majina ya maafisa wale wa jeshi la Umar bin Sa'd, Shabath bin Ribii, Hajjaj bin Abjar, Qais bin al-Ash'ath na Yazid bin al-Harith, ambao walitia sahihi zao kwenye barua zilizo na mwaliko wa yeye kuja Kufa, na akawauliza kama wao hawakufanya hivyo (kutia sahihi). Kila mmoja katika watu hawa aliongoza askari si chini ya 500, na unafiki wao wa undumilakuwili ulikuwa sasa unafichuliwa, na uhai wao wote wa baadaye ukawa uko hatarini.

Kwa hiyo walikana kufanya mawasiliano ya kuandikiana na Husein ambaye aliwashutumu kwa kukana kwao ukweli bila haya.

Kisha alihoji kwamba kama kweli hawakutaka yeye aende huko Kufa, wangemruhusu kwenda mahali pengine kwenda kutumia maisha yake huko katika hali ya amani na Usalama. Qays bin al-Ash'ath, ndugu wa Ju'da, yule mwanamke ambaye alimpa sumu al-Imam Hasan mume wake, na pia ni ndugu wa Muhammad bin al-Ash'ath, ambaye alihusika na kukamatwa mateka Muslim bin Aqil, alisema, "Kwa nini ewe Husein hutoi kiapo cha utii kwa Yazid?"

Husein alijibu, "Kwa kweli kabisa wewe ungependekeza hivi. Je, huoni kama inakutosha kungojwa na kujibu juu ya kuuawa kwa Muslim bin Aqil? Sitajitosa mwenyewe katika mikono yenu kwa aibu na fedheha, wala nisingekukimbieni kama mtumwa ili kuyaokoa maisha yangu." Kisha Husein alimalizia hotuba yake, na akashuka chini kutoka juu ya ngamia wake.6

Wengi wa watu katika jeshi la Umar bin Sa'd walikuwa watu wa Kufa na hutuba zilizotolewa kwao na watu wao mashuhuri zilibeba uzito mkubwa kwao. Zuhayr bin al-Qays alikuwa na fursa ya kuwa mwenye kumuunga mkono Uthman, mpaka kabla ya kutoa kiapo cha utii kwa Husein, kama ilivyokuwa kwa watu wengi wa Kufa.

Uaminifu wake kwa Husein ukiwa umeanza hivi karibuni tu, alikuwa mwenye kukubalika zaidi kwa watu mjini mwake kuliko Habib bin Muzahir, aliyefahamika kwa muda mrefu sana kama mmoja wa wafuasi (shia) wa Ali, na mmoja wa wale ambao walianza kumwita Husein kuja Kufa. Akilihutubia jeshi la maadui, al- Zuhayr alisema, "Enyi watu wa Kufa, ogopeni ghadhabu ya Mwenyezi Mungu...

Amekuwekeni nyinyi na sisi katika mtihani kupitia kwa dhuria (kizazi) wa Mtume Wake, Muhammad, aliyechaguliwa ili kwamba aone ni kwa jinsi gani mtashughulika nao na mtatenda vipi kuhusu wao.

Nakuombeni nyinyi nyote kuwasaidia wao kuondoa utii wenu kwa Ubaydullah bin Ziyad. Kamwe hamtatendewa mema na Yazid na Ibn Ziyad katika kipindi chao chote cha utawala. Wataendelea kukupofueni na kukutoeni macho yenu, watakukateni mikono yenu na kuwanyonga na kuwauwa watu wema kama vile Hujr bin Adi, washirika wake, ambao waliijua Qur'ani kwa moyo, na Hani bin Urwa."7

Khutuba ya Zuhayr ilikuwa mara nyingi ikikatishwa katishwa na watu wanaojikomba na kujipendekeza wa Ibnu Ziyad. Kisha Shimr akatupa mshale kuuelekeza kwa Zuhayr huku akipiga kelele, “Nyamaza. Mwenyezi Mungu aunyamazishe ulimi wako.”

Zuhayr, hata hivyo aliendelea kuongea na alikatishwa tena na Shimr ambaye alisema, “Hivi karibuni utamuona kiongozi wako na nyinyi nyote mkiuliwa.” Zuhayr alitoa jibu la kijasiri, akasema, “Je, unanitishia kifo? Naapa kwa Mwenyezi Mungu hivyo ndivyo nipendavyo zaidi mimi kufa pamoja nao kuliko kubakia hai nanyi daima.” Kisha aliendelea na hotuba na akawasihi, “Enyi watu, msikubali kupotoshwa na watumwa wa mali kama hawa.

Naapa kwa Mwenyezi Mungu uombezi wa Mtume hautapatikana kwao kwa vile wanamwaga damu ya dhuria wake na ambao wanawaua wasaidizi wao.” Alipoona kwamba maneno yaliyozungumzwa kutoka upande wake yanaleta mishale kama majibu, na kwamba hoja kamili zilikuwa zimetolewa kwa maadui ili waachane na udhalimu wao, Husein alimtaka Zuhayr kuhitimisha hutuba yake.[8]

Ilikuja kuwa wazi, wakati muda kidogo baadaye katika siku hiyo al-Hurr aliondoka kutoka kwenye jeshi la maadui kwenda kujiunga na Husein, kwamba nia ya Husein ya kurekebisha maadui kwa ukweli wake maelezo na maelekezo ya kuadilisha yote yalifanikiwa katika kuwashawishi wao na kujipatia marafiki kutoka miongoni mwao, mafanikio yake siyo ya kupimwa kwa kuangalia idadi ya watu waliogeukia kwenye fikra zake, bali kwa mazingira ambayo kwayo ameyapata mafanikio hayo, katika mitihani isiyo na kifani, ambayo alikuwa akikutana nayo katika wakati ule pamoja na uhakika wa kuchinjwa yeye mwenyewe, na hatari ya kifo kwa maisha ya wale walioingia upande wa Husein.

Tokea pale ugavi wa maji uliposimamishwa, na kiu ikawatesa sana wafuasi wa Husein, pamoja na watoto wadogo, al-Hurr alikuwa amechanganyikiwa sana kiakili kwani alijichukilia yeye mwenyewe kuhusika katika kubakia kwa Husein kwenye ardhi ya Karbala na kumfanya apige hema zake katika sehemu mbali na mto.

Kumbukumbu za namna ya ukarimu mno ambao kwamba Husein aliwagawia maji al-Hurr, watu wake na wanyama pia katika wakati ambao walikuwa wamedhikika sana kwa sababu ya kiu lazima zitakuwa bado ziko katika fikra zake. Aligundua kwamba Umar bin Sa’d alitamani kuwepo amani na Husein, na alikuwa amefikiria kwamba vita visingepiganwa dhidi ya Husein ambaye khutba yake siku ya 10 Muharram ilileta athari kubwa kwa al-Hurr lakini mapokezi yake ya baridi yalizuia matumaini yake. Alimuona Umar bin Sa’d na akamuuliza kama kweli angepigana na Husein.

Umar akasema ndio atapigana, al-Hurr alimuuliza kama hakukuwa hata sharti moja katika yale yaliyopendekezwa na al-Husein kwa ajili ya kurudisha amani ambalo linakubalika. Umar bin Sa’d alijibu, “Kwa jina la Allah kama uamuzi ungekuwa kwangu basi kwa hakika ningeyakubali mapendekezo ya Husein. Nitafanya nini, wakati mtawala wako hakubali.”[9]

Al-Hurr hakuwa na cha kungojea, na hatua ilikuwa imefika haswa kwa maamuzi ambayo alikuwa ameyafikia akilini mwake, baada ya kuchunguza undani wa makusudio ya moyo wake kwa kiasi

kikubwa, na kuyapatia picha ya kivitendo.

Al-Hurr alichukua uzito mkubwa wa kuyaficha makusudio yake mpaka wakati wa mwisho, kwa hofu ya kuchukuliwa mateka hata kama shaka ndogo sana ya utovu wake wa uaminifu ingelifahamika. Hata hivyo, wasiwasi wake wakati alipokuwa anaondoka kwenda kambini kwa Husein ulikuwa ulionwa na al-Muhajir bin Aws, mtu wa kabila lake, ambaye alimuuliza, "Ewe al-Hurr ni nini makusudio yako? Je, unataka kuanzisha mashambulizi?" Al-Hurr alinyamaza kimya, lakini mtetemeko mdogo ulimpata mwilini mwake.

Al-Muhajir mara moja aliliona hilo na akamuuliza, "Je, unajionaje, ewe al-Hurr? Kamwe sijawahi kukuona ukiwa katika hali hii. Wakati nilipokuwa nikiulizwa kutaja jina la mtu aliye shujaa sana kuliko wote wa mji wa Kufa, jina lako lilikuwa linajitokeza katika midomo yangu. Ni kitu gani kiko nyuma ya mabadiliko haya katika tabia?" Al-Hurr alijibu, "Mbele yangu nina uchaguzi wa kuchagua kati ya pepo na moto kwa saa hivi, na sitapendelea kitu kingine chochote kile kisi- chokuwa pepo, hata kama nichanwe vipande vipande na kuingizwa motoni." Alipokwisha sema hivi, alimpiga farasi wake na akavuka kwenda kwenye kambi ya Husein.
Alijikabidhi mwenyewe kwa al- Husein, akisema, "Ewe mwana wa Mtume, maisha yangu yawe ni fidia kwako. Mimi ndiye mwenye hatia ambaye nimekuzuia katika njia yako, nikazifuatilia karibu sana hatua zako wakati wa safari yako na nikakufanya upige kambi hapa (katika ardhi ya Karbala).

Naapa kwa Mwenyezi Mungu, kamwe sikuwazia hata kwa fikra ndogo kwamba watu hawa wangeyakataa masharti yako yote ya amani, na kwamba mambo yangekuja kuwa katika hali hii, vinginevyo nisingejishughulisha mimi mwenyewe kutenda dhidi yako kama ambavyo nimefanya.

Sasa mimi niko hapa (mbele yako) nikijionea aibu kabisa mimi mwenyewe, na ninaomba msamaha wa Mola wangu ili kwamba niweze kushiriki kwa moyo wangu wote na nafsi yangu yote katika mitihani yako yote mpaka niwe nimejitoa mhanga maisha yangu chini ya miguu yako." Husein alimhakikishia kwamba toba yake itakubaliwa na Mwenyezi Mungu.

Alipokwisha hakikishiwa hivyo, na pia baada ya kupata msamaha kutoka kwa Husein, al-Hurr alifikiria kwamba angeelezea maneno machache ya ushauri na nasaha vile vile kwa askari wa jeshi la Umar bin Sa'd.

Aliwahutubia yeye mwenyewe wanajeshi wa Kufa, akisema, "Enyi ndugu zangu kwa nini hamkubali (hata) moja ya masharti yaliyotolewa na Husein, ili kuzuia vita dhidi yake."

Askari hao walipendekeza jambo hilo lirejeshwe kwa Umar bin Sa'd. Lakini Umar bin Sa'd alisema kwamba uamuzi wa kifanyike nini katika suala hili hauko mikononi mwake vinginevyo angefanya kama ambavyo imependekezwa (kukubali masharti hayo ya amani).

Maelezo haya yalimpandisha al-Hurr hasira kali, ambaye alifoka kwa kusema, "Enyi watu wa Kufa, Mwenyezi Mungu akuangamizeni! Mlimwita hapa mtu huyu mtukuka wa heshima kuu, na katika kuwasili

kwake mkamtoa kwa adui yake. Mlikuwa mmetanguliza mbele ahadi yenu ya kutoa mhanga uhai wenu kwa ajali yake, na mumefanya isiwezekane kwake kupumua kwa uhuru, na sasa mumedhamiria kumkaba koo.

Mmemzunguuka na mumemzuia kwenda popote pale ambapo angechagua kwenda katika ardhi hii pana ya Mwenyezi Mungu, na sasa amekuwa kama mfungwa katika mikono yenu. Ameachwa bila msaada, na mmemzuilia yeye, wanawake alionao na watoto, yale maji yatembeayo ya mto Furati ambayo uhuru wa kuyatumia uko wazi kwa Mayahudi, kwa waabudu moto na Wakristo, na ambamo nguruwe na mbwa wa Iraq hugaagaa.

Ni Husein tu na kundi lake ambao wamefikishwa kwenye milango ya mauti kwa sababu ya kiu. Ni jambo la kulaumika kwa kweli, kwa kitendo hiki ambacho mmekifanya kwa dhuria ya Muhammad baada yake. Namwomba Mwenyezi Mungu asiikate kiu yenu katika Siku ya Hukumu wakati haja kubwa sana ya kuhitaji maji itakapowashika.

Kama hamtaki kujilaumu wenyewe kwa matendo yenu mnayoyatenda, na kufungua ukurasa mpya na kubadilika hapa na sasa hivi. Al-Hurr aliitikiwa kwa salaam ya mishale iliyotupwa kumlenga yeye, na akaondoka kurudi kwa Husein.[10]

Muda ulikuwa umesogea mbele sana siku hiyo wakati Umar bin Sa'd alipomwita Durayd, mshika bendera wa jeshi lake, na akaurusha mshale wa kwanza kuelekea kwenye jeshi la Husein na kuyataka majeshi ya Yazid yashuhudie kwamba yeye (Umar bin Sa'd) amekuwa mtu wa kwanza kushambulia katika vita kwa kurusha mshale kuuelekeza kwa adui.[11]

Mbali na kutangazwa kuanza kwa vita, mishale iliyotupwa na adui haikusababisha hasara kubwa na wafuasi wa Husein walijibu kwa kutupa mishale mingi kuelekea kwa adui.

1. Tabari, cha II, uk. 326.
2. Tabari, cha II, uk. 327.
3. Tabari, cha II, uk. 325- 326
4. Tabari, cha II, uk. 326; Irishad, uk. 350..
5. Tabari, cha II, uk. 329-330.
6. Tabari, cha II, uk. 330-331; Irishad, 352.
7. Tabari, cha II, uk. 321-322.
8. Tabari, cha II, uk. 232.
9. Tabari, cha II, uk. 332-333
10. Tabari, cha II, uk. 334-335; Irishad, 353-254.
11. Tabari, cha II, uk. 335; Irishad 354

# Sura Ya 27: Masahaba Wa Husein Na Mihanga Yao Ya Kushangaza

Imependekezwa kutoa katika ibara zifuatazo, pamoja na maelezo ya maendeleo ya vita vya Karbala, mukhtasari wa maisha na sifa bainifu za masa- haba wa Husein:

1. Abdallah bin Umayr al-Kalbi, aliyekuwa sahaba wa Ali ibn Abi Talib, alikuwa shujaa sana na raia mtukufu wa Kufa. Alikuwa amemwoa Umm Wahb, binti ya Abd. Baada ya Muslim bin Aqil kuuawa kishahidi, wakati majeshi yalipokuwa yanakaguliwa kule Nukhayla kabla ya kupelekwa Karbala, Abdallah, ambaye nyumba yake haikuwa mbali aligundua kwam- ba walikuwa wanakusudia kwenda kumpiga vita Husein.

Alikuwa siku zote akitamani kupigana dhidi ya washirikina, na akiwafikiria wale ambao wamefanya vita dhidi ya Husein kuwa hawana tafauti na waabudu sanamu, aliamua kuwapiga vita makafiri kama hao. Mke wake alikubaliana naye na akafuatana naye kwenda Karbala kujiunga na Husein.[1]

Abdallah bin Umayr alikuwa wa kwanza miongoni mwa wafuasi wa Husein kuingia katika uwanja wa vita ambako Yasir na Salim, watumishi wa Ziyad na mtoto wake Ubaidullah, wametoa changamoto kupigana na yeyote yule ambaye angethubutu kupigana nao. Walikataa kupigana na Abdallah bin Umayr, ambaye walisema walikuwa hawamfahamu.

Akikasirishwa na hili, Abdallah aliwaua wote wawili; lakini katika mapambano hayo dhidi ya Salim, vidole vya mkono wake wa kushoto vilikatwa. Akiwa amejeruhiwa lakini (pia) akiwa amefanikiwa, Abdallah alikariri (alisoma) beti zikiweka sifa zake mbele, na kwa kuonya aliongeza kusema,

"Ewe Umm Wahb, naahidi ningerudia rudia kusonga mbele na kuchoma kwa nguvu na mkuki wangu na kutoa mapigo kwa upanga wangu kama vile achepukavyo mbele kijana ambaye humwamini Mwenyezi Mungu."

Alipokwisha msikia Abdallah bin Umayr akisema haya, Umm Wahb, mke wake, alijitumbukiza katika uwanja wa vita, akisema kwa sauti kubwa, "Wazazi wangu wawe fidia kwako, usiache hata jitihada moja katika kuwasaidia dhuria wa Mtume."

Akiwa na wivu kwa ajili ya heshima yake, Abdallah bin Umayr alijaribu kumshawishi mke wake arudi hemani kwake haraka sana bila kuchelewa, lakini hakuwa katika hali ya kukubali na alisema, "Sitaweza kukuacha peke yako katika uwanja wa vita, sio kabla ya mimi nami niuawe."

Kisha aliitwa na Husein ambaye alimwambia kwamba wanawake wameondolewa kwenye wajibu wa kupigana vita vya Jihad. Basi alirudia kwa wanawake wa familia ya Husein. Abdallah bin Umar pia alirudi

kutoka kwenye uwanja wa vita.[2]Alijiunga tena kwenye vita katika kipindi cha baadaye na aliuawa kishahidi baada ya Muslim bin Awsaja (kuuawa kishahidi pia).

2. Al-Hurr bin Yazid al-Riyahi alitoka kwenye familia kongwe na tukufu. Attab, wa ngazi ya nne kutoka kwa al-Hurr katika mpangilio wa kupanda wa nasaba yake, alikuwa mmoja wa watumishi maalum wa Nu'man bin al-Muudhir, mfalme wa Hira. Mmoja wa watoto wake, Qays, alipanda akashika madaraka makubwa baada yake. Mjukuu wa Qays, Zayd bin Umar ibn Qays alikuwa mshairi na Sahaba wa Mtume. Alikuwa ami yake al-Hurr, akiwa binamu wa baba yake, Yazid.

Akiwa mmoja wa watu watukufu wa Kufa, al-Hurr alikuwa afisa katika jeshi la Ubaydullah bin Ziyad aliyetumwa katika eneo la al-Qadasiyya kuweka uangalizi mkali katika barabara.

Baadaye aliamriwa kumwinglia kati Husein ili kumzuia asiifikie Kufa. Kama ilivyokwisha sema, al-Hurr alikuwa na uzoefu binafsi wa utukufu wa tabia ya Husein na ukarimu wake wa wazi usio na kupendelea, wakati ambapo, ili kuwatuliza al-Hurr, watu wake na farasi wao kutokana na kiu kubwa ya maji isiyovumilika, Husein aliwapatia wote maji. Baadaye al-Hurr alimlazimisha Husein kuuacha mpango wake wa kwenda al-Kufa na kupiga kambi hapo Karbala katika sehemu iliyo mbali kutoka mtoni. Katika siku ya 10 ya Muharram al-Hurr aliondoka na kulikimbia jeshi la Umar bin Sa'd na kujiunga na sahaba wa Husein.

Al-Hurr alimwomba Husein aruhusiwe kujitoa mhanga maisha yake kabla ya wengine wote, kwani alikuwa yeye ndiye ambaye aliyempa upinzani wa mwanzo. Alipokwisha pata ruhusa ya Husein, al-Hurr aliingia katika uwanja wa vita na akawashambulia maadui kwa juhudi kubwa na uhodari. Hapo mapema, wakati al-Hurr alipokimbia toka jeshi la Umar bin Sa'd, Yazid bin Sufyan al-Tamimi, askari mmoja katika jeshi, alisema kwamba angempatia al-Hurr mchomo mmoja tu wa mkuki wake kama angegundua kutoroka kwake.

Wakati al-Hurr alipokuwa akiutumia upanga wake kwa mafanikio makubwa, afisa mmoja katika jeshi alimkumbusha Yazid bin Sufyani kuhusu nia yake ya kumuua al-Hurr na kwa hilo mtu huyo alimtaka al-Hurr kukubali kupigana naye. Hili likiwa limekwishakubaliwa al-Hurr mara moja alimuua adui yake.[3] Tukio hili liliamsha woga fulani katika nyoyo za adui kiasi kwamba hakuna mtu aliyethubutu kuamka kupigana na al-Hurr ambaye baadaye alitoka kwenye uwanja wa vita. Alikutana na kifo chake baadaye na maelezo mengi kuhusu hilo yatatolewa hivi punde.

3. Muslim bin Awsaja al-Asadi alikuwa ni mfuasi maarufu wa Husein. Mswalihina, aliyependa sana kusimamisha sala za usiku, yeye alimwona Mtume. Alikuwa mpanda farasi mashuhuri na alijipatia sifa kubwa katika vita zilizopita, kama vile katika vita vya kuivamia Azerbayjan nchini Iran katika mwaka wa 20 A.H. Anahesabiwa yeye kuwa chanzo cha kutegemeka cha hadith. Alikuwa ametukuzwa sana katika Uarabu yote.

Baada ya Ubaydullah bin Ziyad kuwa ameteuliwa kuwa gavana wa Kufa, Muslim bin Aqil alikaa na Hani bin Urwa na akachukua jukumu la kuwakusanya wale ambao walitoa kiapo cha utii kwa Husein. Muslim

bin Awsaja sasa alishughulika kama mwakilishi maalumu wa kuchukua viapo vya utii na ahadi ya kuwaunga mkono watu wa nyumba ya Mtume. Inabakia bado ni jambo lisiloeleweka vizuri mahali alipokwenda baada ya kifo cha kishahidi cha Muslim bin Aqil na kwa namna gani alivyopanga kwa ustadi hata kuweza kufika Karbala, akiwa tena na umri uliosonga mbele sana kwa miaka.

Baada ya Abdallah bin Umayr na al-Hurr, Nafi bin Hilal al-Jamali alijiunga katika vita, na akamwuua Muzahim bin al-Harith. Hasara waliyoipata jeshi la Ibnu Ziyad mikononi mwa wafuasi wa Husein ilimtia wasi wasi mkubwa mno Amr bin Al-Hajjaj, na aliwaonya watu wa jeshi lake dhidi ya kukutana na wapiganaji wa Husein katika mapigano ya mmoja kwa mmoja, kwani wanajeshi hawa wa Husein ndiyo askari wapanda farasi walio bora kabisa katika nchi kuliko wengine wote ambao walikuwa wanapigana ili kuokoa maisha yao.

Kisha alilishambulia jeshi la Husein kwa kutumia kikosi chote cha jeshi cha upande wa kulia kikiwa chini yake. Shambulio lilipingwa kwa ushupavu mkubwa kiasi kwamba lilibidi liondolewe, lakini lilimwacha Muslim bin Awsaja akigaagaa chini ardhini ndani ya dimbwi la damu yake. Habib bin Muzahir alimuuliza kama alikuwa na matakwa yoyote yale ya mwisho ayaseme. Muslim alinyoosha kidole kwa Husein kuwa jibu lake na akasema, “Matakwa yoyote ya mwisho niliyo nayo yanamhusu yeye tu (Husein).”

Hivyo alikufa akiwa mfuasi wa kwanza katika wafuasi wa Husein katika kuyatoa mhanga maisha yake kwa ajili ya mjukuu wa Mtume.

Wakati habari za kifo cha Muslim bin Awsaja zilipokuwa zinapokelewa kwa shangwe kubwa katika safu za vikosi vya adui, Shabath bin Ribii, ambaye aliongoza kikosi cha askari wa miguu katika jeshi la Umar bin Sa’d alitokea mbele kwa ghafla akisema, “Fedheha gani hii! Mtu kama Muslim bin Awsaja ameuawa na ninyi mnashangalia kifo chake.4
Naapa kwa Mwenyezi Mungu nimeshuhudia matendo makubwa ya kijasiri na yaliyo magumu mno aliyoyafanya kwa ajili ya Uislamu.” Kifo cha Muslim bin Awsaja kilitia nguvu ari ya kupigana ya askari wa adui.

Kwa hiyo, Shimr bin Dhi Jawshan, alishambulia kikosi cha upande wa kushoto cha jeshi la Husein na alipingwa kwa nguvu nyingi sana. Abdallah bin Umayr ambaye kwamba utajo wa ujasiri umekwisha fanywa alijitahidi tena kwa juhudi kubwa na akawaua askari wawili wa jeshi la adui. Kisha naye akashambuliwa na Hani bin Thubayth al-Hadrami na Bukayr bin Hayy na akauawa, akiwa msaidizi wa pili wa Husein kukutana na mwisho wake.5

Mke wa Abdallah bin Umayr, aliposikia kifo cha mume wake aliingia kwenye uwanja wa mapambano kuona maiti yake na akikaa karibu yake alianza kuondoa vumbi na damu kutoka usoni mwake, akisema, “Pokea hongera zangu kwa kufanikiwa kuipata pepo.” Hata hivyo ukatili uliozidi nguvu, ulimshawishi na kumchochea Shimr kumfanya mama huyu asiye na ulinzi kuuawa.6

4. Burayr bin Hudayr al-Hamadan alikuwa mtu wa Kufa na alikuwa sahaba mtu mzima (mzee) wa Ali bin Abi Talib, mtiifu aliyependa sana kusali. Aiijua Qur’ani kwa moyo na alikuwa akiwaelekeza watu na

kuwafundisha Qur'an ndani ya msikiti wa Kufa na aliitwa kiongozi wa wale watu ambao waliijua Qur'an kwa moyo. Alijiunga na Husein mahali fulani katika njia ya safari yake kwenda Karbala.

Maelezo ya hotuba yake katika kuijibu hotuba ya Husein, na maelezo yake kuonyesha moyo wake mchangamfu wakati ni masaa machache tu yaliyokuwa yamemtenganisha na kifo yamekwishatolewa.

Wakati Yazid bin Maqil alijotokeza mbele kutoka jeshi la Umar bin Sa'd kutoa changmoto kwa sahaba wa Husein kwa mapambano ya mtu mmoja mmoja alimwita Burayr ambaye alimfahamu kwa muda mrefu. Pia walikuwa wamezoea kuhojiana wenyewe kwa wenyewe kuhusu uhalali na uthabiti wa kidini wa misimamo iliyochukuliwa na Ali na Mu'awiyah. Yazid bin Maqil alilirejea suala hilo tena, na iliamuliwa kwamba wote wawili lazima wamwombe Mungu amlaani mwongo katika wawili hao na auawe kwa upanga na yule ambaye yuko katika haki na sawa.

Hapa walianza kupigana hao wawili. Yazid alipiga dharuba la kwanza ambalo lilisababisha majeraha fulani tu ya juu juu, lakini Burayr ambaye alipiga dharuba la pili, liliikata kofia ya chuma ya Yazid, na upanga wake ulipenya ukaingia kichwani mwake. Yazid alianguka chini kutoka juu ya farasi wake.

Wakati Burayr alipokuwa anachomoa upanga wake Radi bin Munwidhi alimshambulia. Akimwangusha chini ardhini, Burayr alimrukia kifuani mwake. Makelele yake yalimleta Ka'b bin Jabir bin Amr al'Asadi kuja kumsaidia. Alimshambulia Burayr, lakini askari mwingine wa jeshi la Umar bin Sa'd alimsihi asifanye hivyo kwani Burayr aliijua Qur'an kwa moyo na aliwafundisha wengine namna ya kuikariri. hata hivyo Ka'ab bin Jabir, alimuua Burayr.7

5. Munhij bin Sahm alikuwa mtoto wa mjakazi wa Husein, aliyeitwa Husayniyya. Alikuwa ameolewa na Sahm, na alimtumikia Ali bin Husein ambaye alifuatana na mwanae katika safari ya Husein huko Karbala. Munhij aliuawa mwanzoni kabisa mwa vita.

6. Umar bin Khalid alikuwa ametoka miongoni mwa watu watukufu wa Kufa na alikuwa mtu mtiifu na mnyenyekevu kwa watu wa nyumba ya Mtume. Hapo mwanzoni alimuunga mkono na kumsaidia Muslim bin Aqil, lakini watu wengi katika wakazi wa Kufa walipomkimbia, na matumaini yote ya kufaulu kwa njia yake hiyo ilibidi yaachwe, Umar bin Khalid alikimbilia mafichoni.

Alipozisikia habari kwamba Husein alikuwa amefika Hajir akielekea Kufa, Umar bin Khalid *mawla* wake, Sa'd, Mujammi bin Abdalah, mtoto wake, Aidh, na Jabir bin al-Harith al-Salmani walijiunga na Husein sehemu iitwayo Udhayb al-Hijanat.

Wakati huo huo al- Hurr alifika hapo kumzuia Husein asiendelee na mwendo wa safari yake, na alipinga kuingizwa kwa Umar bin Khalid na washirika wake katika kundi la Husein. Kwa msisitizo wa Husein, pingamizi hilo liliondolewa.

Katika siku ya 10 ya Muharram, Umar bin Khalid na ndugu zake wanne waliyashambulia majeshi ya adui kwa pamoja na panga zao. Askari wa adui waliwazunguuka watu hawa kuwatenga kutoka sahaba

wengine waliobakia wa Husein.

Husein alimpeleka ndugu yake, Abbas kwenda kuwanusuru. Peke yake, Abbas aliwafukuza maadui, na akawafanya watu hawa majasiri watembee juu ya farasi wao mbele yake ili kuhakikisha usalama wao. Hata hivyo, mara tu walipowaona maadui wanawafuata, walikasirishwa kiasi kikubwa kwamba walifuata wafukizaji wao, wakiwashambulia kwa nguvu zao zote, mpaka kila mmoja wao akafa akipigana katika sehemu hiyo hiyo.8

Maelezo ya Sa'd, Mujammi, A'idh bin Mujammi na Jabir bin al-Harith yanatokea chini ya majina yao yaliyo orodheshwa (7) mpaka kumi (10).

7. Sa'd, *mawla* Umar bin Khalid aliuawa kishahidi kama ambavyo imewisha kuelezwa.

8. Mujammi bin Abdallah alizaliwa wakati Mtume bado alikuwa anaishi. Baba yake alikuwa sahaba wa Mtume na yeye mwenyewe alikuwa sahaba wa Ali ambaye ubavuni mwake alipigana vita huko Siffin. Alimwambia Husein kwamba watu maarufu wa Kufa wamehongwa na wameuza uaminifu wao kwa serikali, na kwa hiyo, wote walikuwa dhidi yake. Nyoyo za watu wa kawaida zilikuwa, kwa mujibu wake, zinapendelea upande wa Husein, lakini katika wakati wa vita, panga zao zingegeuzwa kuwa dhidi yake. Aliuawa kishahidi kama ilivyokwishaelezwa.

9. A'idh bin Mujammi alikuwa mtoto wa Mujammi bin Abdallah na aliuawa kishahidi kama ilivyokwisha elezwa.

10. Jabir bin al-Harith al-Salmaani, mtu mashuhuri katika Shi'a wa Kufa alizaliwa wakati wa uhai wa Mtume na alipigana upande wa Ali katika vita vya Siffin. Alitoa kiapo cha utii kwa Husein kwa kupitia mkono wa Muslim bin Aqil, na alishiriki katika vita ambavyo Muslim bin Aqil alivipanga. Hata hivyo, mambo yaligeukia kwenye maangamizi kwa upande wa Muslim bin Aqil na Jabir akajificha. Alikipata kifo cha kishahi- di kama ambavyo imekwishaelezwa.

11. Jundub bin Hujr al-Kindi alikuwa mtu mwenye kujulikana sana, maarufu wa kundi la Shia wa Kufa na sahaba wa Ali bin Abi Talib. Aliongoza vikosi vya Kinda na Azd katika vita vya Siffin. Alikutana na Husein katika safari yake ya kwenda Kufa kabla ya kufika kwa al-Hurr kudhibiti maendeleo yake kuelekea Kufa. Alikufa akipigana kwa ajili ya Husein katika hatua za mwanzo za vita vya tarehe 10 Muharram hapo Karbala

12. Yazid bin Ziyad ibn Muhaasir al-Kindi alikuwa askari shujaa kutoka kwa Shi'a wa Kufa. Alijiunga na Husein kabla ya kuwasili kwa al-Hurr, na alibakia naye Husein katika safari yake. Wakati wa kukaribia Karbala, mjumbe wa Ibnu Ziyad alimletea Hurr barua ikimwelekeza kumlazimisha Husein avunje safari yake haraka sana mara tu al-Hurr atakapoipata barua hii, Yazid bin Ziyad alimtambua mjumbe kuwa mtu atokanaye na ukoo wake mwenyewe wa Kindi. Kwa hiyo, yeye alimkaripia sana na kumlaumu kweli kweli kwa kuleta ujumbe wa kimakosa, wenye dhambi.9

Alikuwa bingwa wa kupiga mishale, na katika tarehe 10 ya Muharram (61 A.H) alipiga mishale mia moja, ilikuwa ni mitano tu ambayo ilikosa sehe- mu zao zilizokusudiwa kupiga. Alipofikia mwisho wa mishale yake, aliingia kwenye uwanja wa vita ambako aliuawa mwanzoni tu wa vita hivyo.[10]

## Shambulio La Kwanza La Jumla

Haishangazi sana zaidi ya inavyokumbukwa kwamba kundi la wafuasi wa Husein wasiozidi watu 150 kwa nje, wakiwa wamechakazwa na kiu ya siku tatu, wangeweza sio tu kulizuia jeshi la Umar bin Sa'd lililokuwa na watu wasiopungua 30,000, bali pia wangefanya mashambulio ya mara kwa mara na yenye mafanikio, ndani ya jeshi la adui wapanda farasi na kulifanya kuwa mchafukoge (vurugika).

Mapigano haya yasiyolingana yaliendelea hivyo hivyo kuanzia asubuhi mpaka karibu ya mchana, na maafisa wa jeshi la adui waliona ugumu kuamua juu ya njia ya utendaji hatua iliyokadiriwa vizuri mno kwa kuleta mwisho wenye kufaa na wa mapema sana.

Baada ya mabishano fulani kati ya makamanda wa majeshi ya wapanda farasi na wa askari wa miguu, Husein bin Tamin alielekezwa aende na jeshi lililowekwa eneo la al-Qadisiyya kufunga njia zote za kuingia na kutoka za Kufa. Pia alipewa wapiga mishale 500 kupiga mishale kwenye kambi ya Husein bin Ali.[11]

Mvua ya hakika ya vyuma vyenye ncha lazima vitakuwa viliwaangukia Husein na sahaba zake ambao walikabiliana na shambulio hili kishujaa, wakitumia panga zao kama ngao zao, na wakafanya shambulizi kubwa la dhamira juu ya adui, shambulio hili kubwa ambalo lilishuhudia mapigano makali sana linaitwa shambulio la kwanza la jumla na lilifanywa saa moja kabla ya kuingia adhuhuri. Wakati wafuasi wa Husein walipowarudisha nyuma adui, walipata hasara kubwa sana. Watu hamsini kati ya idadi yao ndogo waliuawa na kadhalika farasi wao wote.

Haiwezekani kutambua mpangilio ambao ndani yake watu hawa hamsini wafuasi wa Husein waliuawa lakini majina yao yametolewa moja moja au katika makundi kama ilivyoonyeshwa hapo chini na maelezo mafupi ya maisha yao pia yametolewa pale ilipowezekana:

Al-Harith bin Banhaan
Shabib bin Abdallah al-Nahshali
Qarib bin Abdallah
Nasir bin Nayzar.

Hawa walifuatana na Husein kutoka Madina. Al-Harith alimtumikia Ali, na kisha Hasan na kisha akafuatana pamoja na Husein katika safari yake. Shabib alipigana upande wa Ali kwenye vita vya Ngamia (Jamal), Siffin na Nahrawan. Mama yake Qarib, aitwaye Fakiha alimtumikia mama yake Sakina, mke wa Husein. Baba yake Nasr alikuwa na nasaba ya kifalme na alifundishwa na Mtume. Nasr alitumia ujana wake akiwa katika kundi la Ali, na kisha akabakia katika kuambatana na watoto wake.

Janada bin Ka'b al-Ansar,
Abd al-Rahman bin Abd Rabb al-Ansar alijiunga na Husein mjini Makkah, Jabir bin Hajjaj al-Taymi,
Jabla bin Ali al-Shaybani,
Hubab bin Amir bin Ka'b al-Taymi, na
Zarghama bin Malik al-Taghlabi.

Hawa hapo mwanzo walimuunga mkono Muslim bin Aqil, lakini wakati Ubaydullah bin Ziyad alipofanikiwa kuwageuzia mbali watu katika kumuunga mkono na kumsaidia, walikimbia kwenda kujificha, na baadaye walipoisikia safari ya Husein ya kwenda Kufa, walipanga kuungana naye hapo Karbala.

Al-Harith bin Imru al-Qays bin Abis al-Kindi,
Juwayn bin Malik bin Qays al-Taymi,
Halas bin Amr al-Azd,
Ndugu yake al-Nu'man,
Zuhayr bin Salim bin Amr al-Azdi,
Mas'ud bin al-Hajjaj al-Taymi,
Abd al-Rahman bin Mas'ud,
Abdallah bin Bishr al-Khath'ami,
Amr bin Zabi'a bin Qays al-Taymi,
Qasim bin Habib bin Abi Bishr al-Azdi.

Hawa waliwasili Karbala na jeshi la Umar bin Sa'd. Abd al-Rahman bin Mas'ud na Masud bin Hajjaj walikwenda kwa Husein tarehe 7 Muharram kutoa heshima zao kwake na kamwe hawakurudi tena kwenye uhudumu wao wa kijeshi. Watu watano wa kwanza katika kundi hili walivuka na kwenda kwa Husein wakati mapendekezo yote ya kuleta amani yaliy- ofanywa naye yalipokataliwa, na vita ikawa haikwepeki. Wale wengine watatu pia waliobakia walikwenda kwake katika nyakati zisizojatwa maalum.

Shi'a wa Basra walikuwa wakikutana katika nyumba ya mama mmoja, aliyeitwa Mariyya, bint ya Munqidh, ambaye alikuwa kipenzi cha watu wa nyumba ya Mtume. Wakati habari zilipofika Basra kuhusu safari iliyokusudiwa ya Husein kwenda Kufa, na kufungwa kwa barabara zielekeazo katika mji huo na gavana wa Basra, Yazid bin Nubayt alionyesha nia yake ya kwenda kumsaidia Husein. Kwa vile mpango huo ulikuwa wa hatari, watu wengi hawakuungana na shauku hiyo ya Yazid. Hata hivyo, aliondoka kwenda safari hii ya hatari pamoja na watoto wake wawili:

Abdallah, na Ubaydullah,[12]
Adham bin Umayyah,
Sayf bin Malik al-Abdi,
Amir bin Muslim al-A'bdi al-Basri,
Salim, mtumwa wa Amir bin Muslim.

Walikutana na Husein sehemu iitwayo al-Abtah ndani ya mipaka ya Makkah, na wakafuatana naye kwenda Karbala.

Mtumwa mwaminifu wa Hasan, kwa jina aliitwa Salim, aliuawa pia kishahidi katika shambulio hili. Inaonekana kwamba katika mwendo wa safari yake, Waarabu wengi walivutiwa na msafara wa Husein kwa matu- maini yasiyo na msingi, na kwamba walimwacha mara tu walipoutambua ukweli. Lakini wengine waliambatana naye na waliuawa katika mapigano ya mwanzoni. Hao walikuwa ni:

Abd bin Muhajir al-Juhani,
Uqba bin Salat al-Juhami,
Mujammi bin Ziyad bin Amr al-Juhani,
Qasit bin Zuhair bin al-Harith al-Taghlabi,
Muqsit, pia ndugu wa Qasit,
Kardus, pia ni ndugu wa Qasit.

Ndugu hawa walikuwa masahaba wa Ali. Kisha waliungana na kundi la Husein mpaka alipoondoka kwenda Madina. Baada ya hapo ndugu hawa walifanya makazi hapo Kufa na kwa kufika kwa Husein hapo Karbala waliweza kuungana naye.

Umayyah bin Sa'd bin Zayd al-Tai alikuwa mkongwe aliyebobea ambaye alipigana katika vita vya Siffin akiwa katika upande wa Ali. Alifika Karbala wakati Husein alikuwa anafanya mazungumzo ya kupatikana amani na Umar bin Sa'd.

Zahir bin Amr al-Kind alikuwa Sahaba wa Mtume. Alishiriki katika vita vya Khaybar, na alifahamika sana kwa ushujaa wake, na alikuwa na mapenzi makubwa na Ahlul-l'Bait. Wakati Ziyad alipokuwa gavana wa Kufa na Amr bin Hamiq al-Khuzai akasimama kuwa dhidi yake, Zahir alijiunga naye. Hata hivyo, alifanikiwa kujificha na akakwepa kukamatwa.
Aliitekeleza ibada ya Hijja katika mwaka wa 60 A.H. na akakutana na Husein, na aliungana na vikosi vya kijeshi vya sahaba wake alibakia pamoja naye na akafuatana naye kwenda Karbala.

Suwar bin Abi Umayr al-Nahmi alikuwa msimulizi wa hadith ambaye alifika Karbala baada ya Husein akiwa amefungua mazungumzo ya amani. Tarehe 10 ya Muharram alishiriki katika Jihad hiyo, alijeruhiwa na akakamatwa na akapelekwa kwa Umar bin Sa'd ambaye alitaka kumuua.

Askari watokanao na kabila lake walilipinga hili na wakamwondoa. Hata hivyo, alikufa kutokana na majeraha.

Shabib ibn Abdallah alikuwa mtu wa Kufa na alikuwa *mawla* wa al-Harith bin Sari al-Hamadani, na Sahaba Mtume. Alishiriki katika vita vya Ngamia (Jamal), Siffin na Nahrawan akiwa upande wa Ali na akafika Karbala akiwa pamoja na Sayf na Malik, watoto wa bwana wake.

Abd al-Rahman bin Abdillah bin Kadan al-Arhabi alikuwa mmoja kati ya ujumbe wa pili wa watu wa

Kufa ambao uliomwona Husein. Baada ya kuuawa kwa Muslim bin Aqil na kufika kwa Husein hapo Karbala aliweza kuungana na Husein.

Ammar bin Abi Salama al-Dulani alipigana upande wa Ali katika vita vya Ngamia (Jamal), Siffin, na Nahrawan.

Ammar bin Hasan al-Ta'ai alikuwa Shia maarufu sana. Baba yake aliuawa katika vita vya Siffin, akiwa sahaba wa Ali. Ammar alifuatana na al-Husain kutoka Makkah hadi Karbala.

Kinana bin Atiq al-Taghlabi alikuwa mtu wa Kufa, na alikuwa maarufu kwa ujasiri wake. Alikuwa msimamishaji Sala na aliijua Qur'an kwa moyo. Alijiunga na Husein hapo Karbala kabla ya vita havijapiganwa.

Muslim bin Qasir al-Azdi alifanywa kuwa mlemavu wakati akipigana kati- ka Vita vya Ngamia (Jamal). Alitokea Kufa kumsaidia Husein.

Na'im ibn Ajlan al-Ansari na ndugu zake, Nasr na al-Nu'man, walikuwa masahaba wa Ali. Kaka yake alimtangulia kufa. Wakati Husein alipowasili Iraq, Na'im aliweza kuungana naye Karbala akitokea Kufa.

Habsha bin Qays al-Nahmi alikuwa mjukuu wa sahaba wa Mtume, na yeye mwenyewe alikuwa msimulizi wa hadith.

Hajjaj bin Zayd al-Taymi alikuwa mtu wa Basra. Wakati akiondoka Makkah, Husein alipeleka barua kwa watu mashuhuri wa Basra, pamoja na Mas'ud bin Amr al-Azd. Mas'ud alikusanya watu wa koo za kabila lake za Bani Tamimi, Bani Hanzala, Bani Sa'd na Bani Amir na aliwasihi na kuwashawishi kwenda kumpa msaada Husein, na kundi moja la watu miongoni mwao liliahidi kufanya hivyo.

Mas'ud aliandika barua katika kujibu na aliikabidhi kwa al-Hajjaj ili aifikishe kwa Husein. Mjumbe ali- itoa barua na pia alijitoa mhanga maisha yake kwa ajili ya Husein.

Habab bin al-Harith
Hanzal bin Umar al-Shaybani
Zuhayr bin Busr al-Khath'ami
Imran bin Ka'b al-Ashjai
Maani' bin Ziyad

Hakuna lolote linalojulikana kuhusu watu hawa.

## Mashambulizi Katika Kambi Ya Husein

Wakitiwa moyo (wa kupigana) kutokana na askari wengi waliouawa kutoka kwenye kikundi kidogo cha Husein chenye askari waaminifu, na mashujaa, jeshi la Umar bin Sa'd lilianzisha mashambulizi katika kambi ya Husein. Lengo lao lilikuwa kufika nyuma ya kambi ya Husein, na kuwazunguka watu wake kwa

nyuma ambako kulisimama safu za mahema ya watu wa Husein yaliyofungwa kwa kukamatana moja moja kwa kamba kwa umadhubuti na uimara kiasi kwamba yaliyoonekana kama ukuta imara au ngome.

Alipoona hivi, Umar bin Sa'd aliamuru kamba zikatwe. Wanajeshi wa Husein hapo walirudi kwenye mahema na wakawashitukiza na kuwaua wavamizi wale. Kwa kushindwa huku kwa jaribio lake la kutaka kuwazunguuka wapiganaji wa Husein, Umar bin Sa'd aliamuru mahema yachomwe moto. Kuungua kwa mahema yenyewe kulilishinda lengo na kusudio la adui, na katika kukasirika Shimr alitaka kulichoma hema la Husein moto ili kuwaua watu wote waliokuwemo ndani yake.

Shabath bin Rib'ii, kamanda (kiongozi) wa kikosi cha miguu katika jeshi la Umar bin Sa'd alimwambia Shimr, "Bado mpaka sasa sijawahi kusikia jambo lenye dhambi kubwa zaidi ya hili likitamkwa." Hakuruhusiwa kutekeleza mipango yake ya kikatili na upinzani uliotolewa na watu wa kundi lake mwenyewe. Wakati huo huo Zuhayr bin al-Qayn alifanya shambulio kali kwa adui kwa msaada wa marafiki zake kumi, na kumrudisha sana nyuma Shimr, akaua mmoja wa watu wake mashuhuri. Tukio hili liliwakasirisha maadui na wakafanya shambulizi kali la nguvu la kujibu, na kusababisha umwagaji mwingi wa damu. Adui alishindwa tena.

Wafuasi wawili tu wa Husein ndio walipoteza maisha yao. Walikuwa ni: Bakr bin Hayy al-Taymi ambaye alijiunga na Husein baada ya kuja Karbala na majeshi ya Umar bin Sa'd.

Amr bin Janaada bin Ka'b al-Khazraji, kijana aliyekuwa mdogo wa karibu miaka kumi ambaye alifuatana na wazazi wake kuja Karbala. Baada ya baba yake kufa kishahidi hapo Karbala katika shambulio kubwa la kwan- za la adui, mama yake alimwelekeza apigane kwa ajili ya al-Husein. Amr alimuomba Husein ruhusa afanye hivyo, lakini ruhusa haikutolewa.

Amr aliomba kwa kusihi kwamba mama yake mwenyewe alimwagiza kupigana kwa ajili ya Husein. Basi alipata ruhusa ya kwenda kupigana. Aliingia kwenye uwanja wa vita na askari wa upande wa adui walimkata kichwa. Kwa hili mama yake akasema kwa sauti kubwa, "Vizuri sana, mwanangu! Umeufariji mno moyo wangu katika kuyatoa maisha yako mhanga kwa ajili ya Husein." Adui walimtupia mama yule kichwa cha mwanawe, laki- ni aliwarudishia kichwa hicho, na akiokota rungu la chuma alikwenda kupambana na maadui yeye mwenyewe. Alikatazwa na Husein asifanye hivyo kwani wanawake wamesamehewa katika kupigana Jihad.

## Mashambulizi Wakati Wa Sala Za Mchana

Wakati huo saa ya sala za mchana ikaingia. Abu Thumaama Amr bin Abdallah al-Saa'id alimwelezea Imam Husein kwamba maadui walikuwa wamemsogelea karibu sana, na akaonyesha haja ya kusimamisha Sala za mchana na Husein kwani zingekuwa ni za mwisho katika uhai wake ambazo angezifanya na Imam. Husein alimtaka awaombe watu wa upande wa adui kusimamisha mapigano katika kipindi chote cha Sala. Husein bin Tamim alitokea ndani ya vikosi vya jeshi na alisema, "Sala zenu hazi- takubaliwa."

Habib bin Muzahir alirudia tena, “Hazitakubaliwa? Je, unad- hania kwamba Sala za mtoto wa Mtume hazikubaliwi, na za kwenu ndiyo zinakubaliwa?” Hili lilipelekea Husein bin Tamin kumshambulia Habib, na mapambano ya watu wawili hawa yakafuatia, na Husein bin Tamim alishindwa vibaya sana katika mapambano hayo, lakini aliondolewa akapelekwa kwenye usalama.

Habib bin Muzahir sasa aliingia katika orodha. Alikuwa miongoni mwa masahaba mashuhuri wa Ali kama Mitham al-Tammaar na Rashid al-Hijrii na pia mmoja katika sahaba zake na sahaba wa Hasan na Husein.
Itakumbukwa kwamba alikuwa amechukua nafasi muhimu katika kuzifadhili harakati za kumwita Husein kuja Kufa na kwamba barua ya kwanza aliyoandikiwa na shia wa Kufa ilikuwa ina sahihi zake. Pia, katika kufika kwake Kufa,

Muslim bin Aqil aliahidiwa kila aina ya msaada kutoka kwake. Katika mahala pengine mbali mbali, Habib alijaribu kuhojiana na maadui wa Husein juu ya njia zao za kiuovu. Katika mkesha wa tarehe 10 ya Muharam, alikuwa amepata idadi ya juu ya watu wa ukoo wa Bani Asad ambao walikuwa wanaishi katika maeneo ya Karbala kumuunga mkono Husein. Umar bin Sa’d, hata hivyo, alitishika na ujumbe wa Habib, na alipeleka askari mia tano (500) waliopanda farasi ili kuwazuia Bani Asad wasimfuate Habib.

Habib alikuwa kamanda wa kikosi cha kushoto cha jeshi la Husein, na alipigana kwa ujasiri mkubwa na alimuua askari mmoja wa Bani Tamimi kwa pigo moja la upanga wake. Askari mwingine wa upande wa adui alimshambulia kwa mkuki, na Habib akaanguka chini kutoka juu ya farasi wake na adui yake ambaye hapo kwanza alikuwa amemshinda, Husein bin Tamim alimpiga kichwani kwa upanga wake na Habib akaanguka chini akiwa amekufa. Kifo cha kishahidi cha Habib kwa uwazi kabisa kilimwathiri Husein.

Mwisho wa Jihad ya al-Hurr sasa inabakia kuelezewa. Farasi wake alikuwa amekwishauawa. Baada ya kifo cha Habib, al-Hurr aliamua kujitoa mhanga mwenyewe. Alianza kupigana sambamba na Zuhayr bin al-Qayn lakini mpango huu ulivunjika kutokana na shinikizo la jeshi la miguu ambalo lilimtenganisha na kumzunguuka al-Hurr. Al-Hurr kwa matokeo ya hali hii alipigwa akaanguka chini.

Wakati mwili wa al-Hurr ulipokuwa unarudishwa kutoka uwanja wa vita, Husein mwenyewe aliondoa vumbi na damu kutoka kwenye uso na akasema, “Al-Hurr, wewe uko huru katika dunia hii na pia katika ulimwengu ujao.”

Abu Thumaama al-Saa’idi, mpanda farasi hodari sana nchini Uarabuni mtu maarufu sana katika Shi’a wa Ali ambaye aliambatana naye katika vita vyote alivyopigana (Ali), akaufanya mji wa Kufa makao yake baada ya Hasan kuondoka mjini pale. Alimuunga mkono na kumsaidia Muslim bin Aqil kwa nguvu zote baada ya yeye (Muslim bin Aqil) kuwasili Kufa.

Wakati hali ilipokuwa ni ya hatari, Muslim bin Aqil akamkabidhi Abu Thumama mafungu ya pesa na kazi ya kumkusanyia silaha. Baada ya kifo cha kishahidi cha Muslim bin Aqil, Abu Thumama aliondoka Kufa na Naafii bin Hilal na akajiunga na Husein katika safari yake ya kwenda Iraq.

Katika siku ya 10 ya Muharram alielezea kwa Husein haja yake ya kujiunga kwenye Sala zitakazoongozwa naye (Husein) kabla ya kwenda kukutana na Mola wake. Husein alimbariki Abu Thumama kwa kukumbuka kusimamisha Sala katika wakati kama huu wa hatari. Pia alimtuma kwamba watu wa upande wa adui waombwe kusimamisha vita katika kipindi chote cha kusimamisha Sala. Hili lilisababisha mlipuko wa vurugu na ghasia ambazo ndani yake Abu Thumama alikuwa miongoni mwa wale ambao waliuawa.

## Sala Ya Adhuhuri

Mapigano hayakusimamishwa. Katika nyakati za hatari na hofu muundo wa Sala fupi umeelekezwa, unaoitwa *"salat al-Khawf,'* yaani Sala ya hofu. Akiwa na imani kamili katika uthabiti na ushujaa wa sahaba zake, Husein alimwelekeza Sa'id ibn Abdallah al-Hanafi na Zuhayr bin al-Qayn kusimama mbele yake ili kwamba aweze kuswali Sala ya mchana (ya adhuhuri).

Wote sahaba wawili hawa wajitoleao mhanga nafsi zao wenyewe walisonga mbele pamoja na karibu nusu ya wafuasi wote wa Husein, na wakisimama mbele yake, walimkinga kama alivyoelekeza.

Sa'id bin Abdallah al-Hanafi alikuwa mtu maarufu miongoni mwa Shi'a wa Kufa na alifahamika kwa ujasiri na uchamungu wake. Alikuwa ameahidi msaada wa uaminifu kwa Muslim bin Aqil pindi atakapowasili Kufa.
Alithibitisha ukweli wa maneno haya fasaha ambayo kwayo, mnamo usiku wa mwezi 10 ya Muharram, yeye aliahidi kuyatoa mhanga maisha yake kwa ajili ya Husein, kwa kusimama pamoja na Zuhayr bin al-Quyn mbele ya Husein kumkinga asipatwe na mishale wakati akisimamisha Sala zake za mchana.

Si chini ya mishale kumi na tatu ilimwingia mwilini mwake kabla ya kumalizika kwa Sala. Kisha alianguka chini akafariki.

Zuhayr bin al-Qayn bin Qays al-Bajali alikuwa mtu wa Kufa na alikuwa miongoni mwa watu wa daraja kubwa kidogo wa Uarabuni. Alipigana kati- ka vita nyingi, alihesabika kwa ujumla kuwa miongoni mwa wale ambao wakidai ulipizaji kisasi kwa ajili ya Uthman, wafahamikao kama wa Uthmaniyya kama watofautishwavyo kutoka Alawiyya, ambao walikuwa wafuasi wa Ali.

Tayari ilikwishaelezewa kwa kurudia jinsi gani katika kurudi kwake baada ya kufanya ibada ya Hija mwaka ule, alikutana na Husein sehemu iitwayo Zarud na jinsi gani kwa haraka na kwa ukamilifu alivyobadilishwa kuingia katika itikadi za Husein.

Aliwekwa kukiongoza kikosi cha majeshi ya Husein. Kuonyesha huruma na upendo, kwa maneno na vitendo, juu ya utiifu wake wa kudumu kwa Husein pia vimekwisha tajwa. Alipewa jukumu la kusimama na Sa'id bin Abdallah al-Hanafi mbele ya Husein kumkinga kutokana na mishale wakati wa kusimamisha Sala zake za mchana. Sa'id alikufa kutokana na majeraha yaliyosababishwa na mishale na Zuhayr pia alikuwa amejeruhiwa vibaya sana. Wakati alipoona kwamba maadui walikuwa kwa hatari sana wako karibu na Husein alifanya shambulizi lake la mwisho na akafa akipigana.

Salman bin Muzarib bin Qays al-Bajali, binamu yake Zuhayr bin al-Qayn alifuatana na Zuhayr na aliuawa kishahidi wakati wa mchana ule.

Amr bin Quraaza bin Ka'b al-Ansaar alikuwa mtoto wa Sahaba wa Mtume na alikuwa mtu wa Kufa. Alifika Karbala katika mwezi wa Muharram mwaka wa 61 A.H. na alitumwa na Husein kwa Umar bin Sa'd apendekeze kwake kufungua mazungumzo ya amani. Wakati wa mchana wa mwezi 10 ya Muharram, Amr alingia katika vita na baada ya kufanya mapigano kiasi fulani alirudi kwa Husein kwenda kumlinda kutokana na mishale, akiutumia mwili wake mwenyewe kama ngao mpaka akauawa kishahidi.

Nafi' bin Hilal al-Jamali alikuwa mkubwa wa kabila lake na aliijua Qur'an kwa moyo. Alipigana katika upande wa Ali katika vita vya Ngamia (Jamal), Siffin na vya Nahrawan na akajiunga na Husein katika safari yake akienda Iraq. Wakati adui alipoanza kuzuia maji yasimfikie Husein, alienda na Abbas na watu wengine ishirini kuchukua maji kwa nguvu.

Waliwasukuma nyuma walinzi waliowekwa hapo mtoni na wakafanikiwa kuleta kiasi cha maji kwenye kambi ya Husein. Nafi' alikuwa bingwa wa kutumia upinde na katika mchana wa tarehe 10 ya Muharram aliwaua watu kumi na mbili wa maadui mbali na kuwajeruhi wengine wengi kwa mishale yake. Alikamatwa na maadui na mikono yake yote miwili ilivunjwa. Alichukuliwa akapelekwa kwa Umar bin Sa'd ambako Shimr alimuua wakati ambapo Nafi' alimshukuru Mwenyezi Mungu kwamba alikuwa anakufa mikononi mwa viumbe Vyake walio wabaya mno kuliko viumbe vingine vyote.

Shawdhab bin Abdallah alikuwa mtumwa wa Abis bin Abi Shabib al- Shakri na alifuatana na bwana wake kwenda Makkah. Huyu Abis bin Abi Shabib al-Shakri alimletea Husein barua moja kutoka Kufa iliyoandikwa na Muslim bin Aqil.

Wote wawili bwana na mtumwa walifuatana na Husein katika safari yake ya kwenda Karbala. Wakati alipoulizwa na bwana wake siku ile ya tarehe 10 ya Muharam kuhusu kipi amepangilia cha kukifanya, Shawdhab mara moja alijibu kwamba alikuwa hana nia nyingine yoyote ile isipokuwa kupigana kwa ajili ya Husein na kuuawa. Shawdhab kisha alitoa heshima zake za mwisho kwa Husein na alitoka kwenda kupigana na akafa kifo cha kishahidi.

Abis bin Abi Shabib al-Shakhri alikuwa miongoni mwa viongozi wa Shi'a wa Kufa, ni mzungumzaji wa busara, msalihina sana, na aliyezoea kukesha wakati wa usiku. Wakati Muslim bin Aqil alipoisoma barua ya Husein kwenye mkusanyiko wa watu wa Kufa, yeye Abis alitoa hotuba yenye ushawishi mkubwa na alimhakikishia Muslim msaada wake kwa kipindi atakachoishi.

Baada ya watu 18,000 walipokwishatoa kiapo cha utii kwa Husein, Muslim aliandika barua kwa Husein, akiipeleka kwa kumtumia Abis ambaye alikwenda pamoja na mtumwa wake Shawdhab, na walitoa barua hiyo kwa Husein huko Makkah. Abis na mtumwa wake kisha walisafiri pamojna na Husein kutoka Makkah kwenda Karbala. Baada ya Shawdhab kujitoa mhanga maisha yake, Abis alimwomba Husein kumruhusu kuingia katika uwanja wa mapambano.

Akiipokea ruhusa hiyo, Abis aliziendea safu jeshi la upinzani (adui), na akatoa changamoto kwa mtu yeyote katika majeshi ya adui atoke kupam- bana naye katika mapambano ya ana kwa ana. Hata hivyo, hilo ni tishio alilolitoa yeye kiasi kwamba hakuna hata mtu mmoja aliyethubutu kuikubali changamoto yake hiyo. Umar bin Sa'd aliamuru kwamba Abis apigwe mawe mpaka afe.

Kwa hiyo mawe yalianza kummiminikia Abis kutoka pande zote. Katika mapigano ya namna ya woga wa namna hii, Abis aliondoa kofia yake ya chuma na akawashambulia maadui, akipepea upanga wake, na kuwaswaga mamia ya askari mbele yake. Kisha idadi kubwa ya maaskari walimzunguka na wakamuua.

Abdallah na Abd al-Rahman bin Urwa walikuwa wajukuu wa Haraaq al-Ghiffar, sahaba wa Ali. Walifika Karbala wote pamoja na wakajitoa mhanga maisha yao kwa ajili ya Husein katika mchana wa mwezi 10 ya Muharram.

Hanzala bin Asad al-Shaybaani alikuwa mtu maarufu katika Shi'a wa Kufa, na alikuwa mzungumzaji mzuri. Aliijua Qur'ani kwa moyo. Alijiunga na Husein hapo Karbala, na tarehe 10 ya Muharram wakati wa mchana, baada ya wafuasi (wapenzi) wengi wa Husein walipokuwa wamekwishauawa, aliwahutubia maadui, akiwaonya kwa ukali kuhusu njia mbaya na ya dhambi walioichukua. Aliwataka waogope ghadhabu na hasira za Mwenyezi Mungu katika Siku ya Hukumu, na wajizuie kumuua Husein. Kisha alienda kupigana, na baada ya muda kidogo, aliuawa.

Saif bin al-Harith bin Sari na Malik bin Abd bin Sari bin Jabir al-Hamadani walikuwa mabinamu wa kwanza. Walijiunga na Husein hapo Karbala wakati majadiliano ya kuleta amani yalikuwa bado yanaendelea kati ya Husein na Umar Sa'd. Wote wawili walikufa wakipigana kwa ajili ya Husein.

Jawn, Mhabeshi, alikuwa mtumwa wa Fadhl bin Abbas bin Abdul Muttalib ambaye alimuuza kwa Ali. Ali alimtoa zawadi kwa Abu Dharr. Baada ya kifo cha Abu Dharr, Jawn alirejea Madina kumtumikia Ali, Hasan na Husein kwa mfuatano wa mmoja baada ya mwingine. Tarehe 10 ya Muharram, alisisitiza juu ya kujitoa mhanga maisha yake kwa ajili ya Husein ili kuweza kuipata pepo. Aliona haiwezekani kabisa kumtelekeza Husein katika wakati wa dhiki na taabu zake. Alikwenda kupigana na baada ya muda fulani aliuawa.

Mtumwa wa Kituruki alitolewa kwa Husein na mwanawe, Ali Zainul- Abidiin. Aliihifadhi Qur'ani kwa moyo. Alipokwishapata ruhusa ya kupigana, aliingia katika uwanja wa vita, na baada ya kuawa askari wengi wa upande wa maadui alianguka chini akiwa amejeruhiwa vibaya sana. Husein alimwendea, na akaweka mikono yake kuzunguka shingo yake, wakati uso wake ukiwa umegusana na uso wa mtumwa anayekufa, aka- fungua macho yake, akatabasamu na (kisha) akafariki dunia.

Anas bin al-Harith al-Asadi alikuwa miongoni mwa Masahaba wa Mtume na alisimulia hadith zake. Alimsikia Mtume akitabiri mhanga utakaotole- wa na Husein, na akawa ametamani kuwa katika upande wake (Husein), kama tukio hilo lingetokea katika uhai wake.

Anas alikuwa mzee sana wakati wa Vita vya Karbala vilipopiganwa. Alifika Karbala akiwa na Husein na

alipopata ruhusa ya kupigana, aliziamsha nyusi zake za macho zilizolegea kwa kuzikaza kwa kitamba, na alijifunga kiunoni barabara kwa kilemba chake, na akafa akipigana kwa ajili ya Husein.
Hajjaj bin Masruq al-Jufi alikuwa ni Shi'a wa Kufa aliyeheshimiwa sana, na sahaba wa Ali. Alijiunga na Husein kule Makkah na alikuwa ndiye mwadhini wa Sala zilizoongozwa na Husein. Alipigana na aliua watu wengi wa upande wa maadui. Hatimaye aliuawa kishahidi.

Ziyad bin Arib al-Hamdani alikuwa mwenye kufanya ibada (kusimamisha Sala), mwenye kujihini na alikuwa akitukuzwa kwa ushujaa wake. Alifanya mashambulizi ya ari kubwa na hatimaye aliuawa kishahidi.

Salim bin Amr bin Abdallah alikuwa mtumwa wa ukoo wa Bani Kalb wa Madina. Aliungana na Muslim bin Aqil wakati Musilm bin Aqil alipopigana kwa kuokoa maisha yake. Baada ya Muslim kujitoa mhanga maisha yake Salim alikamatwa, lakini alifanikiwa kutoroka na kujificha. Wakati aliposikia habari za kuwasili kwa Husein hapo Karbala, aliungana naye na akauawa kishahidi siku ile ya mwezi 10 ya Muharram.

Sa'd bin al-Harith alikuwa mtumwa wa Ali ambaye alifuatana na Husein kutoka Madina hadi Karbala ambako aliuawa kishahidi.

Umar bin Jundab al-Hadrami alikuwa mmoja wa Shi'a wa Kufa, na alipi- gana katika upande wa Ali katika Vita vya Jamal (ngamia) na Siffin. Katika mwaka wa 51 A.H., wakati Hujr bin Adi alipokosana na serikali ya Bani Umayyah, aliungana na wafuasi wa Hujr, lakini wakati Hujr alipokamatwa na kupelekwa Syria Umar alijificha. Alikuwa mmoja wa watu waliomuunga mkono Muslim bin Aqil na kwa siri wakaungana na Husein baada ya kifo cha kishahidi cha Muslim bin Aqil na yeye aliuawa kishahidi tarehe 10 ya Muharram 61 A.H.

Qa'nab bin Amr al-Numari alikuwa mtu wa Basra, na aliipata shahada siku ya mwezi 10 Muharram pale Karbala. Yazid ibn Thubayt al-Abdi alikuwa mtu wa Basra. Mazingira ambayo kwamba alikiongoza kikundi cha wakazi wa Basra kwenda kwa Imam Husein na akakutana naye pale al-Abtah karibu na Makkah, habari zake zimekwisha simuliwa tayari kwenye maelezo ya kujitoa mhanga maisha ya watoto wake, Abdallah na Ubaydullah. Alikwenda kupigana Siku ya tarehe 10 ya Muharam baada ya watoto wake walipokwishauawa na yeye alili- pata taji la kishahidi.

Yazid bin Mughfil al-Ju'fi alikuwa mmoja wa masahaba wa Ali, na alikuwa ameteuliwa kukiongoza kikosi cha kulia cha jeshi lililopelekwa kuzima maasi ya Ahwaz. Alipigana katika vita vya Siffin katika upande wa Ali. Tarehe 10 ya Muharram alipigana na maadui wa Husein na akapata shahada (akauawa kishahidi).

Rafi bin Abdallah alikuwa mtumwa wa Muslim ibn Qasir, yuke aliyekuwa mlemavu. Baada ya kufika Karbala na bwana wake, alipigana kwa ajili ya Husein na aliipata shahada siku ya tarehe 10 ya Muharram.

Bishr bin Amr al-Hadrami al-Kindi kwa asili alitokea Hadhramaut, lakini aliifanya Kufa kuwa maskani yake. Mmoja wa watoto wake alikamatwa ndani ya mipaka ya Rayy, lakini alimpeleka mmoja wa watoto wake wengine kupanga namna ya kuachiliwa ndugu yake, akipendelea kukaa katika kundi la Husein ambalo alijiunga nalo wakati majadiliano ya kupatikana amani yalipokuwa yakifanywa hapo Karbala. Mwishowe aliji- toa mhanga maisha yake kwa ajili ya Husein tarehe 10 ya Muharam.

Suwayd bin Abi al-Mataa' al-Khath'ami alikuwa amesonga mbele katika umri, aliyetawaliwa na Sala, na kujinyima, ambaye ametenda matendo ya kuonekana wazi katika vita vingi. Baada ya kupigana na adui, alianguka chini akiwa amejeruhiwa sana kiasi kwamba walimkatia tamaa.

Hata hivyo, alikuwa na uhai kiasi aliobakia nao, na aliposikia kwamba Husein ameuawa kishahidi, alijinyanyua kwa mhemuko usiozuilika, na akaanza kuwashambulia maadui walio karibu yake kwa kisu kikubwa ambacho bado alikuwa amebaki nacho. Kisha alishambuliwa na maadui na kuuawa.

Walikuwa ni nani watu hawa wote ambao waliungana kumsaidia Husein mbele ya matatizo mengi yasiyoelezeka na uhakika wa kufikwa na mauti?
Jambo moja linajitoeza dhahiri, nalo ni, kwamba wengi wa watu hawa walikuwa hawaeleweki vizuri au walikuwa watu wasiokuwa maarufu. Nane kati yao walikuwa Masahaba wa Mtume, nao walikuwa ni:

- Muslim bin Awsajah,
- Zahir bin Amr al-Aslami al-Kindi,
- Shabib bin Abdallah,
- Abd al-Rahman bin Abd Rabb bin al-Ansar,
- Ammar bin Abi Salama al-Dulani
- Muslim bin Qasir al-Sadafi,
- Habib bin Muzahir,
- Anas bin al-Harith al-Asadi.

Vita vya Karbala vilitokea miaka hamsini baada ya kifo cha Mtume, na wale katika Masahaba zake ambao walikuwa hai katika mwaka wa 61 A.H. lazima watakuwa wamepita zaidi ya miaka 50 ya umri wakati wa vita vya Karbala. Baadhi yao lazima watakuwa wamezeeka zaidi ya hapo, kama vile, 1. Muslim bin Awsaja, 2. Abd al-Rahman bin Abd Rabb bin al-Ansari, 3. Habib bin Muzahir, 4. Anas bin al-Harith na 5. Suwayd bin Amr al- Khath'ami. Watu wa kundi la umri huu hawakubali wenyewe kujiingiza katika vita kwa msingi tu wa mihemko ya ghafla na hisia kali za muda.

Miongoni mwa wale ambao walijitoa mhanga mkubwa kwa ajili ya Husein, wafuatao walikuwa sahaba wa Ali, na kwa hiyo, wanawekwa kicheo kwa hadhi ya kuwa tu chini kuliko sahaba wa Mtume:

- Abdallah bin Umar al-Kalbi,
- Mujammi bin Abdallah al-Muzhiji
- Janada bin al-Harith al Salmaani
- Jundab bin Hujr al-Kindi
- Umayyah bin Sa'd al-Ta'i
- Al-Harith bin Bahban
- Shabib bin Abdallah al-Nahshadi
- Na'im bin Aljan al-Ansaari
- Hulas bin Umar al-Azdi
- Al-Nu'man bin Umar Azd
- Qasit bin Zuhayr al-Taghlabi
- Jabala bin Ali al-Shaybani
- Karduus bin Zuhayr al-Taghlabi
- Miqsat bin Zuhayr al-Taghlabi
- Abu Thumaama al-Sa'idi
- Shazib bin Abdallah
- Jawn, mtumwa wa Abu Dharr al-Ghiffari,
- Hajjaj bin Masruq
- Sa'd bin al-Harith

Amr bin Jundab al-Hadrami, na Yazid bin Mughfil al-Ju'fi. Wengi katika wao walipigana katika upande wa Ali katika vita vya Ngamia, vya Siffin na vya Nahrawan, na baadhi yao walikuwa wafuasi wake.

Kwa mashahidi, ni wachache sana katika wao walioihifadhi Qur'an kwa moyo. Walikuwa:
1) Burayr bin Hudayr al-Hamdaani, (2) Abd al-Rahman bin Abd Rabb al- Ansaari. (3) Nafi' bin Hilaal al-Jamali (4) Hanzala bin Asad al-Shaybani, (5) Kinaana bin Atiq al-Taghlabi, na mtumwa mmoja wa Kituruki.

Wafuatao miongoni mwa mashahidi walikuwa ni watu wasomi na vyanzo vya hadithi nao ni:

- Muslim bin Awsaja,
- Habsha bin Qays al-Nahmi
- Zahir bin Amr al-Aslami
- Suwar bin Abi Umayr al-Nahmi,
- Abd al-Rahman bin Abd Rabb al-Ansaari,
- Habib bin Muzahir,
- Nafi bin Hilal al-Jamali
- Shuwayb bin Abdallah na Anas bin al-Harith.

Wapiganaji hodari na wale wanaotambulika kwa vipaji na mafanikio yao ya kivita pia waliwakilishwa miongoni mwa sahaba za Husein ambao kwamba shahada zao tayari tumekwishaziandika. Hawa walikuwa ni:

- Al-Hurr ibn Yazid al-Riyahi,
- Muslim bin Awsaja,
- Al-Harith bin Imru al-Qays al-Kindi;
- Abd al-Rahman bin Abdallah bin Kadan al- Arhabi,
- Mas'ud bin Hajjaj al-Taymi,
- Sa'id bin Abdallah al-Hanafi,
- Zuhayr bin al-Qayn al-Bajali,
- Aabis bin Abi Shabib al-Shakri,
- Ziyad bin Arib al-Hamdan, na
- Suwayd bin Amr bin Abi al-Mataa' al- Khath'ami.

Wengi wa wale ambao majina yao hutokea katika makundi mbalimbali katika ibara zilizopita walikuwa wanafahamika sana kwa usimamishaji wa Sala, kujihini kwao, uchamungu wao na watu hawa walikuwa ni heshima kwa nyakati zao na njia zao mbalimbali. Maisha yao yalikuwa mifano ya kuigwa katika hali zao zote na waloitoa mifano ya maisha ya maadili na tabia za Kiislamu. Ilikuwa ni kutokana na hawa

kuliko watu wa kawaida waendeshayo watu kwamba Husein alipenda kuungwa mkono na kusaidi– wa katika vita yake na Yazid.

Husein angeweza kuchagua watu bora wachamungu, waswalihina, wenye kujihini wa wakati wake kuwa masahaba zake, kuwa na watu wachache, waliosogea mbele sana katika umri, walio tayari kuyatoa maisha yao, ili kwamba kule kutokea kwao tu katika uwanja wa vita peke yake kungefungua macho ya Waislamu na kuwalazimisha kuitafakari hali mbaya ambamo Uislam ulikuwa umetumbukia ndani yake.

Historia imeandika hadithi fupi fupi kuhusu vitendo vya jeshi la Umar bin Sa'd wakati baadhi ya masahaba wa Husein walipokuja kuhuzunika. Vitendo hivi ni vyenye kutoa heshima sana, na viliandikwa na wale ambao wasingeweza kuwa na uhodari wa kumsifu Husein na sahaba zake.

Wala wasingeweza kupenda kusaidia katika kuandika hadithi zote kama hizo. Heshima kubwa ambazo kwazo baadhi ya masahaba wa Husein walikuwa wamezipata kwa watu kwa ujumla inafananishwa na heshima kama aliyopewa Muslim bin Awsaja na kamanda (kiongozi) wa jeshi la Umar bin Sa'd, Shabath bin Ribii, wakati alipowaona watu wa jeshi lake wakifurahia kifo cha yule sahaba wa Husein alisema;

"Inasikitisha kiasi gani! Mtu kama Muslim bin Awsaja amekufa na nyinyi mnajihusisha katika kuonyesha furaha! Mimi mwenyewe binafsi nimeona matendo makubwa na ya ajabu ambayo ameyatenda kwa sababu ya Uislamu."

Kama Husein angekwenda Karbala na watu wa familia yake tu pekee, ingeweza kusemwa, kama kwa hakika ilivyo hata sasa hivi baadhi ya watu wanajaribu kuhoji kwamba vita hivyo vilikuwa ni ugomvi mkubwa wa tangu miaka mingi kati ya matawi mawili ya familia moja – ukoo wa Bani Hashim na ukoo wa Bani Umayyah – ambao walidumu katika vita wenyewe kwa wenyewe. Lakini Husein alikuwa pamoja naye, watu maarufu na mashuhuri waliopatikana karibu kutoka kabila zote na sehemu zote za Bara Arabu na kitu chenye kuwaunganisha kati yao si kingine ila ile heshima ya zile kanuni na kuwepo kwa lengo maalum – ambalo ni – utekelezaji na kutimiza wajibu wa kidini.
Umuhimu wa mikataba hii (viunganisho) ambayo iliunganisha wafuasi wake hapo Karbala, kwa Husein ulikuwa ni msisitizo mkali wa ukweli kwamba Husein alimsihi sana kila mtu katika wafuasi wake katika nyakati mbali mbali, na hata baada ya kuingia giza la usiku wa mwezi 9 Muharram, kuondoka na kumwacha pekee akabiliane na adui. Ilikuwa ni sehemu ya mbinu na mpango wa Husein kuwafanya watu wafikiri wao wenyewe, kuchukua maamuzi kwa mujibu wa sauti ya dhamira zao wenyewe, ziziso shawishika kabisa kwa hali za kutoka nje na kuchukua wajibu kamili kwa vitendo vyao.

Siku ya tarehe 10 Muharram, ilikuwa siyo kwamba Husein aliwaleta wafuasi wake wengi ili kuweza kulifikia lengo lake, bali tu ni kwamba kila mmoja wa wafuasi wake, kwa hiari yake mwenyewe, alijitoa mhanga maisha yake kwa malengo ambayo Husein alikuwa nayo katika fikra.

Kichocheo cha matendo yao, kwa mtu mmoja mmoja au kwa pamoja, kilitolewa au kilipatikana kwa sauti ya dhamira ya kila mmoja katika wao, na hii ndiyo ilikuwa sababu kubwa kwa uthabiti wao na makusudio yao.

1. Tabari, cha II, uk. 335
2. Tabari, cha II, uk. 335-337.
3. Tabari, cha II, uk. 342.
4. Tabari, cha II, uk. 343.
5. Tabari, cha II, uk. 344.
6. Tabari, cha II, uk. 346.
7. Tabari, cha II, uk. 338-339.
8. Tabari, cha II, uk. 356
9. Tabari, cha II, uk. 307.
10. Tabari, cha II, uk. 355-356.
11. Tabari, cha II, uk. 345.
12. Tabari, cha II, uk. 235-236.

# Sura Ya 28: Mihanga Iliyotolewa Na Banu Hashim.

Wakati baada ya kupigana vita na jeshi la Umar bin Sa'd katika siku ya 10 Muharram mwaka wa 61 A.H hapo Karbala, na marafiki wote wa Husein walipopata shahada, jamaa zake waliingia kwenye medani ya vita kupi- gana na adui na kujitoa mhanga maisha yao kwa ajili ya Husein.

Ni udhihirisho wa nadra sana wa utii, upendo na uaminifu wa masahaba wa Husein kwa ajili yake kwamba muda maadam hata kama ni mmoja wao anabakia hai, hakuna hata mtu mmoja wa ukoo wa Hashim aliyebakia angepatwa na huzuni.

Yafuatayo ni maelezo mafupi ya maisha ya ndugu wa al-Husein na *jihad* zao katika mpangilio ambao waliingia katika medani ya vita:

1. Ali al-Akbar alikuwa mtoto wa Husein na wa kwanza katika mashahidi wa ukoo wa Hashim.[1] Mama yake, aitwaye Laila, alikuwa bint wa dada wa mtawala wa Syiria, Mu'awiyah, na binamu ya Yazid. Alikuwa ame- heshimiwa na kutukuzwa sana na marafiki na hata maadui pia. Mu'awiyah aliwahi kuwaambia watumishi wake kwamba Ali bin Husein alikuwa mtu mwenye haki kabisa ya ukhalifa, kwani alikuwa mjukuu wa Mtume na alichanganya ndani yake ushujaa wa Bani Hashim, ukarimu wa Bani Umayyah na heshima binafsi ya kabila la Thaqif ambalo kwalo mama yake alitokezea.

Kwa mujibu wa al-Mufid, Ali al-Akbar alikuwa na umri wa miaka kumi na tisa pale wakati masaibu ya Karbala yalipotokea. Alikuwa na uzuri wa ujanadume usio na kifani na madahiro. Alikuwa kipenzi makhsusi wa Husein kwa sababu alikuwa na mshabihiano mkubwa na Mtume katika sura yake na mwenendo wake. Alikuwa anaitwa Ali al-Akbar kwani alikuwa mkubwa kuliko ndugu yake Ali al-Asghar (Abdallah) ambaye alikuwa pia ameuawa kishahidi hapo Karbala. Hata hivyo, alikuwa mdogo kuliko

kaka yake, Ali Zayn al- Abidin.[2]

Baada ya wafuasi wa Husein kuwa wamekwishajitoa mhanga maisha yao, Ali al-Akbar alikuwa wa kwanza miongoni mwa ndugu zake kumwomba Husein amruhusu kwenda kutekeleza Jiha.

Akiamsha mikono yake juu, Husein alisema, “Ee Mwenyezi Mungu! Kuwa shahidi wangu kwa uonevu wa kikatili wa watu hawa ambao anawaendea yule kijana mzuri, ambaye zaidi ya yote amefanana na Mtume wako kwa sura na mwenendo. Wakati tulipotamani kumwona Mtume Wako, tulitumia kuangalia sura yake huyu.” Dua hii fupi inabeba ushahidi wa kutosha kuhusu uchungu wa moyo wa Husein na kujizuia.

Kisha Ali al-Akbar alijitambulisha kwa maadui kwa mashairi yenye maana kwamba, “Mimi ni Ali, mtoto wa Husein na mjukuu wa Ali bin Abi Talib. Naapa kwa Mwenyezi Mungu wa al-Ka’aba, tunayo stahili bora zaidi ya kumrithi Mtume Wake. Kwa jina la Allah kizazi cha mtu wa uzawa wa haramu hawezi kuamua mambo yenye kutuhusu sisi.”[3]

Hapa hakuna maneno yaliyotumika kumvutia msomaji juu ya ushujaa wa mzungumzaji, kwa sababu ilikuwa siyo lazima kufanya hivyo, baada ya tangazo kwamba mzungumzaji alikuwa wa ukoo wa Hashim. Ali al-Akbar alikwenda moja kwa moja kwenye kiini cha jambo ambalo liko katika mzozo, na akadai kwa ajili ya Bani Hashim kile cheo bora cha kumrithi Mtume kama Makhalifa wake, akitweza, kwa rejea fupi na zenye nguvu, visingizio vya Yazid kwenye ukhalifa.

Ali al-Akbar aliwashambulia maadui mara nyingi, mara zote akiingiza kuimba mashairi ambayo yamekwishatajwa. Ingawa alijeruhiwa mno, alishikilia kufanya mashambulizi kwa maadui katika mfuatano wa haraka haraka, mpaka alipopata fursa Murr bin Munqidh, askari, alimpiga kwa mkuki ambao ulimchoma ukaingia kifuani mwake. Ali al-Akbar alianguka chini kutoka kwenye farasi wake, na maadui walimzunguka na kuukata mwili wake kwa panga zao katika vipande vipande.

Kifo cha Ali al-Akbar kilikuwa kwa hakika msiba mkubwa kwa Husein ambaye alitamka kwa mshangao, “Namwomba Allah awaangamize watu hawa ambao wamekuua wewe mwanangu! Maisha baada yako hapa duniani hayana thamani kama ilivyo vumbi.”[4] Maiti ya Ali al-Akbar kisha ilichukuliwa na vijana wengi wa ukoo wa Hashim na kuletwa katika hema lililofanywa kama kituo cha kuangalilia jeshi la al-Hashim linapopigana.

2. Abdallah ibn Muslim ibn Aqil alikuwa mtoto wa Rukayya, binti ya Ali bin Abi Talib, na kwa hiyo, katika kuongezea kwamba alikuwa mtoto wa binamu ya Husein, Muslim, pia alikuwa mtoto wa dada yake, Rukayya. Alikuwa shahidi wa kwanza hapo Karbala, kutoka miongoni mwa dhuria wa Aqil. Alikuwa kijana mdogo sana katika wakati huo. Kifo cha Ali al-Akbar kilisababisha sauti kubwa za maombolezo na vilio kutoka kambi za Husein kiasi kwamba baadhi ya vijana wadogo, pamoja na Abdallah bin Muslim, walitoka nje ya mahema katika hali ya huzuni kubwa na fadhaa. Hii ilimpa nafasi askari mmoja wa upande wa adui kumuua (Abdallah bin Muslim kwa mshale aliotupiwa.[5]Tafsiri nyingine ya tukio hili ni kwam- ba askari mmoja asiye na huruma alimshambulia kwa mkuki na kumuua.[6]

3. Muhammad bin Muslim bin Aqil alikuwa ndugu wa Abdallah bin Muslim kwa mama mwingine. Baada ya kifo cha Abdallah kizazi cha Aqili kilifanya mashambulizi ya pamoja kwa adui, na Husein alitamka kwao kwa sauti kubwa, "Enyi watoto wa ami yangu! Yashikilieni mauti!" Mwishowe mshale aliotupiwa Muhamad bin Muslim ulimchoma na akauawa.

4. Ja'far bin Aqil aliingia katika medani ya vita baada ya Abdallah bin Muslim alipokwishauawa kishahidi. Alianza vita vyake kwa maneno, "Mimi ni mwenyeji wa Makkah, na ninatokana na familia ya Talib, kizazi cha Hashim na nyumba ya Ghalib. Kwa kuhakikisha sisi ndiyo viongozi wa makabila yote na Husein ndiye aliye mtu tohara kabisa kuliko wote katika watu walio tohara." Aliuawa kwa kupigwa mshale.

5. Abd al-Rahman bin Aqil alikuja katika medani ya vita na akasoma beti za utangulizi za kivita. Kisha aliingia katika vita, akapigana, na baada ya muda kidogo mshale aliotupiwa na muuaji wa ndugu yake Ja'far, ulimuua yeye pia.

6. Muhammad bin Abi Sa'id bin Aqil alipigana katika vita vya Karbala. Alijeruhiwa vibaya sana katika paji la uso kwa mshale, na baada ya muda mfupi tu baadaye alijiunga kwenye safu za mashahidi (alikufa kifo cha kishahidi).

7. Muhamad bin Abdallah bin Ja'far bin Abi Talib alikuwa mtoto wa bina- mu yake Husein, Abdallah, kwa Khawsaa bint ya Hafsa bint Thaqif na ali- tokana na kabila la Bakr bin Wa'il. Muhammad na ndugu yake, Awn ambaye alikuwa mtoto wa Zainab bint Ali, walikuwa wametumwa na baba yao kufuatana na Husein. Ndugu hawa wawili walikutana na Husein muda mfupi tu baada ya yeye kuondoka Makkah, na kutoka hapo walisafiri wote pamoja naye kwenda Karbala. Aliingia kwenye medani ya vita baada ya Abd al-Rahman bin Aqil na baada ya kufanya mapigano machache alikutana na shahada yake, akiwa ameuawa na Amr bin Nahshal al-Tamim.

8. Awn bin Abdallah bin Jafar alikuwa mtoto wa dada yake Husein, Zainab, na aliingia katika uwanja wa vita baada ya ndugu yake Muhammad, na muda mfupi baadaye Abdallah bin Qurba al-Tai' alimuua.

9. Al-Qasim bin Hasan alikuwa mpwa wa Husein. Alikuwa mtoto mdogo wakati vita vya Karbala vilipotokea, na alikuwa kijana mwenye sura nzuri sana hivyo askari mmoja wa upande wa jeshi la adui alielezea kutokea kwake katika uwanja wa vita kama tazamo la mara moja la mwezi mpya. Alikuwa hakuvaa koti la chuma wakati alipokwenda kupigana na ugwe (kamba) wa kiatu chake kimoja ulikatika.[7] Haya yalionyesha wazi kwamba alikuwa hakujizatiti au hakujiandaa kwa vita, bali alikuwa amekwenda tu kupigana katika shauku yake ya kumsaidia Husein.

Umar bin Sa'd bin Nufayl al-Azdi alipiga dharuba kwenye kichwa cha al- Qasim kwa kutoka kwenye farasi wake. Husein alikwenda haraka sana kumsaidia al-Qasim na akakikata kiganja cha muuaji kutoka karibu na kiwiko kwa upanga wake. Jeshi la adui lilimshambulia Husein ili kumwokoa muuaji wa al-Qasim, lakini walifanya hivyo katika mtindo usio wa mpangilio hivyo kwamba ikawa kwa kweli ni kumkanyaga kanyaga juu yake muuaji mpaka kufa.

Kisha kundi hilo likatawanyika, Husein akasimama kwa muda kidogo karibu na maiti ya al-Qasim, akiwa ameshikwa na huzuni isiyoelezeka. Kisha akaichukua (maiti hiyo) na kuipeleka mahali maiti ya Ali al-Akbar na maiti nyingine za ndugu zilipokuwa.

10. Abu Bakr bin Hasan aliuawa kwa mshale. Mama yake alikuwa Umm Is'haaq, bint ya Talha al-Tamimii.

11. Muhammad bin Ali bin Abi Talib alikuwa mdogo zaidi kuliko ndugu yake Muhammad bin al-Hanafiyya. Baada ya kifo cha Ali, alikaa na kuishi na ndugu (kaka) zake, Hasan na Husein kwa mfuatano, mmoja baada ya mwingine. Siku ile ya tarehe 10 ya Muharam alishiriki katika *jihad* hapo Karbala, na baada ya kuangamiza maadui wengi, na yeye aliuawa kwa kupigwa mshale. Kichwa chake kilikatwa na kikachukuliwa kupelekwa kwa Umar bin Sa'd.[8]

12. Abdallah bin Ali alikuwa mmoja wa watoto wanne aliowapata Ali kwa mama yao, Umm al-Bani Fatimah, bint ya Hizaam, ambaye alitokana na familia iliyofahamika kwa ushujaa wake. Watoto wengine watatu walikuwa. Abu al-Fadhl Abbas, mkubwa wao kabisa, Uthman na Ja'far, huyu wa mwisho akiwa ndiyo mdogo kabisa katika wao.

Abdallah bin Abi Mahl, mtu mkubwa wa Kufa, alikuwepo katika baraza la Ubaydullah bin Ziyad wakati Shimr alipoondoka kwenda Karbala, pamoja na barua ambayo iliandikwa kwa Umar bin Sa'd ikimwagiza kumuua Husein na sahaba zake kama wangekataa kutoa kiapo cha utii kwa Yazid. Abdallah bin Abi al-Mahl alipata kutoka kwa Ubaydullah bin Ziyad uhakikisho wa usalama kwa ajili ya watoto wa Umm al-Banin ambao wakati huo walikuwa hapo Karbala na Husein kwa vile mama yao alikuwa ana uhusiano wa kindugu naye, na aliipeleka dhamana hiyo ya usalama na ulinzi kwa Abbas na ndugu zake kupitia kwa mmoja wa watumwa wake.

Ndugu hao wanne, hata hivyo walimwambia mjumbe huyo kwamba wao hawakuhitaji kibali cha Ibnu Ziyad kwa ajili ya usalama (wao), na kwam- ba usalama na ulinzi wa pekee wa Mwenyezi Mungu ulikuwa unatosha kwa ajili yao.
Shimr alitokana pia na familia hiyo hiyo kama Umm al-Banin, na baada ya kuitoa barua ya Ubaydullah bin Ziyad kwa Umar bin Sa'd alikutana (alionana) na Abbas na ndugu zake kuwaambia kwamba wamepatiwa dhamana ya usalama. Wao waliukataa ulinzi huo kwa dharau kwani haukumjumlisha Husein.[9]

Katika siku ya 10 ya Muharram, Abbas aliwapeleka ndugu zake kwenda kupigana kwa ajili ya Husein kabla ya yeye mwenyewe hajaenda kujitoa mhanga maisha yake. Abdallah ambaye alikuwa mkubwa baada ya Abbas aliingia kwenye medani ya vita na baada ya mapigano makali sana alikutana na kifo cha kishahidi.

13. Uthman bin Ali aliitwa hivyo kwa sababu Uthman bin Maz'un aliyekuwa sahaba mkubwa na maarufu wa Mtume, alikuwa rafiki wa Ali binafsi. Alipigana kwa ajili ya Husein na alianguka chini akiwa amejeruhi- wa na mshale. Kisha aliuawa kwa kukatwa kichwa.

14. Ja'far bin Ali alishiriki katika vita vya Karbala baada ya Uthman bin Ali na aliuawa.

15. Abu al-Fadhl Abbas alizaliwa katika mwaka wa 26 A.H, na alikuwa na miaka kumi na nne, wakati Ali alipouawa kishahidi. Kisha Hasan alichukua jukumu la kumlea, na baada ya kifo cha Hasan katika mwaka wa 50 A.H, Abbas alitumia maisha yake na Husein. Alikuwa na umri wa miaka 34 wakati matukio hayo ya kuhuzunisha ya Karbala yalipotokea.

Abbas alikuwa maarufu kwa uzuri, madaha, urefu, nguvu na ushujaa na alikuwa akiitwa Qamar (mwezi mkamilifu wa ukoo wa Hashim). Husein alimfanya kuwa mshika bendera wa jeshi lake dogo, Abbas aliishika bendera hiyo juu sana kwa ushujaa usio wa kawaida na kwa heshima maalum.

Upendo wake mkubwa na utii kwa Husein ulimfanya amfuate Husein katika medani ya vita kama kivuli chake. Wakati wafuasi wengine na ndugu wa Husein walipokuwa wamekwishakufa kama mashahidi, Abbas alisimama peke yake mbele ya ndugu yake kumlinda. Alipoyaona maisha hayavumiliki alimwomba Husein ruhusa ya kupigana. Ruhusa ilitolewa kwa shingo upande, na Husein alimtaka atafute maji. Abbas alichukua kiriba cha maji na alikwenda kufuata mto. Alifanikiwa kupigana kujipatia njia yake kumfikisha mtoni na akakijaza chombo chake na maji.

Yeye mwenyewe alikuwa na kiu kali sana, iliyopita kiasi na akachukua maji mkononi na kuyaelekeza midomoni kama anayetaka kuyanywa, lakini alikumbuka kiu kali aliyonayo Husein na watoto wake, mara moja aliy- atupilia mbali maji hayo, na asijaribu kuonja hata lau tone moja.

Akiwa amekibeba kiriba cha maji kwenye mabega yake alitoka kule mtoni na kuelekea kwenye kambi ya Husein. Adui sasa akajizatiti kwa bidii zao zote katika kuzuia hata tone moja la maji kumfikia Husein. Kwa hiyo, wao walimzunguuka Abbas ambaye alikuwa ameelemewa na kile kiriba cha maji ambacho kimening'inia kwenye mabega yake na bendera ya jeshi la Husein ikiwa katika moja ya mikono yake.

Hata hivyo, Abbas alifanya mashambulizi ya nguvu sana kwa maadui ili kujinasua kutoka kwenye kundi hilo hasimu lakini Hukayn bin Tufayl alimkata mkono wake. Ili aweze kuilinda heshima na utukufu wa bendera hiyo, Abbas aliihamishia kwenye mkono wake wa kushoto ambao nao pia, muda mfupi baadaye ulikatwa na Zayn bin Warqa al-Juhni.

Abbas alijitahidi kuishikilia bendera ya jeshi lake kwa kutumia kifua chake kuikandamiza kwenye mgongo wa farasi wake wakati dharuba moja iliyopigwa kwa kutumia kirungu ilipomwangusha chini ardhini. Wakati Husein alipomfikia Abbas alikuwa katika pumzi za mwisho, anakaribia kufa.

Imeelezewa na Ali bin Abi Talib katika *Nahjul-Balaghah* kwamba Mtume wa Waislam alikuwa akitumia kuwaweka watu wa nyumba yake na familia katika mstari wa mbele wa vita katika nyakati za hatari, akiwatumia wao kama ngao kuwakinga masahaba zake.

Kuachwa kwa kanuni hii kulifany- wa katika vita vya Karbala. Wafuasi wa Husein na marafiki walijitosa wao kwanza katika kupigana vita na maadui na kuupata utukufu wa ushahidi. Walifuatiwa na ndugu wa

Husein, na mwisho wa wote alikwenda Husein, na kupigana hiyo vita takatifu.

Sababu za kuachwa kanuni hii zinaweza kugunduliwa kwenye tofauti kubwa iliyopo kati ya matokeo yaliyotegemewa ya vita vya Karbala na matokeo ambayo yangeweza kutarajiwa kibusara ya vita vilivyopiganwa huko nyuma.

Katika vita nyingine zote, ilitegemewa kwamba baadhi ya washiriki wangebakia salama na hai katika mwisho wa mapigano hayo. Kwa hiyo, ili kuhakikisha kwamba wengi wa wale ambao walibakia sala ma na bila kuumizwa walikuwa Masahaba wake, Mtume aliwatumia ndugu au jamaa zake kukabiliana na hali zilizo za hatari sana. Siku ya 10 ya Muharram, kila mmoja katika wafuasi wa Husein, wapenzi na ndugu wote kwa pamoja, walijitolea kukabiliana na kifo, na hakuna swali (au hoja) lililojitokeza juu ya jamaa wa Husein la wao kupelekwa kwanza kupigana kuwanusuru wapenzi wake. Hali zilizokuwepo hapo

Karbala zilikuwa za namna kwamba dakika baada ya dakika majaribu ya wapenzi na jamaa wa Husein, na kwa kweli, majaribu ya Husein mwenyewe, yaliongezeka kwa ugumu na joto lenye kuongezeka na mateso ya kiu.

Imam Husein alikuwa na imani ya dhahiri katika uthabiti na uaminifu wa wafuasi wake na ndugu zake, hata hivyo hakulichukilia kwamba ni jambo jema kuwahatarisha kwenye mitihani mikali kama kuwawekea mikazo inayozuilika kwenye uwezo wao wa kustahimili. Ilikuwa kwa hiyo, ikieleweka kwamba angepaswa kuamua kuwatoa kwenda kupigana kwa utaratibu ule alioutumia, kwa utambuzi kamili wa uwezo wa uvumilivu wao, na wake yeye mwenyewe.

Ingekuwa ni jambo rahisi vya kutosha kwa Husein kuyatoa mhanga maisha yake mwenyewe kwanza kabisa katika njia ya haki.

Muhanga huu usingekuwa na daraja la juu zaidi kuliko mhanga, tuseme wa Kristo, ambaye kwa mujibu wa Wakristo alisulubiwa kwa sababu ya kutangaza na kueneza imani (dini) ya kweli, au mhanga wa Socrates ambaye alikunywa sumu kwa kutetea kanuni zake.

Heshima maalum na umuhimu wa mhanga wa Husein vilitokana na ukweli kwamba alivumilia mhanga wa kila mmoja wa wafuasi na wapenzi wake na ndugu zake mbele ya macho yake mwenyewe.

Kutengana kwa mtu na wafuasi wake waaminifu na vipenzi wa zamani, mmoja baada ya mmoja, wakiondoka daima dawamu, kuwaona wapwawe vijana na wazuri wa kupendeza wakiuawa kwa ukatili sana, kushuhudia mtotowe mtanashati na mwenye kuleta matumaini katika maisha akichomwa mkuki na kukatwa katwa mpaka kufa, na kumwona nduguye, mshika bendera wa jeshi la mtu huyo akilemazwa na kuuawa, kutaja tu mifano michache ya misiba yenye kuhuzunisha sana, ilikuwa ni majanga ambayo kwamba kila moja yao (katika hayo) lilikuwa lisilovumilika zaidi kuliko kifo chake mwenyewe mtu.

Tendo kubwa la kumvika taji halikuwa lile tu kwamba alijitolea mhanga maisha yake katika njia ya haki,

bali kwamba, kwa ajili ya kupata radhi za Mwenyezi Mungu, ndiyo alitoa mihanga, mmoja baada ya mwingine ya watu ambao walikuwa vipenzi sana kwake kuliko maisha yake mwenyewe na kwamba alijizuia kule kutoa muhanga maisha yake binafsi mpaka alipokuwa amepitia mkasa wote huu wa kusikitisha. Hakuna mwingine tena anayeelekea kuwahi kupata daraja hii ya juu ya subira na uvumilivu. Je, Husein angeweza kutegemea hayo kwa yeyote yule ambaye angemwacha afe baada yake yeye?

16. Abdallah bin Husein, anayefahamika zaidi kama Ali-Asghar, (Ali mdogo), kitoto kichanga alikuwa katika mikono ya baba yake, Husein wakati mshale uliotupwa na adui ulipomuua.[10]
Kwa mujibu wa hadith nyingine Husein alikuwa amemnyanyua mikononi mwake wakati wa msisitizo wa Umar bin Sa'd, Harmala bin Khalid al-Asadi alipotupa mshale uliolengwa kwa mtoto huyo asiye na hatia, ukamchoma na kumuua.

Tendo hili la ukatili uliovuka mpaka lililoelekezwa dhidi ya mtoto mchanga asiye na hatia limekutana na shutuma nzito sana kutoka kwa watu ulimwenguni kote, bila kutofautisha itikadi au umbali wa nchi. Liliwaanika kwenye aibu ya kudumu milele, wale maadui wa Husein kama watu ambao wamezima misisimko yote ya dhamira, hisia zote za kibinadamu na wakajiachia wenyewe, kwa ajili ya kupenda mamlaka ya kilimwengu (kidunia), kushushwa hadhi hadi kwenye daraja za chini zaidi kuliko zile za wanyama.

1. Tabari cha II, uk. 256-257.
2. Al-Irshad, uk. 358.
3. Tabari cha II, uk 356; Irshad, uk. 358.
4. Tabari cha II, uk. 357.
5. Tabari cha II, uk. 357.
6. Al-Irshad, uk. 359.
7. Tabari cha VI, uk. 256; Irshad, uk. 253-254.
8. Tabari cha VI, uk. 257
9. Tabari cha VI, uk. 237; Irshad, uk.242.
10. Tabari cha VI, uk. 257; Al-Akhbar al-Tawel, uk. 255; Irishad, uk. 154.

# Sura Ya 29 : Jihad Ya Mwisho Na Kifo Cha Kishahidi Cha Husein.

Baada ya kifo cha Ali al-Asghar ni dhahiri kwamba jambo moja pekee lililobakia kwa Husein kufanya lilikuwa ni kufa. Lengo hili lingeweza kutekelezwa kwa urahisi kwa kuweka upinzani hafifu kwa maadui na kukiruhusu kichwa chake kikatwe kutoka mwilini mwake kufuatia mapigano madogo tu. Majibu yake ya kisilika juu ya hali yake lazima iwe kwamba yalikuwa tofauti sana. Vipi angeweza kuwa ameyasahau mafanikio ya kishujaa ya Hamza, Ja'far na Ali na ujasiri usio kifani ambao uliweka chapa katika vita vya

Badr, Uhud, Khandaq na Siffin.

Husein alikwenda hemani kwake kupata pumziko lake la mwisho kabla ya kwenda kupigana, na akachana shuka iliyotengenezwa Yemen, sehemu nyingi mbalimbali juu yake, na akaivaa chini ya nguo zake nyingine zote, inawezekana akitegemea kwamba nguo hii iliyorarukararuka, ingeweza kuachwa mwilini mwake baada ya kuuawa kwake, mwili wake utakapokuwa umeporwa nguo nyingine zote.[1]

Akiwa mwenye huzuni, amevunjika moyo, na mwenye kiu isiyovumilika kama alivyokuwa wakati alipowakabili maadui akiwa peke yake kabisa, upanga mkononi, Husein alitia hisia za woga hivyo katika nyoyo za maadui wake kiasi kwamba hakukua na hata adui mmoja aliyekuwa na ujasiri wa kumkabili. Akigundua kuvunjika moyo huku kwa maadui, Shimr alijaribu kuwatia moyo.

Akizipanga upya safu za maaskari aliliweka jeshi la watembeao kwa miguu mbele ya jeshi la wapanda farasi na akawaamuru wapiga pinde wamimine mishale kwa Husein. Hivyo kwa wingi sana mishale ilitupwa kwake, kiasi kwamba mwili wa Husein ulifanana na mwili wa mnyama aitwaye nungunungu![2]

Kisha Shimr alitoa amri kwa sauti kubwa kwa askari wake kumuua Husein. Jeshi lenye askari wengi sana la Umar bin Sa'd lilifanya tena mashambulizi juu ya al Husein kutoka pande zote, na panga zao, mikuki na mishale ilitumika kwa uhuru kabisa dhidi yake. Farasi wake lazima alikuwa amejeruhiwa mno kiasi kwamba Husein alishuka chini.

Hata ingawa alikuwa chini, aliendelea kushambulia maadui zake, na mara alipolifanya jeshi lote kukimbia alikwenda mtoni. Akitambua kwamba Husein angekunywa kiasi fulani cha maji kukata kiu yake, Husein bin Tamim alimtupia mshale ambao uliupiga mdomo wa Husein bin Ali ambamo humo damu nyingi ilimtoka. Husein alichukua damu iliyojaa kiganya chake na akairusha juu angani, na kumshukuru Mwenyezi Mungu.[3]

Wakati huohuo Shimr alisogea mbele na kikosi kimoja cha jeshi kwenda kwenye mahema ya wanawake wa kundi la Husein ili wakawapore na kuwanyang'anya vitu vyao. Husein aliwaonya, akiwataka kuzingatia kwa kiasi fulani kanuni za ungwana na wasifanye makosa dhidi ya wanawake wa nyumba yake. Shimr alirudi nyuma, akijionea haya kwa yale ambayo ameyafanya.[4]

Kisha Shimr alimzunguuka Husein, akiwa na askari wake wa miguu ambao walisukumwa nyuma na kufukuzwa kila wakati Husein alipopambana nao. Askari mmoja wa jeshi la adui alizungumzia kumhusu Husein akisema, "Sijamwona mtu yeyote yule ambaye alikuwa amejeruhiwa, ambaye kizazi chake, jamaa zake na wapenzi wake wote wakiwa wameuawa kwa panga, lakini bado yeye akatokea kuwa imara na aliyetulia na ambaye akashambulia maadui zake kwa ushujaa wa waziwazi kabisa kama Husein.

Watu wa kikosi cha askari wa miguu walimzunguuka Husein kutoka pansde zote, lakini kila alipowashambulia kwa upanga wake, walikuwa wanakimbia kwenda upande wa kulia na kushoto kama kondoo wafanyavyo wanapotimuliwa na mbwa mwitu anayeshambulia."[5]

Wakati huohuo Husein alikuwa akirudiarudia maneno ambayo yalilengwa kutoa mwongozo kwa maadui na pia kuonyesha alama za matokeo ya vita. Kisha Husein alishambuliwa kwa nguvu sana na kwa kurudiwarudiwa. Alianguka chini, akiwa na majeraha mengi sana na akashindwa kusimama kutokana na udhaifu.

Mtoto wa Hasan, mdogo kuliko ndugu yake, al-Qasim, aliyeitwa Abdallah bin Hasan, akimwona ami yake Husein, anasujudu juu ardhini, alikwenda akimkimbilia wakati Bahr bin Ka'b bin Ubaydullah al-Taymi alikuwa anakwenda kumshambulia Husein kwa upanga. Abdallah alimlaumu, lakini Bahr alimkata mmoja wa mikono yake kwa upanga wake, na Harmala aliachia mshale kuelekea kwake, ukamchoma na ukamuua.

Husein alibakia bado anasujudu juu ya ardhi, akiwa ameumizwa sana na kuchoka, kwa kipindi kirefu kidogo kwa sababu kila mtu alikuwa anajaribu kukwepa kushiriki katika kosa hili kubwa na baya sana na ovu la kumuua (Husein).

Hatimaye Shimr akawakemea watu wake akisema; "Sasa mnangojea nini nyinyi?" Kwa swali hili al-Malik bin Nasr al-Baddi alisogea mbele, na akampiga Husein kwenye kichwa kwa upanga ambao ulichoma ngozi yake ya kichwa,6 na mwishowe upanga wa Zuraa bin Sharik,7 mkuki wa Sinan bin Anas,8 na sime (hanjari) ya Shimr viliyamalizia maisha ya mtu yule aliyekuwa mfano mzuri wa uadilifu. Hapo kichwa cha shahidi wa haki, cha shahidi katika njia ya Allah, kilinyanyuliwa juu kwenye ncha ya mkuki.

Ilikuwa ni siku ya Ijumaa, mwezi 10 Muharram mwaka wa 61 A.H. ambapo tukio hili la kuhuzunisha lilipofanyika.

1. Tabari juz. 6 uk. 240.
2. Al-Irshad, juz. 6, uk. 257.
3. Tabari juz. 6 uk. 250
4. Tabari juz. 6 uk. 253.
5. Al-Irshad, uk. 257/ Al-Akhbar al-tawal, uk. 255
6. Tabari juz. 6 uk. 257; Al-Irshad al-Tawal, uk. 255.
7. Al-Akhbar al-Tawal, uk. 255.
8. Tabari juz. 6 uk. 260; Al-Akhbar al-Tawal uk.256.

# Sura Ya 30: Baada Ya Shahada Ya Husein.

Hata baada ya Husein na wapenzi wake wote na ndugu zake walipokuwa wamekutana na vifo vyao vya kishahidi, uonevu wa Yazid, bin Ziyad na vibaraka wao haukufikia mwisho. Ni zile namna tu za ukandamizaji na uonevu ndizo zilipata mabadiliko; mauaji yalibadilishwa na unyang'anyi, kuchoma mali moto na kuning'iniza vichwa vya mashahidi kwenye ncha za mikuki.

Wanawake wa familia ya Husein, iliyokuwa salama kutokana na ufedhuli na kushushiwa heshima wakati wa uhai wa Husein, walikuwa sasa wanaondolewa hata stara za nguo walizozitumia kufunika vichwa vyao, na wanaachwa kukutana na matusi mengi na walichukuliwa kutoka sehemu na kupelekwa sehemu nyingine kama wafungwa wa kawaida tu.

Maiti ya Husein iliibiwa kilemba chake, shati lake, shuka yake kutoka Yemen, na nguo zake za ndani ambazo alikuwa amezivaa kwa mara ya mwisho.

Upanga wake pia ulichukuliwa. Kisha jeshi lilifanya uporaji na unyang'anyi kwenye mahema yaliyokuwa na wanawake wa familia[1] ya Husein ambao kutoka kwao walinyang'anya hata nguo ambazo zilifunika vichwa vyao.[2]

Kisha mahema yaliwashwa moto, na askari kumi waliopanda farasi walikanyaga juu ya maiti ya Husein chini ya kwato za farasi wao.[3] Kichwa cha Husein kilichokatwa kilikuwa cha kwanza kupelekwa kwa Ibnu Yazid kupitia kwa Khawali bin Yaziud al-Asbahi. [4]

Kisha vichwa vya baadhi ya mashahidi wengine vilipelekwa kwake pia. Miongoni mwa watu wa al-Husein waliopona alikuwa ni mwanawe aliye kuwa mgonjwa, Ali bin Husein, baadhi ya wanawake na baadhi ya watoto.

Tarehe 11 Muharram, 61 A.H Umar bin Sa'd aliizika miili ya watu wa jeshi lake, baada ya kukamilisha taratibu zote za mazishi. Hata hivyo, aliziacha maiti za Husein na wafuasi wake bila kuzikwa na bila kushughulikiwa kwa jambo lolote.

Wakati wa jioni aliwachukua watu waliobakia wa familia ya Husein kama wafungwa kuwapeleka Kufa na vile vichwa vya mashahidi ambavyo vilikuwa bado havijapelekwa kwa Ibn Ziyad vilichukuliwa pia na majeshi. Ilikuwa ni baada tu ya majeshi ya Yazid yalipoondoka kwenda Kufa kwamba maiti za mashahidi zisizokuwa na vichwa zilizikwa na baad- hi ya watu wa kabila la Banu Asad ambao waliishi karibu ya Karbala.

Vichwa vya mashahidi vilikabidhiwa kwa Ubaydullah bin Ziyad huko Kufa na kwa dharau na jeuri aliichokoachokoa midomo na meno ya Husein kwa fimbo.

Hili lilimuudhi sana Zayd bin Arqam, Sahaba wa Mtume, ambaye alikumbuka kuwahi kumuona Mtume akiibusu midomo hiyo na meno hayo. Kisha Zayd alianza kulia. Ubaydullah bin Ziyad alisamehe kutokumtolea amri ya kuuawa kwa sababu ya uzee wake.

Kabla ya kuwasili hapo Kufa kwa msafara huo wenye kuhuzunisha wa watu wa Husein waliobaki na kuporwa, ilitolewa ilani kwamba mtu yeyote asije akatoka nje ya nyumba yake, na askari doria walipelekwa kwenye sehemu mbalimbali kwa sababu ya wasiwasi fulani maalum.

Wengi wa watu waliamini kwamba wafungwa ambao kwa ajili ya kuwasili kwao sehemu ya sokoni ilipambwa, walikuwa wanawake wa maadui wa Uislamu walioshindwa, na idadi kubwa ya watazamaji

walikuwa ni wenye furaha. Hata hivyo, baadhi yao walikuwa wamejawa na huzuni kwani walikwishaujua ukweli.

Vichwa vya mashahidi, vilivyotungikwa juu sana kwenye ncha za mikuki, viliwaongoza wafungwa wanaotokana na familia ya Mtume wakati msafara ulipoingia Kufa. Mwanamke mmoja ambaye alikuwa akilishuhudia hadhara hii kutoka juu ya ghorofa ya nyumba yake, aliwauliza wafungwa kuhusu familia zao na alipotambua kwamba walikuwa dhuria wa Mtume, yeye na watu wote wa kundi la watazamaji walilia na kuomboleza kwa sauti kubwa.

Ali bin Husein, kwa sauti dhaifu na ya kutetema aliwaambia watu, “Ni nyinyi ndiyo ambao mmemwaga damu yetu, na sasa wanawake wenu wanalia machozi juu ya msiba wetu. Mwenyezi Mungu ataamua kati yenu na sisi.” Umati huo, uliposikia maneno haya walishusha pumzi na wakalia sana kwa sauti za juu zaidi.

Katika hatua hii Zainab aliuhutubia mkusanyiko wa wanaume wengi akise- ma, “... Enyi watu wa udanganyifu na utapeli! Nyinyi mnalia? Kamwe Mwenyezi Mungu asikatishe machozi yenu. Nazisinyamazishwe sauti za vilio vyenu vya maombolezo.
Je, mnalia na kupiga mayowe kikweli katika kuomboleza? Kwa kweli ni vyema kwenu nyinyi kwamba mngelia zaidi na kucheka kidogo zaidi.

Je, mlijaribu kamwe kugundua ni kiasi gani mmeupasua moyo wa Mtume wa Mungu, mlivyowaweka wanawake waheshimiwa wa familia yake katika sura ya wageni, na kuwatukana? Je, mnastaajabishwa kwamba mbingu ilimwaga machozi? Hili si chochote kabisa ikilinganishwa na adhabu katika maisha yajayo ambayo kwa kweli itakuwa kali sana.

Kisha hakutakuwepo mtu yeyote yule wa kukusaidieni. Msifurahie muhula huu mfupi. Mwenyezi Mungu hana haja ya kufanya haraka kwani hatambui kwamba Angekosa nafasi ya kukuadhibuni. Bila shaka yeyote ile atakuachieni wenyewe mlivyo kwa muda kidogo.”

Imeelezewa kwamba wakati wa kutolewa hotuba hii yenye kugusa hisia, wote waliokuwepo walibakia wametingishwa mno na wote walikuwa wanalia. Kwa hotuba ya Zainabu, Bashir bin Huzaym al-Asad alisema, “Kamwe sijawahi kumwona mwanamke, ambaye ameishi katika faragha, akatoa hotuba yenye nguvu kama hii. Ilionekana kana kwamba baba yake, Ali bin Abi Talib ndiye alikuwa anatoa hotuba fasaha. Aliunyamazisha umati wa watu kwa ishira ya mkono wake na utulivu wa dhati ukapatikana hapo.

Kisha watu walihutubiwa na Fatimah bint Husein na Umm Kulthumu bint Ali na Ali ibn Husein. Hutuba hizi zilifungua macho ya wenyeji wa Kufa, na kuvunjavunja udanganyifu wa kuduwaza wa Bani Umayyah walioumwaga kwa watu wa Kufa.

Kisha Ibn Ziyad aliamuru kwamba wale wanusurika wa Husein waletwe kwenye Baraza lake. Ile tabia ya kijeuri na dharau ambayo kwayo amekitendea kichwa cha Husein, na uathirikaji wa Zayd bin Arqam kuhusu hilo umekwisha elezewa tayari. Baada ya kuuliza kwake, Zainab alitambulishwa kwa Ibn Ziyad,

na majibizano yafuatayo yalitokea baina yao.

**Ibnu Ziyad**: “Mwenyezi Mungu ashukuriwe kwamba amekudhalilisheni, amekuuweni na kuufichua uwongo wenu.”

**Zainab**: Sifa zote njema zinamstahiki Mwenyezi Mungu swt., ambaye ametunuku heshima juu yetu sisi pamoja na Muhammad mteuliwa, na ambaye ametutangaza sisi kuwa tohara, kama tohara yenyewe iwezavyo kuwa madai ya haki. Sisi hatuko kama usemavyo. Ameaibika na kudhalilika yule ambaye ni mwenye dhambi na mchafu. Uwongo umefichuliwa wa yule ambaye siku zote haiweki haki mbele kama lengo lake. Ni wengine, na siyo sisi, ndiyo watu wa namna hiyo.”

**Ibnu Ziyad**: Je, umeona ni kitu gani Mungu amekifanya kwa ndugu yako (Husein) na ndugu wengine?”

**Zainab**: “Nimeona kwamba Mwenyezi Mungu amewafanyia upendeleo tu. Walikuwa ni watu wateule wa Mwenyezi Mungu ambao walikuwa wamepangiwa kupata Shahada. Walikwenda kwenye madhabahu ya kuji- toa mhanga maisha yao kwa miguu yao wenyewe. Siku haiko mbali sana ambapo mtakapokuja kukabiliana nao mbele ya Mwenyezi Mungu kujibu makosa yenu mabaya na maovu.”

**Ibn Ziyad**: “Mungu ametimiza matakwa ya moyo wangu kwa kumuangamiza ndugu yako mpinzani na ndugu zako wengine wasiotii amri na walio waasi.”

**Zainab**: “Ndiyo, kwa hakika umewaua jamaa zangu, ndugu na marafiki. Kama hili limetosheleza matamanio yako basi jifurahishe nalo.”

Kisha Ubaydullah aligeukia kwa Ali bin Husein, na alipokuwa hakupata lolote lile lililokuwa zuri zaidi katika mahojiano aliamuru auawe. Zainab akamng’ang’ania mpwa wake na akataka auawe pamoja naye.

Ibnu Ziyad alitulia na akamuacha Ali bin Husein ambaye alitoa hotuba ifuatayo yenye maneno ya kukumbukwa kwake:
“Usijaribu kunitishia kwa kifo. Je, hujui kwamba kuuawa ni katika njia yetu na kwamba shahada (kujitoa mhanga) ndiyo sifa yetu.”

Akijisikia kuabika sana, Ibn Ziyad alivunja baraza kwa siku hiyo, akaamuru wafungwa wawekwe katika hali ya umateka mpaka kurudi kwa mjumbe wake kutoka Damascus, na kwamba raia wote wa hapo Kufa wakusanyike ndani ya msikiti mkuu wa mji, ambamo humo alipopanda katika mimbari alifanya rejea za kumuumbua na kumshushia mno hadhi yake Ali bin Abi Talib. Abdallah bin Afif, mmoja wa Shi’a wa Kufa, ambaye alipoteza macho yake yote mawili, wakati akipigana kwa ajili ya Ali katika vita mbalimbali, alisimama na akampinga Ibn Ziyad na akamkemea kwa ukali.

Aliamuriwa kukamatwa lakini askari mia saba watokanao na kabila lake walimwokoa na wakamchukua na kumpeleka nyumbani kwake. Hata hivyo, bila ya huruma aliuawa usiku uleule.

Siku iliyofuatia, kichwa cha Husein kilitembezwa katika eneo la sokoni kikatundikwa na kuning'inizwa katika mlango uingiao katika jumba la utawala wa Ibn Ziyad.[5]

Amri zililetwa kwa Yazid kwamba wafungwa wapelekwe Damaski. Ubaydullah bin Ziyad alielekeza kwamba kichwa cha Husein, kinyanyuliwe na kuwekwa juu sana katika ncha ya mkuki, kizungushwe katika mji na halafu vichwa vyote vya mashahidi vipelekwe Damascus.

Wanawake walipandishwa juu ya ngamia, na Ali bin Husein, bila kuridhika au kutaka na akiwa ametwikwa mnyororo mzito wa chuma kuzunguka shingo yake yote, aliwafuata chini ya ulinzi na uangalizi wa Shimr na Muhaffiz bin Thalaba al-Aidhi.[6]

Katika safari yake ya kwenda Damascus msafara huu wenye bahati mbaya wa familia ya Mtume ulipitia katika miji mingi na maeneo mengine yanayokaliwa na watu na katika sehemu chache sana maandamano ya watu wenye hasira yalifanyika kutokana na udhalilishaji waliofanyiwa wanusurika wa al-Husein, na hisia nzito za huzuni zilionyeshwa juu ya mauaji ya Husein na ndugu na wasaidizi wao.

Baada ya kupatwa na mateso makubwa sana, wanusurika wa Husein wali- ingia mjini Damascus wakati wa alfajiri.

Maduka makubwa ya mji yalipambwa makusudi kwa jambo hilo, na umati wa watazamaji ulikuwa mkubwa kiasi kwamba haikuwezekana mpaka wakati wa mchana ndipo msafara huu wenye kusikitisha ulipofikia jengo kubwa la kiutawala la Yazid.

Ibn al-Qiftii ameandika kwamba wakati vichwa vya mashahidi pamoja na familia ya Mtume walipokuwa wakisindikizwa kwenda kuiingia mji wa Damascus, Yazid alikuwa anawangalia kuingia kwao kwenye mlango wa jumba la kiutawala akiwa sehemu iitwayo Yahrum, na mara tu alipoviona vichwa vya mashahidi, alikariri aya ambazo kwazo fikra au wazo muhimu lilikuwa kwamba alifikiria ameyaweka mambo sawa na Mtume.

Ukumbi wa hadhara wa Yazid ulikuwa umepambwa makhususi kwa ajili ya jambo hilo na alikuwa anajishughulisha na uchezaji bao. Watu wa famil- ia ya Mtume walifikishwa kwa Yazid kama watumwa na wajakazi kutoka nchi ya Uhabeshi (Ethiopia) au Dailam au kutoka miongoni mwa Waturuki.

Maelezo ya kupotosha kabisa ya vita vya Karbala yalitolewa na Sahr ibn Qays, wakati ambapo Yazid alikuwa akisoma katika hali ya kuwa amelewa beti zenye maana ya: "Ingekuwa, kwamba wahenga wangu waheshimiwa waliopigana vita vya Badr wangeshuhudia jinsi gani vile wafuasi wa imani (dini) ya Muhammad walivyotupwa katika kuchanganyikiwa kwa michomo ya mikuki, hapo tena wangenisalimu kwa kunibariki, na pengine wangesema, 'Tunaomba kamwe Yazid asipatwe na ugonjwa wa kupooza.' Watu wa ukoo wa Bani Hashim walitumia kucheza mchezo wa hila kuupata utawala. Kwa kweli, hakuna habari za pepo au moto zilizokuja kwao, wala hakuna wahyi wowote ule uliteremshwa."

Alipoyasikia maneno haya, Zainab alianza kutoa hotuba nzito ya kuvutia kufichua unyonge wa misingi

ambamo juu yake utawala na mamlaka ya Yazid yalimojengewa. Alisema: “Ukweli ulioje ambao Mungu wangu ameueleza kwamba watenda mabaya hatimaye huja kubatilisha na kudhihaki alama za Mwenyezi Mungu.

Ewe Yazid, unafikiria kwamba kwa vile umetuzuia sisi milango yote, katika mbingu na juu ya ardhi, na umetushusha kwenye hali ngumu ya wafungwa, basi hata mbele ya macho ya Mwenyezi Mungu sisi pia tumedharaulika, na wewe ni mheshimiwa, au kwamba kufaulu huku kusiko na mashiko halisi umekupewa kutokana na kuwa uko karibu na Mungu?

Ukiwa mwenye furaha kwa fikra hii huwa umetazama mabegani mwako kwa vile kwa sasa hivi unaona tu kwamba ulimwengu unanyenyekea chini ya amri zako, mambo ya nchi yako yakiwa katika mpango na hali nzuri, na utawala wako na serikali yako imewekwa katika usalama kutokana na hatari zote. Je, umesahau onyo la Mwenyezi Mungu lisemalo:

‘**Makafiri wasilichukulie hili, kwamba muhula tunaowapa utawafaa chochote. Tunawapa muda ili kwamba waweze kujitumbukiza wenyewe katika kutenda dhambi mpaka kutosheka kwa mioyo yao, kwani mwishowe, adhabu yenye kufedhehesha imekwishaandaliwa kwa ajili yao**.’

Je, ubora wa hali ya taadhima ya Kiislamu inakutaka wewe kuhifadhi faragha ya wanawake wenu na hata vijakazi wenu na kuwafunga wajukuu wa kike wa Mtume wako na kuwafanya wakimbie huku na huko na kupenda wapigwepigwe mabegani na wahenga wenu makafiri?

Usijisahau, kwani kipindi kifupi sana kijacho na wewe pia yatakutokea haya. Kisha utatamani sana kwamba mikono yako ingelikuwa imeondolewa uwezo wa kufanya kazi na ulimi wako kunyimwa uwezo wa kuongea, kwamba usingefanya yale ambayo umeyafanya na kwamba usingesema yale ambayo umeyasema.

Ni kipi kitakachokuwa kibaya zaidi kuliko kitu kingine katika Siku ya Hukumu, Mwenyezi Mungu atakuwa msuluhishi wa suala lako hili, Muhammad, mteule atakuwa ndiye mlalamikaji (kwa Mwenyezi Mungu) na (Malaika) Jibril atakuwa shahidi yake.

Kisha watafuatia pia wale ambao wamewasaida na wakashirikiana pamoja nanyi katika matendo yenu maovu na wakakuungeni mkono katika kuyapora madaraka (utawala) juu ya Waislamu, tambua jinsi kilivyo kikali kisasi kinachochukuliwa na Waislam juu ya madhalimu na wakandamizaji.

Ingawaje mabadiliko yaliyosababishwa na wakati yamenishusha hadi kwenye hali isiyotamanika ya kufanya nikuhutubie mtu kama wewe usiye na maana kabisa kama ulivyo mbele ya macho yangu, naliona hili kama sehemu ya balaa kubwa hata kule kukukemea tu, lakini nashindwa kujizuia mwenyewe. Huruma kubwa iliyoje kwamba wale ambao wanamwabudu Mwenyezi Mungu wapaswe kukutana na vifo vyao kwenye mikono ya makundi ya watu mashetani!

Ewe Yazid, kama unakula kiapo cha kufanya juu chini au kutoacha juhudi yoyote ile bila kufanywa,

naapa kwa Mwenyezi Mungu hutaweza kufunika kumbukumbu zetu, wala kufutilia mbali kuwepo kwetu duniani, wala kufanikiwa katika kuharibu lengo letu halisi. Doa la umwagaji damu huu wa dhulma litabakia kwako mpaka Siku ya Mwisho na kamwe hutaweza kulisafisha kabisa.

Uamuzi wako hapana shaka yoyote ni ukaidi, maisha yako ni mafupi sana, na kundi la wale wanaokuzunguka kila upande litatoweka kabisa hivi karibuni. Siku imekaribia wakati itakaponadiwa, 'Laana ya Mwenyezi Mungu iko juu ya madhalimu.' Shukurani zote ni kwa Mwenyezi Mungu ambaye amehukumu kwamba mwisho wa watangulizi wetu watukufu wa kuheshimika upaswe kuwa katika wema, na wenye baraka nyingi, na ile roho ya muadhama wetu wa mwisho kutoka katika shahada na rehema Zake. Yeye peke yake anatutoshelezea sisi na ndiye nguzo yetu bora na msaada wetu."

Kisha Yazid aligeukia kwa Ali bin Husein, na ili amuumize hisia zake, alikariri aya ya Qur'ani, yenye maana, "**Msiba wowote ule unakutokeeni ni kutokana na matendo yenu wenyewe.**" Ali bin Husein akamwambia yeye kwamba aya hiyo haikumhusu yeye na kundi lake na kwamba aya ya Qur'ani ambayo ilimhusu yeye na wafuasi wake ilikuwa ni tofauti na hii nayo ina maana ya kwamba msiba ambao uliwapata ulikuwa ni katika kutimiza neno lililowekewa ahadi ambalo lilikuwa limeandikwa tokea mwanzo wa kuumbwa ulimwengu, na ambalo kutimizwa kwake kulikuwa ni lazima.

Akichukulia kwamba hakuna mtu yeyote ambaye angekuwa na ujasiri wa kuudhishwa na utovu wa adabu wowote ule ambao angeuonyesha kwenye kichwa cha Husein hapo Damascus, aliyarudia yale Ibn Ziyad aliyoyafanya kule Kufa.

Aliigusa midomo na meno ya Husein kwa fimbo. Abu Barza al-Aslami mara moja akamkumbusha Yazid kwamba Mtume wa Mwenyezi Mungu alitumia kuibusu midomo na meno ya Husein, na akaongeza kusema kwamba katika Siku ya Hukumu ni Ibn Ziyad tu pekee ndiye ataomba shifaa kwa niaba ya Yazid.

Hatua ilifikia wakati Yazid alitambua kwamba kila mtu katika baraza lake mwenyewe alimfikiria kwamba ana hatia. Katika jaribio lake la kujitetea, mbali na kuufichua uharibifu wake mwenyewe wa tabia na upotofu, alikubali kujifanya ameguswa sana na ulevi wa mafanikio kiasi cha kutoka kwenye sera za tangu zamani za Bani Umayyah za kuwaficha watu na kuwasahaulisha juu ya familia ya Mtume. Aliwauliza watu, "Je mnajua kwa nini janga limempata Husein?

Ni kwa sababu tu Husein alifikiria kwamba baba yake, mama na babu yake walikuwa bora zaidi kuliko baba yangu, mama na babu yangu. Sasa masuala haya yamewekwa sawa na ukweli wa kwamba wakati baba yake alipopigana dhidi ya baba yangu, ulimwengu unajua ni kwa manufaa ya upande wa nani uamuzi wa vita ulipotangazwa.

Ni kweli, hata hivyo kwamba mama yake alikuwa bora zaidi kuliko mama yangu na pia kwamba babu yake alikuwa bora zaidi kuliko babu yangu kwani hakuna Mwislamu awezaye kumfikiria mwingine yeyote yule kuwa sawa na Mtume.

Hata hivyo, walipotosha maana ya aya ya Qur'ani, wakimaanisha kwamba Mwenyezi Mungu ni Mola wa Ufalme na utawala. Humpa ufalme yeyote amtakaye na kumnyima ufalme yule amtakaye. Humtukuza amtakaye na humtweza yule amtakaye. Hakika, yeye ni mwenye uwezo juu ya kila kitu."

Ingeonekana kutoka kwenye hotuba hii kwamba kuwa na sifa ambazo humtunukia heshima, Yazid aliikubali hali ya udhalili wake kwa Husein. Aliegemeza hoja yake ya mwisho kuthibitisha ubora wake juu ya ule wa Husein kwa kigezo cha kushinda na kuchukua madaraka. Hoja hii pia ingetumika kwa madhalimu na watesaji wengine wa wanadamu wenye kufahamika kuthibitisha uadilifu wao na kutokuwa na hatia kwao. Aya hiyo haifanyi mafanikio ya ushindi na kuchukua madaraka (utawala) kuwa vigezo vya uadilifu.

Yahya bin al-Hakam, mmoja wa Bani Umayyah, alikuwa amesikitishwa mno kwa maovu yaliyofanywa dhidi ya Husein na watu wengine wa famil- ia ya Mtume kiasi kwamba alianza kuonyesha huzuni yake waziwazi kutokana na kifo cha kishahidi cha Husein na kumsema vibaya Ubaydullah bin Ziyad pale hadharani. Yazid alimpiga Yahya kifuani mwake kwa mkono wake na akasema; "Je, hutanyamaza kimya?"7

Mke wa Yazid, Hind bint Abdallah bin Amir aliingia haraka sana mle barazani kwake huku akilia na kuomboleza akisema, "Ole, kichwa cha kipenzi cha Fatimah, binti ya Mtume, katika hali mbaya ya kuhuzunisha hivi."

Watu wa Husein waliosalimika vitani hawakupelekwa haraka nyumbani kwao Madina, bali walibakia kwa muda mrefu katika hali ya umateka hapo Damascus.
Yazid aliwaachia huru na aliwapatia nyumba wakati tu alipoona dalili za kuongezeka kwa hali ya wasiwasi na kutoridhishiwa na utawala wake kulipojidhihirisha katika nchi na Bani Umayyah wakagundua makosa yao ya kisiasa. Kisha wanawake wa familia zilizochaguliwa wali- waendea wanawake wa familia ya Husein kwenda kuwapa pole na kuwafariji kutokana na vifo vya mashahidi, na maombolezo yakafanyika kwa muda wa siku tatu.

Al-Numan bin Bashir al-Ansar ambaye alikuwa ameondolewa kwenye ugavana wa Kufa kwa kutokumtendea Muslim bin Aqil ukatili baada ya kuwasili kwake pale Kufa, sasa alielekezwa kupanga kuwapeleka Madina watu wa Husein waliosalimika vitani kwa uangalizii unaostahili na kwa taadhima. Yazid aliwapeleka watu wake thelathini pamoja na al-Numan bin Bashir ambaye aliwatendea jamaa wa familia ya Mtume kwa heshima, taadhima na wema katika safari yote ya kwenda Madina.

Hii ilikuwa ni sehemu ya jaribio la Yazid lisilofanikiwa, la kujaribu kutaka kujikosha na kosa la mauaji ya Husein na sahaba zake na ndugu zake. Akiongea na Ali bin Husein katika faragha, alisema, "Mungu amlaani mwana wa Marjana kama ningewahi kukutana na baba yako moja kwa moja, ningelikubali kila jambo ambalo alikuwa amelipenda na kamwe nisingeridhia kifo chake. Vyovyote vile, lile ambalo limekadiriwa na Mungu limetokea. Sasa waweza kwenda Madina, fanya mawasiliano na mimi na nijulishe nijue ni kitu gani unahitaji." 8

Jambo ambalo halijawahi kutokea katika uzito na urefu wa muda wake, lilikuwa ni vilio na maombolezo ambayo yalitokea katika mji wa Madina wakati wa kuwasili kwa msafara wa watu wa Husein waliosalimika katika vita.

Mwanamke atokanaye na familia ya Abdul Muttalib, nywele zake zikiwa timtim, alikuwa akikariri ibara zenye maana, “Jibu gani mtakalotoa kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu wakati atakapokuulizeni katika Siku ya Hukumu, ‘Vipi mliwatendea dhuria wangu baada yangu?’ Wao sasa hivi wameshushwa katika hali kama hii kwamba baadhi yao ni mateka, na wengine katika wao, damu yao ilimwagwa chini na wamefunikwa na vumbi. Je, haya yalikuwa ndiyo malipo ya huduma zangu kwamba mpaswe kuwatendea kizazi changu katika mtindo huu?”[9]

1. Akhbar al-tawal, uk. 256.
2. Tabari, juz. 6, uk. 260
3. Tabari, juz. 6, uk. 261-262 na Irshad, uk. 258.
4. Akhbar al-Tawal uk. 256.
5. al-Irshad, uk. 260.
6. Tabari, juz. 6, uk. 264 al-Irshad, uk. 260.
7. Tabari, juz. 6, uk. 265.
8. Tabari, juz. 6, uk. 269/al-Irshad, uk. 263.
9. Tabari, juz. 6, uk.221

# Sura Ya 31: Mazingatio Ya Kina Juu Ya Umateka Wa Wanawake Wa Familia Ya Husein

Lengo la Yazid halikuwa ni kumuua Husein tu kwa kisingizio cha kukataa kwa Husein kutoa kiapo cha utii kwake, bali pia na kuangamiza kitovu (kituo kikuu) cha kiroho ambacho kwa kuwa mlezi wa mafundisho ya Uislamu, hakiweza kushirikiana na yeyote yule katika zoezi la kuendesha utawala usio halali, Mfululizo wa matukio yote ambayo yalianza na uonyeshaji wa ukaaji wa Husein mjini Madina kuwa ni chanzo cha hatari kwa maisha yake, safari yake kutoka Makkah chini ya mazingira yenye kufanana na hayo, na yale mauaji makubwa ya Karbala na matokeo ya kufungwa na kutembezwa kwa wanawake wa familia ya Husein kutoka sehemu moja kwenda nyingine, katika hali ya umateka, yote haya yali- chochewa bila namna yoyote ile ya shaka, na maelekezo ya Yazid.

Kama Ubaydullah bin Ziyad asingewapeleka wanawake hao Damascus katika hali ya umateka kwa agizo la Yazid, na kama Yazid hakuwa amenuia kweli kuwadhalilisha, basi wangepelekwa moja kwa moja Madina.

Badala ya kuwapokea kwa busara na mema, Yazid aliamuru waletwe kwake kwenye ukumbi wa mikutano mbele ya wajumbe wake wa baraza na akaonyesha dhihaka juu ya kichwa cha Husein mbele

yao wote. Ilikuwa tu baada ya muda mrefu kupita ambapo Yazid akatoa nyumba kwa ajili ya makazi ya wanawake hao wa familia ya Husein. Wanawake wa baadhi ya familia zilizochaguliwa za mjini Damascus baadaye waliwatembelea wanawake wa familia ya Husein ili kutoa rambirambi zao kwa vifo vya mashahidi hao.
Husein alikuwa ameshauriwa asiwachukue wanawake na watoto pamoja naye wakati alipoanza safari yake kutoka Makkah kwenda Kufa. Hata hivyo, alishikilia uamuzi wake huo, wakati mwingine akisema kwamba huu ulikuwa ni uamuzi wa Mwenyezi Mungu kwamba wapaswe kufanywa wafungwa, au pengine angesema kwamba lolote lile ambalo limeamuliwa na Mwenyezi Mungu kuwa, lazima lije kutokea.

Msimamo huo huonyesha kwamba akizijua vyema kabisa hatari zote hizi na vipingamizi vyote ambavyo viliandamana na kuweko kwa wanawake hawa pamoja naye katika safari yake, Husein alichagua kuwachukua pamoja naye. Je, yalikuwa ni mawazo ya Husein kwamba kuwepo kwa wanawake pamoja naye katika safari hiyo kungesaidia jambo moja muhimu katika kulifikia lengo lake?

Husein kamwe hakukusudia kupigana kwa kutumia rasilimali za kimaada (silaha na vitu vinginevyo) ili kupata maslahi ya kidunia. Alikataa kutoa kiapo cha utii kwa Yazid ili kuisalimisha haki na uadillifu. Yeye aliamua kushikilia msimamo wa kukataa kwake mpaka pumzi ya mwisho ya uhai wake, ili kwamba haki iweze kuwepoiliyo wazi kabisa na isiyofichika kwa watu kuweza kuiona – na pia ili kwamba mtu yeyote asije akapotezwa kabisa katika kushikilia kwamba kitendo na mwenendo wa tabia ya Yazid vilibeba ridhaa ya Uislamu au vilihusiana kwa namna yoyote ile na Uislamu. Ilikuwa ni katika umuhimu wa juu sana kwa kulitimiza lengo lake kwamba maadui zake wapaswe kuona ni vigumu kutafsiri chochote kati ya vitendo vyake.

Lengo hili lilifaulu kwa mafanikio makubwa sana kwa kuwepo wanawake wa nyumba yake pamoja naye pale Karbala, na kuwa na haki kwake, na uonevu mwingi na makosa mengi yasiyo na idadi ambayo aliyavumilia yaling'ara kwa mwanga mng'avu sana kiasi kwamba hakuna kiwango chochote cha upotoshaji kingeweza kuleta dalili japo kidogo za shaka au wasiwasi juu ya hayo.

Utawala wa Bani Umayyah ulitumia dhidi ya Bani Hashim mkakati mujarabu wenye sanaa ya kumfanya Uthman bin Affan kama Khalifa aliyedhulimiwa na kuuwawa, wakiwashikilia Bani Hashim kwa ujumla, na hususan Ali, kuhusika na mauaji yake.

Ili kuongeza hoja na nguvu kwenye propaganda hii, shati la Uthman lililotapakaa damu na vidole vya mke wake Naila vilivyokatwa, vyote vilionyeshwa kwa watu kwenye mikutano iliyofanywa mara kwa mara kuomboleza mauaji ya Uthman ndani ya msikiti mkuu mjini Damascus. Umati mkubwa wa watu walishughulishwa katika kulia na kupiga vichwa vyao na vifua katika kuomboleza juu ya Khalifa huyo aliyefariki.

Watu wa Bani Umayyah walifanikiwa kupata kuonewa huruma kwa kujifanya kama wao ndiyo warithi wa Uthman na wakadai kulipiza kisasi kwa damu yake. Matokeo mabaya ya propaganda hii ya uwongo

yasingeweza kusitishwa isipokuwa mpaka dhuria ya Mtume ipatwe na msiba kama huo mikononi mwa warithi wa Abu Sufyani.

Kwa kumuua Husein, adui bila ya kujua walifanikisha kuleta mapinduzi katika nyoyo za watu na kusababisha mabadiliko ya hisia za watu katika kuunga mkono familia ya Mtume. Wakiwa wamelewa ushindi, Bani Umayyah walizorota kuufahamu mgeuko huu kamili na usiotazamiwa wa hisia za umma. Mpaka mwezi 10 ya Muharram walikuwa wakirejelea kwenye kumbukumbu ya mauaji ya Uthman katika kuhalalisha matendo yao. Kuzuiwa kwa ugavi wa maji kwa Husein na sahaba zake kulichukuli- wa na wao kama ni kulipiza kisasi kwa kukataliwa ugavi wa maji kwa Uthman, ingawa hakukuwa na Bani Hashim yeyote aliyehusika chochote na jambo hilo.

Maovu yaliyokithiri yaliyofanywa hapo Karbala, kuanzia na kuuawa bila huruma masahaba na ndugu wa Husein, pamoja na mtoto wake mchanga, na mauaji yake mwenyewe, kukanyagwa kanyagwa maiti yake chini ya kwato za farasi, kuporwa na kuchomwa moto mahema yaliyokuwa yakikaliwa na wanawake wa familia ya Husein, kunyanyuliwa juu kwa kichwa kilichokatwa cha Husein kwenye mkuki na taabu nyingi zisizoelezeka na ufidhuli, ambayo yote haya watu wa Husein waliosalia katika vita waliyapata, yalikuwa kwa namna ya ukatili wa kuchukiza sana kiasi kwamba marafiki wa Bani Umayyah walinyamazishwa kabisa na wakaepuka kuongea masaibu ya Uthman katika mazingira ya matukio ya Karbala na matokeo yake yaliyofuatia mara tu baada ya hapo.
Inashangaza kuona kwamba wakati shati la Uthman lililotapakaa damu na vidole vya mke wake Naila vilionyeshwa kwa watu ambao walitokana na kundi la Khalifa aliyekufa (Uthman), na walikuwa hawana ushahidi wa kuwatambulisha wale ambao walilitenda jinai hiyo, vichwa vilivyokatwa vya mashahidi wa Karbala vikiwa vimenyanyuliwa juu kwenye mikuki, na mateka wa familia ya Husein, wakiandamana pamoja na kichwa cha Husein mwenyewe, waliongozwa huku na huko na wauaji hao wenyewe, wakifanya uchunguzi wowote wa kuchukua muda kwa ajili ya kuwahakiki wahalifu wenyewe, au kuwatambua, kuwa hauna umuhimu kabisa. Matokeo yalikuwa kwamba hata huruma za wale ambao, kwa sababu ya upendeleo wao kwa Uthman, waliwapendelea Bani Umayyah, walitengwa nazo na zikahamishwa kwa Bani Hashim.

Kama Husein asingewachukua wanawake wa familia yake pamoja naye, ingeweza kuwa ni vigumu kwamba msiba wa Karbala uweze kutangazika kwa mapana sana na kwa athari kubwa katika kipindi kifupi sana kama hicho, na upotofu wa Bani Umayyah ukadhihirika kwa nguvu na kwa haraka sana kwa watu.

Ni muhimu sana kwamba haki ilikuja kufahamika na kutambulika kwa mfano huu, kwani masula sio machache katika nchi za Kiislamu, kama kwa hakika ilivyo katika sehemu nyingine pia, ambamo humo mwanga wa haki kuhusu kadhia za namna hii huwa umezimwa, na hakuna mtu yeyote ambaye amefanikiwa katika kuufikia ukweli kupitia utusitusi uliotanda. Hasan bin Ali alitiliwa sumu na hata sasa hivi utambu- lisho wa mtu yule ambaye anahusika kimsingi kwa kutenda jinai hiyo bado limewekwa kuwa ni lenye kutiliwa mashaka.

Kama watu 72 au 125, idadi iliyokisiwa ya wale ambao walijitolea mhanga maisha yao kwa ajili ya al-Husein na misingi yake, waliuawa hapo Karbala, wakizungukwa na pazia za silaha za makundi ya Yazid, wakiwa wametengwa kabisa na dunia yote iliyobakia, kiasi kwamba, bila kutaja uwezekano wa kuwafikiwa na mwanadamu, hata kuwapelekea habari lilifanywa kuwa jambo lisilowezekana, ingekuwa ni rahisi sana kwa Yazid na vibaraka wake kutoa upindishaji wowote ule kwenye maelezo ya tukio hili, kama ikibidi lazima kutoa maelezo yoyote yale.

Kwani wangekuwa ni hao wauaji tu ndiyo wangekuwa mashahidi wa tukio hilo na wangeweza kulipa mapambo ya rangi yoyote ambayo ingewafaa kwa lengo lao.

Ni nani wangekuwa pale kama mashahidi wa matukio yote kuweza kuukanusha moja kwa moja ule uwongo ambao ungetolewa na maadui wa Husein? Wangeweza vizuri kabisa kuelezea tabia ya Husein katika namna tofauti kabisa.

Kwa mfano, angeweza kushutumiwa na ukaidi wa wazi wa kuidharau mamlaka iliyokuwa madarakani. Au wasiwasi pia ungeweza kuletwa juu ya nia na mwenendo wa Husein, mbali na mihanga yake yote hiyo mikubwa na isiyo na kifani iliyochukuliwa kuongoza katika mwamko wa wema na uadilifu. Katika kurasa za historia, Yazid angeweza kuibuka kama mtetezi wa Uislamu, na Husein angekuwa kama mwasi na mueneza fitina.

Hakuna mbadala kwa ajili ya wale wanawake wasio na marafiki na walio watoharifu wa familia yake, walioongozwa na kupelekwa toka mji mmoja kwenda mji mwingine kama wafungwa, nyoyo zao zikiwaka moto kwa huzuni na hisia kali, damu ya Ali na Fatimah ikitiririka ndani ya mishipa yao, ndimi zao zikitoa matamshi kwenye khutuba zenye kugusa sana, zikikumbusha ufasaha wa lugha wa Mtume na ya Ali, ungeweza kupatikana kwa Husein kwa ajili ya uenezaji baada yake wa falsafa ya Shahada (mihanga) na uenezaji wa uadilifu na haki.

# Sura Ya 32.: Maelezo Mafupi Juu Ya Wafungwa Watokanao Na Familia Ya Husein.

Maelezo yamekwishatolewa katika Sura ya nyuma kuhusu kila shahidi wa Karbala. Sasa zinafuata taarifa fupifupi juu ya wale walio mashuhuri mion- goni mwa watu wa Husein waliosalimika vitani ambao walishikiliwa mateka:

1. Ali bin Husein alikuwa mtoto mkubwa wa Husein alizaliwa mwaka wa 38 A.H wakati babu yake Ali alipokuwa ndiye Khalifa, na alikuwa chini ya umri wa miaka mitatu wakati Ali alipouawa katika mwaka wa 40 A.H. Alikuwa zaidi kidogo ya miaka 22 umri wake wakati alipofuatana na baba yake katika safari ya

kwenda Iraq. Haijulikani lini haswa alipatwa na maradhi, lakini mwezi 10 ya Muharram mwaka wa 61 A.H alikuwa mnyonge sana kiasi cha kushindwa hata kukaa tu, na kwa hivyo hakuweza kushiriki katika jihadi hiyo ya Karbala.

Baada ya kuuawa wafuasi wote, marafiki na ndugu wa Husein, na yeye Husein mwenyewe, Ali bin Husein alichukuliwa mateka na akafungwa minyororo.Alilazimika kuchukua safari iliyo na maumivu na udhalilishaji kutoka Karbala hadi Kufa, na kutoka hapo kwenda Syria kwa miguu pamoja na wanawake wa familia yake.

Hali yake lazima haikuwa ya kutweza kudogo ya kuhudhuria baraza ya Ibn Ziyad kule Kufa na ile ya Yazid mjini Damascus, ambako yeye, mama zake, shangazi na wanawake wengine wa familia yake walifikishwa mbele ya baraza hizo kama wafungwa.

Baada ya kuachiwa huru huko Syria, yeye alikwenda Madina kutumia muda uliobakia wa maisha yake katika Sala. Alifariki katika mwaka wa 96 A.H. Majina yake yanayofahamika sana ni Zayn al-Abidin na Sayyid al- Sajjad na ameacha mkusanyiko wa maombi yake mwenyewe na dua kwa kitabu kifahamikacho kama *al-Sahifa al-Kamila* ambacho ni kitabu kinachotukuzwa sana. Kaswida (taabini) ya al-Farzdaq kumhusu yeye ni sanaa kubwa katika fasihi ya Kiarabu.

2. Zainab alikuwa binti mkubwa wa Ali na Fatimah, binti ya Mtume. Alikuwa ameshika nafasi ya kuonekana wazi mno miongoni mwa watu wa Husein waliopona katika vita. Alikuwa bado mdogo sana wakati mama yake alipofariki dunia. Baba yake alimlea na kumkuza na alimwoza kwa Abdallah, mtoto wa ndugu yake Ja'far. Alifuatana na Husein kutoka Madina hadi Karbala na wakati huo alikuwa na umri wa miaka kama 50 hivi.

Wakati mmoja, aliposikia kutoka kwa Husein hapo Karbala kwamba hati- mae amejiandaa mwenyewe kwa ajili ya kifo, kwani kulikuwa hakuna njia mbadala iliyobaki kwake, wakati Zainab alipojipiga uso wake na kupasua nguo zake kutokana na huzuni iliyozidi kiwango, al-Husein alimuapisha asitatue vazi lake au kujiparura uso wake au kunyanyua sauti kubwa ya maombolezo kwa ajili yake baada ya kifo chake.

Zainab aliyatia moyoni maelekezo haya na katika hali zilizokuwa na mitihani mkali sana hakuzisaliti ishara zozote za hofu isiyofaa na ikaweza kuleta kufurahia miongoni mwa maadui kwa mateso apatayo. Alikuwa ni yeye Zainab ambaye alimpa Husein nguo ya kuvaa ndani kati ya nguo zake zote nyingine za ndani, na aliipasuapasua katika sehemu nyingi mbalimbali ili kuifanya isifae kwa makusudio ya kuporwa baada ya kifo chake.

Baada ya tarehe 10 ya Muharram, msafara wa watu wa Husein waliopona vita uliondoka Karbala, ukitanguliwa na vichwa vya mashahidi vilivyoinuliwa kwenye mikuki, pamoja na Ali bin Husein, dhaifu na aliyefungwa minyororo, akifuatia kwa miguu ngamia waliowabeba wanawake na watoto na wakawasili Kufa, makao ya serikali ya Ubaydullah bin Ziyad, mji ulikuwa umewekwa katika hali nzuri, sehemu ya sokoni ilipambwa na watazamaji walisongamana sehemu zote zenye kufaa kutazamia mambo ili kuuangalia msafara wa wale ambao, kama walivyoambiwa, walikuwa ni maadui wa Waislamu.

Katika mazingira haya ambayo yalikuwa siyo ya kirafiki kabisa na katika hali zenye kuvunja moyo kupita kiasi na kuhuzunisha, Zainab alitoa hotuba nzito, ambayo ndani yake hakuelezea hali yake ya kuhuzunisha na kusikitisha, wala hakuomba afanyiwe huruma bali kwa lawama kali kabisa aliyapitia tena yale matendo ya kihaini ya maadui zake na kuwataka kuzichunguza nyoyo zao na kutafakari juu ya makosa yao mabaya.

Macho yote yaliyokuwa yameamshwa kushuhudia taabu na mateso ya wafungwa hao yaliinamishwa chini kwa aibu. Ufasaha huohuo ulikuwemo kwenye hotuba yake ndani ya baraza ya Yazid huko Damascus.

3. Umm Kulthumu alikuwa bint wa pili wa Ali na Fatimah, mdogo kuliko Zaynab. Jina lake lilikuwa Zaynab al-Sughra na Umm Kulthumu lilikuwa ndiyo '*Kuniyat*' yake. Aliolewa na binamu yake aitwaye Muhammad bin Ja'far bin Abi Talib na alifanywa mjane wakati baba yake akiwa yungali hai. Baada ya kifo cha mume wake, aliishi na ndugu (kaka) zake. Alifuatana na Husein wakati alipoondoka Madina kwenda Makkah na akabaki naye mpaka kuuawa kwake kishahidi. Yeye pia alitoa khutba ya kusisimua sana katika sehemu ya sokoni hapo Kufa baada ya khutba ya Zainab.

4. Rukaya alikuwa bint ya Ali bin Abi Talib kwa mke wake Umm Wahb, bint ya Rabia. Rukaya na kaka yake mmoja aitwaye Umar walizaliwa mapacha. Aliolewa na Muslim bin Aqil.

Yeye pamoja na mumewe walifuatana na Husein kutoka Madina, na aliendelea kubakia naye wakati mume wake alipotumwa kwenda Kufa kutoka Makkah. Katika mwendo wa safari ya Husein kutoka Makkah taarifa ziliwasili za kuuawa kishahidi kwa mume wake, aliendelea kusafiri na kaka yake mpaka alipokwishafika Karbala alimtoa mhanga mwanawe, Abdallah bin Muslim kwa ajili ya Husein mnamo mwezi 10 Muharram mwaka wa 61. A.H. Alishiriki pamoja na Zainab na Umm Kulthumu, dada zake, katika taabu zote kubwa na za huzuni zilizowakuta watu wa Husein waliopona vita, na hatimaye alirejea pamoja nao Madina.

5. Layla al-Thaqafiyya alikuwa mama wa Ali al-Akbar bin Husein. Uhusiano wake na Mu'awiyah na Yazid kumetajwa katika maelezo yenye kumhusu Ali al-Akbar. Alikuwa pamoja na Husein hapo Karbala na alishiriki katika matatizo na dhiki za kuchukuliwa mateka pamoja na dada zake Husein.

6. Rabab bin Imru al-Qays alikuwa ndiye mama yake Sakina bint Husein na ndugu yake wa kiume, Ali al-Asghar bin Husein (Abdallah). Alikuwa hapo Karbala, akiwa amefautana na Husein kutoka Madina. Alipitia miti- hani yote ambayo wanawake waliosalimika wa familia ya Husein walikabiliana nayo, lakini badala ya kurejea pamoja nao Madina wakati waliporejeshwa uhuru wao alibakia Karbala katika hema lililoko karibu na kaburi la Husein kwa mwaka mmoja, na akawa anakusanya makundi ya watu, mchana na usiku kuomboleza mauaji ya bint ya Husein. Rabab alirejea Madina baada ya mwaka na hapo napo pia aliutumia wakati wake katika kumlilia Husein, na tendo hili lilichukua muda mrefu.

7. Mama wa Fatimah bint Husein alikuwa Umm Ishaaq bint Talha bin Ubaydullah al-Taymi. Hasan al-Muthanna, mtoto wake Imam Hasan alim- womba ami yake, Husein kumpa mmoja wa bint zake amwoe. Hata hivyo, alizuiliwa na adabu kuonyesha chaguo lake. Husein alimchagua Fatimah kwa ajili

ya ndoa hiyo iliyopendekezwa kwa vile yeye alifanana sana na mama yake mwenyewe, Fatimah, bint ya Mtume.

Wakati Husein alipokuwa anaondoka kwenda kwenye jihadi ya mwisho alikabidhi wasia wake na nyaraka nyingine muhimu kwa Fatimah zije kutolewa kwa Ali bin Husein wakati atakaporejewa na fahamu zake. Alibakia hai kwa miaka mingi baada ya msiba wa Karbala na anatambuli- ka kama msimuliaji wa hadith. Mtoto wake wa kiume Abdallah bin al- Mahd alikuwa akisimulia hadithi kutoka kwake. Wakati mume wake, Hasan bin al-Hasan, alipofariki dunia, alifunga wakati wa mchana na aliu- tumia usiku wote katika Sala mara kwa mara kwa kipindi cha mwaka mzima katika hema lililosimamishwa karibu na Kaburi lake. Kisha alirejea Madina.

8. Sakina bint Husein alikuwa dada kamili wa Ali al-Asghar. Alikuwa mdogo sana wakati vita vya Karbala vilipopiganwa. Maelezo ya maisha yake, baada ya tukio hilo yamekosa uthibitisho wa kutegemeka. Sasa yanafuata maelezo mafupi ya wanawake ambao kwa namna fulani maalum walihusika na matukio ya Karbala ingawaje hawakuwa pamoja na Husein katika tarehe 10 ya Muharram.

(1) Umm Salama alikuwa mwanamke mwenye tabia njema za kipekee sana miongoni mwa wake za Mtume, ambaye alimwoa katika mwaka wa pili baada ya kuhama Makkah. Alikuwa amebakia hususan hasa katika kuwapenda watu wa Nyumba ya Mtume hata baada ya kifo cha Mtume.

Al-Tirmidhi ameelezea kwamba tarehe 10 ya Muharram aliona katika ndoto Mtume akilia, kichwa chake na ndevu vyote vimefunikwa na vumbi, na alimwambia kwamba Husein ni hivi karibuni tu amekwishauawa.
(2) Umm al-Banin Fatimah bint Hizaam bin Khalid alikuwa amechaguliwa na Aqil kwa ombi la ndugu yake Ali bin Abi Talib, kama mwanake aliyetoka kwenye familia ifahamikayo waziwazi kwa ushujaa na ujasiri, ili kwam- ba kizazi chake kutokana naye (mwanamke huyu) kiweze pia kuwa jasiri sana na kujaaliwa kupata sifa za kijeshi. Alikuwa na watoto wanne wa kiume majasiri ambao katika hao Abbas alikuwa ndiye mkubwa na wote hao waliojitolea mhanga maisha yao kwa ajili ya Husein mnamo mwezi 10 ya Muharram.

Haiwezekani kueleza hisia nzito za huzuni zilizohisiwa na mama ambaye alipoteza vijana wanne mashujaa katika siku moja ndani ya masaa machache tu! Imesimuliwa kwa uaminifu kabisa kwamba, baada ya kupa- ta taarifa za msiba wa Karbala, Umm al-Banin alitumia kwenda kila siku kwenye maeneo ya makaburi ya al-Baqi na mtoto mdogo wa kiume wa Abbas, aliyeitwa Ubaydullah, ili kusoma hapo mashairi ya maombolezo kuhusu Abbas ambayo yalikuwa ni yenye kuumiza sana nyoyo yaliyoweza kuvuta watu, siyo wa Madina tu bali pia wakati mwingine hata yule adui mkubwa wa watu wa nyumba ya Mtume kama vile Marwan kuyasikiliza yakisomwa.

Ingefaa kuongeza maelezo mafupi hapa kuhusu wale wanawake pia ambao walikuwa wamehusiana na baadhi ya wafuasi wa Husein, na walifanya kitu chenye umuhimu maalum kuhusiana na matukio ya Karbala. Maelezo haya ni kama ifuatavyo:

1. Dalham bint Amr alikuwa mke wa Zuhayr bin al-Qayn. Alikwenda pamoja na mumewe kutekeleza ibada ya Hijja katika mwaka wa 60 A.H na katika kurudi kwao walitokea kukaa Zaruud mahali ambapo Husein alikuwa naye pia akikaa akiwa katika safari yake ya kutoka Makkah kwenda Iraq. Zuhayr bin al-Qayn alikuwa wakati huo ni miongoni mwa kundi la Waislamu la Uthman na alikuwa na mshughuliko mdogo sana na familia ya watu wa nyumba ya Mtume (Ahlil Bait). Husein alimtuma mtu mmoja kwenda kwa Zuhayr kumtaka Zuhayr amwone.

Zuhayr hakupenda kuonana na Husein, na ilikuwa ni mke wake Dalhan, aliyemwonyesha ni kuchukiza kusikofaa kiasi gani, kwa yeye kukataa kwenda kuonana na mjukuu wa Mtume. Hivyo Zuhayr akihimizwa na mke wake alikwenda kuonana na Husein na alirejea akiwa ni mtu aliyekwishabadilika kabisa, akiwa kipenzi cha Husein ambaye alijitoa mhanga maisha yake kwa ajili ya Husein.

Zuhayr alimtaliki Dalham na kumrudisha kwa mama yake, na yeye mwenyewe akafuatana na Husein kwenda Karbala.

2. Umm Wahb bint Ma'bad alikuwa mke wa Abdallah bin Umayr al-Kalbi. Waliishi Kufa. Wakati Abdallah bin Umayr alipotambua maandalizi ya hali ya kivita ya Ubaydullah bin Ziyad pale Nukhayla, na kuwasili kwa Husein Karbala, aliwasilisha nia yake ya kwenda kumsaidia Husein kwa mke wake ambaye mara moja, bila ya kupinga alikubali na akamwomba amchukue pamoja naye pia kwenda Karbala.

Kwa hiyo, wote wawili waliondoka kwenda Karbala usiku mmoja na kuungana na Husein na wafuasi wake. Alikuwa ni mwanamke pekee aliyeuawa hapo Karbala na damu isiyo na hatia ya mwanamke huyu asiye na ulinzi iliyomwagika hapo Karbala iliongeza sura mpya kwenye maovu yaliyotendwa hapo.

3. Mke wa Muslim bin Awsaja alikuja na mume wake mpaka Karbala. Alimpeleka mke wake kukaa katika hema zilizokuwa zikitumiwa na wanawake wa familia ya Husein.

4. Bahriyya bint Mas'ud, alikuwa mke wa Janaada bin Ka'b al-Ansari. Alifuatana na Husein pamoja na mume wake kutoka Makkah. Alimtuma kijana wake, Amr bin Janaada kwenda kujitoa mhanga maisha yake kwa ajili ya Husein, baada ya Janaada mwenyewe alipokwisha kutana na kifo cha kishahidi. Mama huyo alikitupa kuwarudishia maadui kichwa cha yule mwanawe ambaye maadui hao walikuwa wamekitupia kwenye jeshi la Husein na mama huyo akamshangilia mwanawe kwa mhanga wake ulio-tukuka ambao ulimfanya awe na furaha isiyo na kifani.

# Sura Ya 33: Haiba Na Mafanikio Ya Husein

# Yahakikiwa

Mihanga yote katika kuutetea ukweli na haki kabla ya masaibu ya Karbala ilifanywa na watu binafsi wakitenda wao peke yao, kama Zakariyya na Yahya, na wajumbe wengi wengine wa Mwenyezi Mungu pamoja na Kristo ambaye kwa mujibu wa Wakristo, alisulubiwa, au kama vile Socrates ambaye alikunywa kikombe cha sumu.

Mihanga iliyotolewa hapo Karbala ilitofautiana vikubwa sana na mihanga mingine yote kwani hiyo ilitolewa na kundi la wanaume na wanawake na watoto ambao kwamba wanaume walitoa maisha yao baada ya kuvumilia mateso yasiyoelezeka na wanawake na watoto walilazimika kupatwa na mateso yasiyovumilika na dhiki iliyofuatana na umateka.

Wanaume na wanawake na watoto hawa walitokana na makundi ya umri wakati mwingine yakitengana kwa mbali sana kati ya moja na jingine, na idadi yao ilizidi mia moja, na miongoni mwao, mbali na watu huru mara nyingi walikuwa wakutwe humo watumwa, Waarabu na Waturuki, Wahabeshi na Waajemi, waliotokana na tabaka zote zenye kuheshimika za jamii. Hawakuwa na mahali pa kukutana pamoja kati yao isipokuwa umoja wa lengo.

Bila shaka watu wengi mno kwa hiari na kwa uamuzi unaojieleza na uchaguzi waliunganisha mawazo yao, fikra, nia zao, malengo yao na sababu zao za utendaji katika zile za kiongozi wao Husein. Kwa hiyo, ni sawa kabisa kusema kwamba ulimwengu hauna kiongozi na haku- na baraza la watu wa kuonyesha ni nani ambaye angeweza kufanana hata kwa kidogo sana na Husein na wafuasi wake.

lazima ionekane kuwa si wa namna nyingine isipokuwa nzuri ajabu, kwamba ubora wa uongozi wa Husein ulikuwa kiasi kwamba alipokea utii mkubwa wa dhati kutoka kwenye idadi kubwa ya wafuasi wake, ambao waligawanyikana katika jinsia, umri, asili, usuli na hali ya kijamii kiasi kwamba hakuna mfano hata mmoja uwezao kutolewa, wakati yeyote kati ya wafuasi wake angeelezea hisia yoyote ile ambayo ingewaza kuwa na mwelekeo japo mdogo kabisa wa kwenda kinyume na mawazo au fikra zake yeye mwenyewe (a.s.).

Ni jambo la ajabu ya kipekee kwamba wakati ambapo Husein alitoa hotu- ba nyingi kwa maadui zake akiwashawishi waache kumwonea, hakuwahi kuongea hata mara moja na rafiki na ndugu zake kuwasihi wamsaidie. Hasha, kinyume chake aliitumia kila fursa akijaribu kuwazuia wasiungane naye, wakati wao hawakupoteza nafasi yoyote ya kumuelezea hisia zao za nguvu kabisa za upendo.

Kwa njia ya mfano wake mwenyewe wa dhamira isiyobadilika ya kudumisha ukweli na haki, Husein aliwafundisha wafuasi wake kiakili kufuata njia ya wema na kutetea kweli na haki kwa ajili yao wenyewe na kujitoa mhanga maisha yao kwa ajili ya malengo haya. Kwa hiyo katika vita vya Karbala, kila mmoja wa wale waliokuwa pamoja na Husein alijitokeza mbele kwa hiari yake mwenyewe kukutana na mauti akiyaangalia moja kwa moja machoni, wakati wote akiwa na imani juu ya haki na uhalali wa sababu

yake.

Utiaji fora usiokifani wa haiba ya Husein. Husein angeteuliwa kwa ubora wa sifa kama angetoa sauti yake pekee dhidi ya Ukhalifa wa Yazid baada ya kuwa umekubalika kwa watu wengi, lakini alipanda kwenye utukufu wa juu zaidi, wakati aliposisitiza changamoto yake (upinzani wake) na akayakabili makundi makubwa na mengi ya Yazid.

Husein angepata cheo cha juu sana cha shahidi kama baada ya kupitiwa na mitihani yake yote, angejitoa mhanga maisha yake yeye mwenyewe tu. Bali alipanda kwenye vilele vya ushahidi visivyoweza kufikiwa, kwa mhanga wa wafuasi wake wote watiifu, vipenzi wake wakubwa na ndugu zake wa karibu kabisa na muhanga wake yeye binafsi pale Karbala.

Husein angekuwa kiongozi wa watu asiyeshindikana kama, katika mazingira ya kukatisha tamaa, yenye kuvunja moyo na yenye kutisha mno ambayo alijikuta akiwa ndani yake pale Karbala angeliweza kuwabakiza wafuasi wake na kuwa pamoja naye kwa kuwahutubia hotuba nzito zenye kutia hamasa kubwa.
Kwa hakika alipanda kwenye utukufu wa juu zaidi, usio na kifani kwa kutumia kila fursa kuwashauri vinginevyo sahaba zake ili wasifuatane naye na kakutana na kifo kilicho hakika. Ustahiki wake mwenyewe na dhamira thabiti ya kutetea ukweli kuliacha alama hai katika akili za wafuasi wake, kiasi kwamba kila mmoja wao alipata thibitisho la uimara wake mwenyewe na uamuzi.

Husein angebakia kutolinganishika kama angekikaribisha kifo kabla ya wafuasi wake na ndugu zake wakiwa hawajauliwa. Alipata daraja la juu zaidi la mafanikio kwa kuziongezea juu ya huzuni zake, kule kuhudhuria kunakovunja moyo, yale mauaji ya sahaba zake wapenzi wote na ndugu wa karibu.

Husein aliongeza sifa yake ya kiroho kwa kutekeleza bila kutetereka, kila fundisho la Uislamu na kila wajibu ulioamriwa na Uislamu hata wakati alipokabiliwa na mateso yenye kuumiza sana.

Alitenda kufuatana na hali ya kupenda usawa ya Uislamu kwa kuzibeba maiti za watumwa ambao walijitoa mhanga maisha yao kwa ajili yake kwa namna (heshima) ile ile kutoka kwenye medani ya vita kama alivyobeba za wale sahaba zake wapenzi mno na ndugu wa karibu.

Alisimamisha Sala za mchana (Adhuhuri na al-Asri) katika wakati uliopangwa hata wakati vita ilipokuwa imefikia ukali wake kabisa. Husein alikuwa anatekeleza jihad na mara moja akifanya lengo lake lifahamike kwa uonyeshaji wa kivitendo.

Umaarufu wa Husein ungebakia usio kifani kama jihad yake ingemalizika kwa kujitoa mhanga wapenzi wake na ndugu, na mhanga wake mwenywe. Aliongezea kwenye umaarufu wake kwa kuwachukua pamoja nayewanawake na hata watoto wa familia yake kwenda nao katika safari yake ya Iraq - dhidi ya ushauri wa wapenzi wake ambao walijali sana kutoa maoni yao katika jambo hili.

Kwa njia hii aliandaa utangazaji wa lengo la kufa kwake kishahidi katika namna ambayo hakuna mtu

mwingine yeyote ambaye angeweza kufanya hivyo, kwani kila mmoja katika wao alikuwa na utambuzi wa kina kabisa juu ya wajibu wake na kushikilia ukweli hivyo kwamba, hata katika baraza la Ubaydullah bin Ziyad kule Kufa, na lile la Yazid hapo Damascus, hakuna hata mtu mmoja miongoni mwa watu wa Husein waliopona vita aliinamisha kichwa chake mbele ya utawala wa Bani Umayyah na dharau aliotupiwa Yazid na Husein ilidumishwa baada ya kifo chake, siyo tu na Ali bin Husein, Zainab na Umm Kulthumu, bali pia na watoto kama vile Sakina na Muhammad bin Ali ibn Husein.

# Sura Ya 34: Ni Nani Aliyeshinda Pale Karbala?

Katika vita vyote washiriki huwa wana malengo fulani ya kutimiza na kufaulu kunatolewa na kundi ambalo linafanikisha lile lengo lake na kushindwa hukasimiwa kwenye kundi ambalo hushindwa kulifikia lengo lake. Nini yalikuwa malengo ya Husein katika Vita vya Karbala na ni kwa kiwango gani amefanikiwa katika kulifikia lengo lake? Kitu gani Yazid alikuwa anapenda kukitimiza kwa kuingia katika vita na Husein? Je, yeye alifanikiwa katika kulifikia lengo lake?

Husein hakumpinga Yazid kwa sababu ya uadui binafsi kwake. Kama Husein angependelea tu kubakia hai katika ulimwengu au kama Yazid alikuwa tu angependa kwamba Husein akate mawasiliano yote na mambo ya kisiasa, hakuna haja ya vita kati ya watu hawa wawili ambayo ingeweza kutokea.

Kilichofanya vita kati yao viwe si yenye kuepukika ilikuwa kwamba baada ya yeye kufanya alazimike kuwa Khalifa juu ya Waislamu, Yazid pia alidai kuwa mrithi wa Mtume wa Uislamu. Katika kufanikiwa kwa lengo hili Yazid alimuona Husein kama ndio kipingamizi halisi, ingawaje Husein pengine angeepuka kula kiapo cha utii kwake katika hali ya kimya kimya.

Yazid alichochea kwa nguvu sana uhuishaji wa uyakinifu wa kipagani, lakini Husein alikuwa ngao ya kiroho na ibada ya Mwenyezi Mungu. Yazid alitenda na alisaidia uonevu na dhuluma, bali Husein alihusika na kudumisha ukweli na haki. Yazid alidhamiria kuziangamiza sheria na sifa pekee za Uislamu ambazo Husein aliiona kazi hiyo ni wajibu wake kuzidumisha na kuzilinda.

Ilikuwa ni kwa sababu hizi kwamba wakati akielezea nia yake katika kumpiga vita Husein, Yazid alidhihirisha msimamo wake wa kibeberu kwa kusema kwamba Husein amewafanya watu wajue haki zao, kwa hiyo, amehatarisha kuwepo kwa majumba mengi makubwa na makasiri makubwa, na kwamba ilibidi apigane na Husein ili kuulinda utawala wake na kusalimisha mali na utajiri wake.

Husein, kinyume chake, yeye alielezea mapambano yake dhidi ya Yazid kwa mashairi yenye maana; “Mwenyezi Mungu anatambua vyema kwamba chochote kile anachokimiliki Yazid hicho ni mali ya watu wengine kabisa. Alikuwa hana haki ya kukitwaa kwa matumizi yake binafsi. Kama, kwa kuwa mbadhilifu kama alivyo, angechagua kufanya uadilifu, angebadilisha njia zake (na mwenendo wake) na angetuliza

fitina zake.”

Kama walivyo madhalimu wote, Yazid alilenga kupoozesha hisia za watu na kudumaza ari yao ya kuongea ukweli. Watu walikwishaacha kutumia akili zao katika kutafakari juu ya usawa wa madai ya mtawala wao juu ya madaraka. Hata kama kwa bahati isiyo ya kawaida mtu alifikiria kuhusu hilo, ujasiri wa mtu ulishindwa kutamka uamuzi ulio huru. Lengo la Husein lilikuwa kwamba uwezo wa hisia za watu ambao ulikuwa unafifia au kupungua nguvu na ujasiri wao wa kuzungumza waziwazi ambao ulikuwa umedhoofishwa, ni lazima vihuishwe na kudumishwa.

Katika mwaka wa 60 A.H. Waislamu mara kwa mara walishuhudia uovu na matendo ya karaha ya serikali ya Syria, lakini kwa ujumla walikuwa wamezidiwa na hali ya utepetevu na ukosefu wa hisia. Utokeaji wa ghafla wa tukio lisilo la kawaida ulihitajika kuwatikisa watu kutokana na uzito wao wa kiakili na kuziamsha hisia zao. Kifo cha kishahidi cha Husein kililitimiza hili kwa namna yenye athari kubwa. Mfano wake mtukufu uliwapa watu ujasiri wa (kuweza) kuelezea hisia zao.

Walipoona kwamba alikuwa sio Husein peke yake, bali sahaba zake wazee na vijana pia walijitoa muhanga kwa utulivu kamili, au waliposikia taarifa za tabia kama hizo, watu walikuja kukifikiria kifo kuwa chepesi zaidi kati- ka njia ya haki kuliko ambavyo wamewahi kukifikiria kabla ya hapo.

Kufanya jambo zaidi kupita kiasi mara nyingi huzaa matokeo ambayo ni kinyume cha vile ilivyokusudiwa. Yazid aliulundika uonevu juu ya uonevu dhidi ya Husein ili kwamba mwisho wake wa kusikitisha uwe kama onyo kwa wengine walioelekea kumpinga. Husein alikabiliana na ukatili wake wote kwa utulivu na subira, kiasi kwamba katika shauku yake ya ukatili, Yazid alishindwa kuutambua mpaka ambao kwamba watu labda wangeweza kuuvumilia uonevu, na ambao zaidi ya hapo hisia zao zilizolala, zenye ganzi zingeamshwa kwa nguvu kiasi cha kuufanya uonevu urudi nyuma na kujiangamiza wenyewe.

Al-Hurr bin Yazid al-Riyahii, afisa wa jeshi na baadhi ya watu katika jeshi la Yazid walijiunga na Husein katika siku ya mwezi 10 Muharram. Katika siku ya tatu baada ya mauaji ya Husein wakati Ubaydulah bin Ziyad alipoonyesha utovu wa adabu kwenye kichwa cha Husein, Zayd bin Arqam, sahaba mkongwe wa Mtume, alilalamika na kukipinga kitendo hiki. Wakati Yazid alipokirudia kitendo hiki cha Ibn Ziyad mjini Damascus cha utovu wa adabu mbaya sana kwenye kichwa cha Husein, sio tu Abu Barza al-Aslam bali hata balozi wa kikristo wa Mfalme wa Roma alimkosoa kwa ukali na uwazi kabisa.

Huu ulikuwa ndio ushindi wa Husein. Uongo (batili) ulikuja kupingwa wazi azi kabisa na kuchochea kutoafikiana kwa papo kwa hapo.

Kabla ya vita vya Karbala, nani angeweza kuwa na ujasiri kuongea habari za Husein kwa heshima kubwa mbele ya baraza laYazid? Baada ya watu wa Husein walioharibikiwa na kuporwa walipokwisha kufikishwa katika baraza yake kama wafungwa, Yazid ilimbidi asikilize kwa utulivu sifa nyingi zilizokuwa zikitolewa juu ya Husein.

Moja ya alama za uhakika kabisa ya kushindwa ni kwamba kundi lililoshindwa hujitoa kutoka kwenye

msimamo lililokuwa limeuchukua kabla ya kuanza kwa mapigano. Kile ambacho kimesababisha vita kinaonekana kuwa kutowezekana kutimizwa. Vita kati ya Husein na Yazid vilikuwa vimeanzishwa kwa sababu Yazid alikuwa amesisitiza juu ya kupata kutoka kwa Husein kiapo cha utii kwake. Al-Husein alilikataa hili kwa uthabiti imara kabisa.
Je, Yazid alisimama imara kwenye dai lake hilo? Yazid alikuwa amependa kupata kiapo kutoka kwa Husein, siyo katika wadhifa wa Husein kama mtu tu wa kawaida, bali katika wadhifa wake kama mrithi wa kiroho wa Mtume. Baada ya kifo cha Husein, mtoto wake, Ali ibn Husein alichukua nafasi ile ile hasa kama baba yake. Ali ibn Husein na watu wote wa familia ya Husein waliosalimika baada ya vita vya Karbala walishushwa hadhi kufikia hali ya kuwa wafungwa. Kama Yazid asingesalimu amri kwenye suala la kiapo cha utii, angepaswa kulirudia dai lake kwa Ali ibn Husein. Hakuna kitu kama hicho ambacho kilipendekezwa kwake, kitu ambacho kinaonyesha wazi kwamba Yazid alikuwa amejitoa kwenye msimamo wake wa awali.

Matokeo yake, ni lazima ikubalike kwamba mwishoni, kati ya washindani hawa wawili, Husein aliibuka kuwa mshindi na Yazid kuwa ndiye aliyeshindwa.

# Sura Ya 35: Wenye Hatia Wajisikia Aibu.

Majeshi yaliyokuwa chini ya mamlaka ya Husein yalikuwa yamezidiwa sana kwa idadi na yale ya Yazid hapo Karbala kiasi kwamba, ingeweza kutabiriwa kwa urahisi kwamba licha ya upinzani mkali sana uliotegemewa kuwekwa, majeshi ya Yazid mwishoni lazima yashinde. Ama kuhusu Husein, alikuwa hana shaka kwamba vita vingeishia kwa maafa upande wake.

Hata hivyo, yeye alishikamana na njia aliokwisha jichagulia mwenyewe, na siyo yeye wala mtu yeyote kati ya wale ambao walikufa pamoja naye wala mtu yeyote kati ya wale walionusurika vitani ambaye alijutia kabisa kile alichokitenda au matokeo yake. Kinyume chake, siyo tu maadui zake na wauaji wake, bali pia wale ambao walishindwa kumsaidia walikuwa wamepatwa na aibu kubwa sana.

Al-Hurr bin Yazid al-Riyahi, afisa katika jeshi la adui alikitelekeza cheo chake na akajiunga na Husein katika siku ya 10 ya Muharram kwa kulipa au kufidia kosa la matatizo aliyoyasababisha kwa Husein kwa kumzuia asiendelee na safari yake ya kwenda al-Kufa na kumfanya aweke kambi yake hapo Karbala katika sehemu ambayo si rahisi kuufikia mto.

Hali ya hatia ilihisiwa na wenyeji wale wa Kufa ambao walikuwa wameahidi kutoa msaada wao kwa Husein kupitia kwa Muslim bin Aqil lakini ambao hawakuweza kwenda Karbala kumsaidia Husein au hawaku- fanya jaribio lolote la kuungana naye pale. Unyofu wa majuto yao ulionyeshwa pale muda mfupi tu baada ya masaibu ya Karbala, wao walipokuja kuitwa, “Wenye kutubia” kwa zile juhudi zao za kulipiza kisasi cha mauaji ya Husein.

Miongoni mwa wale ambao walichelewa kutoa msaada kwa Husein alikuwa Abdallah bin al-Hurr al-Ju'fi. Akiwa njiani kwenda Kufa, Husein mwenyewe alimtaka ampe msaada lakini Abdallah hakutimiza ombi hilo ili kwamba asije akahatarisha maisha yake.[1]

Aibu ilimuandama katika uhai wake wote na alionyesha kujuta na kutubia kwake katika ibara zenye maana, "Nitaendela kujisikitikia kwamba Husein aliomba msaada wangu, na sikuzipata baraka za kukubali na kutekeleza haja zake."[2] Baada ya matukio hayo ya kuhuzunisha ya Karbala, wakati Ubaydullah bin Ziyad alipolalamika kwa Abdallah kuhusu kupuuzia kumwona kwa muda mrefu na kutokwenda kupigana dhidi ya Husein, na akadokezea juu ya dhana ya kuwaonea huruma maadui zake, hisia za Abdallah zililipuka katika mashairi yenye maana, "Mtawala ambaye ni bwana wa zamani katika udanganyifu ananiuliza kwa nini sikujiunga katika vita dhidi ya mwana wa Fatimah, wakati mimi nimepatwa na aibu kwa kukosa kumsaidia Husein. Kwa kweli, yule ambaye hachagui njia ya haki lazima ajisikie aibu." Kisha aliondoka Kufa. [3]

Qurra bin Qays ambaye alikuwa mjumbe wa Umar bin Sa'd kwa Husein alikuwa akisema baadaye katika uhai wake kwamba kwa hakika angefu- atana na al-Hurr kujiunga na kundi la Husein kama al-Hurr angemwarifu juu ya nia yake ya kuondoka kwenye utumishi wa Yazid. [4]
Radii bin Munqidh al-Abdii ambaye alimuua Burayr al-Hamdan kwa kusaidiwa na Ka'b bin Amr al-Abdi alikuwa akitumia kuelezea aibu yake kwa maneno yafuatayo, "Kama isingekuwa imejaaliwa hivyo, mimi nisingejiunga na vita hivi nikapata kushuhudiwa na Ibn Jabir... napenda ningekuwa nimekufa na kuzikwa kabla ya kuuliwa kwa Burayr na vita dhidi ya Husein. [5]

Shabath bin Ribi'i, mmoja wa makamanda muhimu wa jeshi la Umar bin Sa'd alisikiwa akisema, "Mungu hatafanya wema kwa watu wa nchi hii. Ni uovu ulioje huu kwamba kwa kipindi cha miaka mitano tumepigana dhidi ya kizazi cha Abu Sufyan tukiwa upande wa Ali bin Abi Twalib na mwanawe, Hasan, kisha tulijiunga na kizazi cha Mu'awiyah na Ziyad katika kufanya mashambulizi dhidi ya Husein ambaye, kwa mafanikio binafsi, alikuwa bora mno kuliko mtu yeyote hapa ulimwenguni. Huu ulikuwa ni mkengeuko ambao unabakia bila kusawazika. [6]

Mkubwa zaidi kuliko watu hawa katika jinai lake alikuwa ni Umar bin Sa'd, kamanda wa majeshi ya Yazid hapo Karbala. Mmoja wa marafiki zake, Humayd bin Muslim, ameelezea kwamba, wakati wa kurudi kwake kutoka Karbala, pale alipoulizwa juu ya matokeo ya hapo (Karbala), Umar bin Sa'd alisema, "Usiniulize juu ya jambo lolote. Hakuna msafiri atakayefikia mwisho wa safari yake akiuendea mwisho mbaya namna hii kama ilivyo kuwa kwangu mimi. Nilifanya ukaribu wa uhusiano wenye matokeo yenye nguvu kidogo sana na nimetenda jinai mbaya sana."[7]

Makosa ya Ubaydulah bin Ziyad, gavana wa Kufa yalikuwa mabaya zaidi. Alipeleka majeshi yote Karbala chini ya uangalizi wake mwenyewe na akamwamuru Umar bin Sa'd kumuua Husein na marafiki zake. Wakati Yazid alipokufa, maasia yalitokea katika nchi yote ya Iraq na ilimbidi Ibn Ziyad akimbie kutoka Basra.

Alimchukua pamoja naye mtu wa kumwongoza. Katikati ya safari hiyo alimwambia mtu huyo kwamba kwa vile Husein bin Ali alimpinga mtawala, basi mtawala huyo alimwamuru yeye (Ibn Ziyad) kumwua Husein. Kwa hiyo, yeye alishikilia kwamba uajibikaji na mauaji ya Husein lazima uwe juu ya Yazid na siyo juu yake yeye.8

Maelezo haya yasiyo na maana yoyote ni jaribio tu la kuhamisha jukumu lake hilo kwa Yazid na linachipuka kutoka kwenye hali ya kujuta kwa kuchukua sehemu muhimu katika mauaji ya Husein. Vinginevyo wakati Yazid alipomtaka Ibn Ziyad kuishambulia Hijaz na jeshi na kumpiga Abdallah bin al-Zubeir, kwa nini asingemkatalia Yazid kwa kusema, "Nimemwua mjukuu wa Mtume kwa amri ya mtu huyu mwovu, na sasa siwezi kuishambulia Ka'abah."9

Mtu mhalifu kabisa kuliko wote alikuwa Yazid bin Mu'awiyah. Hili linathibitishwa na maelezo ya Ibn Ziyad yaliyokwishanukuliwa. Alipotambua kwamba Husein alikusudia kwenda Kufa, alimfanya Ibn Ziyad gavana wa hapo kuhakikisha kwamba hatua kali kabisa kuliko zote zinachukuliwa dhidi ya Husein. Ilikuwa ni baada ya kupata ruhusa yake kwamba, baada ya vita vya Karbala, kichwa cha Husein na vichwa vya mashahidi wengine wa Karbala pamoja na watu wa Husein waliokoka vitani walipelekwa na Ibn Ziyad mpaka Damascus. Kwa kweli yeye mwenyewe binafsi alikitendea kichwa cha Husein utovu mkubwa wa adabu.

Baada ya kujulishwa ukatili wote ambao Husein na sahaba zake waliupata, na baada ya kifo chake, ukatili waliofanyiwa watu wa Husein waliopona vita, Yazid hakuonyesha dalili yoyote ile ya kumchukia Ibn Ziyad. Bali kinyume chake alimruhusu aendelee na ugavana wa Kufa. Mmoja wa ndugu zake, Abd al-Rahman, ambaye alikuwa gavana wa Khurasan tangu mwaka wa 58 A.H alikwenda Damascus aliposikia kifo cha kishahidi cha Husein na alipata mkopo 10 wa ***crore dirham*** mbili (ambazo kwa sasa ni takriban dirham 36,500,000) kutoka hazina ya Khurasan ambako, kwa mujibu wa mapatano naye, kiasi hicho kilibakia kikiwa kimehifadhiwa.
Baada ya Abd al-Rahman ugavana wa Kurasan alipewa ndugu yake, Salm bin Ziyad. 11

Hapo mwanzoni Yazid alifurahia sana kifo cha Husein. Hata hivyo, wakati ilipoonekana kwamba mapinduzi yalikuwa yanasukwa, macho ya Yazid yalifunguka na alikuwa akilalama, "Ole wangu! Kwa kumuua Husein bin Ali, Ubaydullah bin Ziyad amenifedhehesha na kunifanya mlengwa wa chuki mbele ya macho ya Waislamu, Amepandikiza mbegu ya uadui na kinyongo dhidi yangu katika nyoyo zao. Watu wema na wabaya pia miongoni mwa Waislamu wanayaona mauaji ya al-Husein kama kosa la uovu mkubwa kabisa na wananichukia sana na kuniondoa kinyaa kwenye utu. Ubaya gani mtoto wa Marjana ameufanya! Namwomba Mungu Amlaani."12

1. Irshad, uk. 237.
2. Al-Akhbar al-Tawal, uk. 258.
3. Tabari, Juz. 6, uk. 270.
4. Irshad, uk. 249/ Tabari, uk. 244.
5. Tabari, juz. 6, uk. 248
6. Tabari, juz. 6, uk. 250.

7. Al-Akhbar al-Tawal 257
8. Tabari, juz. 6, uk. 250.
9. Tabari, juz. 6, uk. 6.
10. Al-Wuzara wa al-Kuttab, uk. 18.
11. Al-Wuzara wa al-Kuttab, uk. 19 na Kitabu tabari, juz. 6, uk. 271-272.
12. Tabari, juz. 7, uk. 19.

# Sura Ya 36 : Hisia Za Ulimwengu Wa Kiislamu

Wakati maelezo kamili ya ukatili wa kinyama ambao Husein na wapenzi wake na ndugu zake waliyotendewa hapo Karbala yalipokuja kufahamika, kila moyo wa Mwislam ulitupwa kwenye wimbi la huzuni na ghadhabu kali. Wahalifu wa jinai hizi walichukiza mno, na hayo mauaji ya Husein yaliwatia fedheha tele.

Kwa vile watu wa Kufa walionekana kuhusika sana juu ya masaibu hayo makubwa, walijipatia wenyewe jina baya sana, hivyo kwamba iliwachukua karne nyingi kuweza kusahau fedheha hiyo. Abu Uthman al-Nahdi, Sahaba wa Mtume, aliyaacha makazi yake ya Kufa, akikataa kuishi sehemu ambayo mtoto wa Mtume ameuawa. Fedheha hiyo itokanayo na msiba huo ilienea katika maeneo yote ya Iraq.

Baadhi ya wale ambao wamewaua mashahadi wa Karbala walikuwa wamekasirikiwa mno na ndugu zao wa karibu. Mke au dada yake Ka'b bin Jabir ambaye alimuua Burayr al-Hamadani alikataa kuongea naye kwani alipigana dhidi ya mtoto wa Fatimah, na akamuua Burayr al-Hamadan.[1]

Margana, mama yake Ubaydullah bin Ziyad, alimlaani kwa kupigana dhidi ya al-Husein na kusababisha auawe.[2]

Hata kabla Yazid hajaanza kuhamisha lawama ya mauaji ya Husein kwa Ibn Ziyad na kumzungumzia vibaya, baadhi ya washauri wake tayari walikwishaanza kufanya rejea zenye dharau kwa Sumayyah, bibi (nyanya) yake Ibn Ziyad na Yazid alilazimika kuzisikia kashfa hizi akiwa kimya,

Yahya bin al-Hakam alisoma mashairi yenye maana, 'Vichwa vilivyokat- wa kutoka kwenye miili yao katika bonde la Karbala vilikuwa na uhusiano wa karibu zaidi na sisi, kuliko na Ibn Ziyad, aliyezaliwa na mtumwa akichipukia kwenye shina la kudharaulika. Tazama! Kizazi cha Sumayyah kimeongezeka kama mchanga, na kizazi cha binti ya Mtume kimefutiliwa mbali.

Siyo tu watu walioishi wakati mmoja na Yazid waliomchukia, bali pia baadhi ya kizazi chake cha baadaye waliyajua na kuyachukia matendo yake maovu. Mtoto wake, Mu'awiyah bin Yazid aliyakiri hadharani makosa madogo madogo ya udhaifu wa baba yake na akakataa kukikalia kiti kilichoachwa wazi na baba yake. Umar bin Abdul-Aziz, Khalifa wa Bani Umayyah katika karne ya pili ya hijiriya aliamuru kuchapwa viboko ishirini kwa mtu ambaye atatanguliza kuweka maneno, Amir al-Muuminin

(kiongozi wa waumini) kwenye jina la Yazid.

Mauaji ya Husein, na Ukhalifa wa Yazid vilichukuliwa kama matukio ya kuaibisha Waislamu wenyewe wakati mwanafalsafa maarufu na mshairi, Abu al-Ala al-Ma'arri, akiandika katika karne ya 4 ya hijiriya, alisema, "Mabadiliko ya wakati huniletea maono yaliyo ya ajabu na mageni kiasi kwamba nimepoteza shauku yote ya kuyashuhudia.
Kwa nini! Je, Maquraishi wenu hawakumuua Husein, na je, mtu mwovu kama Yazid hakupanda kwenye kiti cha Ukhalifa wenu?"

Ni dhahiri kabisa chuki iliyohisiwa kwa undani na jumla na watu wote dhidi ya utawala unaohusika na mauaji ya Husein ulikuwa ni mwanzo wa (kufanyika) mapinduzi.

1. Tabari, juz. 6, uk. 247.
2. Tabari, juz. 7, uk. 7.

# Sura Ya 37: Dalili Za Mapinduzi

Dalili za mapinduzi yaliyokuwa yanakaribia kutokea yalikuwa yaonekane wazi tangu kwa watu wa Husein waliopona vita, wakiwemo zaidi wanawake, watoto wadogo kadhaa, na mwanawe mkubwa, lakini akiwa dhaifu sana na asiyejisikia vizuri walipoanza kutembezwa kama wafungwa katika mitaa ya Kufa. Wafungwa hawa hawakuruhusiwa kulia na ingawa ilikuwa imepangwa kwamba tukio hili litekelezwe kwa kusherehekea, vilio vya maombolezo viliamshwa na watazamaji walipowaona watu wa Husein waliopona vitani wenye huzuni na katika kuzisikia hotuba nzito zenye nguvu za Zainab, Umm Kulthumu na Ali bin Husein.

Maafisa wa Yazid hawakuruhusiwa kuingia kwenye vitongoji vingi au maeneo ya humo njiani kutoka Kufa kwenda Damascus wakati walipokuwa wanawaongoza watu wa Husein waliopona vita kwenda Syria. Katika sehemu nyingi watu walitoa upinzani wa silaha, na nguvu kwa kweli ilitumika katika sehemu chache zikaliwazo na watu.

Madina na Makkah ilikuwa ndio vitovu vya usimamizi vya ulimwengu wa Kiislamu. Madina lilikuwa Jiji la Bani Hashim, wengi wao walikuwa wametokana na Abu Talib, na waliutoka mji pamoja na Husein. Watu wengine wa familia hiyo wote walikuwa Madina.

Abd al-Malik bin Abi al-Harith al-Sulami ambaye alizichukua habari za kuuliwa kwa Husein na kuzipeleka Madina anasema kwamba wakati zilipotangazwa, mara sauti kubwa za vilio vya kuomboleza na kusikitikia vilisikika vikitoka kwenye nyumba za Bani Hashim ambavyo kwamba kamwe hajawahi kusikia mfano wake kabla ya hapo.

Vyovyote vile ambavyo watu wa Madina wangeweza kutojali wao wasingeweza kubakia bila uchangamfu wa kutojihusisha na hali ya huzuni ya kuvunja moyo ya roho nyingi zilizoteseka sana kwa muda mrefu kiasi hicho.

Kwa sababu hiyo, watu wa Madina waliona kwamba ilikuwa ni laz- ima kupeleleza na kujua mapema zaidi kiasi iwezekanavyo, juu ya tabia za Yazid. Katika mwaka wa 62 A.H, tume iliundwa yenye baadhi ya watu mashuhuri wa Madina, akiwemo Abdallah bin Hanzala, waliondoka na kwenda Syria kuchunguza tabia ya Yazid.

Ingawaje wao walipewa fedha nyingi sana kama hongo, wajumbe hao, katika kurudi kwao kutoka Syria walitaarifu hivi, "Tumerudi kutoka kwa mtu ambaye hafuati dini, yeye anakunywa pombe, anacheza dufu, anasikiliza muziki wa waimbaji wanawake, anacheza na majibwa na anatumia muda wake na walevi na mafisadi katika kupiga porojo na maongezi yasiyo na maana. Kwa hivyo sisi tunaachana na kiapo cha utii tulichokitoa kwake.[1]

Jalal al-Din Suyuti ameandika katika kitabu kiitwacho *Tarikh al-Khulafai* kwamba wajumbe wa tume hiyo walieleza hivi, "Sisi tumechagua kumpinga Yazid wakati tulipotambua kwamba adhabu ya Mwenyezi Mungu ingechukua umbo la mawe yakituangukia kutoka mbinguni kwani ni mtu ambaye aliona ni halali kulala na wajakazi ambao wamechangia kitanda na baba yake, na binti zake na dada zake, anakunywa pombe na anaacha kusimamisha Sala zake."

Mjumbe wa tume hiyo, al-Mundhir bin al-Zubeir alisema, "Yazid amenipa hongo ya dirham mia moja elfu (laki moja) ambazo zisingenizuia kukufa- hamisheni habari zenye ukweli.

Nakuelezeni wazi kwamba yeye (Yazid) anakunywa sana pombe kiasi ambacho anashindwa na kuacha kusimamisha Sala zake." Pia alikubaliana na yale maelezo ambayo wajumbe wengine wa tume hiyo walisema kuhusu Yazid.

Tabia ya Yazid iliwatenganisha wenyeji wa Madina na yeye kiasi kwamba mwanzoni mwa mwaka wa 62 A.H, watu wa Madina walimwondoa gavana wao, Uthman bin Muhammad bin Abi Sufyan, binamu yake Yazid, na wakaweka mzingiro (karantini) kwa Bani Umayyah wapatao karibu elfu moja ambao waliishi Madina.

Hii ilisababisha kuchukuliwa hatua za kukandamiza kulipiza kisasi na Yazid, ikifuatiwa na maandamano ya kuchukiwa kwao kukubwa na kinyongo cha Waislam. Yazid alipeleka jeshi chini ya uongozi wa Muslim bin Uqba kuuzima uasi huo hapo Madina.

Akiunguzwa na ghadhabu kali, aliamuru kwamba Madina ifanyiwe uporaji na mauaji kwa muda wa siku tatu bila kupumzika na kwamba jeshi lingeweza kutwaa chochote kile ambacho wangekiteka, pamoja na wafungwa wa vita.

Mateka wa Madina lazima watakuwa wamewajumuisha wanawake na watoto wa familia za masahaba

wa Mtume na wafuasi wao. Maagizo ya Yazid yalikuwa ya wazi kwamba wangegawanywa miongoni mwa askari wa jeshi hilo. Raia wengine wa Madina waliobaki walitoa baia (kiapo cha utii) kwa Yazid kama watumwa wake, wakimpa mamlaka isiyo na mipaka kamili juu ya maisha yao, mali zao na watu wanaowategemea.

Wakati Yazid bin Abdallah bin Rabi'a bin Aswad, mtoto wa binti ya Umm Salama, mjane wa Mtume, alikataa kula kiapo cha utii kwa Yazid katika sura hii, aliuawa mara moja. Wakati Yazid alipoyasikia maelezo kamili juu ya matukuo haya, alisoma mashairi ambayo kwamba kidokezo kikubwa kilikuwa kwamba shambulio juu ya Madina lilikuwa ni kulipiza kisasi kutokana na kushindwa kwa ndugu zake katika vita vya Badr.

Mambo hapo Makkah napo pia yalikuwa yamebadilika. Wakati Abdallah bin al-Zubeir, ambaye kwa muda mrefu alitamani kupata wadhifa wa kuwa khalifa, aliliona wimbi la jumla la hasira kubwa miongoni mwa watu dhidi ya Yazid kwa kusababisha kuuliwa kwa Husein hapo Karbala, aliiona kama ni nafasi inayofaa sana kuendeleza maslahi yake binafsi, na akatoa hotuba nzito yenye nguvu akiwashutumu vikali wenyeji wa Kufa kwa kigeugeu chao, akimsifia sana Husein na akaelezea wazi makosa ya Yazid. Kama matokeo ya hotuba hizo, wakazi wa Makkah, kwa ujumla, walikubali kula kiapo cha utii kwa Abdallah bin Zubeir.

Haya yalikuwa maendeleo yasiyopendeza na yalisababisha wasi asi mkub- wa sana kwa Yazid. Alijitahidi kuwapata watu wengi maarufu wa Makkah kwa kiasi alichoweza kukipata, lakini kosa la kumfanya Husein auawe lilikuwa baya la uovu mkubwa mno kiasi kwamba, ingawa baadhi ya watu hawakupenda kutoa kiapo cha utii kwa Abdallah bin al-Zubeir, walishikil- ia kumchukia Yazid. Abdallah bin Abbas alikuwa mmoja wa watu kama hao. Alikuwa ni mtoto wa ami yake Mtume, aitwaye Abbas.

Yazid alimwandikia barua Abdallah bin Abbas, akimsifu kwa kutokula kiapo cha utii kwa Abdallah bin al-Zubeir, na akataka kufanya ionekane kama dalili ya uaminifu kwake yeye. Aliahidi kumtumia zawadi inayostahiki katika muda wa karibuni sana. Siku iliyofuata Abdallah bin Abbas alimpa Yazid jibu lenye kuchoma sana moyo ambalo ndani yake alizielezea hatua zote kwa urefu ambazo Yazid alikuwa amezichukua kumzuia al-Husein kuondoka Madina na Makkah na ukatili aliokuwa amemfanyia hapo Karbala.

Alisema kwamba hata baada ya vifo vyao, Husein na sahaba zake walikuwa bado hawajazikwa, kwamba wanawake wa familia yake walinyang'anywa nguo za kujifunika vichwa vyao na wakatembezwa kutoka Iraq mpaka Syria kama wafungwa. Alieleza matu- maini kwamba Mwenyezi Mungu angemtesa Yazid kwa ghadhabu Yake, na alitupilia mbali (alilikataa kabisa) pendekezo la kuzawadiwa alilokuwa ameahidiwa na Yazid.

Aliongeza kusema kwamba kwa kuuawa wahenga (mababu) wake makafiri, walio na dhambi na wachafu katika vita vya Badr, Yazid alikuwa analipiza kisasi kwenye kizazi cha Mtume.

Katika kuisoma barua hii yenye kumfedhehesha, hasira ya Yazid haikujua mipaka, na alifikiria juu ya

kumuua Abdullah bin Abbas, lakini kwa vile alikuwa ameshughulishwa katika uadui na Abdallah bin Zubeir, hakuweza kuendelea na jambo lolote dhidi yake.

Baada ya kushambuliwa na kuangamizwa kwa wakazi wa Madina, Muslim bin Utba alisonga mbele kuelekea Makkah kama alivyoelekezwa na Yazid, lakini alifariki dunia katika mwezi wa Muharram mwaka wa 64 A.H. Hata hivyo, alimteua Husein bin Numayr kuwa kiongozi wa jeshi kama alivyoelekezwa na Yazid. Husein alivamia Makkah na akaizingira Ka'bah, na katika mwezi 3 wa Rabi I, mwaka 64 A.H. siyo mawe tu bali hata moto uwakao pia ulimiminwa kwenye Nyumba ya Mwenyezi Mungu ambayo ilishika moto.[2]

Haya yalikuwa mafaniko ya mwisho ya Yazid. Alifariki dunia mnamo mwezi 14 Rabiul-Awwal, mwaka wa 64 A.H. Kwa kifo chake hicho, ugomvi na vita vilikwisha, na Husein bin Numayr akarudi.

Al-Fakhri anasema kwamba jumla ya kipindi cha utawala wa Yazid kilikuwa miaka mitatu na nusu. Katika mwaka wa kwanza wa utawala wake alimuua Husein bin Ali, katika mwaka wa pili aliuvamia mji wa Madina na akauacha uporwe mali na kutekwa nyara kwa muda wa siku tatu, na katika mwaka wa tatu alipeleka kikosi maalum dhidi ya Makkah ambacho kiliichoma moto Ka'abah. Kwa jinai hizi tatu mbaya na za uovu mkubwa mno, masaibu ya Karbala yalitoa mshtiko mkubwa wa kutisha kwa ulimwengu wa Kiislamu kiasi kwamba hakukuwa na mtu mwenye akili timamu ambaye aliyajua maelezo ya tukio hili la kusikitisha sana kwa undani zaidi aliyeweza kujizuia asiathirike kwalo.

Tendo hili la Yazid halikuwa la dhambi na kosa la jinai tu, bali pia lilikuwa ni kosa la kijinga la kisiasa la dhahiri ambalo kwa sababu yake, Yazid na washauri wake wa kudharaulika kama vile Ubaydullah bin Ziyad na Shimr waliwafanyia uadui hata wale ambao, licha ya imani yao juu ya ukuu wa Mtume wa Mwenyezi Mungu na kushikamana kwao na dini ya Uislamu, walitaka kushikilia mpaka mwisho, sera yao ya kutokuingilia kati, na kuivumilia serikali ya Bani Umayyah, ingawa hawakuwa na hisia za kushikamana nayo au utii kwayo.

Baada ya kifo cha Yazid katika mwaka wa 64 A.H hisia za chuki zilizokuwa zimefichika za watu wa Iraq dhidi ya Ubaydullah bin Ziyad zilijionyesha kwa nguvu kiasi kwamba ilibidi (Ibn Ziyad) akimbie kutoka Basra bila kusindikizwa.[3]Na asingeweza kujiamini wakati akiwa safarini alipomsikia mpanda ngamia mmoja akisoma beti zenye maana, "Ewe Mwenyezi Mungu! Mlaani Ziyad na kizazi chake, ambaye amewaua, bila hatia au kosa lolote lile Waislamu wengi ambao walikuwa wakisimamisha Sala wakati wote, wakikaa macho usiku (kwa ajili ya kusali na kuomba dua) na walikuwa wacha –Mungu na wenye kujizuia."

Hali ya hisia hapo Kufa katika maeneo ambayo Ibn Ziyad mwenyewe alihusika nayo inaweza kukadiriwa kwa ukweli kwamba baada ya kifo cha Yazid, vuguvugu lilianzishwa kwamba Ibn Ziyad atambuliwe kama mtawala, Yazid bin al-Harith al-Shaybani, askari na mjumbe katika jeshi la Yazid aliipinga rai hiyo, akisema, "Tunatamani kuachana na mtoto wa Sumayyah. Kwa kweli hatuwezi kuukubali utawaka wake."[4]

Kilele katika kuonyesha kukerwa na Yazid kilikuwa kimefikiwa wakati mtoto wake na mrithi, Mu'awiyah bin Yazid, alipopanda mimbari na akasema, "Enyi watu! Taasi ya Ukhalifa ilikuwa ndiyo kamba ya Mwenyezi Mungu yenye nguvu, lakini babu yangu, Mu'awiyah bin Abu Sufyan, alibishania haki ya kuhusika nayo pamoja na Ali bin Abi Talib ambaye, kwa ukweli halisi kabisa, alikuwa ndiye mwenye haki na cheo hicho, na akachukua njia zote za kulaumiwa ama kushutumika ambazo nyinyi nyote mnazifahamu.
Kwa vyovyote, yeye amelifikia kaburi lake likiwa limezunguukwa na madhambi yake. Kisha kiti hicho cha Ukhalifa kikaenda kwa baba yangu, ambaye naye pia hakukistahili kabisa kabisa. Yeye amemua Husein, mtoto wa binti ya Mtume. Mwishowe na yeye pia aliufikia mwisho wa siku zake na kaburi lake, akiwa amenaswa kwenye madhambi yake."

Kisha alikatisha na kulia, "Msiba mkubwa sana kwetu sisi ni ile hisia iliyoko ndani yetu sisi kwamba alifikia mwisho wenye kufedhehesha kwani alikiua kizazi cha Mtume, akaruhusu kunywa ulevi (pombe) na akakufurisha utakatifu wa Nyumba ya Mwenyezi Mungu. Sasa, kwa vile mimi nimekuwa mgeni kwenye starehe za Ukhalifa mpaka sasa, kwa nini basi nionje uchungu wake?

Shughulikieni mambo yenu wenyewe. Mimi sihusiki lolote na masuala ya Ukhalifa. Hata kama dunia ni yenye kupen- deza na ni neema, tumekwishapata kiasi cha kutosha na kama kwa kweli ni isiyofaa, chochote kile ambacho tumekipata kama fungu letu kutokana nayo (basi) hilo ni zaidi kuliko chenye kutosheleza."

Kisha akajitenga ndani ya kasri, na alifariki dunia siku arobaini baadaye. Halafu ghasia (zahama) zililipuka mjini Khurasan na magavana wa ki-Bani Umayyah waliopelekwa pale waliondolewa. Watu walijiingiza kwenye mapigano mpaka mwishowe wadhifa wa Ukhalifa ukatoweka kwenye kizazi cha Abu Sufyan moja kwa moja, na mzee Marwan bin al-Hakam alikubaliwa kuwa khalifa nchini Syria, na cheo cha Ukhalifa kilishikiliwa na kizazi chake kwa muda mrefu.

1. Tabari, juz. 7, uk. 6-7.
2. Sahih Muslim, juz. 1, uk. 420; na Tabari, juz. 7, uk. 14.
3. Al-Akhbar al-tiwal, uk. 276-277.
4. Tabari, juz. 7, uk. 28.

# Sura Ya 38: Wenye Kutubia

Wakati Ubaydullah bin Ziyad alipokuwa amerejea Kufa kutoka makao makuu ya jeshi lake pale Nukhayla baada ya mauaji ya halaiki pale Karbala Shi'a wa Ali walishikwa na aibu kwa kuzembea kwao kutokwenda kumsaidia Husein. Walijichukulia wenyewe kuwa ni wenye kuwajibika kwa yale mazingira ya kuvunja moyo sana ambamo Husein aliuliwa, kwani ilikuwa ni kutokana na mialiko yao na ahadi zao za kumsaidia walizompa ndipo yeye alitoka Makkah kuja Kufa.

Waliamua kwamba lile kosa la jinai kubwa la kutokuwa na msimamo, na kutokuwa wakweli kwenye ahadi yao na matokeo yake yakawa ni kumfikisha Husein kwenye mauti yake, lilitia doa jina lao kiasi kwamba hawakuweza kuwa na matumaini ya kusafisha na kurudisha heshima yao isipokuwa kwa kuwaua wale wote ambao wametia mikono yao katika mauaji ya Husein na wapenzi wake na kama ikibidi, kuyatoa mhanga maisha yao katika kulifikia lengo hili.

Kwa hiyo, waliwasiliana na watu watano watiifu wakubwa wa watu wa nyumba ya Mtume, Suleimana bin Surad al-Khuzaa'i, sahaba wa Mtume, al-Musayyab bin Najaba, sahaba mashuhuri sana wa Ali bin Abi Talib, Abdallah bin Sa'd bin Nufayl al-Asadi, Abdullah ibn Waalin al-Taymii na Rifa'a ibn Shaddad al-Bajali. Wao na wengine wengi walikutana kwenye nyumba ya Suleiman bin Surad.

Al-Musayyab bin Najaba kisha akatoa hotuba yenye kuwalaumu vikali ndugu zake wa mji kwa kosa la kumwita Husein kuja Kufa na kumpa ahadi za kumsaidia, na wasiende kumpa msaada huo hapo Karbala ambapo, baada ya kupatwa na ukikatili usioelezeka, akauawa. Aliwaambia kwamba fedheha ambayo kwamba wamejigubika nayo ingeweza kutulizwa kama watawaua wale ambao wameshiriki katika mauaji ya Husein, au kuyatoa maisha yao (kufa) katika kulijaribu hili. Rifaa bin Shaddad alifuata kwa kutoa hotuba yenye kumuunga mkono al-Musayyab.

Wazungumzaji wengine pia walielezea maoni kama hayo hayo, na Suleiman bin Surad al- Khuzai alichaguliwa kwa uamuzi wa pamoja kuwa kiongozi wa kundi hilo. Kisha Suleiman bin Surad alisimama na akatoa hotuba iliyojaa huzuni na hamasa sana. Baadhi ya dondoo kutoka kwenye hotuba yake zaweza pia kutolewa hapa.

Yeye alisema, "Tulisubiri kwa hamu kubwa kufika kwa watu wa Nyumba ya Mtume, lakini walipofika tulionyesha kutojihusisha na kuwa wazembe kiasi kwamba katika nchi yetu na siyo mbali kutoka tulipo sisi mtoto wa Mtume akauawa.
Aliponyanyua kwa nguvu sauti yake katika kuomba uadilifu na msaada, hakukuwepo mtu yeyote yule wa kumwitikia. Watu wenye dhambi walimgeuza kuwa shabaha ya mishale yao na mikuki yao na wakamuua. Hawakukomea kwenye hili tu, bali walimvua nguo zake baada ya kifo chake.

Sasa kama mnataka kufanya jambo lolote lile, basi amkeni sasa. Ghadhabu na hasira ya Mwenyezi Mungu imekwishaguswa. Amueni hapa na tena sasa hivi, msirejee kwa wake zenu na watoto wenu mpaka muwe mumechukua hatua ili kupata radhi za Mwenyezi Mungu.

Naapa Wallahi, nafikiri Mungu hatakuwa radhi nanyi maadamu hamjawatendea waovu kama walivyokutendeeni nyinyi au hamjajitoa mhanga maisha yenu katika jitihada hii. Hebu kuweni wenye kuonyeka kabla. Msikiogope kifo, kwani yeyote yule aogopaye kufa, hupoteza heshima."

Mfumuko mkubwa wa mhemuko uliushika mkusanyiko ule baada ya kusikia hotuba hii yenye mguso. Abdullah bin Walin al-Taymii aliteuliwa kuwa mweka hazina wa kundi hili. Suleiman bin Surad aliandika barua kwa Sa'd bin Hudhayfa bin Yamaan wa Madaain na kwa wengine pia kuwafahamisha mantiki na malengo ya vuguvugu lililofadhiliwa na kundi hilo lililisimamiwa na yeye. Barua hizo kwa ujumla zilikariri

yale aliyoyasema katika hotuba ambayo kwamba dondoo yake imekwishatolewa.

Sa’d aliisoma barua ya Suleiman kwa Shi’a wa Mada’in, na wote walikubali kuwasaidia wale wote ambao waliamua kuwapiga maadui wa watu wa nyumba ya Mtume. Sa’d alipeleka jibu kwa Suleiman bin Surad kama ilivyostahili.

Hali kadhalika hilo lilikuwa ndio jibu lililotolewa na wale wengine pia. Harakati zote hizi zilifanyika katika usiri mkali, na idadi kubwa ya watu ilijiunga katika harakati hizi zilizoshauriwa, lakini hakukuwa na hatua zozote zilizoweza kuchukuliwa kuyapa sura ya kivitendo malengo haya mpaka baada ya kifo cha Yazid mnamo mwezi wa Rabul-Awwal ya mwaka wa 64 A.H. Harakati hiyo ilipata nguvu sana baada ya kifo cha Yazid kiasi kwamba iliweza kuenezwa kwa uwaziwazi.

Ilifika Misri pia, na shauku kubwa ilipatikana hapo kwa kutokana na mfululizo wa hotuba za mara kwa mara juu ya jambo hili zilizotolewa na Ubaydullah ibn Abdillah, ambaye aliongelea kuhusu mauaji ya Husein kwa maneno yenye mguso wa kusisimua sana.

Kama ilivyoamuliwa hapo awali, watu wote waliojitolea kwenye harakati hii walikusanyika hapo Nukhayla mwezi mosi ya Rabiul-Thani, mwaka wa 65 A.H. Hata hivyo, kati ya watu 10,000 ambao waliahidi kujitokeza ni watu 4,000 tu waliojitokeza kwa kushiriki katika harakati hii.[1]

Pendekezo la Suleiman bin Surad kwamba mhalifu mkubwa kabisa aliyepo kuhusiana na mauaji ya Husein alikuwa Ubaydullah bin Ziyad, na kwamba yeye lazima awe mtu wa kwanza kabisa kuuawa lilikubaliwa.[2]

Tarehe 5 ya mwezi wa Rabiul-Thani mwaka wa 65 A.H. watu hawa watafutao kulipa kisasi kwa mauaji ya Husein waliondoka kwenda Syria.[3]

Kwanza kabisa walilitembelea kaburi la Husein ambako waliutumia mchana mmoja na usiku katika maombelezo na Sala. Hotuba za Suleiman bin Surad na wengineo zilihimiza shauku na hamasa ya wasikilizaji kwenye msisimko.

Mashujaa hawa walijiweka katika mpango wa kivita hapo Ayn al-Warda. Majeshi ya Syria chini ya uongozi wa Ibn Dhi al-Tila na Husein bin Numayr yalifika baada ya siku tano kuja kupigana nao vita. Baada ya kufanya maandalizi yake ya mwisho, Suleiman bin Surad alitangaza kwamba kitokeapo kifo chake basi atarithiwa katika uongozi na al- Musayyab bin Najab, Sa’d bin Nufayl, Abdallah bin Walin na Rifaa bin Shaddad kwa mfuatano wa mpango wa majina yao yalivyotolewa.
Tarehe 8 mwezi Jamadul-Awwal, mapigano ya kwanza yalitokea, na watubiaji ambao idadi yao ilifikia watu 4000 tu waliwashinda adui ambao walikuwa 10,000 kwa idadi yao, lakini siku iliyofuata nguvu mpya ya wanajeshi 8000 ilipokelewa kutoka kwa Ubaydullah bin Ziyad. Idadi hii iligeuza kabisa mizani dhidi ya watubiaji, ambao walipigana vikali sana mpaka upevu wa usiku lakini walipata majeruhi wengi.

Siku iliyofuatia hali yao ikawa mbaya zaidi, na Suleiman bin Surad aliuawa. Al-Musayyab bin Najaba

alichukua nafasi yake akawa kiongozi na akapigana kwa ushu- jaa mkubwa sana. Na yeye pia aliuawa.

Abdallah bin Nufayl kisha naye akauchukua uongozi wa wenye kutubia wakati habari zilipowafikia kwamba msaada kutoka Madain na Basra ungewafikia watubiaJi punde. Hata hivyo, ilionekana kwamba kusingekuwa na matumanini juu ya kufika kwao wakati wa uhai wa wale wanaopigana katika vita. Wakati huo huo Abdallah bin Sa'd na Abdallah bin Walin wakawa pia wameuawa.

Kwa vile jioni ilikwishaingia, vita vilisimamishwa. Kati ya watu watano waliochaguliwa kuwa viongozi wa watubiao, alikuwa ni Rifaa bin Shaddad tu alibaki na watu mamia wachache tu, wengi wao wakiwa wamejeruhiwa au wameachwa hawafai kwa kupigana. Katika hali isiyofaa ya namna hiyo, watubiaji walijitoa (katika mapigano) wakati wa usiku. Hivyo ndivyo lilivyokwisha jaribio la kwanza la kulipiza kisasi cha mauaji ya Husein.

1. Tabari, juz. 7, uk. 67.
2. Tabari, juz. 7, uk. 69.
3. Tabari, juz. 7, uk. 74.

# Sura Ya 39: Umwagaji Damu Usio Haki Walipizwa.

Watubiaji hawakufaulu katika jaribio lao la kutaka kulipiza kisasi kwa wale waliohusika na mauaji ya Husein kutokana tu ya idadi kubwa ya jeshi la maadui. Si muda mrefu baadae alipotokea al-Mukhtar bin Abi Ubaud al- Thaqafi ambaye alikusudia kutoa adhabu inayostahili kwa wale wote ambao walishiriki katika kumuua Husein.

Baba yake al-Mukhtar alikuwa amejitambulisha katika vita vilivyopigwa wakati wa utekaji wa Uajemi (Iran) na majeshi ya Uislamu. Miongoni mwa Shi'a wa Kufa, al-Mukhtari alikuwa akifahamika sana na mapenzi yake makubwa kwa watu wa nyumba ya Mtume, na Muslim bin Aqil aliwahi kukaa nyumbani kwake kwa muda fulani, lakini al-Muktar alikuwa ameondoka Kufa kwa shughuli zake binafsi kabla ya hatua za matokeo ya kimsiba kuhusu Muslim bin Aqil kuanza kuonekana.

Alirudi Kufa baada tu ya Muslim bin Aqil na Hani bin Urwa wote wawili walipokuwa wamek- wishauawa, na akaona kwamba Amr bin Hurayth amesimamisha bendera kuhakikisha usalama wa maisha na mali za wale ambao walichukuliwa hifadhi chini yake. Alipochukulia kwamba ni jambo lenye kufaa kufanya hivyo, al-Mukhtar alichukua hifadhi chini ya bendera hiyo.

Hata hivyo, yeye alikataliwa usalama wa mtu na mali, na Ubaydullah ibn Ziyad alimpiga kwa fimbo na kumsababishia maumivu makali sana kwenye moja ya macho yake. Kisha alitupwa gerezani, na alikuwa

ndani ya gereza wakati masaibu ya Karbala yalipotokea.

Dada yake alikuwa mke wa Abdallah bin Umar, na kwa vile Yazid haku- penda kumuudhi Abdallah bin Umar, aliamuru kuachiliwa huru mara moja kwa al-Mukhtar kwa ombi lake. Bin Ziyad, hata hivyo, alimwachia al-Mukhtar kwa sharti kwamba kama hakuondoka Kufa ndani ya siku tatu, kuuawa kwake kungekuwa halali. Matokeo yake, al-Mukhtar aliondoka Kufa kama ambavyo ilikuwa imeamuliwa.[1]

Kwa zaidi ya mwaka mmoja, al-Mukhtar alisafiri kutoka mahali fulani na kwenda mahali pengine nchini Hijaz, wakati wote akielezea nia yake ya kulipiza kisasi mauaji ya al-Husein, na asipumzike mpaka amefanya hivyo.[2]

Al-Mukhtar alikuwa Makkah wakati jeshi la Syria chini ya Husein bin Numayr liliposonga mbele dhidi ya Abdallah bin al-Zubeir na kuuzingira mji wa Makkah. Wakati ambapo katika tarehe 3 Rabiul al-Awal, mwaka wa 64 A.H, Ka'abah ilipochomwa moto, na majeshi ya Husein bin Numayr yalipoingia Makkah, al-Mukhtar alipigana dhidi ya majeshi ya watu wa Syria kwa ujasiri mkubwa na wavamizi walishindwa. Wakati huo huo, kifo cha Yazid kilitangazwa, na uvamizi ukasimamishwa. Al-Mukhtar, hata hivyo alibakia kukaa na Abdilah bin Zubair kwa zaidi ya miezi mitano.

Katika kipindi kirefu hiki cha mpito, mapinduzi yalitokea huko Kufa, na naibu wa Ubaydullah bin Ziyad, aliyeitwa Amr bin Hurrayth alikuwa ameondolewa na wakazi wa Kufa. Walimfanya Amr bin Mas'ud kuwa gavana wa Kufa na alitoa kiapo cha utii kwa Abdallah bin Zubeir na kuwafanya watu wa Kufa wamkubali kuwa khalifa wao.

Hali hii ya kutotulia ilichukuliwa na al-Mukhtar kuwa yenye kufaa kwa utekelezaji wa mipan- go ya kulipiza kisasi kwa wauaji wa Husein, na hivyo aliondoka kwenda Kufa.[3] Watu mashuhuri wa Shi'a wa Kufa walikubaliana na rai zake.[4] Wakati watu waliobaki wa kundi la watubiaji liliporudi pamoja na Rifa'a bin Shaddad baada ya kushindwa, al-Mukhtar alikuwa yuko kifungoni.[5]

Ilikuwa tena ni kwa msaada wa Abdallah bin Umar ambao aliandika kwa wote wawili Abdallah bin Zubeir na Ibrahim bin Muhammad bin Talha, gavana wa Kufa, kwamba al-Mukhtar alipata uhuru wake tena.

Watu mashuhuri na mashujaa pamoja na Ibrahim ibn Malik al-Ashtar wal- iungana na al-Mukhtar katika kuendeleza zaidi lengo la kulipiza kisasi kwa umwagaji wa damu ya Husein. Iliamuliwa kwamba tarehe 14 mwezi Rabiul-Awal mwaka wa 66 A.H, hatua lazima zichukuliwe kuanza kufanya kile ambacho kikundi kimelenga kukifanya. [6]

Wauaji wa Husein walikuwa ndani ya Kufa yenyewe. Walikuwa wakilip- wa na serikali ya Syria na kuwiwa utii wao kwa watawala wa nchi hiyo. Walikuwa pia wakazi wa Kufa ambayo ilikuwa chini ya msukosuko wa Abdallah bin Zubeir. Tendo lolote litakalochukuliwa na al-Mukhtar dhidi ya wakazi waovu kama hawa wa Kufa lingemuingiza katika matata na Abdallah bin Zubeir. Kama tatizo hili lilikuwa ni la kuamuliwa, kwa nini basi lisijaribu kutatuliwa hapa mwanzoni.

Kwa hiyo, al-Mukhtar, alifanikiwa kumwondoa madarakani gavana wa Kufa aliyeteuliwa na Ibn Zubeir, siyo kwa kutumia nguvu moja kwa moja, bali ilikuwa ni kuweka shinikizo dhidi yake hivyo kwamba gavana huyo alikimbia kuitoka Kufa. Al-Mukhtar aliweka serikali yake mwenyewe hapo. Alitekeleza kazi yake na katika kufanya hivyo alikumbana na hali fulani fulani zilizokuwa ngumu.

Ubaydullah bin Ziyad aliivamia Mosul akiwa na jeshi la Syria na al-Mukhtar alimpeleka Yazid bin Anas na watu 3,000 kupigana naye. Adui alishindwa, lakini wakati Yazid bin Anas, ambaye alikuwa hajisikii vyema alipofariki, Warqa bin Azid aliamua kuakhirisha mapigano mpaka kufika kwa nguvu mpya kutoka Kufa kwa kuzingatia idadi kubwa ya jeshi la adui. Alipozipata habari juu ya hali hii, al-Mukhtar alipeleka watu 7000 chini ya Ibrahim bin al-Malik al-Ashtar kumsaidia Warqa.

Mkubwa wa majeshi ya adui alipoona kwamba al-Mukhtar ameachwa takriban pekee kabisa, kwani Ibrahim alikuwa amepelekwa Mosul, alifikiria kuwa hii ni fursa nzuri sana ya kufanya uasi dhidi ya al-Mukhtar, na hivyo walifanya shambulio dhidi yake. Waliokuwa maarufu miongoni mwa wakubwa hawa walikuwa Shabath bin Ribi'i, Shimr bin Dhi al-Jawshan, Muhammad bin al Ash'ath, Zahr bin Qays, Hajjar bin al-Abjar, Yazid bin al-Harith al-Shaybani na Amr bin al-Hajjaj al-Zubaydi.

Al-Mukhtar aliendeleza mapigano na adui, na akapeleka ujumbe kwa Ibrahim bin al-Malik al-Ashtar kurudi Kufa mara moja. Alirudi katika siku tatu.

Wakati sasa ulikuwa umeshawadia kwa kutoa adhabu ya maadui wa dhuria ya Mtume na kuwakamata kwao kukaanza kufanyika.

Wakati kundi la kwanza la watu mia tano waliokamatwa kuhusiana na jambo hili walipoletwa kwa al-Mukhtar, yeye alitangaza kwamba wale waliokuwepo Karbala katika wakati wa kuuliwa Husein ni lazima waonyeshwe kwake kwani hatawaacha wabakie hai. Wengine wote waliachiliwa huru baada ya kuchukua kutoka kwao kiapo cha utiifu.[7]

Mnamo mwezi 24 ya Dhul Hijja mwaka wa 66 A.H. ilitangazwa kwamba mtu yeyote yule atakayefunga mlango wa nyumba yake na akabakia ndani yake angepata usalama labda kama alishiriki katika mauaji ya dhuriya wa Mtume.[8]

Kwa vile wauaji wa Husein walikuwa pia wamejificha pia majumbani mwao, Abu Amra Kaysaan, kiongozi wa Shurta (polisi), ambaye ndiye aliyekuwa anawatambua wote, aliamriwa aende na wafanyakazi elfu moja na kuzibomoa nyumba za wale wote ambao walishiriki katika matendo ya kinyama hapo Karbala. Nyumba nyingi zilibomolewa na maadui wengi wa Ahlul Bait waliuawa.

Maarufu miongoni mwa wauaji wa Husein ambao waliuawa walikuwa ni: Shimr bin Dhi al-Jawshan, Abdallah bin Asad, al-Malik bin Nasr al-Badii, Haml bin Maalik al-Muharabii, Ziyad bin Maalik, Imraan bin Khalid, Abd al-Rahman bin Abi Khushkara al-Bajali, Abd al-Rahman bin Qays al- Khawlaani, Abdallah bin Salkhab, Abdul-Rahman ibn Salkhab, Abdallah bin Wahb, Uthman ibn Khalid al-Juhani, Bushr ibn Saat, Qubayz Khawtii, Yazid al-Asbahii, Umar bin Sa'd, Hukaym bin Tufayl al-Taai, Zayd bin

Rifaad al-Juhani, Harmala bin Kaahil al-Asad, Amr bin Sabiih al-Sa'di na Qays bin al-Ash'ath.

Baada ya kukamilisha kazi yake hapo Kufa, al-Mukhtar alimpeleka Ibrahim al-Malik al-Ashtar tena kwenda kupigana na Ibn Ziyad. Baada ya mapigano makali sana jeshi la Syria lilishindwa katika sehemu iitwayo Khaazir na Ubaydulah bin Ziyad aliuawa. Husein bin Numayr al-Sakuni na Sharhabiil bin Dhi al-Kalaa pia waliuawa.

Ibrahimn alikata kichwa cha Ubaydullah bin Ziyad, na akakipeleka kwa al-Mukhtar ambaye alikitoa kwa Muhammad bin Hanafiyya.[9]

Ibrahim kisha aliitiisha Mosul na nchi zinazoizunguka kuwa chini yake. Kisha akaenda kukaa Nisibin na al- Mukhtar akabaki peke yake hapo al-Kufa.

Uadui ulikuwa umekwishaibuka kati ya al-Mukhtar na Abdullah bin Zubeir ambaye alikuwa bado anaimiliki Basra nchini Iraq, na alikuwa amembadilisha gavana wa Basra kwa kumweka ndugu yake mwenyewe aliyeitwa Mus'ab ibn Zubeir.

Wauaji wa Husein ambao walifanikiwa kukikwepa kifo mikononi mwa al-Mukhtar kama vile Shabath bin Ribi'i, Muhammad bin Ash'ath, Murra bin Munqidh al-Abdi, Sinan bin Anas na Abdallah bin Urwa al-Khath'ami walikimbia kutoka Kufa na wakaenda moja kwa moja mpaka kwa Abdallah bin Zubeir huko Barsra.[10]

Walimshinikiza kupigana na al- Mukhtar. Pole pole kiasi cha wakazi 10,000 wa Kufa waliondoka na kwen- da Basra, na wakiongozwa na Muhammad bin al-Ash'ath walimhakikishia Ibn Zubeir kupata ushindi dhidi ya al-Mukhtar.

Wakati huo huo, Abdallah bin Zubeir alikuwa amemtupa gerezani Muhammad bin Hanafiyya, pamoja na watu wake wanaomtegemea na wale wenyeji wa Kufa ambao walikuwa Makkah, akionyesha mwisho wa wakati ambao ndani yake walitakiwa watoe kiapo cha utii kwake, na kushindwa kufanya hivyo angewachoma moto wakiwa hai.
Muhammad bin al-Hanafiyya alimwarifu al-Mukhtar kuhusu balaa hili na al-Mukhtar alipeleka jeshi kutoka Kufa ambalo liliwaweka huru mateka na lilikuwa tayari pia kumuua Abdallah bin Zubeir. Muhammad bin al-Hanafiyya alilikataza hili kwani ilikuwa sawa na kuinajisi Ka'abah.

Mwishowe, labda kabisa kwa kukubaliana na matakwa ya ndugu yake mkubwa, Mus'ab bin Zubeir aliivamia Kufa akiliongoza jeshi kubwa sana. Ibrahim alikuwa Nisibin, na al-Mukhtar peke yake alipambana naye. Alipigana kishujaa sana kwa siku kadhaa akiwapoteza baadhi ya watu muhimu katika jeshi lake kama vile Ahmar bin Shumayt na Abdallah bin Kaamil. Mmoja wa maadui wakubwa wa dhuriya ya Mtume, Muhammad bin al-Ash'ath, aliuawa pia katika vita hivi.[11]

Mwishowe wakati wenzi wake wote waaminifu walipokwisha kuuawa na watu wakatupwa katika hali ya kuchanganyikiwa, al-Mukhtar alijikuta amezingirwa katika ngome. Kisha al-Mukhtar alitoka nje akiwa na

wasaidizi wake wachache waliobakia na akapigana vita vyake vya mwisho kwa ushujaa mkubwa na alikufa akiwa katika kupigana siku ya mwezi 14 Ramadhani mwaka wa 67 A.H, akiwa na umri wa miaka 67. [12]

Uadui na usugu wa adui zake ulishuka kwenye viwango vya chini kabisa vya ubaya wakati mke wa al-Mukhtar alipouawa hadharani kwa kukataa kwake kumlaani mume wake marehemu.[13]

1. Tabari, juz. 7, uk. 59.
2. Tabari, juz. 7, uk. 62.
3. Tabari, juz. 7, uk. 63.
4. Tabari, juz. 7, uk. 64.
5. Tabari, juz. 7, uk. 80
6. Tabari, juz. 7, uk. 100.
7. Tabari, juz. 7, uk. 121.
8. Tabari, juz. 7, uk. 121.
9. Al-Akhbar al-Tiwal, uk. 288.
10. Tabari, juz. 7, uk. 124, 128-130, 146.
11. Tabari, juz. 7, uk. 151.
12. Tabari, juz. 7, uk. 155, 161.
13. Tabari, juz. 7, uk. 158.

# Sura Ya 40 : Kuanguka Kwa Bani Umayyah.

Kihistoria ni kweli kwamba wakati watu wowote wapatapo lile daraja la utawala ambalo huwapatia wale walioko kwenye uongozi wa mambo yao, siyo tu mahitaji ya maisha bali pia na wingi wa mambo ya anasa, wanakuwa mawindo ya kupenda starehe, roho mbaya, ubinafsi na umimi, na kutaka kuona mbele na kuchukua njia yenye walau upinzani mdogo kabisa. Matokeo yake wanakuwa waoga.

Bani Umayyah walishindana na wafalme wa Roma na Uajemi katika mali (utajiri) na fahari na katika kadiri ya milki zao za nchi wanazozitawala. Kuangamia kwao kuliharakishwa na Yazid, ambaye alimuua al-Husein, bila ya kujali utukufu wake wa kiroho na ile nguvu yake isiyoshindika ya uadilifu.

Yalikuwa ni yale mauaji ya kikatili na kidhalimu ya Husein ambayo yalimpa Abdallah bin Zubeir kisingizio cha kupinga mamlaka ya Yazid, akawageuza wakazi wa Madina ambao hapo awali walikuwa ni watu wasiojishughulisha wakawa dhidi yake Yazid, akashawishi lile kundi la wenye kutubia makosa yao kuanzisha kampeni ya nguvu ingawa isiyo na mafanikio, ya kulipiza kisasi kwa wauaji wa Husein, akamchochea al-Mukhtar kujiingiza katika idadi ya mapigano ili kuwauwa wauaji wa Husein, akamsukuma Zayd bin Ali bin al-Husein katika mwaka wa 112 A.H. kuasi dhidi ya Bani Umayyah, na kuacha nyuma kundi ambalo kisiasa lilikuwa na madhara sana kwa Bani Umayyah, ingawaje yeye mwenyewe hakufanikiwa (katika kampeni hizo).

Mwishowe, ilikuwa ni hamu hiyo hiyo ya kutoa adhabu kwa umwagaji wa damu ya al-Husein ambayo iliwasaidia Bani Abbas kuwaangamiza na kuwatokomeza kabisa Bani Umayyah.

Baadhi ya vyama hivi vilikuwa vya kisiasa hasa kwa asili ambayo dhuria ya a-Husein, wenyewe walijitenga navyo kabisa.

Wakati Abu Muslim al-Khurasani aliposiamamisha bendera ya uasi dhidi ya Bani Umayyah pale Marv na lengo lililotangazwa la kulipiza kisasi kwa mauaji ya Husein, maelfu ya watu walikusanya nguvu kumsaidia na mfalme wa mwisho wa Bani Umayyah, Marwan bin Muhammad aliuawa katika vita vya Zab [1] na pamoja naye mamlaka ya Bani Umayyah yakaangamia kabisa.

1. Tabari, juz. 9, uk. 136.

# Sura Ya 41: Utawala Wa Bani Abbas.

Madai ya Ukhalifa yaliyotolewa na kizazi cha Abbas, ami yake Mtume, kwa ajili yao wakati fulani baada ya mauaji ya Husein pale Karbala na kufuzu ambako kuliambatana na jitihada za Abu Muslim al-Khurasani katika kuyatanguliza mbele maslahi ya Bani Abbas na kuzitenganisha huruma za Waislamu kwa Bani Umayyah kulitegemea hasa zaidi hisia za upendo wa watu juu ya watu wa nyumba ya Mtume.

Ingawaje uvaaji wa nguo nyeusi uliofanywa na Bani Abbas haukuhusika na kuonyesha sura yoyote ile ya huzuni juu ya kuuliwa kwa Husein pale Karbala, wale ambao hawakujua ukweli halisi walililifikiria hilo la uvaaji wa mavazi meusi kuwa ni udhihirisho wa huzuni kwa kuuawa Husein.

Maoni haya yalitiwa nguvu na lile jambo la kwamba, ilikuwa ni tarehe 10 ya Muharram mwaka wa 132 A.H wakati ambapo, baada ya mauaji ya khalifa wa mwisho wa Bani Umayyah, Marwan, Bani Abbas na wafuasi wao, wakiwa wamevalia mavazi meusi, walikusanyika katika msikiti wa Sala za jamaa mjini Kufa.

Kwa kweli kundi hili lilikusanywa pamoja hivyo ili kuomboleza juu ya kifo cha muasisi wa kundi hilo, Muhammad bin Ali bin Abdallah bin Abbas[1] na kuuawa kwa Ibrahim bin Muhammad[2] kiongozi wa kundi hilo ambaye pia alikuwa mtoto wa muasisi huyo.

Watu walikuwa wamevutiwa na kundi hilo kwa kukumbuka sifa bora na madai ya watu wa nyumba ya Mtume kwenye Ukhalifa. Kiapo cha utii ambacho kilikuwa kikitumika kuchukuliwa kutoka kwa watu na waeneza propaganda wa Bani Abbas kilikuwa si kwa mtawala yeyote yule kwa kutajwa jina. Ilikuwa ni katika mpango ufuatao: “Nachukua kiapo cha utii kwako kwa kukitii Kitabu cha Allah, Sunna za Mtume na mtu atakayeidhinishwa na watu wa Nyumba ya Mtume.” [3]

Wakati mnamo mwezi 11 ya Muharram mwaka wa 132 A.H. pale utawala wa Bani Hashim (yaani Bani Abbas) ulipotangazwa, Abu Salama Hafs bin Suleiman, rafiki wa watu wa nyumba ya Mtume aliteuliwa kuwa waziri, na Abu Muslim al-Khurasani aliitwa "Muaminiwa wa dhuria ya Mtume."[4]

Dhuria wahusika wa Mtume walijua kwamba jina lao lilikuwa likitumiwa kuhusiana na kundi hilo kwa sababu tu ya kutumikia malengo ya kisiasa. Matokeo yake, wakati barua ya kumpa Ukhalifa ilipopokelewa na Imam Jafar as-Sadiq aliichoma moto hapo hapo, akisema kwamba watu wa Khurasani walikuwa siyo Shi'a (wafuasi) wa Ali wa kweli, na kwamba Abu Salama alikuwa amedanganywa na hivi karibuni atauawa.[5]

Muda mfupi tu baada ya kupanda Abu al-Saffah Abdallah ibn Muhammad ibn Ali ibn Abdallah ibn Abbas kwenye Ukhalifa, Abu Salama akauawa[6] na baada ya al-Saffah, dhuria wa Mtume walipokea kutoka kwa Bani Abbas, utendewaji mbaya na wa kila mara ulio sawa na uleule waliokuwa wakitendewa na Bani Umayyah. Hata hivyo mambo haya hayabadilishi ule ukweli wa kwamba Bani Abbas walipanda madarakani juu ya wimbi la chuki dhidi ya kuuawa Husein

1. Al-Akhbar al-Tiwal, uk. 324.
2. Ibid, uk. 243.
3. Tabari, juz. 9, uk. 99.
4. Tabari, juz. 9, uk. 142.
5. Al-Wuzar Waal Kuttub, uk.57.
6. Ibid, uk. 60.

# Sura Ya 42:Mabadiliko Ya Fikra.

Lengo la haraka la Husein siyo kuangamiza mamlaka ya Bani Umayyah au utawala wa Yazid kiyakinifu, kwani mafanikio ya lengo hilo yangehitaji msaada wa kutosha kijeshi na vifaa vingine vya kimaada. Yeye alijaribu kufungua uwanja mpya wa mapambano, kuzifanya kifra za watu kuwa shabaha ya mashambulizi yake.

Alipendelea kuanzisha mapinduzi ya kiroho. Majeshi ya Yazid yangeweza kumuua Husein; wasingeweza kwa vyovyote vile kuangamiza (kuua) yale mawazo ambayo Husein aliwataka watu wayachukue kutokana na mfano aliouanzisha yeye.

Qur'ani inawaelekeza Waislamu kumtii Allah, Mtume na kuwatii watu wenye mamlaka miongoni mwao. Wengi mno katika Waislam humtambua Khalifa kama mtu aliyeko katika madaraka ambaye wao wanalazimika kumtii. Mamlaka fulani ya kufanya kanuni za kidini yamekubaliwa pia kwa Khalifa kuwa nayo. Kwa hiyo, mwenendo wa kila

Khalifa lazima uwe umekubaliwa kama ni sahihi, lakini Waislam walio wengi, isipokuwa Shi'a ambao

hawaikubali kabisa mitindo iliyokubalika kwa jumla ya utawalishaji wa Makhalifa kama imethibitishwa na kuhalalishwa, wanawa- gawa makhalifa katika tabaka mbili, 'makhalifa waongofu' na 'wengineo.'

Kuzungumzia kwa jumla, Ukhalifa wa Ali, na kipindi cha Ukhalifa wa Hasan kabla ya mkataba wake na Mu'awiyah vinachukuliwa kukifunga kipindi cha Makhalifa waongofu. Mu'awiyah, Yazid na Makhalifa wengine pamoja na Makhalifa wa Bani Abbas wanachukuliwa kuwa ni mbali na Makhalifa waongofu.

Tofauti hii miongoni mwa Makhalifa na kuwashusha chini wengi mno katika wao lazima kuchukuliwe kama ni matokeo ya changamoto ya Husein na namna maalum ya *Jihad.*

Baada ya upinzani imara wa Husein hapo Karbala, ilikubaliwa kuwa ni mpango wa kudumu kwamba hakuna Khalifa aliyekuwa na mamlaka ya kutunga sheria za kidini, na kwamba alikuwa ni mwenye kupata dhambi kwa matendo yake maovu kama vile Mwislamu mwingine yeyote yule, au hata pengine zaidi.

Hali kadhalika iliamuliwa kwamba wajibu wa utii kwa mtu huyo aliyeko madarakani kwa wakati huo uliendelea tu na kufikia mahali ambapo uasi na uvunjaji wa lengo la Mwenyezi Mungu ulikuwa hauhusiki, na kwamba wakati uridhishwaji wa sheria ya Mwenyezi Mungu uliwezekana tu kwa kumpinga mtu yule aliyeko katika madaraka, ilikuja kuwa ni wajibu kwa kila mtu kujiandaa kutoa upinzani kwake kama ilivyoamriwa na Allah.

Fikra ya kumfuata mtawala kibubusa bila kujitambua kama ng'ombe vipofu wenye kuswagwa hali ambayo ilikuwepo mpaka mwaka wa 60 A.H ilibadilishwa kutokana na matokeo ya kujitoa mhanga maisha yake Husein, kwa hali ya mtu kuyatambua majukumu yake na haja kuziwajibisha serikali za kidhalimu, ili kwamba kuanzia hapo hakuna serikali iliyokubali yenywe kujitia kwenye usingizi wa kuridhika kizembe.

Uvumilivu wa Husein na uimara ulikuwa ni mfano wa kukumbuka katika misiba yote, na umefundisha umadhubuti na ushupavu kwenye nyoyo zenye kuyumbayumba. Katika mwaka wa 71 A.H, majeshi ya Mus'ab bin al-Zubeir yaliogopeshwa na kuwekwa katika hali ya mvurugiko; wakati Abd al-Malik bin Marwan alipomshambulia Mus'ab akiwa na jeshi kubwa zaidi. Mus'ab alimtaka Urwa bin al-Mughira bin Su'ba kumweelezea namna gani Husein alivyokataa kutii amri za Ubaydullah bin Ziyad, na vipi alivyokuwa amejiimarisha yeye kupigana vita vya *jihad*. Alipokwisha yasikia maelezo ya Urwa, ujasiri wa Musab ulirejea na akasoma shairi lenye maana:

"Watu wa familia ya Hashim wameweka mfano hapo Karbala ambao ni bora sana kwa watu wenye akili za kiungwana." Kisha baada ya hapo alikabiliana na adui na akafa akiwa yungali anapigana.

Katika njia ile ile nguvu ya subira ilivyoonyeshwa, na ujasiri wa kutoa sura huria kwenye hisia za kweli za mtu zilizoletwa na Husein, zimekuwa tangu zama hizo ishara za hatari kwa tawala za kidhalimu na kiuonevu zenye kukandamiza, na ule ujumbe uliotolewa na Husein kwenye hisia za kibinadamu utabaki na kudumu milele na milele.

# Sura Ya 43: Matokeo Yenye Mafunzo.

Ingekuwa ni kuufanyia ukatili mtazamo wa Uislamu na ufahamu wake kwamba matokeo ya mhanga wa Husein uonekane umefungika pekee kwenye kundi lolote lile maalum la jamii ya binadamu. Faida inayotiririka kutokana na mhanga wake wanaweza wakaishirikiana wale wote ambao watapenda kujifunza kutokana nayo juu ya namna wanavyoweza kujichunga katika maisha yao. Faida ambazo zinaongezeka kwenye dini, ubinadamu na Uislamu kutokana na matukio ya Karbala zimetajwa hapa kwa ufupi.

## Nguvu Ya Dini Na Imani Ya Kiroho Yaonyeshwa.

Uyakinifu na hali ya kiroho siku zote vimekuwa katika vita baina ya vyenyewe kwa vyenyewe. Dini inashikilia imani ya kiroho hata sasa ingawaje imani ya kiroho haiko katika mtindo katika ulimwengu wa leo. Vita vya Karbala vilikuwa ni vita vya dini dhidi ya uyakinifu (maslahi ya kidunia). Mbali na nguvu zake kubwa mno, jeshi la Yazid halikuweza kukipata kwa kutumia nguvu, kile kiapo walichokitamani sana kutoka kwa Husein, cha utii kwa ajili ya mtawala wake.

Katika majumuisho ya mwisho ilikuwa ni Husein ambaye, ingawa aliuawa na kushindwa kwa muonekano wa nje, ndiye aliibuka mshindi, na pamoja naye ilishinda imani ya kiroho.

## Uthibitisho Wa Ukweli Wa Uislamu Na Uenezwaji Wake.

Alama moja muhimu ya ukweli wa dini ni ile subira ya kijabari na umad- hubuti ambao kwamba waanzilishi wake hukabiliana na shida na dhiki, na wanang'ang'ania kwenye misingi yao mpaka mwisho wa siku zao. Msaada uliotolewa kwenye dini yao na wafuasi wake wa kawaida wakikabiliana na dhiki kubwa kishujaa na wakijitoa mhanga maisha yao wenyewe usingeweza kuthibitisha kwa uhakika ukweli wa imani (dini) yao, kwani pengine wangeweza kuwa wamedanganywa au walikuwa pengine hawau- tambui ukweli wenyewe.

Lakini kama mwanzilishi wa dini, wasiri wake na watu wa familia yake ambao ni wajuzi wa ndani wa siri za maisha yake binafsi, na kwa undani wa karibu sana wameizoea hali ya maadili yake na sifa zake nyingine, wanakubali kukabiliana na mitihani katika kuunga mkono kanuni na misingi yake, na kama ni lazima, kuyatoa maisha yao (Kufa) katika kuthibitisha uhalali wa kanuni za dini yake, ukweli wa misingi yake bila shaka yeyote utakuwa umethibitika.

Pamoja na al-Husein, wapenzi na wafuasi wake wote, na pia ndugu zake walijitoa mhanga maisha yao baada ya kupata mateso makali sana na ukandamizwaji.

Mhanga wa Husein haukumpata kwa kimya kimya. Aliendelea taratibu kuwalingania watu kwenye

Uislamu wa kweli na halisi. Katika tarehe 9 ya Muharram, wakati adui aliposonga mbele dhidi ya Husein wakati wa jioni bila ya kutanguliwa tangazo kabla, aliomba kusimamishwa mapigano kwa usiku mmoja ili kwa usiku mmoja ili utumike tu katika maombi yake mwisho na Sala kwa Mwenyezi Mungu. Husein na wafuasi wake waliutenga usiku wote kwa lengo ambalo mapatano ya kusimamishwa vita yalikuwa yamekusudiwa.

Katika kufanya hivyo, walionyesha na kuthibitisha kwamba katika hali za mitihani mikali sana kanuni na misingi ya dini lazima izingatiwe na kwamba nguvu za kiroho ni bora kuliko nguvu zote za kilimwengu.

Bado hali ngumu zaidi ya mazingira ilikuwepo wakati siku ya tarehe 10 ya Muharram Husein alipoongoza Sala za mchana ndani ya uwanja wa vita katika mfululizo wa mishale baada ya watu wengi wa kundi lake dogo walipokwishauawa.

Haya yalikuwa maonyesho dhahiri ya ukweli wa mafundisho ya Kiislam ambayo yaliujaza ulimwengu kwa wito wa uzinduzi wa haki, uliamsha dhamira ya Waislamu, na kufichua ukatili wa Yazid na uadui wake kwa Uislamu.
Kila mtu wa kundi la Husein alikuwa kama mhubiri. Mashindano ya Burayr na Yazid bin Ma'qil na kuomba laana za Mwenyezi Mungu ishuke juu ya yeyote yule kati yao aliyesema uwongo, na khutuba za Zuhayr bin al-Qayn zinaweza kutolewa kutoka miongoni mwa idadi kubwa sana ya mifano ambayo ndani yake wapenzi wa Husein walizifafanua sababu ambazo zilimshawishi Husein kuchukua mwenendo ambao aliuchukua. Haina umuhimu kwamba jitihada hizi hazikuleta mafanikio ya haraka, kwani kazi ya mhubiri inahusu tu kuwaita watu kwenye kweli ya ujumbe wake hata katika mazingira yenye kuvunja moyo kabisa.

## Mafundisho Ya Kimaadili Na Ya Kijamii Ambayo Yaweza Kupatikana Kutokana Na Masaibu Ya Karbala.

Sawia pamoja na kuwa ni yenye kusikitisha kupita kiasi, matukio ya Karbala si yenye kuleta maomboleza pekee. Yanaelekeza na kubadilisha ili kuupandisha uhai wa binaadamu katika daraja za juu sana za rehema na Ucha-Mungu.

Baadhi ya mafundisho makuu ya matukio ya Karbala yametajwa na kuelezewa kwa ufupi chini ya vichwa vya habari vifuatavyo:

**Uhuru:** Uhuru maana yake ni kuwa huru wa kutenda kwa mujibu wa inavyoamua dhamira ya mtu bila ya kizuizi chochote kile.

Miongoni mwa vizuizi kwenye uhuru wa kutenda ni mapenzi ya mtu juu ya starehe na vitu ambavyo starehe zinazoendelea umehatarishwa kwa kufuata maamuru ya dhamira ya mtu. Ukombozi kutokana na tamaa unakataa katakata nguvu zote za kidunia za kumfanya mtu mtumwa. Kwa kutenda kwa mujibu wa mwongozo wa dhamira yake, Husein alionyesha kujikomboa kwake kutokana na matamanio katika

hali za taabu na dhiki zenye kutisha mno.

Kwa mujibu wa umuhimu ambao jitihada ya Husein zilitoa kwenye uhuru, raia wa nchi huru kwa kweli ni watumwa kama watafuata mambo maovu. Kwa upande mwingine raia wa nchi iliyofanywa utumwa wako huru kama mbali na kuteseka kwa ukandamizaji, wanafuata haki na kumwabudu Mwenyezi Mungu.

**Uimara:** Ni uimara kama tu katika kufuata njia ngumu na ya hatari katika vitendo mtu kamwe hatasita wala kukwepa na atadumisha utulivu wake na ushwari. Katika kuzimiliki sifa hizi, mashahidi wa Karbala wanachukua nafasi ya mbele kabisa.

Husein alikuwa amekataa kuapa kiapo cha utii kwa Yazid baada ya kuchunguza undani wa roho yake, na baada ya kupima katika sehemu ya ndani kabisa ya akili yake zile hatari za hali hiyo, na baada ya kujiridhisha mwenyewe kwamba kwa ukubwa wowote ule wa makali ya mateso yake utakaoweza kutokeza, umadhubuti wa uamuzi wake usingetikisika. Wasaidizi wote wa Husein hapo Karbala, pamoja na watoto, walisimama imara katika kuupa athari upinzani uliodhamiriwa na Husein kwa Yazid.

Katika safari ya Husein kwenda Kufa, al-Hurr alikuwa amekutana naye na akiyatabiri mauaji ya Husein kama akishikilia kufuata mwelekeo wake wa kwenda Kufa, alimwomba ajionee huruma mwenyewe na auache mpango wake. Husein alijibu kwamba kifo kilikuwa si kitu kama mtu atakuwa amesimama katika haki. Hivi ndivyo, Ali al-Akbar bin Husein alivyowahi kueleza.

Maadui wa Husein waliijua nguvu ya azma yake. Mnamo siku ya tarehe 9 ya Muharram, Umar bin Sa'd alipokea barua ya Ibn Ziyad ikimuelekeza kwamba ni lazima apate kutoka kwa Husein kiapo cha utii kwa Yazid bila ya masharti au ampige vita.

Umar bin Sa'd mara moja akasema, "Husein kamwe hawezi kukubali kwa namna hii. Roho ya baba yake inadunda ndani ya kifua chake." Na kila mtu aliona kwamba Husein, kama ukingo wa uimara na umadhubuti, alihimili gharika za mateso na maumivu ambayo yalikuwa yamemzunguka katika medani ya vita.

**Kuandaa kundi:** Umoja wa hisia, mawazo, malengo na vitendo vinahita- jika kwa ajili uandaaji wa makundi ya watu. Kufanya jambo kwa lengo moja, ambako kunaweza kuonyesha tabia ya kiongozi sio uhakikisho kwamba angejikusanyia wafuasi ambao wote kwa jumla watashirikiana naye katika sifa hii.

Tunazijua neema nyingi sana ambazo wana wa Israeli walizipata kupitia kwa Nabii Musa, lakini walipotakiwa kupigana kuika- mata Nyumba Takatifu (*al-Bayt al-Muqaddas*) watu wote isipokuwa wawili tu, walikataa kupigana na wafilisti. Yaliyomtokea Kristo hayakuwa mazuri zaidi.

Idadi ya watu ambao waliikubali imani (dini) mikononi mwake ilikuwa ni ndogo. Na alikuwa ni mmojawao aliyemsaliti na kumfanya akamatwe.

Biblia inatuambia kwamba Kristo aliwaambia wafuasi wake kusingekuwa na hata mtu mmoja miongoni mwao ambaye hangeangukia katika kutenda kosa kuhusu yeye. Mmoja wa wanafunzi wake wateule,

Petro, alimkana Kristo mara tatu.

Wale wanafunzi wengine hawakutoa msaada wowote ule kwa Kristo na hawakushikilia kwenye njia ya haki. Hali kadhalika matukio kama hayo yalitokea katika Uislamu, na hayo pia ni katika wakati wa uhai wa Mtume.

Tukio moja la namna hiyo lililoelezewa katika Qur'ani linasimulia kuhusu vita vya Uhud, wakati walipopelekewa na Mtume chini ya uongozi wa Abdallah bin Jubayr kukilinda kinjia chembamba katika mlima wa Uhud na kwamba wasilitoke lindo lao hili kwa hali yoyote ile, walikiacha kinjia hicho bila ya ulinzi na wao walikimbilia kwenda kupora vitu vya adui aliyeshindwa, na hivyo wakasababisha Waislamu washindwe. Hata hivyo, wafuasi wa Husein hawakuonyesha dalili yoyote ile ya kuhitilafiana kwa maneno au kitendo toka kwa kiongozi wao katika vita vya Karbala.

**Kujiheshimu:** Uislamu uliitambua silika ya kibinaadamu ya kuokoa maisha na Qur'ani ikakufanya kujilinda kuwa ni jambo la wajibu pale iliposema, "**Usiyaweke maisha yako hatarini.**" Njia iliyoteuliwa na Husein kwa ajili yake mwenyewe kwa utekelezaji unaostahili wa majukumu yake ilikubaliana na kanuni iliyoelezewa na yeye mwenyewe kwa maneno, "Kifo ni bora zaidi kuliko fedheha na aibu," na haya: "Kifo cha heshima ni bora zaidi kuliko maisha ya aibu." Maneno haya ndiyo maadili ya hekima ya mbele kabisa, ya watu na mataifa ya ulimwengu yenye kujiheshimu. Kwa misemo mifupi hii, akiwa ameamriwa kwa utukufu wa akili na aliye- julishwa vyema juu ya kujiheshimu, Husein aliongeza uzito wa mfano wake mwenyewe na akaifikisha kwa walimengu kwa ujenzi wake wa maadili.

**Subira:** Sifa ya subira ilikuwa imehusishwa na Husein kwa ukamilifu kiasi kwamba anaitwa '*Sayyid al-Swaabirin*,' yaani kiongozi wa wale wenye subira." Ilikuwa siyo kwamba vinyume vya bahati visivyotegemewa vilimpata Husein na sahaba zake pale Karbala, ambavyo dhidi yake hapakuwa na fursa yoyote iliyopatikana, na ambazo zilikuwa kwa lazima zivumiliwe. Mateso yalichukuliwa kama hatari zilizokwishapangwa, kama maendeleo yakaribishwayo ili kwamba haki iweze kuwepo.

Ule ukweli kwamba Husein aliwapeleka wafuasi wake wote, wapenzi wake wote na ndugu zake wote kwenye uwanja wa vita, kuifanya kazi yao na hatimae kufa, bila ya yeye mwenyewe kushiriki katika mapigano; ulikuwa ni mfano, ambao ulisababisha daraja kubwa la subira, ambalo ni Husein peke yake tu aliyeweza kulionyesha. Hata hivyo, moyo huo ulichangiwa kikamilifu na masahaba wote wa Husein. Uhimizaji wa Abu al-Fadl Abbas kwa ndugu zake akisema, "Songeni mbele ili niweze kushuhudia kuuawa kwenu," unaonyesha shauku hiyo hiyo ya kuteseka kwa kukubali kikamilifu kabisa.

**Ushujaa**: Ujasiri, kwa maana yake iliyo halisi, haihitaji tu kwamba mtu lazima apigane vita, wakati inapostahili kufanya hivyo, na halafu afanye kile ambacho wajibu ungemtaka kufanya, bila hata kujali matokeo mabaya sana, lakini pia kwamba mtu lazima afanye subira wakati kupigana kutakapokuwa hakustahili, na kutoonyesha papara na kutojali tu kungesaidia, hata ingawa njia kama hiyo ingejaa matatizo mengi.

Ni mwelekeo mmoja tu wa ushujaa wa Husein ambao ulionekana waziwazi hapo Karbala. Mwelekeo

mwingine wa ushujaa wake aliuonyesha yeye mwenyewe mapema zaidi wakati alipokuwa akiendelea kuchunga kwa miaka kumi, yale masharti ya mkataba uliofanywa kati ya kaka yake Hasan na Mu'awiyah. Katika kipindi hiki kirefu cha wakati, matukio mengi machungu yalitokea lakini Husein aliyavumilia bila ya kufanya lolote la kuweza kufanya mambo kuwa mabaya zaidi katika hali ambayo tayari ilikuwa ni ngumu.

Ilikuwa ni pale tu alipolifikiria kuwa ni wajibu wake kuzitia changamoto na kupigana na nguvu za uonevu na udhalimu (ukandamizaji) kwamba Husein aliishinda hata milima kwa uimara na umakini. Vitendo vya ushujaa vilivyotimizwa na Husein na watu wake hapo Karbala vinawashangaza watu hata leo hii.

Ni ushujaa gani uliopita kiasi ulioonyeshwa na Husein na masahaba wake wakati waliposimamisha Sala zao za jamaa za wakati wa mchana katika medali ya mapambano ya Karbala wakati vita ilikuwa katika makali yake yaliyozidi mno na mishale ilikuwa inamiminwa kwa wingi juu yao na adui, hivyo kwamba mmoja wa masahaba wa Husein, Sa'idi bin Abdallah al-Hanafi, ambaye alisimama mbele yake kumkinga kutokana na mishale, alianguka chini akafa kutokana na majeraha mengi aliyopata kwa kupigwa mishale mingi katika mwili wake, mara tu Sala zilipomalizika!

**Kujinyima**: Kutoa umuhimu wa kwanza kwenye mahitaji ya wengine juu ya mahitaji binafsi ya mtu ina maana ya kujihini. Mifano mizuri sana ya sifa hii ilionyeshwa na Husein, na wasaidizi wake hapo Karbala. Husein alitoa funzo la kukumbukwa kuhusu kujinyima wakati alipokuwa njiani kuelekea Iraq, bila ya kujali hali zake mwenyewe za baadaye, aliyatoa maji aliyokuwa ameyahifadhi na kumpa al-Hurr na watu wake ambao walikuwa wanakufa kwa kiu, ingawaje walikuwa ni madui ambao walikuwa wamepewa kazi ya kumzuia kuendelea na safari yake ya kwenda Kufa.

Hapo Karbala, kila mmoja wa wafuasi wa Husein na ndugu waliambatanisha ubora wa kuyalinda maisha ya Husein kwa kulinganisha na maisha yao wenyewe kiasi kwamba walitenda kama vile tayari wamekwishaagana na uhai wao. Sa'id bin Abdallah al-Hanafi kusimama kwake mbele ya Husein kumkinga kutokana na mishale kwa kipindi cha Sala za mchana kwa kweli ni mfano usiosahaulika na kujihini.

Kila mmoja wa wafuasi wa Husein alijaribu kujitoa mhanga maisha yake kabla ya wengine ili kuwaokoa, hata kama iwe kwa kipindi kifupi sana. Wote walitambua kwamba hakuna ambaye angebakia hai, lakini bado kila mtu alijaribu kuwawsalamisha wengine madhali yeye mwenyewe alikuwa bado yuko hai.

Abbas na ndugu zake, walipata ahadi mbili za usalama, moja kupitia kwa Abdallah bin Abi al-Mahall, mpwa wa mama yao, na nyingine kupitia kwa Shimr. Ahadi zote mbili zilikataliwa bila kuheshimiwa (zilipigwa mateke). Ilikuwa ni udhihirisho usiokuwa wa kawaida wa moyo wa kujitoa kukikaribisha kifo kwa ajili ya mtu mwingine wakati njia kuelekea kwenye usalama iko wazi kabisa. Ilikuwa ni kujihini kwa Husein na wafuasi wake kwamba, ili kuilinda dini na kuukoa ubinaadamu kutoka katika mateso ya kidhalimu, walijitoa mhanga kikamilifu kabisa hapo Karbala.

**Ukamilifu katika maingiliano ya jamii**: Katika hali ya ustawi na amani, kanuni za adabu za kijamii

huwa kwa kawaida zinazingatiwa. Hata hivyo ilikuwa Husein pekee ambaye, akiwa katika ridhaa ya hali zenye kukatisha tamaa na mateso yenye kuzidi hapo Karbala, alifanikiwa kuyatimiza kabisa matakwa yenye kulazimu ya ukamilifu wa maingiliano ya kijamii kwa kutokuacha kamwe kuyaangalia madai ya yeyote yule kati ya wafuasi wake, wa mbalimbali kama wasaidizi, wapenzi, na ndugu, juu ya kujali kwake na huruma, bila kuonyesha upendeleo usiostahili kwa yeyote yule wala kukataa utambuzi wa mtu ambapo cheo na hadhi vilitoa uhalali wake.

Medani ya vita ilikuwa mbali kiasi kutoka kambi ya Husein. Kila wakati alipomruhusu mtu yeyote kati ya wasaidizi wake au marafiki kwenda kupi- gana, alikuwa akiyaangalia mapigano hayo, na pale askari wake alipo- jeruhiwa, Husein alikuwa akimtembelea. Ni lazima ilikuwa iwe ni vigumu mno kwa Husein kufanya matembezi kama hayo katika jua kali, kwa vile watu wake wote mwishowe walianguka wakipigana.
Katika nyakati zilizokuwa ngumu sana na za hatari ambazo Husein alikuwa anazipitia hapo Karbala, wakati akili ya mwanadamu inapoteza udhibiti wake juu ya ufanyaji kazi wake, ilikuwa ni mafanikio ya Husein kwamba aliyapatia uzingativu kamili majukumu ya kijamii. Katika tarehe

10 ya Muharram, zilikuja habari za kukamatwa kwa mtoto wa Bishr bin Amr katikia nchi (jimbo) ya Rayy. Husein alimwambia Bishr aende kum- saidia mwanawe apate kuachiwa. Wakati Bishr alipokataa kumwacha Husein, Husein alimtaka ampeleke mtoto wake mwingine, Muhammad, kwenda kumsaidia ndugu yake. Husein pia alitoa baadhi ya vipande vya kitambaa cha nguo chenye thamani sana kwa Bishr, ili kwamba bei ambayo nguo hiyo ingeipata, iweze kutumika kupata kuachiwa kwa mtoto wa Bishr.

Wakati yeyote yule kutoka miongoni mwa wafuasi wa Husein au ndugu alipoanguka chini kutoka kwenye farasi wake wakati wa Vita vya Karbala; yeye angemgutiakwa sauti Husein ambaye alifikiria kuwa ni wajibu wake kuijibu miito kama hiyo na kutoa msaada wote uwezekanao.

Pia alijitahidi kuhakikisha kwamba hakuna yeyote katika wafuasi wake waliokufa anakatwa kichwa na ni ukweli kwamba isipokuwa kwa wale ambao hawakumwita Husein, hakuna katika wafuasi wake aliyekatwa kichwa.

Husein alijaribu kuhakikisha kwamba maiti za wafuasi wake zinapata ile heshima iliyostahili. Wakati yeyote yule katika wao alipouawa, Husein kwa kawaida alifuatana na watu wengine ambao walipanga mipango ya uwekaji salama wa maiti ya mpenzi wao. hata hivyo, wakati ndugu wa Husein walipoanza kujitoa mhanga maisha yao wenyewe, kazi ya kuzichukua maiti zao kutoka kwenye medani ya vita na kuzipeleka kwenye hema lake ilimwangukia yeye mwenyewe Husein.

Al-Husein aliwafanya vijana wa ukoo wa Bani Hashim wahusike kwa kuichukua maiti ya Ali al- Akhbar kuipeleka kwenye hema lake kutoka kwenye medani ya vita na yeye mwenyewe aliibeba maiti ya al-Qasim kuipeleka kwenye hema. Husein hakupata nafasi ya kuzika mabaki ya watu wazima, lakini hakuacha kabisa kazi ya kuwazika waliokufa. Yeye mwenyewe aliizika ile maiti ya mtoto mdogo, Ali al-Asghar.

**Kusema ukweli mtupu:** Jitihada ya Husein kutoka mwanzo mpaka mwisho wa msiba wa Karbala ilikuwa ni kuelimisha na kuziweka sawa akili za watu juu ya dhana zote mbaya kuhusu matarajio yake, ili kwamba watu wasije wakamsaidia kwa sababu ya matumaini ya uwongo. Alikuwa akiwaambia watu kwa kukariri mara kwa mara ukweli kuhusu matarajio yake na kutangaza kwa kurudiarudia kwamba matokeo ya mwisho ya safari yake yangekuwa ni mauti. Wakati Husein alipojiandaa kuondoka Makkah, watu walijenga matumaini mema juu ya maisha yake ya baadaye, kwa vile Kufa ulikuwa miji mkuu wa Iraq na ulikuwa makao ya serikali ya Ali. Walifikiria utakuwa ni mji uliojaa wapenzi na marafiki wa Ali. Pia walikuwa wamesikia kwamba barua 129 zilikuwa zimepokelewa kutoka Kufa zikimwita Husein aende huko na kumwahidi msaada wa wakazi wa mji mpaka tone la mwisho la damu yao.

Walikuwa pia wamesikia kwamba watu 18,000 wa Kufa wali- ahidi kutoa kiapo cha utii kwa Husein mikononi mwa Muslim bin Aqil. Hali ya kawaida ya matumaini mema ilitawala kuhusu matarajio ya Husein hapo Kufa, lakini Husein alifikiria ilikuwa lazima kwamba watu hao waambiwe kwamba matumaini yao yalikuwa hayana ukweli wowote.

Siku moja kabla ya kuondoka Makkah, Husein alitoa hotuba ya kukumbukwa, alisema, “Kifo humfuatia mtu kama shada la maua lililozunguush- wa shingoni mwake... Mahali nipapendapo sana ni ile sehemu ambayo, katika kuuawa kwangu, nitaanguka hapo... Yeyote yule apendaye kujitoa mhanga maisha yake pamoja nami, na yuko tayari kufa, anaweza kufuatana nami.” Je, kunaweza kukawa na ushahidi mzuri zaidi wa kusema wazi wazi, ukweli na kuwa na tabia ya kunena bila ya kupendelea kuliko huo?

Baada ya Husein kuwa amekwishaondoka Makkah, baadhi ya makabila wahamaji na watu wengine mbumbumbu wasiojua walijiambatanisha kwenye msafara wake walipojua kwamba alikuwa anakwenda Iraq baada ya kupata mialiko kutoka Kufa.
Idadi yao ilikuwa kubwa sana kiasi kwamba msafara mdogo ambao alikuwa ameuongoza Husein kutoka Makkah ulionekana kama jeshi.

Kwa mshindania madaraka fedhuli, kundi hili la watu lisiloalikwa lingekuja kama baraka, na angejitahidi kadiri ya uwezo wake wote kushikilia makubaliano nao kwa kutoa ahadi za uwongo na kuleta matumaini yasiyo na msingi. Hata hivyo, Husein hakuruhusu uele- waji mbaya huu kuendelea kwa urefu wowote wa muda.

Alipozipata bahari za kuuawa kwa Muslim bin Aqil na Hani bin Urwa hapo Kufa, alisimama mahali paitwapo Zubala, na akazitoa habari hizo za kusikitisha kwa msafara uliokusanyika, akisema, “Yeyote yule miongoni mwenu anayetaka kurudi nyuma anaweza kufanya hivyo, na mimi sita- mwajibisha juu ya hilo.” Baada ya maelezo haya wengi sana katika wau- mini wapya kwenye msafara wa Husein waliondoka wakaenda zao, wakiwaacha wachache tu, na wale ambao walifuatana pamoja naye kutoka Madina.

**Kupinga vita na kuwa na subira:** Amani na sera ya ‘kuishi na kuacha wengine waishi’ inaonyesha kwa neno la ‘Uislamu’ ambalo linapatikana kutokana na neno ‘salaam’ likimaanisha amani. Uislamu

huwataka waumini wake wasisababishe madhara kwa wengine, wala kuchochea matatizo, wala kugombana na wengine bila sababu zinazostahili. Kanuni ambat- ani ya Uislamu ni kwamba batili na udhalimu kamwe visikubaliwe, na kwamba haki isiruhusiwe kuja kuwa huzuni kwa matokeo ya matendo ya mtu.

Kanuni hizi zilionyeshwa kwa mifano katika uhai wa Mtume, wa Ali, wa Hasan na wa Husein. Mfano usio kifani ulionyeshwa na Mtume wakati mkataba wa al-Hudaybiyya ulipofanywa. Mkataba wa Hasan na Mu'awiyah pia ni mfano mwingine. Husein aliitumia miaka ishirini ya maisha yake katika kuridhia kwa uvumilivu katika mkataba wa kaka yake na Mu'awiyah, miaka kumi wakati wa uhai wa Hasan na miaka kumi baada ya kifo chake, ingawa wakati wa kipindi hiki kirefu mambo mengi yalijitokeza katika uvunjaji kamili wa masharti ya mkataba ambao kwa machungu kabisa uliitahini mno subira ya Husein.

Wingi wa mbinu za Mu'awiyah kutaka mwanawe, Yazid awekwe visivyo halali kama khalifa baada yake haukumshawishi Husein kuchukua hatua kuzuia mipango ya Mu'awiyah. Hatua pekee ambayo aliichukua ilikuwa ni kukataa kutoa kiapo cha utii kwa Yazid. Kwani alifikiria kukataa kwake kwenyewe peke yake kungeeleza ukweli wa jambo hili kwa Waislamu kama walikuwa wameachwa na uwezo wowote wa upambanuzi na uelewa na kwa hali yoyote ile asingewekwa kwenye shitaka la kuunga mkono maovu na makosa.

Angeweza kujihisi hahusiki kuhusu vipi ulimwengu kwa ujumla unavyozichukulia jitihada za Mu'awiyah; angeweza kumkubali Yazid kama mfalme au khalifa, ili mradi tu haikumsumbua kuhusu masuala haya, na kama haikumhitaji kuapa kiapo cha utii kwa Yazid. Akiitambua kanuni hii yenye kuongoza ya maisha ya Husein, Mu'awiyah alifikiria hakuna ulazima wa kuchukua hatua kali dhidi yake kwa sababu alijua kwamba Husein angelishikilia amani, na kuendelea katika mwendo wa amani ilimradi hakulazimishwa kutoa kiapo cha utii kwa Yazid.

Wakati Yazid alipomrithi baba yake Mu'awiyah alikidai kiapo cha utii cha Husein kupitia kwa gavana wa Madina, al-Walid, ambaye alikuwa hana msaada wa kutosha wa kijeshi. Kama Husein angekuwa ameelekea sana (kutaka kutawala) labda angeweza kujiweka kama mtawala wa Madina. Hiyo, hata hivyo ingemaanisha umwagaji damu na maandalizi ya vita vya muda mrefu. Husein, kwa hivyo alichagua kuondoka Madina ili kukwepa kumwaga damu ya Waislam, na akaenda Makkah kuonyesha kwamba lengo lake lilikuwa ni kukwepa kushikilia batili, na pia kuokoa maisha yake na maisha ya wategemezi wake, kwani Makkah ilichukuliwa kutoa hifadhi na usalama kwa kila mtu.

Hapo Makkah, Husein hakufanya kitu kwa hali yoyote ile, bali kuonyesha kwamba alikuwa hana lolote lile isipokuwa tu nia kubwa mno ya amani. Abdallah bin al-Zubeir hakuchukuliwa kwa kuheshimika sana na watu wa Makkah kama alivyokuwa Husein kwa sababu ya uhusiano wa karibu wa Husein na Mtume.

Kama Abdallah bin al-Zubeir angeweza kukusanya pamoja jeshi lenye nguvu za kutosha kuiweka ile serikali iliyoanzishwa katika kushughulika na majaribio ya nguvu kwa muda mrefu, ingekuwa ni rahisi zaidi kwa Husein kuorodhesha askari wa jeshi lenye nguvu zaidi la kumuunga mkono. Hata hivyo,

Husein alikaa kwa amani hapo Makkah wakati wote alipokuwa hapo.

Wakati watu wa Iraq walipotambua juu ya kukataa kwa Husein kutoa kiapo cha utii kwa Yazid, walimwandikia maombi 1200 na barua wakimwita kuja Kufa. Baadhi ya barua hizi pia zilipendekeza kwamba kama Husein angependa hivyo, watu wa Kufa wangemwondoa gavana mwenyeji na kumbadilisha wakamweka Husein, ambaye hakupendelea hata kidogo kulitia nguvu wazo hilo, na katika kujibu alisema,

“Imam (kiongozi) ni mtu yule ambaye hutenda kwa mujibu wa Kitabu cha Mwenyezi Mungu, anafungwa na uadilifu, anaifanya haki kuwa kanuni na msingi wa maisha yake, na anajitolea binafsi kabisa kwa ajili ya kupata radhi za Mwenyezi Mungu.”

Muslim bin Aqil ambaye alimtanguliua Husein kwenda Kufa alitoa ushahidi wa makusudio na malengo yasiyo ya kibinafsi ya binamu yake kwa kutenda kwa mwelekeo wa barua ya Husein, iliyonukuliwa sehemu yake hapo juu, alimradi hali ilimruhusu kufanya hivyo. Hakumwingilia kati kabisa Numan bin Bashir, gavana wa Kufa, au taratibu za serikali yake, hata wakati watu 18000 wa Kufa walipokula kiapo cha utii kwa Husein.

Yeye mwenyewe al-Numan alihisi kwamba tabia ya Muslim kwa upande wake ilikuwa siyo ile ya mpinzani, hivyo kwamba wakati vibaraka wa serikali walipomshtaki al-Numan na ulegevu, ingawaje idadi kubwa sana ya watu ilikuwa ikitoa kiapo cha utii kwa Husein, jibu lake lilikuwa kwam- ba angepigana tu na mtu yule ambaye amempiga, na atamshambulia yule tu ambaye atamshambulia yeye na hangetenda kutokana na kudhania tu.

Kuondoka kwa ghafla kwa Husein kutoka Makkah wakati zilikuwa zime- baki siku chacke tu kwa utekelezaji wa ibada ya Hijja ni ushuhuda wa dhahiri wa kuelekea kutokea karibuni sana ambayo aliihisi yeye mwenyewe endapo angebakia pale. Kuchukua hatua za wazi katika kujikinga ili kuzuia hatari ile kungeleta uwezekano wa umwagikaji damu mapema mno.

Husein hakutaka kujiingiza katika vita hapo Makkah kwani kufanya hivi kungenajisi utakatifu wa Nyumba ya Mwenyezi Mungu na ingekuwa pia inapingana na tabia yake yeye ya amani. Yeye aliwachukua pamoja naye wale tu wanawake wa nyumba yake na watoto wake kama ishara bayana na nia zake za amani.

Wakati al-Hurr alipowasili kuja kuingilia maendeleo ya safari ya Husein kuelekea Kufa, Husein alimwambia yeye (al-Hurr) na jeshi lake, “Sikuwa nimefikiria kuja kwenu mpaka pale barua zenu na wajumbe wenu waliponijia, mkiniambia kwamba mlikuwa hamna Imam, na mkanikaribisha nije kwenu ili kwamba labda pengine mngeweza kuungana katika haki kupitia kwangu… Kama hamtaki huku kufika kwangu mimi hapa, basi nitarudi kule nilikotoka.”

Hakukuweza kuwepo tena mfano mwingine wa kuvutia wa uvumilivu zaidi ya huu. Wakati Husein alipoikariba Karbala, al-Hurr alipokea barua kutoka kwa Ibn Ziyad ambayo iliufanya msimamo wa al-

Hurr kuwa mgumu kiasi kwamba alikataa kumruhusu Husein kusonga mbele zaidi, na akasema kwamba alikuwa anayo maagizo ya amri asimruhusu kupiga kambi katika sehemu yoyote ile inayokaliwa, bali akapige kambi katika bonde hame (yenye ukame) ambako maji yangekuwa ni ya taabu sana.

Marafiki na wafuasi wa Husein walipendekeza kwamba wapigane na al- Hurr kwa ajili ya kupata mahali pazuri zaidi pa kupigia kambi yao, kwani jeshi la al-Hurr wakati huo kwa kulinganisha lilikuwa siyo lenye nguvu sana. Husein hakukubaliana na ushauri huo, akikataa kuanzisha vurumai.

Hapo Karbala Husein alianzisha mazungumzo ya kuleta amani na Umar bin Sad, kwa ushahidiu wa wazi na wa kupenda amani na uvumilivu kiasi kwamba Umar bin Sa'd alivutika mno.

Husein pia alipendekeza kwamba yeye angekwenda sehemu za mbali zaidi nje ya Uarabuni ili amani iweze kudumu kama hakumlazimisha kumkubali Yazid kama khalifa halali, au kama mwakilishi wa kweli wa Uislamu. Hatimae Umar bin Sa'd aliandika barua kwa Ibn Ziyad akimpongeza kwa mgeuko mzuri wa mambo na akamwambia kwamba Husein alikuwa yuko tayari kufanya amani na kwamba masharti yake yangeweza kukubaliwa.

Hata katika siku ya 10 ya Muharram, wakati Shimr kwa matusi aliutaja moto uliowashwa katika shimo nyuma ya mahema ya Husein kuwazuia na mashambulizi kutoka upande wa nyuma, kwamba ni kama moto uliotazamiwa katika maisha ya akhera, na Muslim bin Awsaja alimwomba Husein ruhusa ili kumuua Shimr, Husein akakataa kukubali kwani aliona ni karaha kuanzisha vita.

Ingawaje mambo mengi yalitokea ambayo yangeweza kuifanya damu ya mtu ichemke wakati Husein alipotia mguu katika medani ya vita wakati wa asubuhi ya siku ya 10 ya Muharram, hakuonyesha hata dalili ndogo sana ya nia au maandalizi. Hakupanda farasi ambaye hutumika katika vita; bali alipanda ngamia ambaye ni alama ya amani.

Kisha alitoa hotuba ambayo ndani yake alirudia maneno yale ambayo aliwahi hapo mapema kumwambia al-Hurr na Umar bin Sa'd, "Kama hamuoni ni sawa kuja kwangu mimi hapa, (basi) niacheni nirudi kule nilikotoka." Shuhuda hizi zenye nguvu za upendo na amani na uvumilivu zilimlazimisha al-Hurr kulitelekeza jeshi la Yazid.

**Mhanga:** Husein alijitoa mhanga maisha yake kwa mujibu wa mpango uliofikiriwa kwa vizuri sana, ili kwamba zamu yake ya kujitoa mhanga yeye mwenyewe maisha yake imfikie kwa pole pole sana na awe amepata taabu na dhiki zilizo kubwa kabisa na idadi kubwa mno ya misiba kwa kuondokewa na watu awapendao sana, wakati atakapojitoa mhanga yeye mwenyewe.

Siku ya mwezi 10 ya Muharram, kwanza kabisa Husein alipata mateso kutokana na mhanga wa wasaidizi (waunga mkono) wake na wenzake wa tangu utotoni mwake.

Kisha aliteseka kutokana na mhanga wa ndugu na jamaa zake wa damu waliokufa mmoja mmoja; mwanawe kama Ali al-Akbar ambaye alikuwa nuru ya macho yake, nguvu ya moyo wake, na tegemeo

la umri wake wa uzeeni, mpwa kama al-Qasim, ndugu mwaminifu kama Abbas, na kisha mtoto mchanga kama Ali al-Asghar, ambaye shingo yake ilichomwa kwa mshale hatari. Baada ya moyo (watu) wake wote kutolewa mhanga, hatua ilifikia ya yeye binafsi kujitoa katika mhanga.

Kila sehemu ya mwili wake ilichanwa chanwa, kila tone la damu yake lilimwagika katika mhanga, na Husein hakubakia na chochote kile cha kujitoa mhanga, sehemu rahisi kabisa ya kazi yake, kujitoa mhanga maisha yake mwenyewe, ilibakia bado kufanywa. Na kufikia wakati wa mchana kujitoa mhanga kwake yeye kukawa pia kumekwishafanywa, na kichwa cha Husein kilikatwa kutoka katika mwili wake!

**Kamwe mhanga mkubwa na uliokamilika kama huo hautakuja kutolewa tena**.

# Orodha Ya Vitabu Vilivyo Chapishwa Na Al-Itrah Foundation:

1. Qur'an Al-Kariim - Tafsir Al-Kashif Juzuu ya kwanza mpaka Ishirini na Nne
2. Uharamisho wa Riba
3. Uharamisho wa uwongo Juzuu ya kwanza
4. Uharamisho wa uwongo Juzuu ya pili
5. Hekaya za Bahlul
6. Muhanga wa Imamu Husein (A.S.)
7. Mikingamo iliyomzunguka Imamu Ali (A.S.)
8. Hijab vazi Bora
9. Ukweli wa Shia Ithnaashari
10. Madhambi Makuu
11. Mbingu imenikirimu
12. Abdallah Ibn Saba
13. Khadijatul Kubra
14. Utumwa
15. Umakini katika Swala
16. Misingi ya Maarifa
17. Kanuni za Ndoa na maadili ya Familia
18. Bilal wa Afrika
19. Abudharr
20. Usahihi wa Historia ya Uislamu na Waislamu
21. Salman Farsi
22. Ammar Yasir

23. Qur'an na Hadithi
24. Elimu ya Nafsi
25. Yajue Madhehebu ya Shia
26. Ukusanyaji na Uhifadhi wa Qur'an Tukufu
27. Al-Wahda
28. Ponyo kutoka katika Qur'an.
29. Uislamu mfumo kamili wa maisha ya kijamii
30. Mashukio ya Akhera
31. Al Amali
32. Dua Indal Ahlul Bayt
33. Udhuu kwa mujibu wa Kitabu na Sunna.
34. Haki za wanawake katika Uislamu
35. Mwenyeezi Mungu na sifa zake
36. Amateka Na Aba'Khalifa
37. Nafasi za Ahlul Bayt (a.s)
38. Adhana.
39 Upendo katika Ukristo na Uislamu
40. Nyuma yaho naje kuyoboka
41. Amavu n'amavuko by'ubushiya
42. Kupaka juu ya khofu
43. Kukusanya swala mbili
44. Bismillah ni sehemu ya Qur'ani na husomwa kwa Jahara
45. Kuwaongoza vijana wa kizazi kipya
46. Kusujudu juu ya udongo
47. Kusheherekea Maulidi Ya Mtume (s)
48. Tarawehe
49. Malumbano baina ya Sunni na Shia
50. Kupunguza Swala safarini
51. Kufungua safarini
52. Umaasumu wa Manabii
53. Qur'an inatoa changamoto
54. as-Salaatu Khayrun Mina -'n Nawm
55. Uadilifu wa Masahaba
56. Dua e Kumayl
57. Sauti Ya Uadilifu wa Binadamu
58. Umaasumu wa Mitume - Faida Zake Na Lengo Lake
59. Umaasumu wa Mitume - Majibu Ya Aya Zenye Utata
60. Umaasumu wa Mitume - Umaasumu wa Mitume Muhammad (s)
61. Nahju'l-Balaghah - Juzuu ya Kwanza

62. Nahju'l-Balaghah - Juzuu ya Pili
63. Kuzuru Makaburi
64. Maswali Na Mishkili Elfu - Sehemu ya Kwanza
65. Maswali Na Mishkili Elfu - Sehemu ya Pili
66. Maswali Na Mishkili Elfu - Sehemu ya Tatu
67. Tujifunze Misingi Ya Dini
68. Sala ni Nguzo ya Dini
69. Mikesha Ya Peshawar
70. Malezi Ya Mtoto Katika Uislamu
71. Ubora wa Imam 'Ali Juu ya Maswahaba Na Ushia ndio njia iliy onyooka
72. Shia asema haya, Sunni asema haya, Wewe wasemaje?
73. Liqaa-u-llaah
74. Muhammad (s) Mtume wa Allah
75. Amani na Jihadi Katika Uislamu
76. Uislamu Ulienea Vipi?
77. Uadilifu, Amani na Mtume Muhammad (s)
78. Mitala na Ndoa za Mtume Muhammad (s)
79. Urejeo (al-Raja'a )
80. Shahidi kwa ajili ya Ubinadamu
81. Utokezo (al - Badau)
82. Kuanzia ndoa hadi kuwa wazazi
83. Myahudi wa Kimataifa
84. Uislamu na dhana
85. Mtoto mwema
86. Adabu za Sokoni
84. Johari za hekima kwa vijana
85. Maalimul Madrasatain Sehemu ya Kwanza
86. Maalimul Madrasatain Sehemu ya Pili
87. Maalimul Madrasatain Sehemu ya Tatu
88. Tawasali
89. Imam Mahdi katika Usunni na Ushia
90. Maana ya laana na kutukana katika Qur'ani Tukufu
91. Hukumu ya kujenga juu ya makaburi
92. Swala ya maiti na kumlilia maiti
93. Shiya na Hadithi (kinyarwanda)
94. Mariamu, Yesu na Ukristo kwa mtazamo wa Kiislamu
95. Hadithi ya Thaqalain
96. Fatima al-Zahra
97. Tabaruku

98. Sunan an-Nabii
99. Historia na sera ya viongozi wema (Sehemu ya Kwanza)
100. Idil Ghadiri
101. Mahdi katika sunna
102. Kusalia Nabii (s.a.w)
103. Ujumbe -Sehemu ya Kwanza
104. Ujumbe - Sehemu ya Pili
105. Ujumbe - Sehemu ya Tatu
106. Ujumbe - Sehemu ya Nne
107. Shiya N'abasahaba
108. Iduwa ya Kumayili
109. Maarifa ya Kiislamu.
110. Ukweli uliopotea sehemu ya Kwanza
111. Ukweli uliopotea sehemu ya Pili
112. Ukweli uliopotea sehemu ya Tatu
113. Ukweli uliopotea sehmu ya Nne
114. Ukweli uliopotea sehmu ya Tano
115. Johari zenye hekima kwa vijana
116. Safari ya kuifuata Nuru
117. Historia na sera ya vijana wema
118. Myahudi wa Kimataifa
119. Kuanzia ndoa hadi kuwa Wazazi
120. Visa vya kweli

## Back Cover: Shahidi Kwa Ajili Ya Ubinadamu

Huyu ni Imam Husain bin Ali bin Abu Talib - Madhulumu wa Karbala - mjukuu wa Mtukufu Mtume Muhammad (saww) kwa binti yake Fatima.

Masaibu ya Karbala ni maarufu sana. Kila mwaka unapofika mwezi wa Muharram, Waislamu duniani kote hufanya majlisi (mikusanyiko) kwa ajili ya kuomboleza masaibu yaliyompata Imam Husain (as) - mtoto wa Imam Ali (as) na Fatima (as) ambaye ni mjukuu halisi wa Mtukufu Mtume (saww).

Kwa hakika masaibu haya yanazidi kuwa maarufu kadiri miaka inavyozi- di kwenda. Waislamu wanazidi kuathiriwa mno na masaibu haya, na kuwa na hamu ya kutaka kujua zaidi masaibu haya yaliyompata mjukuu huyu wa Mtukufu Mtume (saww) yametokana na nini na yamesababishwa na nini hasa.

Kama ilivyo vitabu vyingi vinavyohusu masuala ya dini vimeandikwa kwa lugha za kigeni, vivyo hivyo maelezo ya masaibu haya mengi yamo kwenye lugha za kigeni, na hivyo Waislamu wengi wazungumzaji wa Kiswahili wamekuwa hawazipati habari hizi moja kwa moja kupitia kwenye vitabu, ila

kwa kuhudhuria majlisi. Hivyo ili kuzima kiu ya waso- maji wetu, haya hapa ni maelezo ya tukio hilo (la kusikitisha) kwa lugha ya Kiswahili.

Kimetolewa na kuchapishwa na:

**Alitrah Foundation**

S.L.P. 19701 Dar es Salaam, Tanzania

Simu: +255 22 2110640 / 2127555

Barua Pepe: alitrah@raha.com [11]

Tovuti: www.ibn-tv.com [12]

---

**URL del envío:**

https://www.al-islam.org/es/shahidi-kwa-ajili-ya-ubinadamu-sayyid-ali-naqi-naqvi#comment-0

**Enlaces**

[1] https://www.al-islam.org/es/person/sayyid-ali-naqi-naqvi

[2] https://www.al-islam.org/es/organization/al-itrah-foundation-0

[3] https://www.al-islam.org/printpdf/book/export/html/25317

[4] https://www.al-islam.org/printepub/book/export/html/25317

[5] https://www.al-islam.org/printmobi/book/export/html/25317

[6] https://www.al-islam.org/es/person/mganga-b-mnuve

[7] https://www.al-islam.org/es/tags/karbala

[8] https://www.al-islam.org/es/tags/history

[9] https://www.al-islam.org/es/tags/muharram

[10] https://www.al-islam.org/es/person/imam-husayn

[11] mailto:alitrah@raha.com

[12] http://www.ibn-tv.com